

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Nane – Tarehe 20 Mei, 2015

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Ledian M. Mng'ong'o) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 53

Ujenzi Kwenye Maeneo ya Wazi Mji wa Himo

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA) aliuliza:-

Wako watu wamejenga kwenye maeneo ya wazi katika Mji Mdogo wa Himo na kuna mchakato unaoendelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi wa kuwamilikisha maeneo hayo:-

(a) Je, ni nini msimamo wa Serikali juu ya hao waliovamia na kujenga kwenye maeneo hayo?

(b) Je, Maafisa wa Ardhi walioyatoa maeneo hayo wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustino L. Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna watu tisa waliovamia na kujenga kwenye maeneo manne ya wazi kati ya maeneo tisa yaliyoko katika Kitalu "G" Mji Mdogo wa Himo. Uvamizi huo ulikiuka Sheria ya Mipango Miji Namba Nane ya mwaka 2007, ambayo inaelekeza mabadiliko yoyote ya mchoro wa Mipango Miji pamoja na kupata idhini ya uongozi wa Wilaya kupitia kikao cha Kamati Ndogo ya Ugawaji Ardhi kilichohalalisha na kupitisha maombi ya kutaka kukamilisha viwanja sharti yapate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani.

Serikali itafanya uchunguzi kubaini uhalali wa watu wote wanaosemekana kumilikishwa maeneo ya wazi na hatua zitachukuliwa kwa kuzingatia sheria zilizopo. Aidha, wavamizi wengine waliojenga kwenye maeneo mawili ya wazi, wameweka pingamizi mahakamani kwamba, wasiondolewe kwenye maeneo hayo kwa sababu wamemilikishwa kihalali. Uamuzi wa suala hilo unasubiri maamuzi ya mahakama.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Himo ulitangazwa kuwa Eneo la Mpango (*Planning Area*) kwa Tangazo la Serikali Namba 176 la mwaka 1996. Aidha, Mji huo ulipewa hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo kwa Tangazo la Serikali Namba 353 la mwaka 2004.

Kama ilivyoielezwa katika sehemu (a) ya jibu hili, uchunguzi huo ukikamilika na kubainika kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa sheria katika suala zima la kubadili matumizi ya maeneo ya wazi na kutumika kwa ajili ya makazi, Maafisa wote waliohusika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Hivyo, Serikali inamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira wakati suala hili linafanyiwa uchunguzi ili kulipatia ufumbuzi kikamilifu.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa watu hawa wanavunja sheria ilhali wakijua kabisa maeneo hayo ni ya wazi na yanapaswa kutumika kwa ajili ya shuguli za Serikali na wanakwenda mahakamani kuweka pingamizi. Je, Wizara ina mpango gani wa makusudi wa kuhakikisha inatumia nyaraka ilizonazo kihalali kuwashughulikia watu hawa na kumaliza kesi hizo mahakamani mapema iwezekanavyo?

(ii) Kwa kuwa kuna Maafisa Ardhi ambao wanakiuka taratibu na misingi ya kazi zao na kusababisha usumbufu huu mkubwa ambao kimsingi haustahili na kukwamisha maendeleo; je,

Wizara inachukua jukumu gani au hatua gani za kisheria kuwashughulikia hawa watu wanaokiuka taratibu na sheria za nchi? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Mbassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, wako wananchi wamevamia kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi. Nataka nieleze kwamba, Mji Mdogo wa Himo awali ulikuwa ni Mji ambao haujapata hadhi yake na ulipandishwa kupata hadhi ya Mji Mdogo mwaka 2004. Kabla ya hapo, ardhi zote kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo bado hazijapewa hadhi ya Miji Mdogo, zinakuwa kwenye Mpango tu wa Mipango Miji ya ndani ya Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, wakati huo chini ya Mpango huo wa Mipango Miji, wananchi hawa walikuwa wameshavamia. Baada ya kupata hadhi ya kuwa Mji Mdogo, sasa Mji Mdogo wowote ule unapokuwa kwenye *Master Plan*, mgongano uliopo ni matakwa ya sasa ya kuweka *Master Plan* ili kila kitu kijengwe kwa uataratibu na Mipango Miji iliyokuwepo. Kwa hiyo, sasa kwa kuwa walishavamia, baada ya mabadiliko haya, kwa kuwa jambo hili liko mahakamani na wanadai walimilikishwa kihalali kwa Mipango Miji, sasa tusbiri mahakama iamue, ili turudi sasa Mji Mdogo wa Himo uwekwe kwenye *Master Plan*.

La pili, suala la Maafisa Ardhi ambao tunao na wamekiuka taratibu hizi; Serikali mpango wetu ni kuhakikisha kila kitu kinaenda kwa mijiibu wa sheria na taratibu zilizopo. Inapotokea Mtendaji wetu kafanya kinyume, hapa sasa lazima tumchukulie hatua. Kwa hiyo, hatua stahili zitachukuliwa na hasa kwa Maafisa Ardhi ambao wanatuletea migogoro ndani ya Serikali. Tumeweka mkakati thabiti wa kuwasimamia kikamilifu ili watende kazi kwa maadili yanayotakiwa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, mamlaka ya kutoa adhabu kwa Maafisa Ardhi inafanywa na Madiwani na wakati mwingine inafanywa na Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa tarehe 30 Novemba 2014, baadhi ya Wakurugenzi walisimamishwa mpaka leo baadhi ya Halmashauri nchini hazina Wakurugenzi. Hivi tatizo ni nini kwa sababu hivi sasa maendeleo yamesimama kwa sababu Wakurugenzi waliokuwepo wamesimamishwa na hakuna Mkurugenzi aliyepolekwa hadi sasa? Kama Wakurugenzi walibainika wana matatizo Serikali kwa nini isiwachukulie hatua na kuleta Wakurugenzi wengine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Ndassa, jambo hili amekuwa kilifuatilia, ili kuhakikisha Wilaya ya Kwimba inakuwa na Mkurugenzi. Juzi tulizungumza hapa, tukiwa hapo nje juu ya jambo hili na kubadilishana mawazo. Bado nirudie jibu ambalo nilimpa juzi kwamba, tunatambua ni kweli wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wapo Wakurugenzi waliingia kwenye matatizo kwa sababu ya utendaji mbovu. Bado mkakati uleule wa kuwachukulia hatua Watendaji wabovu bado unaendelea. Hivi sasa tunafanya *vetting* ya watu ambao wanastahili kupata nafasi hiyo ili watumikie ndani ya Serikali kwa maadili ambayo tunayakusudia.

Kwa hiyo, jambo hili limefikia hatua ya mwisho, tumeshapeleka majina kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuidhinisha ili Wakurugenzi hawa tuwasambaze kwenye Halmashauri zote ambazo tulikuwa tumesimamisha Wakurugenzi kwa kusababisha vurugu wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Na. 54

Ongezeko la Uchafu Jijini Dar es Salaam

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uchafu katika jiji la Dar es Salaam hali inayoleta aibu kubwa kwa wageni na kuongezeka kwa mazalio ya mbu:-

Je, ni hatua gani za haraka zimechukuliwa ili kutatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafi wa miji hapa nchini linasimamiwa na sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji. Hata hivyo, usimamizi wa sheria kutoka wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa, umekuwa siyo wa kuridhisha sana, hali ambayo inasababisha kukithiri kwa uchafu kwenye miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam linao mpango thabiti wa kuimarisha uzoaji taka Jijini na tayari makakati wa kuanzisha dampo litakaloendeshwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kusindika taka kwa kushirikiana na Kampuni ya *Best Green Solution* umeandaliwa.

Katika kupambana na changamoto zilizoko katika Jiji la Dar es Salaam, Jiji hilo limetumia shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa mtambo mpya wa kusukuma taka (*Bulldozer D8*), ununuzi wa malori mawili yenye tani 18 kwa ajili ya kuzoa taka na ununuzi wa *compacter* moja kwa ajili ya kushindilia taka. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016, itanza kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam, ambao unakusudia kuimarisha miundombinu ya barabara za mitaa zinazounganisha kwenye Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, kudhibiti mafuriko kwa kujenga mifereji mikubwa na midogo ya maji ya mvua katika maeneo yote yanayoathiriwa na mafuriko na utekelezaji wa miradi inayohusu usafi na mazingira.

Mradi huu utatelekezwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 300, kati ya hizo katika mwaka wa fedha 2015/2016 ambao sasa tunauzungumza, zimetengwa Dola za Kimarekani milioni 10, sawa na shilingi bilioni 17.3 ili kuanza ujenzi wa miundombinu ya barabara za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali imeanzisha Idara ya Usafi na Mazingira katika halmashauri zote nchini kwa lengo la kuimarisha huduma ya usafi katika miji yote nchini. Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), itaendelea kufuatilia na kuwachukulia hatua Watendaji wanaoshindwa kusimamia suala la usafi, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya shughuli za usafi kwenye Halmashauri zao.

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Jiji la Dar es Salaam ni chafu haijalishi kuna mvua wala hakuna mvua. Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuondoa kero hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama alivyoliuza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi kwamba, uchafu uliokithiri kwenye Jiji la Dar es Salaam, bado kasi ya uzoaji wa takataka hizo siyo ya kuridhisha kwenye Manispaa zake zile. Sasa tumefika mahali ambapo tumeweka mikakati thabiti ya kuhakikisha taka zote zinazozolewa ambazo zinazalishwa pale Dar es Salaam zinasombwa zote.

Kwa sasa hivi Jiji la Dar es Salaam lote, linazalisha taka zaidi ya tani 4,292 kwa siku, lakini uzoaji wake ni tani 2,115 kwa siku, kama asilimia 50, bado hali hiyo haitoshi. Hii ndiyo sababu sasa Jiji la Dar es Salaam limeamua kutafuta eneo lingine la kupeleka taka zetu pamoja na kutambulisha teknolojia mpya ambayo watakamilisha kuingia mkataba na Kampuni ya *Best Green Solution* kutoka Brazili. Eneo limepatikana, taratibu za ukamilishaji wa malipo zitafanywa wakati wowote kuanzia sasa na kampuni hii itaingia. Wamekubaliana na Jiji na eneo la Mkuranga limeshapatikana kwa ajili ya kupeleka taka hizo kwa teknolojia mpya.

Kwa kauli hii, natoa wito kwa Majiji yote na Manispaa zote na Halmashauri za Wilaya zote, kuhakikisha sasa tunabadilika kwa kuwa na teknolojia mpya, badala ya kuzoa taka na kwenda kuzirundika kwenye maeneo mengine, taka zile zitumike. Tuanze kuzibadilisha tupate matokeo mengine kama teknolojia ya Jiji la Dar es Salaam ambayo itaanza kutumika, ambavyo inatakiwa ifanyike. Tumeanza kupitia Miradi mbalimbali kule Mbeya tayari Jiji la Mwanza na Jiji la Tanga, wameanza utaratibu huu wa kubadilisha taka hizi kuwa mali tena kwa sura nyingine. Kwa hiyo, Majiji yote yajipange vizuri kuhakikisha teknolojia mpya sasa inahitajika katika kukabiliana na taka hizi.

Na. 55

Mradi wa TASAF III Nchini

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Mradi wa *TASAF III* una lengo zuri la kusaidia kaya maskini kwa Tanzania Bara na Zanzibar:-

(a) Je, ni kaya ngapi ambazo zimeweza kunufaika na Mradi huo kwa Tanzania Bara na upande wa Zanzibar?

(b) Je, ni kaya ngapi ambazo tayari zimeweza kubadilika kimaisha baada ya kunufaika na Mradi huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kususuru Kaya Maskini Unaotekelezwa Chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ulizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Agosti 2012 na unatekelezwa katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba.

Idadi ya walengwa wanaotarajiwa kufikiwa na Mpango huu ni kaya maskini zaidi ya milioni moja ambazo zina takribani watu milioni saba. Walengwa hawa wanatambuliwa katika Mikutano ya Vijiji na Mitaa, inayoendeshwa na Maafisa kutoka Halmashauri kwa kusimamiwa na Uongozi wa Vijiji, Mitaa na Shehia.

Uhawilishaji fedha kwa kaya maskini ulianza rasmi mwezi Januari 2014, katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji 40, kwenye Vijiji, Mitaa na Shehia 1,983 kwenye Mikoa ya Pwani, Morogoro, Mara, Ruvuma, Mbeya, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Katavi na Kigoma pamoja na Unguja na Pemba kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Jumla ya kaya maskini 260,173 zimekwishanufaika hadi mwezi Machi 2015 na kiasi cha fedha ambacho kaya hizo zimehawilishiwa kwa masharti ya lishe, elimu na afya ni Shilingi 48,387,175,155.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, uhawilishaji ambao umeshafanyika katika maeneo haya kwa kiasi kikubwa, umeshaanza kubadilisha maisha ya watu waliomo katika kaya hizi. Kwanza kabisa, ni katika upatikanaji wa chakula. Kaya maskini 260,173 ambazo zimeanza kupata ruzuku zina uhakika wa kupata zaidi ya mlo mmoja kwa siku. Kwa upande wa elimu, kaya zenye watoto wanaokwenda shule wanatakiwa kuhudhuria masomo bila kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu tulizonazo zinaonesha kwamba, watoto wengi kutoka katika kaya maskini walikuwa hawahudhuri shuleni, lakini baada ya kuanza Mpango huu, sasa wanahudhuria shuleni. Mabadiliko mengine ambayo yameanza kuonekana katika kaya hizi ni uwezo wa kuweka akiba na kuweza kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato. Baadhi ya kaya zimeanza kutekeleza miradi ya ufugaji, kilimo na uchuuzi wa bidhaa ili kuendelea kujijenga kiuchumi.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri, swali langu amelijibu vizuri na nina hakika wanakaya na Watanzania wote wameelewa nini dhima ya TASAF III.

Mheshimiwa Waziri ni miongoni mwa waanzilishi wa TASAF III; hongera Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza, madogo tu.

(i) Kwa zile kaya ambazo tayari zimefanikiwa, je, baada ya kufanikiwa kaya hizo wanatoa elimu gani kwa kaya ambazo bado hazijafanikiwa?

(ii) Je, vipo vigezo gani mlivyoviweka ili kaya husika kujitambua kwamba sasa wao umaskini umewaondoka? Naomba kupata jawabu, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia Shomar, kama ifuatavyo:-

Kabla ya hapo, napenda kumpongeza na kumshukuru sana, kuona athari zinazopata kaya maskini na kwa hiyo kujielekeza kwenye swali hilo.

Swali lake la kwanza ni kuhusu elimu inayotolewa na wale ambao wamefanikiwa kwa kaya ambazo bado ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge lako Tukufu, elimu ambayo tunaipata na zile kaya ambazo bado ni maskini zinapaswa kupata ni kwamba, kuna uwezo wa kuondoa umaskini Tanzania kama Serikali na wananchi watahikana pamoja kuhakikisha kwamba, wale ambao walikuwa hawapati chakula zile fedha sasa zinatumiwa na kwamba wanapeleka watoto wao shule na hatimaye wale wadogo wanapelekwa kliniki. Wale wanaokwenda shule wakipata elimu, watakuwa wamewezeshwa kuwa Wananchi ambao baadaye hawataweza kuwa na umaskini. Kwa hiyo, kaya zilizo maskini ziwe na subira tutazifikia na hatimaye Tanzania itakuwa ni nchi ambayo haina kaya maskini.

Ya pili, vigezo vinavyotumiwa. Walengwa wa mpango huu ni kaya maskini sana ambazo zimetambuliwa katika maeneo ya utekelezaji. Vigezo vikubwa vilivyowezesha kaya hizo kukidhi vigezo vya umaskini ni kushindwa kupata angalau mlo mmoja kwa siku; ya pili, kuwa na watoto ambao wameshindwa kuandikishwa au kuhudhuria masomo kwa kutokuwa na mahitaji ya shule; na kaya zingine zinazoshindwa hata kupeleka watoto wa chini ya miaka mitano kliniki kwa ajili ya kuangaliwa afya yao na kuwa na lishe duni.

Kwa hiyo, TASAF haibahatishi, TASAF inatumia vigezo ambavyo ni mahususi, ambavyo vikitumiwa vizuri tunatambua walio maskini na tukitekeleza Mradi huu na Mpango huu vizuri, basi umaskini utatoweka na hatimaye tutakuwa nchi ambayo ina heshima na watu wake wana maisha bora.

MWENYEKITI: Waheshimiwa wabunge, tunaendelea swali lingine, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Hussein Amar, kwa niaba yake Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

Na. 56

Upatikanaji wa Matrekta kwa Wakulima

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR) aliuliza:-

Zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini na wanategemea kilimo:-

Je, Serikali itaipatia matrekta mangapi Wilaya Mpya ya Nyang'hwale yenye ardhi nzuri na mabonde mazuri ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara ikiwa ni njia mojawapo ya kuunga mkono mpango wa Kilimo Kwanza?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwawezesha wakulima kupata matrekta makubwa na madogo kupitia uchangiaji

wa asilimia ishirini kwa Miradi iliyoibuliwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo (DADPS), mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, mikopo kutoka Benki ya Taifa ya Rasilimali (TIB) kupitia Vyama vya Ushirika (SACCOS) na mikopo kupitia *Private Agricultural Sector Support (PASS)* inayoshirikiana na Benki ya CRDB.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hiyo imewezesha kuongezeka kwa idadi ya matrekta makubwa nchini kufikia 10,064 hadi mwezi Disemba 2014 na hivyo kuwezesha eneo linalolimwa kwa matrekta kwa sasa kuongezeka kutoka asilimia 10 hadi asilimia 14 ya eneo lote linalolimwa. Aidha, eneo linalolimwa kwa jembe la mkono limepungua kutoka asilimia sabini hadi asilimia sitini na nne na eneo linalolimwa kwa kutumia wanyamakazi limeongezeka kutoka asilimia ishirini hadi asilimia ishirini na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwezesha upatikanaji wa zana bora za kilimo, tayari Mkoa wa Geita una jumla ya matrekta makubwa 76 na matrekta madogo 80, ambapo katika Wilaya ya Nyang'hwale yapo matrekta manane na matrekta madogo 18. Wakulima wa Nyang'hwale wanashauriwa kutumia fursa zilizopo za kupata mikopo kama nilivyoeleza hivi punde. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale inashauriwa kuwahamasisha wakulima kujiunga au kuanzisha Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS), ambavyo vitawawezesha kuwapatia mikopo au kuwadhamini ili waweze kupata mikopo katika taasisi za fedha kwa ajili ya kununua matrekta na zana zake.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nashukuru kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa takwimu alizozionesha hapa zinaonesha Mkoa wa Geita kuna matrekta 76 tu na *power tiller* 80 tu, jambo ambalo mimi naona kama tuna vitendea kazi kidogo sana kulinganisha na hali halisi ya mkoa jinsi ambavyo tunategemea kilimo. Vilevile katika Wilaya ya Nyang'hwale kuna matrekta makubwa manane na madogo (*power tiller*) 18 tu. Napenda kujua kutoka Wizara ya Kilimo; mnatusaidiaje tupate matrekta zaidi kwa kuwa swali la msingi limeuliza Serikali itaipatia matrekta mangapi Wilaya ya Nyang'hwale ili Wananchi waendeleo kutumia matrekta?

(ii) Wakulima wetu wa Nyang'hwale pamoja na Mkoa wa Geita kwa ujumla wamehamasika sana kukopa mikopo na wanahitaji sana kukopeshwa hii mikopo, lakini upatikanaji wake imekuwa ni tatizo kubwa; kwa sababu Benki ya TIB katika Mkoa wa Geita haipo. Ukitaka kukopa inabidi uende Mwanza na kuna umbali mrefu. Je, Serikali inatusaidiaje sasa kuweza kuwa na dirisha angalau la TIB katika Mkoa wa Geita ili Wananchi wa mkoa ule waweze kufaidika na mikopo hii ya kilimo? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema au kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba, Mkoa wa Geita una matrekta kama nilivyoyasema, lakini pia na Wilaya ya Nyang'hwale ina matrekta kama ambavyo nimeeleza na Mbunge ameyarejea. Amesema matrekta hayo na *power tillers* hizo ni ni chache, tunakubaliana na hilo. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Mkoa wa Geita umeleta maombi mengine ya matrekta makubwa 114 na Wilaya ya Nyang'hwale katika hayo wameomba matrekta 22. Sasa kama nilivyosema, jukumu hili ni la Wilaya zenyewe kuomba, lakini pia kupitia Vikundi vya SACCOS

ambavyo vinaweza pia vikapata mikopo rahisi kwa maana ya kuwezesha kununua matrekta hayo.

Naomba naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba, Serikali inao mpango mkubwa na madhubuti kabisa wa kuhakikisha tunaweza tukapata matrekta mengi. Mwezi uliopita kati ya tarehe 16 na 22, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Wassira, alienda nchini Poland na tayari Serikali imeshakubaliana na kupata mkopo nafuu kutoka Poland wa Euro karibu milioni mia moja ambazo katika hizo Euro milioni hamsini zitatumika kwa ajili ya kuanza ku-*assemble* matrekta hapa nchini. Kwa hiyo, nina hakika, baada ya mpango huo kuanza, ambao tuko nao katika hatua nzuri sana, matrekta yatakuwepo ya kutosha hapa nchini. Nina hakika Halmashauri nyingi pamoja na watu binafsi pia wataweza kupata matrekta kwa bei iliyo nafuu zaidi.

Naomba nimhamasishe Mbunge aiambie Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale na Mkoa wa Geita kwamba, wajitahidi sasa kuhakikisha wanakuwa na mipango mizuri zaidi ambayo itawawezesha na wao waweze kufaidika na mikopo hiyo ya matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anasema upatikanaji wa mikopo ni shida na kwamba angeomba kuwe na Dirisha la Kilimo kule Benki ya Geita. Kwanza, naomba niseme kwamba, tumesema tunaanzisha Benki ya Kilimo, ambayo kimsingi inaanza kufanya kazi mwezi wa saba. Inaanza kufanya kazi rasmi, huko nyuma tulikuwa tunafanya kazi kupitia Dirisha la Kilimo ndani ya TIB, sasa tunakwenda na benki yenyewe na benki benki hii, *Tanzania Agricultural Development Bank (TADB)* itashirikiana na benki zilizopo sasa hivi. Kwa hiyo, natumaini Benki hii ya TADB itaingia mkataba na benki ambayo iko pale Geita kwa ajili ya kuanza kutoa mikopo na kwa maana hiyo, Wananchi jirani zaidi wanaweza wakapata mikopo hiyo kwa urahisi zaidi; kama nilivyosema baada ya hii ya Benki ya TADB kuanza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Julai 2015. Ahsante sana.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nami nimpongeze Waziri kwa namna alivyotueleza, lakini napenda nimwambie katika Wilaya yetu ya Missenyi sisi tulikuwa tayari tumeshapata *profoma* na tulishakusanya milioni zetu kadhaa na tukawa tumeshaleta wakati matrekta yanatolewa chini ya Jeshi la Ulinzi.

Mheshimiwa Waziri umesema kwamba, matrekta yatakuja kuwa *assembled* hapa nchini, lakini nikiangalia ule utaratibu mpaka ufike utachukua muda mrefu. Nini mpango wa haraka wa muda mfupi wa kuweza kutusaidia sisi ambao tayari tuna pesa zetu tuweze kununua wakati ukiendeleza mipango yako ya ku-*assemble* hapa hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema walipata *profoma* kwa ajili ya kununua matrekta kutoka Suma JKT. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, bado Suma JKT wana mpango wa kuingiza matrekta nchini. Mbali ya mpango wa kuanza ku-*assemble* matrekta, lakini kulishawahi kuwa na mpango wa kuingiza karibu matrekta 4,000 nchini. Kwa hiyo, nitafuatilia mpango huo kujua Suma JKT wamefikia wapi halafu nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge.

Kuhusu huu mpango ambao tunataka kuanza ku-*assemble* matrekta, siyo wa muda mrefu sana kama nilivyokwishawaeleza Waheshimiwa Wabunge. Tayari mkopo umeshapatikana wa walau kuanza na Euro milioni hamsini na kinachotakiwa sasa ni sisi Serikali

kwa ajili ya kukamilisha ile mikataba na Serikali ya Poland, lakini mkopo umeshapatikana na kazi hii inaweza ikaanza mwaka huu huu. Kwa sababu ni suala la ku-*assemble* ni suala ambalo haliweza kuchukua hata zaidi ya mwaka mmoja na mimi nina hakika Wananchi wa Nkenge kule watafaidika na jambo hilo.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, lakini lile swali lake la Suma JKT nitampatia majibu hata leo mchana baada ya mimi kutoka hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Buyogera!

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa akunipa nafasi na mimi niulize swali dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kigoma Wilaya ya Kasulu ndiyo inayoongoza kwa kulima mazao ya chakula, lakini kumekuwa na vikundi vya wakulima ambavyo vimeomba matrekta kwa muda mrefu, hasa Kikundi cha Wakulima Kalela, Kikundi cha Wakulima Rungwe mpya ikiwemo Chuo cha Kilimo pale Kasulu. Ninaomba kupata majibu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuamini kwamba, huwa Wizara yako inaaahidi na inatekeleza.

Je, ni hatu gani zitachukuliwa za haraka ili Wananchi wa Kasulu waweze kupata matrekta. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba, ni kweli vikundi hivyo alivyovitaja vya Kalela, Rungwe Mpya pamoja na Chuo cha Kilimo Mbondo, vilishaleta maombi hayo. Naomba nimhakikishie kwamba, Chuo cha Kilimo cha Mbondo tayari kina trekta, *unless* kama walikuwa wameagiza trekta lingine, lakini mimi nilikitembelea chuo kile na niliona wanalo trekta ambalo pia linawasaidia kwa ajili ya kufanya kazi za pale.

Sasa kuhusu vikundi hivyo kama vilishaomba, kama nilivyokwisha kueleza kwenye maswali yaliyotangulia, nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba, tutafuatilia kama Suma JKT wataingia haya matrekta, basi Wananchi hawa pia waweze kufuatilia hilo. Niseme kwamba, wanaweza pia wakaomba kutumia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ambao na wao pia huwa wanaingiza matrekta.

Mwaka wa jana tumetumia karibu Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuingiza matrekta makubwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, ambao kama Wananchi sijui sasa waliomba katika mifuko ipi. Kwa vyovyote vile nimhakikishie kwamba, jitihada za Serikali ni kubwa na Wananchi hawa watapata matrekta katika kipindi kisicho kirefu sana kama walivyokuwa wameomba. *(Makofi)*

Na. 57

Uwekezaji katika Vinu vya Kuchambulia Pamba

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Zao la Pamba linastawi kwa wingi katika Jimbo la Mbogwe lakini kuna uhaba wa vinu vya kuchambulia pamba hali inayosababisha kupanda kwa bei ya zao hilo:-

Je, ni lini Serikali itayashawishi makampuni yanayoshughulika na Zao la Pamba yawekeze katika vinu vya kuchambulia pamba katika Jimbo la Mbogwe?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbogwe ni mojawapo ya maeneo muhimu katika uzalishaji wa pamba nchini, ambapo uzalishaji wa pamba-mbegu katika msimu wa mwaka 2012/2013 ulikuwa kilo 2,467,400 na msimu wa mwaka 2013/14 uzalishaji ulikuwa kilo 2,168,980.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa usindikaji wa mazao ya kilimo, Serikali imekuwa ikihamasisha wawekezaji binafsi pamoja na wakulima kupitia Vyama vya Ushirika, kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ikiwemo Zao la Pamba. Hata hivyo, uwekezaji katika viwanda vya kuchambua pamba huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa pamba ya kutosha ili kuwezesha viwanda kujiendesha kwa faida na hivyo kurejesha gharama za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa katika Mji wa Ushirombo ulio karibu na Wilaya ya Mbogwe, vipo viwanda viwili vya kuchambua pamba ambavyo vinamilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanya (SHIRECU) na Kampuni ya *Billichant Oil Mills Limited* na vina uwezo wa kuchambua jumla ya marobota 13,824 katika muda wa mwezi mmoja. Aidha, ili kiwanda cha pamba kiweze kujiendesha kwa ufanisi kinahitaji kupata malighafi ya kutosha. Hata hivyo, uzalishaji uliopo katika Wilaya ya Mbogwe na Bukombe wa takribani kilo 13,020,743 unawezesha viwanda vilivyopo katika maeneo hayo kufanya kazi kwa kipindi kisichozidi miezi miwili, hivyo mpango wa kuanzisha viwanda vingine katika maeneo hayo hautakuwa na tija kwa kuzingatia uzalishaji uliopo sasa.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Katika Mkoa Mpya wa Geita kuna vinu kadhaa vya kuchambua pamba kikiwepo COPCOPT, SHIRECU, Chato, Kasamwa na *Billichant*. Serikali ina mpango gani wa kuupatia Mkoa Mpya huu wa Geita viwanda vya kufuma nyuzi na kutengeneza nguo ili kuongeza ajira katika Mkoa wetu wa Geita?

(ii) Serikali ilichukua jukumu la kukusanya ushuru wa Zao la Pamba kupitia Wakala wa Bodi ya Pamba lakini mpaka sasa hivi Halmashauri zetu zimeshindwa kupatiwa huo ushuru na matokeo yake Halmashauri zinaendesha shughuli zake kwa tabu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa Watanzania wa Mkoa wa Geita huo ushuru wa pamba ambapo Bodi ya Pamba imeshindwa kuwalipa? Ahsante.

MWENYEKITI: Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika!

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Manyanda, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni Sera ya Serikali lakini vilevile katika Mpango wa Maendeleo ujao wa Miaka Mitano, mkazo mkubwa utawekwa katika kuanzisha viwanda kwa ajili ya kusindika mazao ya

kilimo badala ya kuyauza mazao ghafi. Kwa mfano, kwa muda mrefu sana Zao la Pamba limekuwa likiuzwa nje likiwa ghafi, kule kuondoa nyuzi hakuongezi thamani kubwa.

Kwa hiyo, kwa kweli Mpango ujao wa Maendeleo utakuwa ni kuhakikisha kwenye Zao la Pamba tunasisitiza uanzishaji wa viwanda kwa ajili ya kutengeneza nyuzi na nguo. Hiyo ndiyo itakayokuwa kazi yetu kwa miaka mitano inayokuja ili kuhakikisha pamba nyingi zaidi kama siyo yote, inasindikwa hapa nchini na tunauza nguo badala ya kuuza pamba ghafi.

Kuhusu suala la ushuru, ni kweli kwamba, mwaka jana kutokana na kushuka kwa bei ya Zao la Pamba, Serikali iliamua kuacha kumkata mkulima moja kwa moja ushuru ili kuhakikisha ule ushuru uliokuwa unakatwa unaongeza tija kwa mkulima na Serikali ilibeba mzigo wa kulipa ushuru badala ya mkulima kukatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutengeneza utaratibu na tumezungumza na Hazina na hivi sasa wanakamilisha utaratibu wa kuzilipa Halmashauri za Pamba ushuru wao kama Serikali ilivyoahidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tupo nyuma ya wakati, tunaenda sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere; kwa niaba yake Mheshimiwa Mbarouk!

Na. 58

Mafunzo ya Ujasiriamali kwa Wafungwa Nchini

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. VINCENT J. NYERERE) aliuliza:-

Magereza siyo sehemu ya adhabu tu bali pia ni sehemu ya mafunzo ya maisha kwa waliokuwa wahalifu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri wakufunzi wa fani mbalimbali za ufundi na ujasiriamali katika Magereza nchini ili kutoa mafunzo kwa wafungwa ili wakimaliza kifungo chao waende wakajenge Taifa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza lina jukumu la kuwahifadhi wafungwa wa aina zote pamoja na kurekebisha tabia kwa wale waliohukumiwa vifungo. Urekebishaji wa tabia za wafungwa hufanywa kupitia mafunzo kwa njia ya vitendo katika Miradi ya Kilimo, Viwanda vidogo vidogo, Ujenzi na Mafunzo ya Ufundi katika Chuo cha Ufundi cha Magereza Ruanda Mbeya pamoja na Gereza la Vijana Wami Morogoro. Lengo la utaratibu huu ni kuwafanya wafungwa wawe raia wema ili watakaporudi katika jamii waweze kutoa mchango katika kukuza maendeleo ya nchi yetu na yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu hayo, Jeshi la Magereza huwa linaajiri Wataalamu wa fani mbalimbali kulingana na mahitaji na pia kuwaendeleza Wataalamu wake katika fani hizo katika kozi fupi na ndefu ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuwajengea

uwezo wa kuwa na weledi wa kutosha wa mafunzo bora katika fani zao kwa ajili ya kuwafundisha wafungwa wanapokuwa Magerezani hususan jinsi ya kuzitumia fani hizo pindi wanapotoka nje ya vifungo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk, swali la nyongeza!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(i) Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni vyema angelieleza Bunge ni wafungwa wangapi ambao tayari wameshapata mafunzo aliyoyaeleza?

(ii) Kutokana na ukubwa wa nchi yetu maeneo ambayo ameyaeleza ni mikoa miwili tu ndiyo inatoa mafunzo kwa hawa wafungwa. Je, Serikali ina mpango gani kwa Magereza yaliyopo Mikoa mingine zaidi ya Mkoa wa Mbeya na Gereza la Wami ambao hawapati mafunzo hayo? Serikali ina mpango gani wa kueneza mafunzo hayo katika Magereza mengine yaliyopo katika Mikoa mingine ndani ya nchi hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la mwanzo ni wafungwa wangapi wamepata mafunzo ya aina hii; ukweli ni kwamba, mafunzo hayo yameanza zamani sana na kila mfungwa ambaye anaingia Gereza lengo ni kupata mafunzo ya namna fulani ambayo yatamsaidia. Kuna wafungwa ambao wanapata mafunzo haya ya kiufundi na wanatoka nayo, lakini pia kuna wafungwa wanaokwenda Magerezani hawajui hata kusoma na kuandika. Kwa hiyo, idadi kuitoa moja kwa moja hapa inaweza kuwa mtihani kidogo lakini inaweza ikapatikana.

Swali la pili, ni Mikoa miwili tu ndiyo yenye kutoa mafunzo. Ukweli ni kwamba, Mikoa miwili ndiyo yenye vyyo vya kutoa mafunzo, lakini kuna Mikoa mingine inatoa mafunzo katika shughuli ambazo wanazifanya kila siku. Kwa mfano, Kilimanjaro wanashona viatu, lakini sikuitaja kwa sababu siyo chuo mahususi, lakini wale ambao wanashiriki katika ushoni wanapata elimu. Mfano mwingine ni Mwanza, pia wanafanya ushoni, nayo ni elimu lakini siyo chuo. Mikoa miwili nimeitaja kwa sababu ni vyyo, lakini urekebishaji unafanywa siku zote katika kuhakikisha elimu inayopatikana inatolewa ili wasije wakarudi Magerezani kwa sababu hiyo tu.

MWENYEKITI: Tunakwenda swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale; kwa niaba yake Mheshimiwa Mary Mwanjelwa!

Na. 59

Ujenzi wa Kitu cha Polisi Ilembo

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MHE. MCH. LUCKSON N MWANJALE) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Ilembo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, lililoulizwa na Mheshimiwa Mwanjelwa, Mbunge wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Ilembo kinakusudiwa kujengwa katika Kijiji cha Ilembo, Kata ya Ilembo, iliyopo Tarafa ya Isangati Wilaya ya Mbeya Vijijini Mkoa wa Mbeya. Kujengwa kwa kituo hicho kutatoa huduma za Ulinzi na Usalama kwa Kata saba ikiwemo Ilembo yenyewe, Iwiji, Izila, Santilya, Isuto, Itawa, Masoko na Iyunga Mapinduzi zenye jumla ya vijiji 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja cha kujenga kituo hicho chenye ukubwa wa ekari moja kimepatikana mwishoni mwa mwaka 2014. Pamoja na kuwa ujenzi wa kituo hicho bado haujaanza, Jeshi la Polisi kupitia Falsafa ya Polisi Jamii, tayari wameanza kuhamasisha Wananchi wakae sawa katika kushikiri kwenye ujenzi wa kituo hicho. Vikao mbalimbali vimefanyika kuweka mikakati ya pamoja ya kufanikisha ujenzi wa kituo hicho ambacho ni muhimu sana kwani baadhi ya Wananchi wake wanategemea Kituo cha Polisi cha Mbalizi kilichopo umbali wa zaidi ya kilomita 120 toka mahali walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu nilioueleza hapo juu, licha ya ufinyu wa bajeti ya Serikali kukidhi mahitaji makubwa ya ujenzi wa Vituo vya Polisi hapa nchini, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itafanya jitihada za makusudi kwa kushirikiana na Wananchi wa Ilembo na Tarafa nzima ya Isangati kufanikisha ujenzi wa kituo hiki haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa umoja wetu na wale ambao wana mahitaji ya Vituo vya Polisi kama ilivyo Ilembo, kuvuta subira na kushirikiana na Wizara yangu kuhamasisha Wananchi kujenga Vituo vya Polisi kwenye maeneo yao kama ambavyo wanatekeleza miradi mingine ya maji, ujenzi wa shule, maabara na zahanati hapa nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, swali la nyongeza!

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwenye majibu yake ya msingi kwamba, Tarafa ya Isangati na vijiji vyake ambavyo ni zaidi ya 50 viko mbali zaidi ya kilomita 120 kutoka kwenye Kituo cha Polisi cha Mbalizi.

Je, Serikali haioni huku ni kutowatendea haki ya kiulinzi na kiusalama Wananchi wake hawa ukiachilia mbali suala zima la Polisi Jamii?

(ii) Kituo cha Polisi Ilembo Serikali iliahidi kutenga fedha tangu mwaka 2014, sasa namtaka Mheshimiwa Naibu Waziri awe *very much specific* kazi hii itaanza lini? Nashukuru.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, kama ifuataavyo:-

Wananchi kuwa wanatendewa haki au kutokutendewa haki, jambo moja ambalo nina uhakika nalo ni kwamba, Wananchi bila ya kituo wanapata huduma za ulinzi wa Serikali, hilo ndiyo muhimu. Mbali na kuwa ulinzi wanaupata, tunataka wapate ulinzi ambao utasogezwa karibu na maeneo yao ili kupunguza tatizo. Serikali itaendelea kusogezwa huduma hizi karibu na Wananchi ili kupunguza tatizo dharura inapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi utanza lini; nimjulisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine kwamba, pamoja na azma nzuri ambayo tulikuwa nayo mwaka jana, Jeshi la Polisi halikupewa hata shilingi ya fedha za maendeleo, kwa hiyo, tusingeweza kufanya chochote.

Kikubwa ambacho tunaweza tukakifanya ni kwamba, kwa pamoja tushirikiane ili tupate fedha zitengwe kwa ajili ya maendeleo ziweze kutoka pia zifanye kazi kama hii. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Wananchi ni mhimili mkubwa katika mambo haya na tukishirikiana mimi, Mheshimiwa Mbunge na wenzetu, kituo hiki tutakijenga mwaka huu huu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaenda swali linalofuata, Wizara ya Fedha. Tuna tatizo la muda, swali linalofuata ni la Mheshimiwa David Silinde; kwa niaba yake Mheshimiwa Selasini!

Na. 60

Faini Inayotokana na Kuchelewa kwa Magari Yanayokwenda Nchi Jirani

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE) aliuliza:-

Bandari imeweka utaratibu wa kutoa magari yanayokwenda nchi jirani kuanzia saa nane mchana na kila gari kupewa kibali kinachoelekeza kufika Kituo cha Ukaguzi Misugusugu ndani ya saa sita na kuchelewa kufanya hivyo gari hutozwa faini:-

Je, ni kiasi gani cha fedha zitokanazo na faini zimekwisha kusanywa na Serikali?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa magari kutakiwa kufika katika Kituo cha Forodha kwa muda maalum umewekwa na Idara ya Forodha kwa kushirikiana na wadau ili kupunguza gharama za ufanyaji biashara na pia kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuweka muda stahiki kati ya kituo na kituo ili kudhibiti tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kushusha mizigo ya *on transit* nchini bila kulipia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile utaratibu huu umelenga kuwabana baadhi ya madereva kuacha tabia ya kusimama njiani bila sababu na hivyo kuwapelekea kufikisha mzigo mapema mahali unakotakiwa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, tumezingatia hali ya miundombinu, wingi wa magari na hatari ya ukwepaji wa kodi iliyopo kati ya eneo na eneo hususan kati ya Dar es Salaam na Misugusugu ambako ndiko soko kuu la bidhaa lilipo. Faini ya shilingi 40,000 kwa kila gari linalochelewa imepunguza vitendo hatarishi vya upotevu wa mapato na mizigo. Aidha, kiasi cha faini kilichokusanywa kwa Vituo vya Misugusugu, Isaka na Makambako kwa kipindi cha kati ya Julai 2013 na Desemba 2014 ni shilingi 160,308,422, ikiwa ni wastani wa shilingi 8,906,023 kwa mwezi.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu aliyonipatia. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Pamoja na utaratibu huu unaotumika kwa sasa hivi bado kuna wafanyabiashara wengi na magari mengi yanaendelea kushusha bidhaa zinazokwenda nje ya nchi ndani ya nchi. Kwa mfano, bidhaa za sukari yapo malalamiko mengi kwamba Sukari inayosafirishwa kwenda nje ya nchi inashushwa nchini na hii inavidumaza viwanda vyetu vya hapa ndani kwa kushindwa kuhimili ushindani na vilevile kuipotezea Serikali mapato.

Je, Serikali inalijua hili na ni hatua gani ambazo inapanga kulikomesha kabisa ili kuweza kufanya ushindani katika bidhaa hii uwe mzuri?

(ii) Inafahamika kwamba magari yote yanayoondoka Bandarini mizigo inakuwa imefungwa kwa lakiri mpaka inapoelekea. Badala ya kutumia utaratibu huu wa kwenda kwanza Misugusugu na kukaguliwa kwa nini usiangaliwe muda ambao gari linatoka mpaka kule linakofika ili kupunguza msongamano na usumbufu kwa wafanyabiashara?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Silinde, kwa kuleta swali hili na Mheshimiwa Selasini kwa kuliuliza swali la nyongeza kwa ufasaha ili kuleta uelewa wa pamoja kwenye jambo hili.

Mizigo ambayo imefungwa kwa ving'amuzi maalum yenyewe haisimami wala haipewi huu muda ambao tunauongelea. Kwa hiyo, mizigo inayokwenda Rwanda, Burundi na Uganda ambako miundombinu mpakani imekaa vizuri, yenyewe haisimamishwi njiani kwa sababu imefungwa ving'amuzi na Mamlaka ya Mapato inafuatilia kupitia ving'amuzi ikiwa Makao Makuu.

Kwa upande wa mizigo inayopitia mpaka wa Tunduma bado kuna jitihada zinafanyika za kutengeneza miundombinu ambayo haitasababisha foleni ndefu ya magari pale mpakani ili nayo ianze kuwekwa ving'amuzi ili inapopita isisimame njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa inasimama njiani kwa sababu baadhi ya magari yanatumia ving'amuzi, lakini baadhi yanayopewa muda huu ni yale ambayo hayatumii ving'amuzi. Kwa hiyo, itakapokuwa imekamilika magari yote yatumia ving'amuzi na yakishatumia ving'amuzi ufuatiliaji wake utafanyika kutoka Makao Makuu ya Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwamba kuna bidhaa nyingine zimekuwa zikishushwa njiani, jitihada ya Serikali iliyofanyika ni hii ya kuweka ving'amuzi ambayo itasaidia sana bidhaa kufuatiliwa kupitia Makao Makuu ya Mamlaka ya Mapato na masuala ya aina hiyo yalishajitokeza. Kwa kuona jitihada za Serikali inazozifanya, kuna bidhaa zilikamatwa ambazo zilikuwa zishushwe njiani na zikatozwa kodi inayostahili.

Kwa hiyo, nitoe rai kwa Watanzania wote ambao wanaweza kutoa taarifa na kwa wale wanaofanya biashara, watambue kwamba, Serikali ipo kazini; na kama mtu atafanya hivyo hatua kali zitachukuliwa ili tuondokane na utaratibu wa kuikosesha Serikali mapato kwa kushusha bidhaa ambayo ilikuwa inaenda nje, lakini pia kwa kuvuruga uzalishaji wa ndani kwa kuingiza bidhaa ambayo hajitolewa kodi.

Na. 61

Ujenzi wa Bandari ya Karema

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Bandari ya Karema ni ya muda mrefu toka ilipoanza kujengwa miaka mitatu iliyopita lakini jambo la kushangaza mpaka sasa ujenzi huo bado haujakamilika:-

Je, ni lini ujenzi wa bandari hiyo utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ujenzi wa Gati la Karema umechukua muda mrefu tangu ulipoanza mwaka 2010. Hali hiyo ilisababishwa na utendaji usioridhisha wa Mkandarasi, Kampuni ya Modspan Enterprises, jambo lililosababisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kusitisha mkataba wa ujenzi huo Aprili 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imebaini umuhimu wa eneo la Karema kujengwa bandari kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya DR Congo pamoja na abiria kutoka Bandari ya Kalemie ya huko Congo, badala ya wazo la awali la kujenga gati dogo kwa ajili ya abiria tu. Kwa mantiki hiyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), ilitangaza zabuni ya kuonesha nia (*expression of interest*) ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari hii.

Zabuni ilitangazwa tarehe 9 Machi 2015 na kufunguliwa tarehe 7 Aprili 2015, ambapo makampuni 21 yalijitokeza na kati ya hayo ni makampuni 10 yalifuzu katika hatua ya awali (*expression of interest*). Kazi ya kufanya tathmini ya zabuni ili kupata makampuni ya kuwasilisha andiko (*request for proposals*), inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi huu wa Mei 2015. Mara zoezi la zabuni litakapokamilika, mshindi ataanza kazi ya kufanya upembuzi yakinifu ambao utatoa aina na ukubwa wa bandari inayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Wizara yangu ni kuhakikisha ujenzi unaanza katika Mwaka wa Fedha 2015/16, ambapo kiasi cha shilingi milioni 800 kimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga gati Karema alifanya vibaya sana na Serikali ilishuhudia madudu ambayo aliyafanya na Mheshimiwa Naibu Waziri akiwa shahidi tulienda kwenye eneo husika. Ni hatua gani ambazo Serikali imemchukulia Mkandarasi ili aweze kurejesha fedha alizoziteketeza ikiwemo mali ya Serikali na Umma kwa ujumla?

(ii) Ujenzi wa Bandari ya Karema unaenda sambamba na ujenzi wa reli kutoka Mpanda – Karema. Serikali imejipanga vipi kuhakikisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kutoka Mpanda kwenda kwenye bandari inayojengwa unafanywa haraka?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kampuni ya Modspan Enterprises walifanya madudu, lakini pia katika kutotekeleza Miradi hiyo ya Ujenzi wa Magati na Bandari kadhaa katika Ziwa Tanganyika, ulikuwepo pia upungufu upande wa mwajiri ambayo ilikuwa ni Mamlaka ya Bandari. *Designs* walizokuwa wamewapa zilikuwa hazitekelezeki katika mazingira ya maeneo yale. Baada ya kubaini ugumu wote huo; kwanza, usanifu wenyewe ulibadilishwa, lakini pia Mkandarasi alilazimishwa kwa mujibu wa Mkataba kukamilisha kazi za maeneo mengine ambazo zilikuwa zinawezekana. Hatua zingine kama zilivyo katika mkataba alikuwa nao zimechukuliwa pamoja na kumshitaki. Kwa hiyo, wanaendelea na madai ya kiasi alichochukua ambacho hakuwa amekifanyia kazi ili kiweze kurejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu reli kutoka Mpanda – Karema, suala hili lina umuhimu wa kipaumbele katika Wizara na sasa hivi fedha imekwishatengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa hiyo reli kuanzia Mpanda – Karema, lakini hii inaunganika na upembuzi yakinifu kuanzia Tabora – Kaliua, Kaliua – Mpanda, Kaliua – Kigoma na kuanzia Mpanda - Kalema.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuko nyuma ya wakati, ninaomba mnisamehe kuhusu maswali ya nyongeza. Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, litaulizwa na Mheshimiwa Keissy kwa niaba yake!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Swali la Mheshimiwa Kikwembe linafanana kwa asilimia mia moja na swali la Mheshimiwa Kakoso. Napenda kuuliza swali la nyongeza tu, ninaomba nafasi. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Hapana, Mheshimiwa Keissy kama huwezi kuuliza swali lake kaa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Ninaomba Swali la Mheshimiwa Kikwembe, Na. 62 lipate majibu, linafanana. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 62

Ujenzi wa Gati la Karema

MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE) aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa Gati la Karema umechukua takribani miaka mitatu bila kukamilika:-

Je, ni lini Gati hili litakamilika ili Wananchi wapate unafuu katika shughuli zao za kila siku?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, lililoulizwa na Mheshimiwa Keissy, kama ifuatavyo:-

MWENYEKITI: Kwa ufupi anataka kujua Gati tu!

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya swali hili ni kweli yanafana sana na Swali Na. 4356 la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ambalo nimelijibu dakika chache zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaomba kurudia maelezo hayo hayo ya ujenzi wa Gati la Karema.

MWENYEKITI: Jibu hilo limetoshwa kama linafanana na majibu ni hayo hayo.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ni yale yale.

MWENYEKITI: Basi, Mheshimiwa Keissy swali la nyongeza!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana tena sana. (Kicheko)

Kwanza, ninaishukuru Serikali yangu kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania kuhamisha Bandari ya Kipili kwa asilimia mia moja.

Leo ni miezi sita Bandari ya Kipili imekamilika, ni lini Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi itaenda kuzindua Bandari ya Kipili iweze kuhudumia vijiji saba vya Kipili, Kirando, Manda Kerenge, Manda Uwire, Mkinga na Karungu; kwa sababu Serikali imetumia shilingi bilioni 1.2, leo ni miezi sita, bandari inaendelea kuchakaa, iruhusu Mv. Liemba iweze kufanya kazi ihudumie wananchi wa vijiji hivyo? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, majibu.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kumjibu Mheshimiwa Keissy swali lake kwamba, ni kweli anachosema ni miezi sita sasa Mamlaka ya Bandari imekwishakamilisha ujenzi wa Bandari ya Kipili. Utaratibu tuliofanya kwa sababu ni suala kubwa la kihistoria kwa eneo lile, tumemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atafute nafasi yake ili aweze kuwa mgeni rasmi siku ya ufunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoona siku zinavyopita, pengine Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kuwa hana muda kwa sasa, nitawaomba Wananchi wa Kipili waridhike ikiwa mimi mwenyewe nitakwenda huko kuwa mgeni rasmi. Kama mnavyojua huu ni mwaka wa kujipitisha pitisha kila mahali, kwa hiyo, itakuwa ni fursa nyingine ya kuweza kwenda kule na kuweka sherehe hii katika hali yake inayostahili. Ahsante sana. (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaenda swali la mwisho ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Sileiman Nchambi, Mbunge wa Kishapu; kwa niaba yake Mheshimiwa Ndassa!

Na. 63

Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Kishapu

MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN) aliluliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kiwanja cha Ndege (*airport/airstrip*) katika Wilaya ya Kishapu?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kishapu ni miongoni mwa Wilaya mpya na inazo shughuli nyingi za kiuchumi kubwa na utajiri wa madini ya almasi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kishapu ulikuwepo uwanja wa ndege mdogo eneo la Mwadui ambao ulikuwa unamilikiwa na Mgodu wa Almasi wa Mwadui. Uwanja huo ulifungwa kupisha shughuli za uchimbaji wa almasi na kuhamishiwa eneo la Ibadakuli ambapo sasa upo Uwanja wa Ndege wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameona haja ya kuwa na uwanja mdogo katika Wilaya hiyo mpya, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, itaifanyia kazi wazo hili ili kuona uwezekano wa mahali ambapo uwanja huo unaweza kujengwa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

(i) Maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri lakini tungependa kujua hilo wazo litafanyiwa kazi lini?

(ii) Tungependa kupata hali halisi ya ujenzi wa Mwanza Airport umefikia wapi na utakamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wazo limeletwa na Mheshimiwa Mbunge na pale ulipokuwa uwanja wa zamani uliofungwa ni eneo lile lile la Kishapu. Kwa hiyo, wazo kama wazo tayari tumekwishalipeleka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na linafanyiwa kazi. Ninachoweza kusema kwa sasa ni kwamba, wawasiliane haraka iwezekanavyo na Mamlaka ya Halmashauri ya Kishapu ili waweze kujua hayo ambayo nimeyasema katika jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Mwanza, mkataba unaendelea na ziko shughuli zinaendelea kufanyika, kwa maana ya urefushaji wa uwanja kwa mita 500 sasa wako katika tabaka la mwisho la lami linawekwa; ujenzi kwa ajili ya maegesho ya ndege za abiria umekamilika; ujenzi wa eneo la mizigo; maegesho na njia za viunga vyake unaendelea na sasa tuko katika taratibu za kukamilisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja huo.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mwaka 2014 Mheshimiwa Naibu Waziri alituhidi kwamba, Tabora tutapa jengo jipya kwa ajili ya abiria. Je, mpango huo bado upona kama upo utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ismail Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mpango upo wa kujenga jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Tabora na mpango huo una fedha na kila kitu kipo sawasawa. Kilichobaki sasa hivi ni kwamba, zabuni imekwishatangazwa, inafanyika tahmini na baadaye itapelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya *no objection* ili ujenzi uanze.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Dodoma kuna wageni wengi wanaokuja kutoka nje ya nchi, Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri, Mabalazi na kadhalika; na kwa kuwa uwanja wetu sasa hivi ni mdogo na hauruhusu ndege kubwa kutua; na kwa kuwa upembuzi yakiniifu ulikwishafanyika kwenye uwanja mpya unaotarajiwa kujengwa katika eneo la Msalato; ninaomba kujua sasa ni lini Serikali itaanza kujenga Uwanja wa Ndege wa Msalato?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kumpata mwekezaji wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Msalato upo katika hatua nzuri. Yako mazungumzo hivi sasa yanaendelea kufanyika katika Wizara ya Fedha na wale ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika Uwanja huo. Sasa kwa sababu tuko katika hatua ya mazungumzo, nisingependa tuseme utaanza kujengwa lini, kwa sababu hiyo inaweza ikatuweka katika hali mbaya katika majadiliano ya Mradi huo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeisha na maswali yamemalizika. Sasa ninaomba niwatambue wageni waliopo Bungeni hapa asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Kwanza kuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ambaye ni Ndugu Magdalena Mawaka Mlengeya, mke wake. Yuko wapi? Tunaomba tukukaribishe, tunakushukuru sana kwa jinsi unavyomlea Mheshimiwa Waziri na anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ni Viongozi 15 wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoka Mkoa wa Simiyu, wakiongozwa na Ndugu Elaston Mbwilo, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa uko wapi?

Yupo pia Ndugu Hilda Kapaya, Katibu wa CCM wa Mkoa wa Simiyu.

Tunawakaribisha sana. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa karibu, nimefurahi kukuona DC wangu. Wanasimiyu wote tunawahakikishia kwamba, Mbunge wenu anachapa kazi vizuri na tunashukuru kwa kumlea. *(Makofi)*

Wapo Watendaji Wakuu wa Wizara, Wenyekiti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Dkt. Yona Budeba, Katibu Mkuu wa Wizara. Karibuni sana na hongereni kwa kazi nzuri mnayofanya.

Kuna Wageni 23 wa Mheshimiwa Kaika Telele, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, wakiongozwa na Mheshimiwa Catherine Telele, mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri na Diwani wa Tarafa ya Ngorongoro. Uko wapi?

Mama karibu. Ahsante sana kwa kazi nzuri, tunakupongeza unavyomlea Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Yupo Ndugu William Sanigo, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Ngorongoro na Ndugu Kajulosi Steven, Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Vijana wa CCM wa Mkoa wa Arusha. Karibuni, tunawashukuru sana.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Kaika Telele ambao ni Wajumbe 12 wa Baraza la Wafugaji kutoka kwenye Kata zilizo ndani ya Tarafa ya Ngorongoro na ni Wajumbe wa Baraza la Wafugaji, wakiongozwa na Ndugu Seketo Odumu, Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake. Wako wapi?

Karibuni sana hapa Bungeni na hongereni kwa kazi nzuri mnazofanya. *(Makofi)*

Kuna wageni 18 wa Mheshimiwa Felister Bura, ambao ni Wachungaji wa Kanisa la Wasabato kutoka Dar es Salaam na Morogoro, wakiongozwa na Mchungaji Baraka Butoke. Wako wapi?

Karibuni sana na tunawashukuruni, endeleeni kuombea amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Kuna wageni 67 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Naibu Waziri wa TAMISEMI, ambao ni Walimu wa Shule za Sekondari, Wakufunzi wa Vyuo, Wakaguzi wa Shule na Wawezeshaji kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Taasisi ya Elimu. Wageni hawa wanatoka katika Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara. Wako wapi wasimame? Karibuni, ahsanteni kwa kazi nzuri mnayofanya. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Jadi Simai Jadi, ambaye ni Ndugu Cheti Mussa Mohammed, Shemeji yake. Karibu Bungeni.

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, ambao ni Madiwani 17 kutoka Songea Mjini wakiongozwa na Mstahiki Meya, Mheshimiwa Charles Mhagama. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, Mbunge wenu anachapa kazi.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Josephine Chaguala kutoka Wizara ya Elimu Makao Makuu wakiongozwa Ndugu Juliana. Wageni karibuni.

Wageni wanne wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, wakiongozwa na Sheikh Abdallah Ilunde; karibuni.

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo ni Ndugu Charles Mkisi, Mkurugenzi wa Shirika la Vijana liitwalo Young Tourism Network la Dar es Salaam; karibu.

Matangazo ya kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Peter Serukamba, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuwa, tarehe 20 Mei 2015, saa nane mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 136, Hazina Ndogo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jason Rweikiza, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa, leo saa nane mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 23, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

MWONGOZO WA MWENYEKITI

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba mwongozo wako, jana Wanafunzi 7,000 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamegoma kwa sababu hawakupelekwa fedha za kujikimu. Katika Bunge lako Tukufu hili nilishazungumzia asilimia mbili inayotakiwa kwenda TEA, asilimia 60 ni fedha ambayo inaenda kwenye elimu ya juu. Sasa pesa hizo hazikupelekwa wanafunzi wamekosa fedha za kujikimu na wanafunzi unakuta wengi wanatoka maeneo ya vijijini, watoto wa maskini, wako pale Dar es Salaam katika hali ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea, Chuo Kikuu cha *Saint Joseph* kilichopo Mbezi, kimeamua kuwarudisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa sababu ya kukosa fedha za kujikimu na wengi wamepanga wako katika maisha magumu hasa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji majibu ya Serikali; kwa nini hawapeleki fedha za kujikimu kwa hawa wanafunzi wa Vyuo Vikuu?

Hawataki kugoma, hawana shida na Serikali yao, lakini wako katika mazingira magumu wanashindwa kusoma, mwisho wa siku wameamua kugoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 7,000. Ukiona mpaka Makamu Mwenyekiti wa Chuo anasema madai yao ya msingi watekelezewe.

Ninaomba mwongozo wako kwa nini Serikali haipeleki fedha kwa wakati vyuoni mpaka wanafunzi wagome na waishi katika mazingira magumu?

MWENYEKITI: Kweli kama tatizo ni hilo tunaomba Serikali itupe majibu kama inayo sasa hivi, ninamwona Naibu Waziri wa Fedha amesimama, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Ester kwa kulileta jambo hilo na kwa kuguswa na maisha halisi ya watoto wengi wa Kitanzania walioko vyuoni. Pili, nawaomba radhi wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa hatua hiyo ambayo watakuwa wamepitia.

Ninaomba nilipatie Bunge lako Tukufu taarifa kwamba, tuliongea na Viongozi wa Vyuo pamoja na Bodi pamoja na Wizara pia inayosimamia. Tangu juzi kulikuwepo na utaratibu wa kuweza kulipa fedha hizo na mpaka jana jioni, tayari fedha ilishatoka Wizara ya Fedha kwenda kwenye Taasisi husika kwa ajili ya kupeleka fedha hizo kwa wanafunzi.

Kwa niaba ya Waziri wa Fedha, nitumie fursa hii kuwaomba na kuwaagiza Wataalamu ambao wanashughulikia kuzifikisha hizo fedha kwa wanafunzi, watoe kwanza fedha hizo ndiyo waweze kukaa vikao, kuliko kusubiri kupitisha kwa utaratibu ambao wanafunzi wetu wataendelea kupata shida.

Nitumie fursa hii pia kuelezea kwa sababu swali lingine limekuja kwa nini fedha hizo zimechelewa. Kulikuwepo na utaratibu hata juzi tulisema hapa wakati tunaongelea kuhusu hizi fedha ambazo zilitengwa, sisi kama Wizara ya Fedha tumeshajipanga kuhakikisha fedha hizi ambazo zimepangwa kwa ajili ya Mifuko halali, ziweze kupelekwa moja kwa moja punde zinapokusanywa, hiyo ndiyo itakayotoa majawabu ya kudumu ya ucheleweshaji wa aina hii.

Tutakapokuwa tumebainisha na tumeongeza kiasi kinachokwenda kwenye fedha zinazokwenda kwenye Mifuko hiyo, basi tunakokwenda tatizo la aina hiyo halitajitokeza tena.

Nawaomba radhi tena wanafunzi kwa sababu ni kweli wanafunzi walishaachana na utaratibu huu wa kugoma. Serikali tutajitahidi kuhakikisha tunawafikishia kwa wakati fedha ambazo wanastahili kupata ili wao wafanye kazi moja ya kusoma na tuweze kupata Wataalamu ambao wameiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa kwamba, Serikali imeshatoa fedha na taasisi zinakopita fedha hizo kabla hazijafika kwa wanafunzi, niwaagize wajitahidi leo hii vyuo vyote vipate fedha hizo wanafunzi waweze kuendelea na masomo yao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaomba Serikali isimamie ili watoto hawa hasipate tabu, maana kwa kweli linakuwa ni tatizo. Mheshimiwa Kombo!

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7). Kitendo ambacho kimetendeka jana jioni katika Bunge lako cha kuleta fomu nyingine ya kusaini kama umo ndani ya Bunge au haumo, utaratibu huu sisi wengine tuko katika Kamati tulionekana hatupo. Nakitaka mwongozo wako nini maana yake; tunaongezewa

posho kwa jioni au tunapunguziwa au Wabunge sasa wamekuwa watoto wa shule wengine wanakuja asubuhi wanaitwa na wengine wanakuja mchana mpaka kudhalilishwa?

Wale wanaokwenda kwenye Kamati lini watapelewa jukumu la kujaza fomu zao; kwa mfano sasa hivi Mwenyekiti wangu wa Miundombinu amenitangazia niende kwenye Kamati saa nane ninatoka saa kumi na mbili au saa moja. Jana hivyo hivyo. Sasa siku yangu ya jana ninasikitika nimekosa posho yangu ya jioni. Naomba ufafanuzi wako Mheshimiwa Mwenyekiti. (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kombo, ufafanuzi huo nitautoa baadae. Katibu, hatua inayofuata!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kukutana hapa leo ikiwa ni Bunge la Ishirini kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, ninatoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia Taarifa inayohusu Wizara yangu iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji, lijadili na kupitisha Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa Mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao imara wa kuanzisha na kusimamia mchakato wa kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile napenda kuwapongeza Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kwa kukamilisha Katiba Inayopendekezwa. Tuna imani kuwa, Wananchi watajitokeza kwa wingi kuipigia kura Katiba mpya ambayo itatufaa kwa kipindi cha miaka 50 ijayo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara na uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhiti, Mheshimiwa Kaika Saming'o Ole Telele, Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa ushirikiano anaonipa katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Vilevile napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Busega, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Pia, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo ninapotekeleza majukumu ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya walioteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kujiunga na Bunge lako Tukufu ambao ni Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja na Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mheshimiwa Hayati Kapteni John Damian Kombo, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na Wananchi wa Jimbo alilokuwa analiwakilisha. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi; *Amina*. Aidha, naomba nitumie fursa

hii kuwakumbuka wananchi wenzetu waliopoteza maisha kutokana na mafuriko, ajali na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushauri, maoni, maelekezo na ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maandalizi ya bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi, kwa Hotuba yake nzuri, yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa Sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2015/2016. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote waliotoa hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kuhusu masuala ya maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia hotuba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya Sekta za Mifugo na Uvuvi, Wizara imezingatia maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Ilani inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na Sekta hizi katika kuwapunguzia Wananchi umaskini na kuongeza Pato la Taifa.

Utekelezaji wa Malengo Makuu ya Ilani ya CCM kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi kuanzia mwezi Novemba 2010 hadi mwezi Aprili 2015, umeainishwa katika aya ya 8 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2014, Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia 2.2, ikilinganishwa na asilimia 2.0 mwaka 2013. Kutokana na takwimu zilizo, idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kuwa ng'ombe milioni 25.8, mbuzi milioni 16.7 na kondoo milioni 8.7. Pia, wapo kuku wa asili milioni 37.0, kuku wa kisasa milioni 32.0 na nguruwe milioni 2.4. Aidha, ulaji wa mazao ya mifugo kulingana na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka. Kwa nchi yetu, viwango vya ulaji wa mazao hayo kwa sasa ni wastani wa kilo 15 za nyama, lita 47 za maziwa na mayai 106 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi pia inayo fursa kubwa katika kuchangia kuondoa umaskini kwa kuwapatia wananchi lishe bora, ajira na kipato. Katika mwaka 2014 Sekta hii imekuwa kwa asilimia 2 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2013.

Kupungua kwa kasi ya ukuaji kumechangiwa na kupungua kwa soko la samaki nje ya nchi na matumizi ya nyenzo duni za uvuvi. Aidha, mchango wa Sekta hii kwa Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 1.4 mwaka 2013 mpaka asilimia 2.4 kwa mwaka 2014. Baada ya maelezo haya ya utangulizi, sasa ninaomba niwasilishe mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2014/15 na Mpango na Malengo kwa Mwaka 2015/16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2014/15 kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli na matumizi ya fedha, yamefafanuliwa kwa ufasaha kuanzia aya ya 15 hadi ya 17 ya Hotuba ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuratibu, kupitia na kusimamia utekelezaji wa Sera, Progaramu, Mikakati na Sheria za Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imefanya mapitio na kuandaa Sera na Sheria za Sekta za Mifugo na Uvuvi ili kuboresha mazingira ya kibiashara kama ilivyoainishwa katika aya ya 18 hadi aya ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia 3.5 kutoka lita bilioni 1.99 mwaka 2013/2014 hadi kufikia lita bilioni 2.06. Aidha, kiasi cha maziwa kinachosindikwa kwa siku kimeongezeka kutoka lita 139,800 mwaka 2013/2014 hadi lita 167,070 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa viwanda vya kusindika maziwa kutoka 74 mwaka 2013/2014 hadi kufikia 82 vya sasa. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhamasisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa ili kuongeza usindikaji kufikia lita 230,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba ambapo jumla ya mitamba 635 ilisambazwa kwa wafugaji wadogo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), imezalisha mitamba 638 na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yalisambaza mitamba 10,731 kwa wafugaji wadogo katika mikoa 25 nchini. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba pamoja na Vituo vya Uhimilishaji vya Kanda ili kuwa na ufugaji wenye tija.

Katika mwaka 2014/2015 uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia 6.2 kutoka tani 563,086 mwaka 2013/2014 hadi tani 597,757 mwaka 2014/2015. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika soko maalum la ndani hususan migodi, maduka makubwa na hoteli za kitalii. Aidha, idadi ya ng'ombe walionepeshwa waliongezeko kutoka ng'ombe 175,000 mwaka 2013/2014 hadi 213,000 mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya masoko ya mifugo imeendelea kuboreshwa kwa lengo la kukuza biashara ya mifugo katika minada ya upili na mipakani. Katika mwaka 2014/2015, Minada ya Pugu, Lumecha, Kirumi na Nyamatata (Misungwi), imekarabatiwa na mizani ya mifugo ilisimikwa katika minada ya upili 11.

Katika mwaka 2015/16, Wizara itajenga minada miwili ya upili ya Longido na Kirumi na kukarabati minada 7 ya mifugo ya upili ya Weruweru (Hai), Meserani (Monduli), Themu (Arusha), Sekenke (Iramba), Igunga (Igunga), Ipuli (Tabora) na Mhunze (Kishapu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, jumla ya ng'ombe 1,337,095, mbuzi 1,056,218 na kondoo 230,221 wenye thamani ya shilingi bilioni 1,027.4 waliuzwa minadani, ikilinganishwa na ng'ombe 1,215,541, mbuzi 960,199 na kondoo 209,292 wenye thamani ya shilingi bilioni 989.3 mwaka 2013/2014. Pia, idadi ya mifugo iliyouzwa nje ya nchi imeongezeka kutoka ng'ombe 1,123 mwaka 2013/2014 hadi ng'ombe 2,139 wenye thamani ya shilingi bilioni 34 mwaka 2014/2015. Aidha, jumla ya tani 23.4 za nyama ya ng'ombe, nyama ya mbuzi tani 1,388.9 na nyama ya kondoo tani 36.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 52.1 ziliuzwa katika nchi za Msumbiji, Vietnam, Oman, Qatar na Falme za Kiarabu.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi wa viwanda na biashara ya mifugo na mazao yake ili kuongeza mauzo ya nyama ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imeendelea kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa

wafugaji wanaozunguka ranchi kumi za mfano za Kagoma, Kalambo, Kikulula, Kongwa, Mabale, Missenyi, Mkata, Mzeri, Ruvu na West Kilimanjaro.

Pia Kampuni ya NARCO ilikamilisha majadiliano na Kampuni ya Allanasons kutoka India yenye nia ya kujenga machinjio ya kisasa katika Ranchi ya Ruvu kwa ajili ya soko la nje.

Katika mwaka 2015/2016, NARCO itazalisha ndama 3,366 kutokana na ng'ombe wazazi 4,488, itaendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu na kununua ng'ombe wazazi 1,200 kwa lengo la kuongeza idadi ya ng'ombe katika ranchi zake. Pia itaendelea kutafuta wawekezaji makini.

Katika mwaka 2014/2015 uzalishaji wa vifaranga vya kuku wa nyama na mayai umeongezeka na kufikia vifaranga milioni 63.6 ikilinganishwa na vifaranga milioni 61 vilivyozalisha mwaka 2013/14. Vilevile uzalishaji wa mayai umeendelea kuongezeka kutoka bilioni 3.9 mwaka 2013/2014 hadi mayai bilioni 4.15 mwaka 2014/2015.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhamasisha utekelezaji wa programu za kuendeleza mifugo midogo ikiwemo kuku wa asili, kuku wa kisasa na kware katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 20 za Mikoa ya Singida, Mwanza, Tabora, Kagera, Simiyu, Morogoro, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuimarisha uzalishaji wa nguruwe nchini kwa kuendeleza Shamba la Ngerengere kwa kuwapatia nguruwe wazazi 10. Aidha, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kutoka tani 79,174 hadi kufikia tani 79,180 mwaka 2014/2015. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha Shamba la Mifugo la Ngerengere ili liweze kuzalisha na kusambaza mbegu bora za nguruwe kwa wafugaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa nguruwe na nyama yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 kumekuwa na ongezeko la ngozi zilizosindikwa kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 1,060,777 na vipande vya mbuzi na kondoo 2,715,436 mwaka 2013/2014 hadi vipande vya ng'ombe 1,388,139 wakati vipande vya mbuzi na kondoo vimepungua kutoka 2,715,436 mwaka 2013/14 hadi kufikia vipande 1,020,000 kwa mwaka 2014/15 vyenye thamani ya shilingi bilioni 39.2. Ongezeko hili limetokana na ukuaji wa usindikaji katika kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka za Serikali za Mitaa 75 na Chama cha Wadau wa Ngozi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Rasilimali za Ardhi, Maji na Malisho kwa Mifugo na Utatuzi wa migogoro. Katika mwaka 2014/15, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI, zimetenga maeneo ya malisho na kufanya eneo lililotengwa kwa ajili hiyo kufikia hekta milioni 1.95 katika Vijiji 620 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 81 zilizopo katika mikoa 22.

Katika mwaka 2015/16, Wizara kwa kushirikiana na wadau itawezesha kutambua na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya ufugaji endelevu katika Wilaya za Kiteto, Busega, Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Kilindi, Igunga, Iramba na Lindi. Ili kuongeza maeneo kwa ajili ya ufugaji, Serikali inakusudia kufuta umiliki wa baadhi ya vitalu vya mashamba na Ranchi za Serikali na kuwapatia wafugaji wenye nia na uwezo wa kuingia kwenye ufugaji wa kisasa na kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kusimamia ujenzi Mabwawa ya Kwamaligwa (Kilindi), Mbangala (Chunya) na Olypasei, yanayojengwa na Wakala wa Kuchimba Visima Virefu DDCA. Katika mwaka 2015/2016 Wizara itawezesha ujenzi wa malambo katika Wilaya za Bagamoyo, Chenga, Kilwa, Busega, Kishapu, Mwanga, Ngorongoro na Tarime na kisima kirefu katika Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuendeleza eneo huru la magonjwa ya mifugo la Uwanda wa Juu wa Ufipa (*Ufipa Plateau*), kwa kuimarisha Kituo cha Ufuatiliaji na Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Kanda ya Kusini Magharibi kilichopo Mjini Sumbawanga.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha Eneo huru la Magonjwa ya Mifugo la Uwanda wa Juu wa Ufipa ulio katika Wilaya za Kalambo, Nkasi na Sumbawanga, kwa kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa wafugaji na wadau waliopo kwenye eneo hilo ili kuongeza kiwango cha ushiriki wao kwenye shughuli za kukinga magonjwa na kuzalisha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau, iliendelea kudhibiti Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuji na Kondoo katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Mara na Pwani, kwa kuchanja mbuzi na kondoo 638,007 na kutoa elimu kwa wafugaji. Matukio ya ugonjwa huu yanaendelea kupungua katika mikoa husika. Katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuzuia na kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu kwa kuratibu, kununua na kusambaza dozi 1,000,000 za chanjo zitakazotumika katika Wilaya zilizo katika hatari ya kuambukizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege hapa nchini na nje ya nchi. Taarifa ya ufuatiliaji inaonesha nchi 13 zina ugonjwa huu, hivyo uwezekano wa ugonjwa huu kuingia nchini bado ni mkubwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), imechukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu kwa kufuatilia mwenendo wa ugonjwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi, imeendelea kutekeleza mpango wa ruzuku ya asilimia 40 kwa dawa za kuogeha mifugo, ambapo lita 119,509 zenye kiini cha pareto na amitraz, zilinunuliwa kwa thamani ya shilingi 1,817,911,200 na kusambazwa katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imechanja ng'ombe 19,491 dhidi ya ndigana kali katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Mbeya, Pwani na Tanga. Katika mwaka 2015/16, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine, itaendelea na utaratibu wa ruzuku ya dawa za kuogeha mifugo kwa kununua jumla ya lita 200,000 zitakazotumika kuogeha mifugo 8,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa udhibiti shirikishi na endelevu wa mbug'oni kwa kutoa ushauri wa kitaalamu katika Halmashauri za Serikali za Mitaa za Kilosa, Kisarawe, Monduli, Mpanda, Ngorongoro, Uvinza, Urambo na Serengeti. Aidha, udhibiti wa mbug'oni katika ikolojia za Katavi, Serengeti, Kigoma, Tabora na Rukwa umeendelea kufanyika. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Programu ya Umoja wa Afrika ya Kuangamiza Mbug'oni na Ndorobo, itatekeleza mkakati wa kudhibiti mbug'oni na ndorobo kwa kununua vitendea kazi na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation* na kuratibiwa na Shirika la Afya Duniani, imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Morogoro na Dar es Salaam kwa njia ya kampeni, ambapo mbwa 81,830 na paka 15,999 walichanjwa, sawa na asilimia 79 ya waliolengwa kuchanjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa magonjwa mengine ya mifugo yanayoambukiza binadamu ni pamoja na Homa Bonde la Ufa, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na Kifua Kikuu kama ilivyoanishwa katika aya ya 46 na 47 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na *FAO* ilikamilisha ujenzi na kuzindua Kanzidata ya Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa mifugo 75. Pia Wizara iliwezesha utambuzi wa mifugo 45,000 katika makundi ya wafugaji wa ng'ombe wa asili ambapo jumla ya ng'ombe 13,054 wametambuliwa kwa njia ya hereni katika Wilaya ya Bagamoyo, Muheza na Kibaha na ng'ombe 120,000 kwa njia ya chapa katika Wilaya za Karagwe na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Sekta Binafsi imeendelea kutumia fursa ya mazingira mazuri ya uwekezaji ambapo wawekezaji katika ujenzi wa machinjio na viwanda vya kusindika nyama wameongezeka kutoka 15 mwaka 2013/2014 hadi 25 mwaka 2014/2015 kama inavyoonekana katika Jedwali Namba Saba. Vilevile uwekezaji katika usindikaji wa ngozi umeongezeka kutoka viwanda saba mwaka 2013/2014 hadi tisa kwa mwaka 2014/2015. Katika mwaka 2015/2016 Wizara itahamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya mifugo kwa ajili ya kuongeza thamani, ajira, lishe na Pato la Taifa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

Uendelezaji wa Sekta ya Uvuvi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara ilifanya sensa ya uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Matokeo yanaonesha kuwepo kwa wavuvi 103,540, zana za uvuvi 7,483,529, vyombo vya uvuvi 29,154 na injini za kupachika 9,416. Aidha, Ziwa lina jumla ya mialo 642 ya kupokelea samaki, kati ya mialo hiyo 25 imeboreshwa. Pia, Sensa ya Uvuvi ilifanyika katika maziwa madogo ya Tlawi, Manyara, Burunge, Basuto, Eyasi, Babati na Bwawa la Nyumba ya Mungu. Katika kipindi cha 2014/2015 jumla ya tani 369,827 za samaki zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi trilioni 1.4 zilivunwa, ikilinganishwa na tani 367,854 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 zilizovunwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, tani na mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo ziliuzwa nje na kuiingizia Serikali mrabaha wa shilingi bilioni bilioni 7.5. Katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha jamii za wavuvi kusimamia, kuendeleza na kutunza rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia mfumo wa ikolojia na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezesaji wa uvuvi na ufugaji wa samaki. Wizara imeendelea kushirikiana na Halmashauri mbalimbali katika kuboresha miundombinu na masoko ya mazao ya uvuvi. Katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika mathalani, jumla ya mialo minne ya uvuvi wa Kibirizi, Muyovozi, Ikola imekamiliwa na Mwalo wa Kirando ujenzi unakamilishwa. Katika Ukanda wa Pwani, Wizara imekamiliwa ujenzi wa vibanda vya kuhifadhi mitambo ya barafu katika Halmashauri za Mafia (Kilindoni), Kilwa (Masoko Pwani) na Rufiji (Nyamisati).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki ya Dunia, imeandaa Mradi wa *Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme (SWIOFish)*, unaotarajia kuanza Julai 2015. Mradi huu unalenga kuboresha fursa za kiuchumi, kijamii na mazingira miongoni mwa jamii za wavuvi kutokana na rasilimali za uvuvi katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 vikundi 51 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa vimehakikiwa kwa ajili ya kupatiwa ruzuku kwa ajili ya zana na pembejeo za uvuvi. Aidha, ruzuku hiyo itatolewa kwa kufuata mwongozo ambapo wadau watachangia asilimia 60 na Serikali kuchangia asilimia 40. Pia, wafugaji wa samaki watapata ruzuku ya chakula cha samaki kwa bei nafuu ya shilingi 500 kwa kilo, sawa na punguzo la asilimia 84 ya bei halisi kupitia Vituo vya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi vya Mbegani, Nyegezi, Kibirizi na Mtwara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuwawezesha wavuvi, Wizara kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PPF, inahamasisha wavuvi kujiunga na Mifuko hii, ili kunufaika na mafao na huduma mbalimbali zinazotolewa na Mifuko hiyo. Katika hatua za awali, Wizara na Mfuko wa Hifadhi ya Taifa wa Jamii – NSSF, waliwekeana Makubaliano ya Utekelezaji ujulikanao kama "WAVUVI SCHEME" na mpaka sasa Mfuko umesajili wavuvi 1,234 katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Aidha, Mfuko wa PPF nao unaendelea na mpango kama huo.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaanza utekelezaji wa Mradi wa SWIOFish. Vilevile, Wizara itaendelea kuwawezesha wavuvi wadogo kupitia mfumo wa ruzuku na kuhamasisha wavuvi kujisajili na kujiunga katika Mifuko hii ili wafaidike na huduma zinazotolewa na Mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, jumla ya vifaranga vya samaki 8,090,000 vimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa samaki. Kati ya hivyo, vifaranga 290,000 vimezalishwa katika Vituo vya Serikali vya Kingolwira (Morogoro), Luhira (Songea), Mwamapuli (Igunga) na Mtama (Lindi). Vilevile, vifaranga 7,800,000 vimezalishwa katika vituo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Uzalishaji wa Kambamiti wa kufuga umeongezeka kutoka tani 320 zenye thamani ya shilingi bilioni 2.56 mwaka 2013/2014 hadi tani 391 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.2 mwaka 2014/2015. Aidha, uvunaji wa mwani umeongezeka kutoka tani 179.3 zenye thamani ya shilingi 84,370,000 mwaka 2013/2014 hadi tani 222.8 mwaka 2014/2015 zenye thamani ya shilingi 133,200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuboresha ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kujenga na kuimarisha vituo vya kuzalisha na kusambaza vifaranga vya samaki milioni kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeandaa Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo (*Livestock Research Agenda*), ambapo nakala 500 zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, Wizara imeandaa Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Uvuvi ambayo iko katika hatua ya uchapishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuratibu na kutathmini utafiti na huduma za utafiti na maendeleo ya ufugaji na uvuvi kulingana na programu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), kwa kuboresha miundombinu na vitendea kazi. TALIRI imeendelea kutekeleza Miradi 59 ya utafiti kupitia vituo vyake saba vya Mpwapwa, Tanga, Uyole, West Kilimanjaro, Kongwa, Mabuki na Naliendele. Aidha, TALIRI kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, imezalisha ng'ombe sita aina ya bonsmara kwa kutumia teknolojia ya uhaulishaji (*embryo transfer*). Majaribio haya ya awali ya uhawilishaji yamedhihirisha kuwa mbari za mifugo bora zinaweza kupatikana hapa nchini kwa kuhusisha mifugo iliyopo na katika mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, TALIRI imesambaza jumla ya ng'ombe 131 aina ya Mpwapwa yakiwemo madume 51 na majike 80. Ng'ombe hao walisambazwa katika maeneo ya Chamwino, Dar es Salaam, Dodoma, Kibaha, Kongwa, Nyamagana, Mpwapwa, Manyoni, Musoma na Ngorongoro, kwa ajili ya kuzalisha mifugo bora na kuboresha ng'ombe wa asili. Pia ng'ombe wa maziwa 26 aina ya *Friesian* walisambazwa katika Halmashauri za Rungwe, Mbozi, Jiji la Mbeya na Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 mbuzi bora 114 walisambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji katika maeneo ya Kibaha, Kongwa, Dar es Salaam, Tanga, Newala, Bahi, Dodoma, Chamwino, Kinondoni na Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 TALIRI iliendesha mafunzo ya ufugaji bora ambapo wafugaji wa nguruwe 150 kutoka Halmashauri za Njombe na Rungwe kuhusu ulishaji wa nguruwe ili kuongeza tija ilifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 TALIRI iliendelea vilevile na tafiti zenye lengo la kujumuisha malisho bora katika mifumo ya uzalishaji na ikolojia mbalimbali na ilihusisha jumla ya wafugaji 264 kutoka katika Halmashauri za Misungwi, Magu, Kilwa na Lushoto. Katika kipindi hicho, marobota 67,329 ya malisho ya mifugo yalivunwa katika Vituo vya Mpwapwa, Uyole, Kongwa, Tanga, Mabuki na West Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi kwa lengo la kundeleva Sekta ya Uvuvi. Taasisi imeendelea kufanya utafiti na kuishauri Serikali na wadau wa uvuvi kuhusu hali ya rasilimali za uvuvi na jinsi ya kuzihifadhi na kuzivuna kwa uendelevu. Ushauri huo umetolewa kupitia tafiti mbalimbali, ikiwemo tathmini ya uwingi wa samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria ambapo matokeo yanaonesha kiasi cha Sangara Ziwa Victoria kuongezeka kutoka tani 939,724 mwaka 2011 mpaka tani 1,230,436 mwaka 2014 kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa matumizi ya rasilimali za uvuvi. Aidha, uwingi wa dagaa umeongezeka na jamii za furu umeshuka kutokana na ongezeko la sangara ambao ni chakula chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti kuangalia mavuno ya samaki (*catch assessment*) na madhara ya minyoo kwa Dagaa katika Ziwa Nyasa unaendelea. Utafiti huu utasaidia kujua kiasi cha samaki kinachopatikana kwa wavuvi na kuainisha madhara ya minyoo katika Dagaa. Tafiti hizi zitasaidia kuimarisha mpango wa kutunza rasilimali za Ziwa Nyasa.

Vilevile, utafiti kuangalia jiolojia na sedimentolojia pamoja na ufuatiliaji wa unadhifu na ubora wa maji ya Ziwa Tanganyika unaendelea. Pia, Utafiti uliofanyika katika Bwawa la Nyumba ya Mungu umeonesha kuwa Sato (*Nile Tilapia*) ambao hawakuwepo katika Bwawa la Nyumba ya Mungu kwa sasa wanapatikana kwa wingi. Wizara kwa kushirikiana na TAFIRI itaendelea kufuatilia hali ya Sato na Perege katika Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuweza kutunza aina zote za samaki kwa manufaa ya wavuvi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti mwingine uliofanyika katika Ziwa Masoko ambalo ni Ziwa la Kreta (Rungwe), umeonesha kuwa ziwa hili lina bioanuwai kubwa ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 *TAFIRI* kwa kushirikiana na wadau wengine wa uvuvi, itaendelea na tafiti za samaki na mazingira katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), Maziwa ya Kati (Rukwa, Kitangiri na Eyasi), Maziwa Madogo, Mito na Bahari ya Hindi, pamoja na kufanya utafiti wa ufugaji samaki hasa katika maeneo yaliyo na changamoto kama vile upatikanaji wa mbegu bora, vyakula bora vya samaki na teknolojia bora ya ufugaji katika maeneo tofauti na utafiti wa kupunguza uharibifu wa mazao ya samaki baada ya uvunaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wakala wa Maabara Vetinari Tanzania (TVLA), imepokea katika maabara zake jumla ya sampuli 6,909 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya magonjwa ya wanyama hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uzalishaji wa Chanjo (*Tanzania Vaccine Institute - TVI*) Kibaha katika mwaka 2014/2015 ilizalisha na kusambaza jumla ya dozi 24,500,000 za chanjo ya mdondo kwa wafugaji wa kuku katika Halmashauri zote hapa nchini. Chanjo hii imeonesha mafanikio makubwa ya kuzuia vifo kwa asilimia 95 kwa wafugaji wanaotumia chanjo hii katika mikoa ambayo imekuwa ikichanja kuku kwa kampeni hususan Mikoa ya Singida, Iringa, Njombe, Mbeya na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TVLA imeendelea kukamilisha vigezo vya kupata lthibati ya Kimataifa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Umahiri wa Maabara (*ISO 17025*). Katika mwaka 2015/2016, TVLA itaendelea kufanya kazi ya utambuzi, uchunguzi na utafiti wa magonjwa ya mifugo na kuimarisha vituo vyake kwa kuvikarabati na kuvipatia vitendea kazi. Aidha, itaendelea kuzalisha na kusambaza dozi milioni 100 za chanjo ya Mdondo, dozi 500,000 za chanjo ya Kimeta na dozi 500,000 za chanjo ya Chambavu. Pia, itaweka mikakati ya kuzalisha zaidi chanjo ya mdondo na kuuza katika nchi jirani ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (*FETA*) kutoa mafunzo ya Wataalam katika Sekta ya Uvuvi ambapo udahili wa wanachuo umeongezeka kutoka 1,073 mwaka 2013/2014 hadi kufikia 1,180 kwa mwaka 2014/2015. Aidha, Wakala umeendesha mafunzo ya kozi fupi kwa maafisa ugani na wavuvi wapatao 1,390 nchini. Vilevile, *FETA* imetoa mafunzo ya kozi za uvuvi kwa Maafisa Uvuvi 122 kutoka nchi za Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na Somalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *FETA* imeendelea kuongeza udahili wa wanafunzi kwa kuimarisha miundombinu na kupanua Kampasi za *FETA* za Mbegani, Nyegezi, Kibirizi, Mikindani na Gabimori kule Mkoani Mara. Vilevile wakufunzi 10 wanaendelea na mafunzo.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuiwezesha *FETA* kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 1,180 hadi 1,500; kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Gabimori na Mtwara Mikindani na kukarabati Kampasi za Nyegezi, Mbegani na Kigoma. Aidha, kituo kipya cha Mbamba Bay kitaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imewezesha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (*LITA*) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 2,215 hadi 2,451. Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyuo vya mifugo ambapo hadi sasa jumla ya vyuo vya binafsi vya mafunzo ya mifugo 21 vinavyotoa mafunzo katika ngazi ya astashahada na stashahada vimeanzishwa. Kati ya hivyo, vyuo vitano vimetambuliwa na Bazara la Veterinari

Tanzania na 16 vipo katika hatua ya kusajiliwa ambapo vyote vimepata ithibati ya NACTE. Aidha, Wakala umejenga madarasa matatu katika Kampasi za Temeke, Mabuki na Kikulula, kukarabati mabweni manne katika Kampasi ya Tengeru na Buhuri na kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 2,451 kufikia 2,500, pamoja na kutoa mafunzo ya ufugaji kibiashara kwa vijana ili waweze kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliandaa, kuratibu na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa kwa lengo la kuongeza elimu kwa wafugaji na wavuvi.

Wizara imeongeza idadi ya wagani wa mifugo kutoka 6,041 mwaka 2013/14 hadi 8,541 mwaka 2014/2015 kati ya 17,325 wanaohitajika. Idadi ya wagani wa uvuvi imeongezeka kutoka 510 mwaka 2013/2014 hadi 664 mwaka 2014/15 kati ya 16,000 wanaohitajika. Aidha, jumla ya wafugaji 9,016 na wavuvi 6,800 wamepata elimu juu ya ufugaji wa kisasa na uvuvi endelevu. Pia, maafisa ugani wa mifugo 150 na uvuvi 47 walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za utoaji huduma za ugani. Vilevile, wafugaji 15 wa ng'ombe wa maziwa walipata ziara ya mafunzo Naivasha, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Nyama Tanzania kwa kuipatia wataalam na vitendea kazi. Aidha, Bodi imeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sheria ya Nyama, Sura 421. Vilevile, Bodi imetambua na kusajili wadau katika Halmashauri za Kwimba, Ilala, Kinondoni, Temeke, Jiji la Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuiwezesha Bodi ya Nyama kusajili wadau 5,000 wa tasnia ya nyama na vyama vyao, kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Nyama, Sura 421 na kusimamia ubora wa mifugo, nyama na bidhaa zake na kusimamia biashara na kutafuta masoko ya mifugo, nyama na bidhaa zake ndani na nje ya nchi. Aidha, Bodi itatoa mafunzo kuhusu taratibu za uchinjaji, usafi na utunzaji wa nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuiwezesha Bodi ya Maziwa Tanzania ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendeleza na kuratibu tasnia ya maziwa kwa mujibu wa Sheria ya Maziwa, Sura 262. Bodi imeendelea kuratibu Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni katika shule 18 na wanafunzi 14,788 ambao hutumia lita 7,394 za maziwa kwa wiki. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni imeanza utaratibu wa kuanzisha mpango wa unywaji maziwa shuleni kwenye shule kumi, Bodi inaratibu vilevile maandalizi ya Wiki ya Maziwa mwaka 2015 itakayofanyika Babati Manyara, ikiwa na kaulimbiu ya ng'ombe wa maziwa ni fursa ya kiuchumi na lishe 'Fuga Kisasa', ambako Waheshimiwa Wabunge wote ninawaalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Bodi itaendelea kuelimisha wadau wa maziwa kuhusu Sheria ya Maziwa, Sura 262 na kusimamia, kuwajengea uwezo wakaguzi wa maziwa kutoka Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya na kuhamasisha Halmashauri kutekeleza Mpango wa Unywaji wa Maziwa Shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imeendelea kusimamia taaluma, viwango na miongozo ya utoaji wa huduma za mifugo kwa kuzingatia Sera na Sheria ya Veterinari, Sura 319. Katika mwaka 2014/15, Baraza limesajili Madaktari wa Mifugo 38 na kufikisha idadi ya madaktari 719 waliosajiliwa. Pia, Baraza limeandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi wa mifugo 302.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limekamiliisha Mwongozo wa Kusimamia Mafunzo ya Wataalam wa Afya ya Mifugo na umeanza kutumika. Aidha, ukaguzi wa vituo na huduma za

afya ya mifugo umefanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 90 zilizoko katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Baraza itaendelea kuimarisha ukaguzi wa maadili ya watoa huduma za afya ya mifugo na kuhakiki mitaala ya mafunzo kwa wataalam na wataalam wasaidiizi wa mifugo ili kuboresha huduma za mifugo zinazotolewa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imefanya kaguzi 4,995 kwa lengo la kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Matokeo ya kaguzi hizo yalionesha kukidhi viwango vya ubora vya kitaifa na kimataifa na hivyo viwanda na maghala kuruhusiwa kuendelea na shughuli za uchakataji na uhifadhi wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu njia bora za uchakataji na uhifadhi wa samaki na mazao yake kwa viwanda 48 vya kuchakata mazao ya uvuvi vilivyopo katika Ukanda wa Bahari ya Hindi (36), Ziwa Victoria (11) na Ziwa Tanganyika (1) ili viweze kuzalisha mazao yanayokidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa vya ubora na usalama kwa mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau kuwekeza zaidi katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi ili kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliimarisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi (Mwanza) na Maabara ya Kuchunguza Mwani wenye Sumu ya Dar es Salaam ambapo watumishi 18 wamepatiwa mafunzo ya kutumia mashine za kupima na kuthibitisha uwepo wa viuatilifu kwenye samaki na maji, uchunguzi wa viuatilifu na mbinu za kuchukua sampuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika 2014/2015 Wizara pia imeiwezesha Maabara ya Taifa ya Nyegezi upande wa Kemikali kukamilisha hatua za kupata Ithibati (*Accreditation*) kwa ajili ya kuhakiki viwango vya mabaki ya kemikali za sumu na madini tembo (*heavy metals*) kwenye chakula, maji na matope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha vituo 17 vya Uboora na Udhidhi wa Mazao ya Uvuvi na Maabara ya Uvuvi – Nyegezi kwa kuvipatia vitendea kazi na mafunzo kwa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha vituo 23 vya doria na kuanzisha vituo viwili vipya vya Buhingu na Namanga na hivyo kufanya jumla ya vituo 25 nchi nzima. Vituo hivyo ni pamoja na Namanga, Singida, Mtwara, Dar es Salaam, Mwanza, Bukoba, Mafia, Kilwa, Musoma, Tanga, Kigoma, Mbamba Bay, Murusagamba, Buhingu, Ikola, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulo, Tunduma, Rusumo, Kabanga na Kanyigo. Vituo hivyo vimeimarishwa kwa kupatiwa watumishi pamoja na vitendea kazi. Aidha, doria zenye siku kazi 5,985 zilifanyika katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi zilizowezesha kukamatwa kwa zana haramu. Vilevile, mafunzo ya doria kwa vitendo yalifanyika kwa Maafisa Uvuvi kutoka Halmashauri za Mwambao wa Bahari ya Hindi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Pwani pamoja na Vikosi vya Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi ambapo jumla ya washiriki 140 walihusika. Mafunzo hayo yaliwezesha kukamatwa kwa vyombo 468, wavuvi 1,065, makokoro 9, nyavu za makila 1, nyavu za macho madogo 550, mbolea ya chumvichumvi kilo 15, zana za milipuko vipande (*detonators*) 10, majongoo bahari kilo 60, mitando 2 na mita 20,000 za kamba za kuvutia kokoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji endelevu wa kudhibiti rasilimali za uvuvi na biashara haramu kwa kufanya doria zenye siku kazi 6,000. Katika mwaka 2015/2016 vilevile Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na wadau mbalimbali itawezesha uanzishwaji wa vikundi vya (BMUs) na kuimarisha vilivyopo ili kuhakikisha usimamizi imara wa rasilimali za uvuvi unazingatia matumizi endelevu ya ikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara inayosimamia masuala ya uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imefanya doria za anga katika Bahari Kuu ya Tanzania kwa saa 144 ili kudhibiti uvuvi haramu. Vilevile, Mamlaka imeshiriki katika doria za kikanda za majini chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Nchi Wanachama wa Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission*). Katika ukaguzi huo meli zote zilikidhi masharti ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania. Aidha, leseni 88 za uvuvi wa Bahari Kuu zilitolewa na kuingiza Dola za Kimarekani 1,863,470 sawa na takribani Shilingi bilioni 3.3 ikiwa ni ada za leseni za meli za uvuvi kutoka mataifa mbalimbali.

Vilevile, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu imeingia kwenye makubaliano na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFIRI*) kufanya utafiti wa kutambua maeneo muhimu ya uvuvi ili kuwasaidia wavuvi kutambua maeneo yenye rasilimali nyingi katika Bahari ya Hindi, kwa lengo la kuwapunguzia gharama za kutafuta samaki baharini. Pia, Mamlaka imeingia kwenye makubaliano na *TAFIRI* ya kufanya tathimini ya vifaa maalum vya kuvutia samaki kwenye maji vilivyowekwa kwenye maji ya kitaifa.

Katika mwaka 2015/2016, Mamlaka pia itashiriki katika kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu na kuboresha mfumo wa kufuatilia meli zinazovua katika Bahari Kuu. Vilevile, kwa kushirikiana na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Kampasi ya Mbegani, itatoa mafunzo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, kuendesha doria za anga na itahamasisha wadau kuwekeza kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Samaki aina ya Jodari katika Bahari ya Hindi, Mashirika ya Kikanda na Kimataifa katika usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za Uvuvi wa Bahari Kuu na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kusimamia na kuhifadhi rasilimali za uvuvi kupitia kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (*MPRU*). Doria zenye jumla ya siku kazi 362 zilifanyika katika eneo la kilometa za mraba 2,000 kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwenye Hifadhi za Bahari tatu na Maeneo Tengefu 15. Wizara imeendelea kukiimarisha Kitengo kwa kuwawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo na kukipatia vitendea kazi. Aidha, miundombinu ya utalii imejengwa katika Kisiwa cha Toteni – Tanga na Mbudya – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Kitengo kitafanya doria zenye sikukazi 400 zinazolenga kudhibiti matumizi haramu ya rasilimali za bahari, hususan uvuvi haramu katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Vilevile, Kitengo kitaendelea kufanya shughuli za uperembaji katika maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uvuvi, ikiwemo kuanzisha viwanda vya kuchakata samaki. Hadi sasa vimeanzishwa viwanda 48 na maghala 84 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi vimeanzishwa. Aidha, Wizara imeboresha Soko la Kasanga (Sumbawanga) na mialo 31 ya kupokelea na kuhifadhi mazao ya uvuvi katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi, Wizara pia inaendelea kuweka mazingira mazuri na kuboresha miundombinu ya uvuvi. Aidha, Wizara inaendelea na utaratibu wa kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi ambapo hadidu za rejea zimeshaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Napenda kuzitambua na kuzishukuru nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Jamhuri ya Watu wa China, Israel, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO* na *WHO* na Mifuko ya Kimataifa ya *GEF* na *IFAD* kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nazishukuru Taasisi za Kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea, Shirika la Misaada la Ireland, Shirika la Misaada la Marekani, Shirika la Misaada la Australia, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza, Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika, Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, Shirika la Maendeleo la Uswisi, Shirika la Ushirikiano la Ujerumani, *United Nations University*, Shirika la Maendeleo la Denmark na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden, kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Pia, nayashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), The New Partnership for African's Development (NEPAD), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCE), Vetaid, Care International, OXFAM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute for Security Studies (ISS-Africa), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish* na *Marine Stewardship Council (MSC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wananchi wote hususan wafugaji, wavuvi na wadau wengine, kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Nachukua nafasi hii kuwaomba waendeleo kushirikiana nasi katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kuwashukuru kwa dhati sana Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara na Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi 68,810,374,000/=. kama ifuatavyo:-

- (i) Shilingi 46,158,922,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi 30,050,702,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE); na shilingi 16,108,220,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC); na
- (ii) Shilingi 22,651,482,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 22,000,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 651,482,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhata kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.mifugouvuvu.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Hotuba hii, nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2015/16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki. *(Makofi)*
(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imeungwa mkono.

Naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji!

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Maji? Mwakilishi wake, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma! *(Makofi)*

MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Pili, namshukuru Mwenyekiti kwa kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ilijadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu Bajeti iliyoombwa kwa ajili ya Wizara hii. Kamati iliridhika na jitihada za Wizara katika kutekeleza baadhi ya ushauri wa Kamati, pamoja na ukweli kwamba, bajeti iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo mpaka kufikia Aprili, 2015, ilikuwa ni asilimia 16 tu ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia malengo iliyojiwekea. Changamoto hizo ni pamoja na:-

Moja, kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya malisho. Hali hii inasababisha migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa mazingira na ueneaji wa magonjwa ya mifugo kutokana na kuhamahama kwa mifugo.

Pili, ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi hasa katika maeneo ya vijijini.

Tatu, uwekezaji mdogo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi hususan katika uvuvi wa bahari kuu na usindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi.

Nne, kuenea kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan magonjwa ya milipuko, magonjwa yasiyo na mipaka na yale yanayoenezwa na kupe na mbung'o.

Tano, upungufu wa mbegu bora za mifugo na samaki ikiwa ni pamoja na huduma hafifu ya uhamilishaji (*artificial insemination*).

Sita, uhaba wa Maafisa ugani wa mifugo na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao katika Halmashauri.

Saba, Wizara kupata asilimia ndogo ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika mpango kazi. Hii inasababisha malengo kutofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi, Wakala na Bodi zilizo chini ya Wizara zimekadiria kukusanya Sh. 43,862,624,975/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 44 ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vikuu vya makusanyo hayo ni pamoja na leseni na ada za vibali vya kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi. Leseni za kuvua na kusafirisha samaki na mazao yake na Mauzo ya Chanjo za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99), inaomba jumla ya Sh. 68,810,374,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 46,158,922,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 22,651,452,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la 7% ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, fedha iliyoombwa ya maendeleo mwaka wa fedha 2015/2016 ni pungufu kwa 8.3% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kuwa fedha zinazotengwa katika bajeti ya miradi ya maendeleo ni asilimia ndogo zinazotolewa inapofika mwisho wa mwaka wa fedha. Kwa vile maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016 ni pungufu kuliko maombi ya mwaka uliotangulia, Kamati inaiomba Serikali kutoa fedha zote zinazoombwa ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayoombwa, inalenga kutekeleza maeneo tisa ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

- (1) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo na uvuvi na matumizi ya wagani;
- (2) Kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo;
- (3) Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi, malisho na nyanda za malisho;
- (4) Kuendeleza ufugaji na ukuzaji viumbe kwenye maji;
- (5) Kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi na kuboresha upatikanaji wa masoko;
- (6) Kuimarisha na kujenga ushirika na hasa ule wa vyama vya wafugaji na wavuvi;
- (7) Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi;
- (8) Kudhibiti ongezeko la matumizi ya zana haramu za uvuvi na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani na Kujenga mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naomba sasa kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa Sekta za Mifugo na Uvuvi zina fursa kubwa katika kukuza pato la Taifa. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa sekta hizi hazijapewa uzito unaostahili kwa kutopewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Visiwa vya Shelisheli vyenye idadi ya wakazi 85,000 ni moja ya nchi zilizofanikiwa katika Sekta ya Uvuvi. Takribani 75% ya nguvu kazi ya Taifa imeajiriwa katika sekta hii. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012 Sekta ya Uvuvi ililingizia Taifa hili Rupia za Shelisheli bilioni 1.2 sawa na Shilingi za Kitanzania Sh. 184,690,000,000/= za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati thabiti ya kuimarisha sekta hizi za mifugo na uvuvi hususan ufugaji wa kisasa na uvuvi wa kina kirefu (*deep sea fishing*). Aidha, ili kufanikisha hili, Kamati inaishauri Serikali kuiweka Wizara hii katika Mpango wa Serikali wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa (*BRN*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri katika maeneo mengine kama ifuatavyo:-

- (a) Upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wizara hii kutopata fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Bunge lilipendekeza nyongeza ya Shilingi bilioni 20 katika bajeti na Serikali kukubali na kufanya bajeti ya maendeleo kufikia Shilingi bilioni 23.4. Mpaka mwezi Aprili, 2014 hakuna fedha yoyote ya nyongeza iliyokuwa imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka 2014/2015, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali ilitoa shilingi bilioni 10.5 kati ya shilingi 23,458,270,000/= zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara hii iliidhinishwa jumla ya Sh. 24,752,405,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya Sh. 3,934,042,500/= tu zilizotolewa, sawa na asilimia 16 ya fedha zote zilizo idhinishwa katika bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatafsiri mwenendo huu wa Serikali kuwa haina nia thabiti ya kutekeleza mikakati yake ya kuzifanya Sekta za Mifugo na Uvuvi kuwa endelevu na zenye uzalishaji bora na wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi ni kati ya changamoto zinazoikabili Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kasi ndogo ya Serikali katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo. Hii imepelekea wafugaji kuhamahama na kusababisha migogoro baina yao na watumiaji wengine wa ardhi kama vile wakulima na maeneo ya Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza migogoro ya ardhi, Kamati inaishauri Serikali kubaini na kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji na kuyaendeleza. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu izifanyie kazi taarifa za Wizara ya Maliasili na Utalii na Kamati Teule ya Bunge, yaani ya Migogoro ya Ardhi 2015, kuhusu tathmini ya maeneo yaliyopoteza sifa ya kuwa hifadhi ili maeneo hayo yatumike kwa wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaihimiza Serikali kwa mara nyingine kuboresha miundombinu ya machinjio ya kisasa, viwanda vinavyoongeza thamani, mazao ya mifugo na bidhaa zake; minada, njia za mifugo na vituo vya kuzuia usambaji wa magonjwa ya mifugo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Umma kwa nia ya kuboresha bidhaa zote za mifugo zikiwemo nyama, maziwa, ngozi, pembe na kwato. Mifugo ikiwa bora itavihakikishia viwanda vyetu kupata malighafi iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi, Serikali itakuwa na uhakika wa masoko ya mifugo na bidhaa zake ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Samaki Ferry lililopo Dar es Salaam lipo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kiseru, lakini uendeshaji na ukusanyaji wa mapato yake unafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2015, Kamati ilitembelea soko hilo. Katika ziara hiyo Kamati ilijulishwa changamoto zinazolikabili la Ferry ambazo ni pamoja na:-

Moja, kuchakaa kwa miundombinu ya soko;

Pili, ongezeko kubwa la watumiaji soko ambapo uwezo wa soko ni kuhudumia watu 2000, lakini kwa sasa linahudumia watu 15,000.

Tatu, kutokuwepo kwa Bodi ya Uendeshaji Soko kama ilivyokuwa imeamuliwa katika makubaliano ya pamoja kati ya wafanyabiashara, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan iliyokuwa mfadhili mkuu wa ujenzi wa soko hili; na

Nne, wavuvi na wafanyabiashara kutoshirikishwa katika mipango na maamuzi yanayohusu uendeshaji wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa changamoto tajwa zimekwamisha uendeshaji wenye tija wa soko kwa wafanyabiashara wa samaki. Kamati inaishauri Serikali ifuatavyo:-

(1) Masoko mengine ya samaki yaanzishwe katika Manispaa za Kinondoni na Temeke ili kupunguza msongamano.

(2) Kuunda Bodi ya uendeshaji wa Soko kupewe msukumo mkubwa na wadau wote washirikishwe.

(3) Kuweka vipaumbele katika kusimamia sera na taratibu zilizopo ili kuhamasisha miundombinu ya uvuvi na masoko ya samaki nchini.

(4) Kuhakikisha kuna uwazi katika mapato yanayotokana na shughuli za *Ferry* na mgawanyo wa mapato hayo.

(5) Kuelekeza Halmashauri ya Manispaa ya Ilala itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya soko na Kuratibu uundwaji wa chombo cha wavuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ni kudhibiti uvuvi haramu na kuimarisha ukaguzi wa mazao ya uvuvi. Kazi hii inaombewa jumla ya Shilingi bilioni 1.8. Pamoja na vifaa vingine, fedha hizo zimepangwa kununua meli moja yenye uwezo wa kufanya doria katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikatambua kuwa Taifa linapoteza mapato mengi kutokana na uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi kutoka nje ya nchi katika eneo letu la bahari kuu. Kamati inaishauri Serikali iweke mipango madhubuti ya kuwekeza katika doria kwenye bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanajishughulisha na ufugaji wa mifugo midogo midogo kama vile kware, kanga, kuku, sungura, bata na biashara nyingine kama mbuzi na vitu vingine. Kamati inashauri ufugaji huu uhamasishwe kwa upana wake ili uwe wa kisasa na wa kibiashara zaidi kwani pamoja na kuwa chanzo cha lishe bora, utaongeza kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. Serikali imeonesha nia ya kujenga bandari ya uvuvi ili kuendeleza tasnia ya uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa eneo lililochaguliwa kujenga bandari hii ni pale Chuo cha Uvuvi cha Mbegani; na kwa kuwa Chuo hiki kina sifa ya *a Centre of Excellence*, Kamati inahitaji kupata uhakika kwamba shughuli za Chuo hazitaathirika. Vinginevyo Kamati inashauri kuwa, Serikali itafute eneo mbadala la kujenga bandari hii.

Aidha, kama itabidi Chuo kuhamishwa, Kamati inashauri Serikali ijenge majengo na miundombinu mipya kwa ajili ya Chuo cha Uvuvi kabla ya kuanza ujenzi wa Bandari hiyo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuenea kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo kumeendelea kuwa changamoto inayoikabili Wizara katika utekelezaji wa mipango yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati iliyopo ya kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha maeneo huru ya magonjwa (*Disease Free Zones*) ya mifugo katika maeneo ambayo yanakumbwa kwa urahisi zaidi na magonjwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2015, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika eneo la lililokuwa Shirika la Uvuvi Tanzania (*TAFICO*) kabla ya kubinafsishwa. Shirika hili lilibinafsishwa kufuatia Sera ya Taifa ya Ubinafsishaji ambayo ililenga Serikali kujitoa katika kuendesha shughuli za kibiashara na kuiachia sekta binafsi ambayo ilitarajiwa kuzalisha kwa ufanisi na tija zaidi. Kabla ya kubinafsishwa, *TAFICO* ilikuwa inafanya vizuri katika masuala ya uvuvi na hususan uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa mali zilizokuwa za Shirika, kama vile majengo ya karakana na gati zilikuwa hazifai tena kwa matumizi. Aidha, Kamati ilishuhudia mmomonyoko wa ardhi katika fukwe za eneo hilo ambao unahatarisha baadhi ya majengo yaliyo pembezoni mwa eneo kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali halisi ya eneo hilo, Kamati inashauri kuwa, ili Taifa letu lifanikiwe katika Sekta ya Uvuvi na hususan uvuvi wa bahari kuu, ni vyema Serikali ikawekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kuanzisha chombo (*National Fleet*) kitakachotumika kwa ajili ya uvuvi huo.

Aidha, Kamati inashauri kuwa, ni vyema Serikali ikawa na hisa katika mashirika yanayobinafsishwa ili kuhakikisha mashirika hayo yanaendelea kuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kutokuwa na wataalamu wa kutosha katika Sekta za Mifugo na Uvuvi limeendelea kuathiri utendaji wa Wizara. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri wataalam wa kutosha ukizingatia kwamba wahitimu wengi wa masuala ya mifugo na uvuvi hawana ajira. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kutekeleza ahadi ya ajira ya moja kwa moja kwa Maafisa Ugani ambao ni wahitimu wa Vyuo vya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Tafiti zimeendelea kupata fedha kidogo na shughuli za utafiti kuathirika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara itafute njia ya ziada ya kupata fedha, hususan fedha za nje, kwa ajili ya shughuli za utafiti kwa kuandaa maandiko mazuri ya miradi mbalimbali. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza adhama yake ya kutenga asilimia moja ya pato ghafi lake (*1% GDP*) kwa ajili ya masuala ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, na hasa wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kunipatia nafasi hii adimu kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, napenda kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kaika Saming'o Telele kwa ushirikiano mzuri walionipatia Kamati katika kipindi chote hiki.

Aidha, nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeda pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashiilah kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. Aidha, namshukuru Katibu wa Kamati Ndugu Grace Bidya akisaidiwa na Ndugu Sophia Vumbi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru familia mume wangu mpenzi, Profesa Ishengoma pamoja na watoto wangu. Pia napenda kuwashukuru wanawake wa Morogoro wa CCM walioniweka kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99, jumla ya Sh. 68,810,374,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

Kama ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

1.0 UTANGULIZI

Meshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilijadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

- 2.1 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kujadili makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Wizara hii. Kamati iliridhika na jitihada za Wizara katika kutekeleza baadhi ya ushauri wa Kamati, pamoja na ukweli kwamba, bajeti iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo mpaka kufikia Aprili 2015, ilikuwa ni asilimia **16** tu ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge.

3.0 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

- 3.1 **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia malengo iliyojiwekea. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- Kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya malisho; hali hii inasababisha migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa mazingira na ueneaji wa magonjwa ya mifugo kutokana na kuhama hama kwa mifugo;
- Ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi hasa katika maeneo ya vijijini;
- Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi hususan katika uvuvi wa bahari kuu na usindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi;
- Kuenea kwa magonjwa mbali mbali ya mifugo, hususan magonjwa ya milipuko, magonjwa yasiyo na mipaka na yale yanayoenezwa na kupe na mbung'o;
- Upungufu wa mbegu bora za mifugo na samaki ikiwa ni pamoja na huduma hafifu ya uhamilishaji (*artificial insemination*);
- Uhaba wa Maafisa ugani wa mifugo na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao katika Halmashauri; na
- Wizara kupata asilimia ndogo ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika mpango kazi; hii inasababisha malengo kutofikiwa.

4.0 MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

4.1 Makusanyo ya Maduhuli

4.1.1 Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi, Wakala na Bodi zilizo chini ya Wizara zimekadiria kukusanya shilingi **43,862,624,975/=** ikiwa ni ongezeko la asilimia **44** ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2014/2015.

4.1.2 Mheshimiwa Spika, vyanzo vikuu vya makusanyo hayo ni pamoja na:-

- i. Leseni na ada za vibali vya kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi;
- ii. Leseni za kuvua na kusafirisha samaki na mazao yake; na
- iii. Mauzo ya chanjo za mifugo.

4.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi

4.2.1 Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (**Fungu 99**), inaomba jumla ya **shilingi 68,810,374,000/=**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 46,158,922,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 22,651,452,000/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la asilimia saba (7%) ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

4.2.2 Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, fedha iliyoombwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni pungufu kwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

4.2.3 Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa fedha zinazotengwa katika bajeti ya miradi ya maendeleo ni asilimia ndogo zinatolewa inapofika mwisho wa mwaka wa fedha. Kwa vile maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016 ni pungufu kuliko maombi ya mwaka uliotangulia, Kamati inaiomba Serikali kutoa fedha zote zinazoombwa ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake.

4.2.4 Mheshimiwa Spika, fedha inayoombwa, inalenga kutekeleza maeneo tisa ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

- i. Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo na uvuvi na matumizi ya wagani;
- ii. Kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo;
- iii. Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi, malisho na nyanda za malisho;
- iv. Kuendeleza ufugaji na ukuzaji viumbe kwenye maji;
- v. Kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi na kuboresha upatikanaji wa masoko;
- vi. Kuimarisha na kujenga ushirika na hasa ule wa vyama vya wafugaji na wavuvi;

- vii. Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta za mifugo na uvuvi;
- viii. Kudhibiti ongezeko la matumizi ya zana haramu za uvuvi na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani; na
- ix. Kujenga mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji wa sekta binafsi.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

5.1 Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, naomba sasa kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara hii.

5.2 Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Sekta za mifugo na uvuvi zina fursa kubwa katika kukuza pato la Taifa. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa sekta hizi hazijapewa uzito unaostahili kwa kutopewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, visiwa vya Shelisheli yenye idadi ya wakazi 85,000 ni moja ya nchi zilizofanikiwa katika sekta ya uvuvi. Takribani asilimia 75 ya nguvu kazi ya taifa imeajiriwa katika sekta hii. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012 sekta ya uvuvi ililingizia taifa hili Rupia za Shelisheli bilioni 1.2¹ (sawa na shilingi **184,690,000,000/=** za Kitanzania).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati thabiti ya kuimarisha sekta hizi za mifugo na uvuvi hususan ufugaji wa kisasa na uvuvi wa kina kirefu (deep sea fishing). Aidha, ili kufanikisha hili, Kamati inaishauri Serikali kuiweka Wizara hii katika Mpango wa Serikali wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

5.3 Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri katika maeneo mengine kama ifuatavyo:-

a) Upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Spika, suala la Wizara hii kutopata fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Wizara. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Bunge lilipendekeza nyongeza ya shilingi **bilioni 20** katika bajeti na Serikali kukubali, (na kufanya bajeti ya maendeleo kufikia shilingi **23,488,270,000/=**).

Mpaka mwezi Aprili, 2014, hakuna fedha yoyote ya nyongeza ilikuwa imetolewa.

Mheshimiwa Spika, Wakati wa kupitia utekezaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka 2014/2015, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali ilitoa shilingi **10,500,000,000/=** kati ya shilingi **23,488,270,000/=** zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi **24,752,405,000/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya shilingi **3,934,042,500/=** tu zilizotolewa, sawa na asilimia **16** ya fedha zote zilizoidhinishwa katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatafsiri mwenendo huu wa Serikali kuwa haina nia thabiti ya kutekeleza mikakati yake ya kuzifanya sekta za mifugo na uvuvi kuwa endelevu na zenye uzalishaji bora na wenye tija.

b) Migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi ni kati ya changamoto zinazoikabili Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kasi ndogo ya Serikali katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo. Hii imepelekea wafugaji kuhama hama na kusababisha migogoro baina yao na watumiaji wengine wa ardhi kama vile wakulima na maeneo ya Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza migogoro ya ardhi, Kamati inaishauri Serikali kubaini na kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji na kuyaendeleza. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu izifanyie kazi taarifa za Wizara ya Maliasili na Utalii na Kamati Teule ya Bunge (Migogoro ya Ardhi 2015) kuhusu tathmini ya maeneo yaliyopoteza sifa ya kuwa hifadhi ili maeneo hayo yatumike kwa ufugaji.

c) Masoko ya mifugo na mazao yake

Mheshimiwa Spika, Kamati inaihimiza Serikali kwa mara nyingine kuboresha miundombinu ya machinjio ya kisasa, viwanda vinayoongeza thamani mazao ya mifugo na bidhaa zake, minada, njia za mifugo na vituo vya kuzuia usambaaji wa magonjwa ya mifugo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa nia ya kuboresha bidhaa zote za mifugo zikiwemo nyama, maziwa, ngozi, pembe na kwato. Mifugo ikiwa bora itavihakikishia viwanda vyetu kupata malighafi iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi Serikali itakuwa na uhakika wa masoko ya mifugo na bidhaa zake ndani na nje ya nchi.

d) Soko la Samaki Feri- Dar Es Salaam

Mheshimiwa Spika, Soko la Samaki Feri lililopo Dar es Salaam lipo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kiseru, lakini uendeshaji na ukusanyaji wa mapato yake unafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Ilala.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2015, Kamati ilitembelea soko hilo. Katika ziara hiyo Kamati ilijulishwa changamoto zinazolikabili soko la Feri ambazo ni pamoja na:-

- i. Kuchakaa kwa miundombinu ya soko;
- ii. Ongezeko kubwa la watumiaji soko ambapo uwezo wa soko ni kuhudumia watu 2000, lakini kwa sasa linahudumia watu 15,000;
- iii. Kutokuwepo kwa Bodi ya uendeshaji soko kama ilivyokuwa imeamuliwa katika makubaliano ya pamoja kati ya wafanyabiashara, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan (iliyokuwa mfadhili mkuu wa ujenzi wa soko hili); na

- iv. Wavuvi na wafanyabiashara kutoshirikishwa katika mipango na maamuzi yanayohusu uendeshaji wa soko.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa changamoto tajwa zimekwamisha uendeshaji wenye tija wa soko kwa wafanyabiashara wa samaki. Kamati inaishauri Serikali ifuatavyo:-

- i. Masoko mengine ya samaki yaanzishwe katika Manispaa za Kinondoni na Temeke ili kupunguza msongamano;
- ii. Kuunda Bodi ya uendeshaji wa Soko kupewe msukumo mkubwa na wadau wote washirikishwe;
- iii. Kuweka vipaumbele katika kusimamia Sera na taratibu zilizopo ili kuimarisha miundombinu ya uvuvi na masoko ya samaki nchini;
- iv. Kuhakikisha kuna uwazi katika mapato yanayotokana na shughuli za feri na mgawanyo wa mapato hayo;
- v. Kuelekeza Halmashauri ya Manispaa ya Ilala itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya soko; na
- vi. Kuratibu uundwaji wa chombo cha wavuvi nchini.

e) Doria katika Bahari Kuu

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, ni kudhibiti uvuvi haramu na kuimarisha ukaguzi wa mazao ya uvuvi. Kazi hii inaombewa jumla ya shilingi **1,800,000,000/=**². Pamoja na vifaa vingine, fedha hizo zimepangwa kununua meli moja yenye uwezo wa kufanya doria katika bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikatambua kuwa Taifa linapoteza mapato mengi kutokana na uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi kutoka nje ya nchi katika eneo letu la bahari kuu.

Kamati inaishauri Serikali iweke mipango madhubuti na kuwekeza katika doria kwenye bahari kuu. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, zishirikiane katika kuhakikisha meli mbili za doria zilizozinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Aprili 2015 zinatumiwa vema katika kuimarisha doria katika bahari kuu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha doria katika maziwa makuu ili kudhibiti uwizi wa zana za wavuvi na uvuvi haramu.

f) Ufugaji wa Mifugo Midogo

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanajishughulisha na ufugaji wa mifugo midogo kama vile kwale, kanga na kuku wa kienyeji kwa ajili ya biashara na matumizi ya nyumbani.

Kamati inashauri ufugaji huu uhamasishwe kwa upana wake ili uwe wa kisasa na wa kibiashara zaidi kwani pamoja na kuwa chanzo cha lishe bora, utaongeza kipato kwa wananchi.

g) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi

Mheshimiwa Spika, Serikali imeonesha nia ya kujenga bandari ya uvuvi ili kuendeleza tasnia ya Uvuvi wa bahari kuu³.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo lililochaguliwa kujenga Bandari hii ni pale chuo cha uvuvi cha Mbegani, na kwa kuwa chuo hiki kina sifa ya 'a centre of excellence', Kamati inahitaji kupata uhakika kwamba shughuli za chuo hazitaathirika, vinginevyo Kamati inashauri kuwa, Serikali itafute eneo mbadala la kujenga bandari hii. Aidha, kama itabidi chuo kuhamishwa, Kamati inashauri Serikali ijenge majengo na miundombinu mipya kwa ajili ya chuo cha uvuvi kabla ya kuanza ujenzi wa bandari hiyo ya uvuvi.

h) Kukabiliana na magonjwa mbalimbali ya mifugo

Mheshimiwa Spika, kuenea kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo kumeendelea kuwa changamoto inayoikabili Wizara katika utekelezaji wa mipango yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati iliyopo ya kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha maeneo huru ya magonjwa (Disease Free Zones) ya mifugo katika maeneo ambayo yanakumbwa kwa urahisi zaidi na magonjwa hayo.

i) Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)

Mheshimiwa Spika, Mwezi Machi, 2015, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika eneo la iliyokuwa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) kabla ya kubinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili lilibinafsishwa kufuatia Sera ya Taifa ya ubinafsishaji ambayo ililenga Serikali kujitoa katika kuendesha shughuli za kibiashara na kuiachia sekta binafsi ambayo ilitarajiwa kuzalisha kwa ufanisi na tija zaidi. Kabla ya kubinafsishwa, TAFICO ilikuwa inafanya vizuri katika masuala ya uvuvi na hususan uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa mali zilizokuwa za Shirika, kama vile majengo ya karakana na gati zilikuwa hazifai tena kwa matumizi. Aidha, Kamati ilishuhudia mmomonyoko wa ardhi katika fukwe za eneo hilo ambao unahatarisha baadhi ya majengo yaliyo pembezoni mwa eneo kuporomoka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ya eneo hilo, Kamati inashauri kuwa, ili Taifa letu lifanikiwe katika sekta ya uvuvi, na hususan uvuvi wa bahari kuu, ni vema Serikali ikawekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kuanzisha chombo (National Fleet) kitakachotumika kwa ajili ya uvuvi huo.

Aidha, Kamati inashauri kuwa, ni vema Serikali ikawa na hisa katika mashirika yanayobinafsishwa ili kuhakikisha mashirika haya yanaendelea kuwa na tija kwa Taifa.

j) Uhaba wa watumishi katika Wizara na huduma za ugani wa mifugo na uvuvi

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutokuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta za mifugo na uvuvi limeendelea kuathiri utendaji wa Wizara.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri wataalam wa kutosha ukizingatia kwamba wahitimu wengi wa masuala ya mifugo na uvuvi hawana ajira. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kutekeleza ahadi ya ajira ya moja kwa moja kwa maafisa ugani ambao ni wahitimu wa vyo vya mifugo na uvuvi.

k) Utafiti wa mifugo na uvuvi

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Tافiti zimeendelea kupata fedha kidogo na shughuli za utafiti kuathirika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara itafute njia ya ziada za kupata fedha, hususan fedha za nje, kwa ajili ya shughuli za utafiti, kwa kuandaa maandiko mazuri ya miradi mbalimbali. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza adhama yake ya kutenga asilimia moja ya pato ghafi lake (1%GDP) kwa ajili ya masuala ya utafiti.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, na hasa wakati wa kuandaa taarifa hii.

Napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Said J. Nkumba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Subira Mgalu, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Asaa Othman Hamad, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Abdusalaam S. Ameir, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Abdalla Haji Ali, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Namelok E. M. Sokoine, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma, Mb - Mjumbe

Nakala ya Mtandao (Online Document)

10. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Moshi S. Kakoso, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Kheri Khatib Ameir, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Meshack Jeremia opulukwa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Donald Kelvin Max, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Haji Juma Sereweji, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt Lucy Sawere Nkya, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Titus Mlengeya Kamani (Mb), na Naibu Waziri, Mhe. Kaika Saning'o Telele (Mb), kwa ushirikiano mzuri waliyoipatia Kamati katika kipindi chote hiki.

Aidha, nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasilillah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla.

Aidha, namshukuru Katibu wa Kamati Ndugu Grace Bidya akisaidiwa na Ndugu Sophia Vumbi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, **Fungu 99**, jumla ya **shilingi 68,810,374,000/=** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI
20 Mei, 2015**

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

MHE. MKIWA A. KIMWANGA - K.N.Y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa chini ya kanuni ya 99(9) kanuni za Bunge za Kudumu toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunitunza ili niweze kulitumikia Taifa langu. Napenda kuishukuru familia yangu kwa msaada mkubwa na kunivumilia hasa katika harakati na shughuli zangu za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wataanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kupokea harakati za mabadiliko nchini. Shukrani hizi za pekee ziwafikie Wenyeviti wenza wa Vyama vya UKAWA, Mheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Makaidi. Vilevile, kwa Makatibu Wakuu, Viongozi wa UKAWA Mheshimiwa Maalimu Seif Shariff Hamad, Mheshimiwa Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Mosena Nyambabe na Mheshimiwa Tozi Matwange. *(Makofi)*

Aidha, shukrani hizi ziende kwa timu ya wataalamu wa UKAWA, Viongozi, Watendaji, Wanachama na wapenzi wa Vyama vyetu vinavyounda UKAWA vya NLD, CUF, NCCR-Mageuzi na CHADEMA.

Nawataka Wanachama wa mapenzi mema na UKAWA kujipanga, kujituma na kujiandaa kushinda kwa kishindo katika ushindi wa kuchukua dola Uchaguzi Mkuu wa Tanganyika na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, salaam zangu za pole kwa Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum ambaye yuko kwenye matibabu nchini India. Ugonjwa wake ni matokeo ya kikosi cha hujuma cha CCM cha *Green Guards* ambacho walimvunja bega na Jeshi la Polisi linaelewa wahusika hao, lakini hakuna hatua zozote za kisheria zilizochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za pekee ziende kwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani Bungeni wanaounda UKAWA kwa kazi nzuri ya kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa Watendaji wa Kambi ya Upinzani ambao wamekuwa msaada mkubwa kwetu na kwa kazi yao nzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Wizara inaonesha kuwa kwa mwaka wa 2014/2015, ilitengewa kiasi cha shilingi 24,752,405,000/= fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 22,552,800,000/= sawa na asilimia 91 ni fedha za ndani na shilingi 2,222,605,000/= sawa na asilimia 91 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya shilingi 3,934,042,500/= zilitolewa na shilingi 2,636,529,190.31 zilitumika. Kati ya fedha zilizotolewa, shilingi 3,393,457,500/= ni fedha za ndani na shilingi 540,585,000/= ni fedha za nje kwa ajili ya ASDP-L.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa kwa Wizara hadi mwezi wa Nne ni asilimia 15.9 tu; na fedha za ndani nazo ni asilimia 15.06 tu. Kwa fedha hizo: Je, ni kweli hapa kuna uwezekano wa kuendeleza sekta hii? Serikali inasema haina fedha, lakini za kutoa kwa tapeli wa IPTL kwenye ESCROW Account, zinalipwa lakini za kukeza kwenye miradi ya mifugo na uvuvi hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kuwa Serikali ya CCM imechoka, ipumzike; Waheshimiwa Wabunge wanasema hatuoni yaliyofanyika. Mara zote tajiri huwa haoni kuwa anafilisika hata kama akiambiwa. Ndiyo hayo yanayoikumba Serikali ya CCM; imefilisika kiuongozi, ikae pembeni ione jinsi Sekta ya Mifugo na Uvuvi ilivyokuwa ni mtambo wa kuzalisha mahela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 pamoja na Mkakati wake wa mwaka 2010, lengo kuu lilikuwa ni kuendeleza Sekta hiyo kwa kuifanya Sekta hiyo kuwa endelevu na ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Wizara zinaonesha kuwa mchango wake katika pato la Taifa halilingani na ukubwa wa sekta. Matatizo yanayoikabili sekta hii kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani, wadau mbalimbali na Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia sekta, kwa nyakati tofauti tumekuwa tunatoa ushauri kwa Serikali nini kifanyike. Kwa kuwa sikio la kufa halisikii dawa, imekuwa ikipuza ushauri huo. Sasa Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, mwaka huu ndiyo mwaka wa mwisho kwa wadau kushuhudia sekta hii ikishindwa kutoa kile kinachotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo la mahusiano ya kikazi kati ya Serikali Kuu, yaani Wizara ya Mifugo na TAMISEMI, kwani mtu anayesimamia kilimo ndiye huyo anayesimamia mifugo kwa ngazi ya Wilaya na anaitwa DALDO. Kama Afisa huyo amesomea kilimo, maana yake kazi zake nyingi zitakuwa ni za kilimo na mifugo itashindwa kuendelezwa. Huu ni udhaifu wa kinfumo. Ushauri kwa hili umetolewa mara nyingi lakini imeshindikana kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka mingi sasa Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikieleza jinsi wanaojita wawekezaji katika ranchi mbalimbali au maeneo mengine ambayo wameshindwa kutumia ardhi hiyo na badala yake wanakodisha maeneo hayo kwa wafugaji. Mfano mzuri ni ranchi ya Kitengule ambayo karibu nusu yake amepewa mwekezaji lakini haitumiki yote na badala yake anawakodisha wafugaji.

Aidha, tulikwishaomba kupatiwa orodha ya majina ya wawekezaji wa ranchi zilizo katika Mkoa wa Kagera na ukubwa wa kila eneo la mwekezaji, lakini hadi leo orodha hiyo haijawahi kutolewa. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba Watanzania hasa wafugaji matatizo yote yanayodumaza sekta, Serikali inayaelewa na imekaa kimya kwa sababu Watendaji wake Waandamizi ni sehemu ya matatizo hayo; wanaogopana kuchukuliana hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishaongelea pia jinsi waangalizi wa Mapori ya Akiba wanavyochukua fedha za wafugaji na kuruhusu mifugo kupata malisho katika maeneo hayo. Lakini fedha hizo zinaishia mifukoni mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, mapori yaliyoko Wilaya za Ngorongoro, Ngara na Biharamulo kuruhusu mifugo toka nchi jirani kuchunguwa humo na taarifa hizo Serikali inazo lakini hatua hazichukuliwi na wafugaji wetu wanakosa sehemu za kulishia mifugo yao na wengine

wanaochungia maeneo hayo wanakamatwa na wanafungwa, wengine wako Magerezani bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ambayo ni kwa muda mrefu imekuwa ikiendelea; husababisha madhara makubwa ya kupoteza uhai wa watu, madhara ya kiuchumi na wananchi kupoteza makazi yao na watoto kukosa haki yao ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya yamekuwepo toka miaka ya 1980 na utafiti wa kuyamaliza ulikwishafanyika na Serikali inaelewa vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo alitoshi, Kamati teule ya Bunge iliyoongozwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka ilifanya utafiti wake na kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, alikuwepo wakati Mheshimiwa Ole-Sendeka anasoma taarifa hiyo na Maazimio ya Bunge Serikali iliyapokea, lakini katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu haikueleza chochote kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge hasa ya Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka...

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa taarifa Msemaji wa Kambi ya Upinzani; suala hili kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba niseme tumeshalieleza na tumeshatoa taarifa kwenye Bunge. Kila Wizara ya kisekta itakapokuja, itatoa ufafanuzi wa maagizo yote ya Bunge yaliyotolewa kuhusiana na taarifa hiyo ya Kamati Teule.

Kwa hiyo, naomba tu msomaji apate hiyo taarifa na tulilisema pia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tumetoa maelezo hapa Bungeni. Kwa hiyo, naomba Watanzania wafahamu hivyo na Wizara hizo zitakapokuja, hayo yote yatatokea kwa sababu hii Serikali ni moja na tunafanya kazi kwa umoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu anagawa kazi kwa Mawaziri wake kulingana na utaratibu unavyotakiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kimwanga, unaruhusiwa kuendelea.

MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA (K.N.Y. MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni alikuwepo wakati Mheshimiwa Ole-Sendeka anasoma taarifa hiyo na maazimio ya Bunge na Serikali iliyapokea. Lakini katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu haikueleza chochote kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge hasa ya Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka iliyohusu kutoa suluhisho la migogoro ambayo inaendelea nchini kote kwa sasa. Mfano Kiteto, Mvomero, Kilosa Rufuji, Mahenge, maeneo ya Jimbo la Morogoro Kusini na Morogoro Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi inaposema, Serikali ya CCM imechoka ni kutokana na kushindwa kutekeleza yale yaliyokwisha fanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wamesikia wafugaji wa asili wanavyoitwa kuwa ni wachungaji na ili mifugo yao iwanufaishe, ni lazima wapunguze mifugo ili wawe wafugaji. Hii ni aina mojawapo ya udhalilishaji kwa wafugaji wetu wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kashfa hii inatokana na ukweli kwamba hawaelewi ukweli kuhusu mifugo ya asili. Mifugo kwao ni utajiri ni sawa na kumwambia mkulima apunguze ukubwa wa shamba lake la Pamba, Kahawa au Korosho. Aidha ni sawa na kumwambia mwenye fedha zake Benki apunguze fedha zake.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema mifugo inaonekana ni mingi kwa sababu ya Serikali imeuza maeneo mengi ya malisho ndiyo sababu yale machache yaliyobaki yanagombaniwa na makundi mengi ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake, Sekta nzima ya Mifugo ina matatizo mengi ambayo tayari ufumbuzi wake ni wa kiutendaji na kibajeti, lakini Serikali ya CCM imeshindwa kuwa na vipaumbele katika kutekeleza ushauri wa kitaalam ulio kwenye makabrasha na pia kutoka kwa wadau ambao wapo katika mazingira halisi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna changamoto katika Sekta ya Mifugo hata moja ambayo haijulikani, au ni mpya na tayari tafiti zimekwishafanyika. Tatizo mara zote ni utekelezaji wa suluhisho la changamoto hizo. Hivyo basi, kwa kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kusimamia na kutekeleza yale yote ambayo imejipangia katika Mpango wake wa Maendeleo kwenye sekta hii, basi waondoke nao waone ni kwa vipi Serikali itakayoundwa na vyama vinavyounda UKAWA itakavyotatua changamoto hizo kwa wahusika wadau wa sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira kwa zaidi ya watu 177,527 na takriban watu milioni nne wanaendesha maisha yao kwa kutegemea Sekta hii ya Uvuvi. Kwa wastani, kati ya 2004 hadi 2010 mauzo ya nje ya samaki na bidhaa za samaki yaliingizia nchi yetu wastani wa dola za Kimarekani milioni 195.17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ni sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lische, kipato na kuingizia nchi fedha yetu fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu wake bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni sekta ambayo haihitaji uwekezaji mkubwa kama unaohitajikakwa sekta nyingine kama vile Sekta ya Madini na Sekta ya Kilimo. Hii inatokana na ukweli kwamba Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na eneo kubwa sana la maji ambao ndiyo sehemu ya kuvuna samaki. Suala ni kuweka mazingira mazuri ya kuvuna samaki hao, badala yake tunashindwa kuvuna, wanavuna watu wa nje na samaki zinazotumika zinaingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji na matumizi ya samaki soko la ndani na la nje bado ni makubwa sana, kiasi kwamba bado samaki wanaovuliwa hawatoshelizi. Bahari Kuu tunayoimiliki bado ina samaki wengi ambao kutokana na uwezo wetu mdogo wa kiteknolojia, hatujawahi kuwavua samaki wengi waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali kuangalia ni jinsi gani wavuvi katika Ziwa Victoria hasa maeneo ya Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera pale wavuvi wanapotoka eneo

la Wilaya moja na kwenda lingine wanatakiwa kulipia leseni wakati tayari leseni wamekata katika Wilaya nyingine.

Mfano, ukiwa Kisiwa cha Bezi Wilaya ya Ilemela unaiona Wilaya ya Ukerewe na Magu, lakini ukifika visiwa hivyo tu, ni lazima ukate leseni upya. Haya ni maajabu. Hili ni tatizo na ni mgogoro, hata ufumbuzi wa hili mmeshindwa kulitolea uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imehoji mara nyingi, pale nyavu zenye matundu madogo zinapokamatwa na kuchomwa moto, ni utaratibu gani unatumika kuwafidia nyavu ambazo zinahitajika kwa uvuvi? Hadi leo hatujawahi kujibiwa.

Aidha, tuliuliza samaki aina ya dagaa na dagaa-mchele wanavuliwa na nyavu za aina gani? Hatukupata majibu hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Serikali ya CCM mmechoka na huu ni muda muafaka wa kukaa pembeni na kuona sekta hii itakavyoongeza mchango katika pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikihamasisha Watanzania kujihusisha na ufugaji wa samaki hasa sato. Wananchi wengi wamehamasika katika ufugaji huo wa samaki. Vituo vya kuzalishia vifaranga vya Ruhira (Songea) Kingolwira (Morogoro), Mwamapuli (Tabora) na Nyengedi (Lindi). Vituo hivi vyote samaki wazazi wamechukuliwa kutoka Ziwa Viktoria lakini hawakufanyiwa utafiti wa kina ili kupata samaki wazazi kwa kutoa vifaranga wenye sifa za kuuzwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika ni kwamba samaki wazazi wanatolewa Ziwa Victoria na kupelekwa maeneo tajwa hapo awali kwa kuwa ndiyo samaki wazazi. Hili ni tatizo kubwa linalowatia hasara kubwa wananchi wanaofuga samaki, kwani vifaranga hao wanakuja kudumaa na wanaweza kufugwa hadi miaka miwili lakini hawaongezeki uzito licha ya kulishwa chakula chenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara haina mbegu bora ya kuzalishia vifaranga wa Samaki ambayo vimefanyiwa utafiti wa kutosha ili kujiridhisha, lakini inafanya usanii wa hali ya juu kwa kutumia mashamba ya wafugaji kuwa ni sehemu yake. Pia ni kwanini inafanya uhamasishaji kwa Watanzania kufuga samaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja hii wananchi wanatakiwa wapate majibu. TAFIRI wamefanya nini ili kuhakikisha wananchi wanafuga samaki kwa biashara kama ambavyo wanafuga kuku wa nyama au kuku wa kutaga mayai?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina urefu wa ukanda wa uvuvi wa baharini unaokaribia kufikia 1,450 kilometa na ukubwa wa eneo la bahari kuu. Bahari ya Hindi ni takriban kilomita za mraba 223,000 zenye uwezo wa kuzalisha samaki 730,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fursa ambazo zipo katika uvuvi wa baharini, kwa miaka yote Kambi Rasmi ya Upinzani toka mwaka 2008 hadi sasa imejaribu kushauri kwa kuionesha ni jinsi gani ajira zaidi zinaweza kupatikana na jinsi gani fedha za kigeni zitaweza kuingizwa. Sasa tunaambiwa kuna bandari ndogo tatu za uvuvi za Kilwa, Rufiji na Mafia na tayari zinatumika. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata maelezo, hizo bandari zinazosemwa ni kwa ajili ya masuala ya ngalawa? Katika bandari hizo ajira kiasi gani zimepatikana na wananchi wa maeneo hayo wamefaidika na lishe? Ukweli ni kwamba hakuna Bandari ya Uvuvi hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unaotunza maeneo ya Bahari ya Hindi katika Kisiwa cha Mafia sasa umekuwa kero kwa wakazi wa kisiwa hicho ambacho wananchi wake wanategemea uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa wananchi wa Mafia na maeneo mengine ya Pwani wanazuiwa kuvua au wanapangiwa mahali pa kuvua; wavue lini na watumie vifaa gani kuvulia, huku wakiambiwa kuwa maeneo hayo ni mpango wa kuhifadhi mazingira kwa uvuvi endelevu.

Maeneo ambayo wakazi wa Mafia wanazuiwa, yamekuwa yakitumika toka enzi za mababu zetu na yalikuwa tegemeo kubwa la wakazi hao kwa kitoweo na mapato na kwamba ni uzushi mtupu kudai kuwa mamlaka zinalenga kuhifadhi mazingira na mazalia ya samaki ili kuongeza kiasi cha samaki baharini na kuwezesha uvuvi endelevu kwa faida ya wananchi wa Kisiwa hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pepo za kusi na kasi ndizo pekee zilizowekwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kudhibiti ongezeko la samaki baharini. Zinapovuma za kusi wananchi hao huhamia kasi, vilevile zivumapo za kasi, huhamia kusi kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa samaki, mazao mengine ya baharini na uundaji vyombo vya baharini, mashua, boti, jahazi na vyombo vingine vya aina hiyo, ndizo kazi kuu Kisiwani. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na Mashirika ya Kiserikali na yasiyokuwa ya Kiserikali imeanzisha miradi mbalimbali visiwani humo kwa lengo la kuhifadhi fukwe na mazingira ya baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Serikali, lengo kuu la hatua hizo ni kuweka mazalia salama ya samaki ili kuongeza idadi ya samaki.

Hivi sasa tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwepo kasi ya kupungua kwa samaki katika ya kilometa za mraba 875 za Mafia, kilometa za mraba 822 zipo chini ya hifadhi ya mradi huo wa hifadhi. Umuhimu wa MIMP unaelezwa kutoishia kwenye hifadhi ya kutunza mazingira Visiwani humo, bali unayo manufaa kwa wakazi takribani 10,000 wanaoishi ndani ya mipaka ya eneo hilo lililo chini ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, sasa ni muda muafaka kwa Watanzania kukinyima dhamana Chama cha Mapinduzi (CCM) kuongoza Serikali kwani imeshindwa kutekeleza mambo yaliyo wazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa miaka takriban tisa ya Uongozi wa Serikali ya CCM ya awamu ya nne tumekuwa tukishauri sana kuhusiana na jinsi gani kama nchi, Sekta ya Mifugo na Uvuvi inavyotakiwa kuendeshwa. Lakini sikio la kufa ni la kufa tu, halisikii dawa. Fedha zinazopitishwa katika Bajeti, lakini hazitolewi na Serikali kwa ajili ya mipango inayopitishwa na Bunge. Hii inatokana na kuwa Serikali inakuwa na vipaumbele vyake ambavyo havipitishwi na Bunge, jambo hili linaonekana kama Bunge linafanya mchezo wa kuigiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani nawaomba Watanzania wote wenye mapenzi mema na nchi yetu, tujitokeze kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura na mwezi Oktoba tuing'oe CCM katika kuongoza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, Kuhusu Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa

Fedha 2015/2016

Kama ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA ROSE KAMILI SUKUM (MB), WIZARA YA MIFUGO NA MAENDELEO YA UVUVI, KUHUSU MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunitunza ili niweze kulitumikia taifa langu. Napenda kuishukuru familia yangu kwa msaaada mkubwa na uvumilivu hasa katika harakati na shughuli zangu za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii pia, kuwashukuru wataanzania wote kwa ujumla kwa kupokea na kulea harakati za mabadiliko nchini. Shukrani hizi za pekee ziwafikie wenyeviti wenza wa vyama vinavyounda UKAWA, Mhe. Prof Ibrahim Lipumba, Mhe Freeman Mbowe(KUB), Mhe. James Mbatia na Mhe. Dk Emanuel Makaidi. Vilevile, kwa makatibu wakuu viongozi wa UKAWA Mhe. Maalimu Seif Shariff Hamad, Mhe. Wilbroad Slaa, Mhe. Mosena Nyambabe na Mhe. Tozi Matwange.

Aidha, shukrani hizi ziende kwa timu ya wataalamu wa UKAWA, viongozi, watendaji, wanachama na wapenzi wa vyama vyetu vinavyounda UKAWA vya NLD, CUF, NCCR-Mageuzi na CHADEMA. Niwatake wanachama na wapenzi wa UKAWA kujipanga, kujituma na kujiandaa kushinda kwa kishindo na kushika dola katika Uchaguzi Mkuu wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Aidha, salaam zangu za pole kwa Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii, Rose Kamili Sukum ambaye yuko kwenye matibabu nchini India. Ugonjwa wake ni matokeo ya kikosi cha hujuma cha CCM cha GREEN Guards ambao walimvunja bega na Jeshi la Polisi linaelewa wahusika hao lakini hakuna hatua zozote za kisheria zimekwishachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee ziende kwa wabunge wote wa Kambi ya Upinzani Bungeni wanaounda UKAWA kwa kazi nzuri ya kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi. Na pia kwa watendaji wa Kambi ya Upinzani ambao wamekua msaaada mkubwa kwetu na kwa kazi yao nzuri kwa taifa letu.

2. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/15

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa kwa mwaka wa 2014/15, ilitengewa kiasi cha shilingi 24,752,405,000/- fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 22,529,800,000/- sawa na 91% ni fedha za ndani na shilingi 2,222,605,000/- sawa na 9% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi April, 2015 jumla ya shilingi 3,934,042,500/- zilitolewa na shilingi 2,636,529,190.31 zilitumika. Kati ya fedha zilizotolewa shilingi 3,393,457,500/- ni fedha za ndani na shilingi 540,585,000/- ni fedha za nje kwa ajili ya ASDP-L.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa kwa Wizara hadi mwezi wa nne ni asilimia 15.9 tu. Na fedha za ndani nazo ni asilimia 15.06 tu. Kwa fedha hizo je, ni kweli hapa kuna uwezekano wa kuendeleza sekta hii? Serikali inasema haina fedha lakini za kutoa kwa tapeli wa IPTL kwenye ESCROW Acc. Zinalipwa lakini kueleza kwenye miradi ya mifugo na uvuvi hazipo.

Mheshimiwa Spika, tunaposema kuwa Serikali ya CCM imechoka ipumzike waheshimiwa wabunge wanasema hatuoni yaliyofanyika, mara zote tajiri huwa aoni kuwa anafilisika hata kama akiambiwa ndio hayo yanayoikumba Serikali ya CCM. Imefilisika kiuongozi ikae pembeni ione jinsi sekta ya mifugo na uvuvi ilivyokuwa ni **mtambo** wa kuzalisha "**mahela**".

3. SEKTA YA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 pamoja na Mkakati wake wa mwaka 2010. Lengo kuu lilikuwa ni kuendeleza sekta hiyo kwa kuifanya sekta hiyo kuwa endelevu na ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, takwimu za wizara hiyo zinaonesha kuwa mchango wake katika pato la taifa halilingani na ukubwa wa sekta. Matatizo yanayoikabili sekta hii kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani, wadau mbalimbali na Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia sekta, kwa nyakati tofauti tumekuwa tunatoa ushauri kwa Serikali nini kifanyike.

Kwa kuwa sikio la kufa halisikii dawa imekuwa ikipuuza ushauri huu, sasa Kambi Rasmi ya Upinzani inasema mwaka huu ndio mwaka wa mwisho kwa wadau kushuhudia sekta hii ikishindwa kutoa kile kinachotarajiwa, tunawaomba wataanzania wote kwa umoja wetu kuiondoa Serikali ya CCM madarakani kwani inafanya kazi kwa mazoea, na Upinzani kwa mwavuli wa UKAWA kwa kushirikiana na wadau wote katika sekta hii tutasimamia yale yote ambayo tayari yapo kwenye makabrasha kwa maendeleo ya sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo la mahusiano ya kikazi kati ya Serikali Kuu, yaani Wizara ya Mifugo na TAMISEMI kwani mtu anayesimamia kilimo ndiye huyo anayesimamia mifugo kwa ngazi ya Wilaya na anaitwa "DALDO".

Kama afisa huyo amesomea kilimo maana yake kazi zake nyingi zitakuwa ni katika kilimo na mifugo itashindwa kuendelezwa. Huu ni udhaifu wa kimfumo. Ushauri kwa hili umetolewa mara nyingi lakini imeshindikana kupatiwa ufumbuzi, Serikali ya CCM imechoka na sasa ni muda wa kukaa pembeni.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema sasa tatizo hilo litatatuliwa pindi tu Serikali mpya ya Vyama vya Upinzani vitakapo ongoza Serikali.

3.1. MALISHO YA MIFUGO NA MIGOGORO YA WAFUGAJI, WAKULIMA NA WAWEKEZAJI

Mheshimiwa Spika, ni miaka mingi sasa Kambi Rasmi ya upinzani imekuwa ikieleza jinsi wanaojiita wawekezaji katika ranchi mbalimbali au maeneo mengine ambavyo wameshindwa kutumia ardhi hiyo na badala yake wanakodisha maeneo hayo kwa wafugaji. Mfano mzuri ni ranchi ya Kitengule ambayo karibu nusu yake amepewa Mwekezaji(Kagera Sugar) lakini haitumii yote na badala yake anawakodisha wafugaji.

Aidha, tulikwishaomba kupatiwa orodha ya majina ya wawekezaji wa Ranchi zilizo katika mkoa wa Kagera na ukubwa wa kila eneo la mwekezaji, lakini hadi leo orodha hiyo haijawahi kutolewa. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba, watazania hasa wafugaji matatizo yote yanayodumaza, sekta serikali inayaelewa na imekaa kimya kwa sababu watendaji wake waandamizi ni sehemu ya matatizo hayo, wanaogopana kuchukuliana hatua.

Hivyo basi, Serikali ijayo ya Upinzani itatoa suluhisho la matatizo hayo kwa kuwa utafiti wake wa kuyaondoa upo.

Mheshimiwa Spika, tumekwishaongelea pia jinsi waangalizi wa mapori ya akiba wanavyochukua fedha za wafugaji na kuruhusu mifugo kupata malisho katika maeneo hayo. Lakini fedha hizo zinaishia mifukoni mwao. Sio hilo tu mapori yaliyoko wilaya za Ngorongoro, Ngara na Biharamulo kuruhusu mifugo toka nchi jirani kuchungiwa humo na taarifa hizo Serikali inazo lakini hatua hazichukuliwi na wafugaji wetu wanakosa sehemu za kulishia mifugo yao na wengine wanaochungia maeneo hayo wanakamatwa na Wafugaji wengine wako magerezani bila sababu. Hoja ni rushwa ndio imetawala katika kupata malisho kwa wafugaji. Hivyo basi, tunawaomba wadau tushirikiane kuiondoa Serikali ya CCM madarakani kwa kutumia sanduku la kura na Vyama vinavyounda UKAWA mwakani turekebishe matatizo yaliyoota mizizi ya wafugaji kunyanyaswa kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ambayo ni kwa muda mrefu imekuwa ikiendelea na kusababisha madhara makubwa ya kupoteza uhai wa watu, madhara ya kiuchumi na wananchi kupoteza makazi yao, watoto kukosa haki yao ya kupata elimu.

Mheshimiwa Spika,matatizo haya yamekuwepo toka miaka ya themanini na utafiti wa kuyamaliza ulikwishafanyika na Serikali inaelewa vyema, kama hilo alitoshi Kamati teule ya Bunge iliyoongozwa na Mhe Ole Sendeka ilifanya utafiti wake na kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni, alikuwepo wakati Mhe Ole Sendeka anasoma taarifa hiyo na Maazimio ya Bunge Serikali iliyapokea, lakini katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu haikueleza chochote kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge hasa ya Kamati ya Mhe Ole Sendeka yaliyohusu kutoa suluhisho la migogoro ambayo inaendelea nchini kote kwa sasa. Mfano: Kiteto, Mvomero, kilosa, Rufiji, Mahenge, maeneo ya Jimbo la Morogoro Kusini na Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaposema Serikali ya CCM imechoka ni kutokana na kushindwa kutekeleza yale ambayo yaliyokwisha fanyiwa tafiti. Tunasema watazania tuiache Serikali iendeleo kulala na Serikali ijayo ya Vyama vinavyounda UKAWA kwa kushirikiana na wadau wote tutatekeleza yale yote yatakayopelekea kumaliza migogoro kati ya wakulima, wafugaji pamoja na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, watazania wamesikia wafugaji wa asili wanavyoitwa kuwa ni wachungaji na ili mifugo yao iwanufaishe ni lazima wapunguze mifugo ili wawe wafugaji. Hii ni aina mojawapo ya udhalilishaji kwa wafugaji wetu wa asili. Kashfa hii inatokana na ukweli kwamba hawaelewi ukweli kuhusu ufugaji wa asili, mifugo kwao ni utajiri ni sawa na kumwambia mkulima apunguze ukubwa wa shamba lake la Pamba, Kahawa, au Korosho.

Aidha ni sawa na kumwambia mwenye fedha zake Benki apunguze fedha zake. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema mifugo inaonekana ni mingi kwa sababu ya Serikali imeuza maeneo mengi ya malisho ndio sababu yale machache yaliyobaki yanagombaniwa na makundi mengi ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja kwamba ardhi nyingi inamilikiwa na vijiji hivyo ni jukumu la vijiji husika kutenga ardhi kwa ajili ya kilimo na mifugo. Ukweli ni kwamba kuna vijiji ambavyo vimesajiliwa kwamba ni vijiji vya wafugaji na vingine ni vijiji vya wakulima kwa mujibu wa sheria lakini bado kunatokea miingiliano inayoleta machafuko. Serikali inaelewa fika ni watu gani ndio chanzo cha kuvuruga utaratibu huo wa kisheria, lakini hatua hazichukuliwi, hii ni kutokana na kuchoka kwa Serikali ya CCM kuongoza. Ni muda mwafaka sasa kwa VYAMA VYA UPINZANI VINAVYOUNDA UKAWA kuongoza Serikali. Kama kijiji tayari kina usajili na hati, MKURABITA utakuwa ni kazi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, sekta nzima ya mifugo ina matatizo mengi ambayo tayari ufumbuzi wake ni wa kiutendaji na kibajeti lakini Serikali ya CCM imeshindwa kuwa na vipaumbele katika kutekeleza ushauri wa kitaalam ulio kwenye makabrasha na pia kutoka kwa wadau ambao wapo katika mazingira halisia katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hakuna changamoto katika sekta ya mifugo hata moja ambayo haijulikani au ni mpya na tayari tafiti zilikwishafanyika. Tatizo mara zote ni utekelezaji wa suluhisho la changamoto hizo.

Hivyo basi, kwa kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kusimamia na kutekeleza yale yote ambayo imejipangia katika Mpango wake wa Maendeleo kwenye sekta hii, basi waondoke nao waone ni kwa vipi Serikali itakayoundwa na vyama vinavyounda UKAWA itakavyotatua changamoto hizo kwa kuwahusisha wadau wa sekta.

3.2. MASOKO YA MIFUGO NA MAZAO YA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa sana ushauri kuhusu minada ya mifugo ambayo inaambatana na machinjio yenye ubora kuwekwa maeneo ya wafugaji na vile vile kuweka vituo vya kukusanyia maziwa kwenye maeneo ya wafugaji. Hoja hii ni kilio cha miaka mingi cha asasi za kiraiazinazojihusisha na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, Tanzania imekuwa ikiagiza nyama ya kuku kutoka nje ya nchi bila ya kufikiria kwamba hapa nchi kuna wajasiria mali wengi ambao wanajihusisha na ufugaji wa Kuku wa nyama na mayai, na vile vile kuku wa Kienyeji. Mpango huo wa kuagiza nyama ya kuku toka nje unapelekea wafugaji wetu kuona kuwa ufugaji haulipi na hivyo ni hasara tupu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba hujuma hii itafika mwisho hapo mwezi Oktoba, kwani Serikali mpya itakayokuwa chini ya Vyama vinavyounda ushirikiano wa UKAWA itamaliza hujuma hizo na kuweka mazingira mazuri ya tasnia hiyo kuweza kuchangia katika pato la taifa pia.

4. SEKTA YA UVUVI

Mheshimiwa Spika, Sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa zaidi ya watu 177,527 na takriban watu milioni 4 wanaendesha maisha yao kwa kutegemea sekta hii ya uvuvi. Kwa wastani, kati ya 2004 hadi 2010 mauzo ya nje ya samaki na bidhaa za samaki yaliingizia nchi yetu wastani wa dola za kimarekani milioni 195.17⁴.

¹investment opportunities in the fisheries industry, December, 2011

Mheshimiwa Spika, uvuvi ni sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingizia nchi fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu wake bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali, ambazo sekta inakabiliwa nazo

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi ni sekta ambayo haihitaji uwekezaji mkubwa kama unaohitajikakwa sekta zingine kama vile sekta ya madini, na sekta ya kilimo. Hii inatokana na ukweli kwamba Mwenyezi Mungu ametujali kuwa na eneo kubwa sana la maji ambao ndio sehemu ya kuvuna samaki. Suala ni kuweka mazingira mazuri ya kuvuna samaki hao, badala yake tunashindwa kuvuna wanavuna watu wa nje na samaki zinazotumika zinaingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mahitaji na matumizi ya samaki kwa soko la ndani na la nje bado ni makubwa sana, kiasi kwamba bado samaki wanaovuliwa hawatoshelezi; bahari kuu tunayoimiliki bado ina samaki wengi ambao kutokana na uwezo wetu mdogo kiteknolojia hatujaweza kuvua samaki wengi waliopo.

Mheshimiwa Spika, tumeitaka Serikali kuangalia ni jinsi gani wavuvi katika ziwa victoria hasa maeneo ya mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera pale wavuvi wanapotoka eneo la wilaya moja na kwenda lingine wanatakiwa kulipia leseni wakati tayari leseni wamekata katika wilaya nyingine.

Mfano; ukiwa kisiwa cha Bezi wilaya ya Ilemela unaiona wilaya ya Ukerewe na Magu lakini ukifika visiwa hivyo tu, ni lazima ukate leseni upya. Haya ni maajabu. Hili ni tatizo na ni mgogoro, hata ufumbuzi wa hili mmeshindwa kulitolea uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imehoji mara nyingi kwanini pale nyavu zenye matundu madogo zinapokamatwa na kuchomwa moto, ni utaratibu gani unatumika kuwafidia nyavu ambazo zinahitajika kwa uvuvi? Hadi leo hatujawahi kujibiwa. Aidha, tuliuliza samaki aina ya dagaa na dagaa-mchele wanavuliwa na nyavu za aina gani? Hatukupata majibu hadi leo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Serikali ya CCM imechoka na huu ni muda mwafaka wa kukaa pembeni na kuona sekta hii itakavyoongeza mchango katika pato la taifa.

5. UFUGAJI WA SAMAKI BILA UTAFITI WA MBEGU BORA

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihamasisha watanzania kujihusisha na ufugaji wa samaki hasa SATO. Wananchi wengi wamehamasika katika ufugaji huo wa samaki. Vituo vya kuzalishia vifarangavya Luhira(Songea),Kingolwira(Morogoro), Mwamapuli(Tabora) na Nyengedi (Lindi).

Vituo hivi vyote samaki wazazi (Parent stock) wamechukuliwa kutoka ziwa Viktoria lakini hawakufanyiwa utafiti wa kina (**cross cross breeding**) ili kupata samaki wazazi kwa kutoa vifaranga wenye sifa za kuuzwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika ni kwamba samaki wazazi wanatolewa ziwa victoria na kupelekwa maeneo tajwa hapo awali na kuwa ndio samaki wazazi. Hili ni tatizo kubwa linalowatia hasara kubwa wananchi wanaofuga samaki kwani vifaranga hao wanakuja kudumaa na wanaweza kufugwa hadi miaka miwili lakini hawaongezeki uzito licha ya kulishwa chakula chenye ubora.

Mheshimiwa Spika, Kama Wizara haina mbegu bora ya kuzalisha vifaranga wa Samaki ambayo imefanyiwa utafiti wa kutosha ili kujiridhisha, lakini inafanya usanii wa hali ya juu kwa kutumia mashamba ya wafugaji kuwa ni sehemu yake. Na pia ni kwanini inafanya uhamasishaji kwa watazania kufuga samaki.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja hii wananchi wanatakiwa wapate majibu TAFIRI wamefanya nini ili kuhakikisha wananchi wanafuga samaki kwa biashara kama ambavyo wanafuga kuku wa nyama au kuku wa kutaga mayai.

6. FURSA KWA UVUVI WA BAHARINI

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina urefu wa ukanda wa uvuvi wa baharini unaokadiriwa kufikia 1,450km na ukubwa wa eneo la bahari kuu - Bahari ya Hindi ni takriban kilomita za mraba 223 000 zenye uwezo wa kuzalisha samaki tani 730, 000⁵

Mheshimiwa Spika, kuhusu fursa ambazo zipo katika uvuvi wa baharini, kwa miaka yote Kambi Rasmi ya Upinzani toka mwaka 2008 hadi sasa imejaribu kushauri kwa kuonesha ni jinsi gani ajira zaidi zinaweza kupatikana na jinsi gani fedha za kigeni zitaweza kuingizwa. Sasa tunaambiwa kuna bandari ndogo tatu za uvuvi za Kilwa, Rufiji na Mafia na tayari zinatumiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata maelezo hizo bandari zinazosemwa ni kwa ajili ya mashua au ngalawa, na katika bandari hizo ajira kiasi gani zimepatikana, na wananchi wa maeneo hayo wamefaidika je na lishe? Ukweli ni kwamba hakuna bandari ya Uvuvi (**Fish Processing port**) hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, mradi unaotunza maeneo ya Bahari ya Hindi katika kisiwa cha Mafia (Mafia Island Marine Park - MIMP), sasa umekuwa kero kwa wakazi wa kisiwa hicho, ambacho wananchi wake wanategemea uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Hivi sasa, wananchi wa Mafia na maeneo mengine ya pwani, wanazuiwa kuvua; au wanapangiwa mahali pakuvua; wavue lini na watumie vifaa gani kuvulia huku wakiambiwa kuwa maeneo hayo ni mpango wa kuhifadhi mazingira kwa uvuvi endelevu.

Maeneo ambayo wakazi wa Mafia wanazuiwa yamekuwa yakitumiwa toka enzi za mababu zetu na yalikuwa tegemeo kubwa la wakazi hao kwa kitoweo na mapato na kwamba ni uzushi mtupu kudai kuwa mamlaka zinalenga kuhifadhi mazingira na mazalia ya samaki ili kuongeza kiasi cha samaki

baharini na kuwezesha uvuvi endelevu kwa faida ya wananchi wa Kisiwa hicho.

Mheshimiwa Spika, Pepo za Kusi na Kasi ndizo pekee zilizowekwa na Mungu kwa ajili ya kudhibiti ongezeko la samaki baharini. Zinapovuma za kusi, wananchi hao huhamia Kasi, vilevile zivumapo za Kasi, huhamia Kusi kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu.

Uvuvi wa samaki, mazao mengine ya baharini na uundaji vyombo vya baharini – mashua, boti, jahazi na vyombo vingine vya aina hiyo, ndizo kazi kuu kisiwani. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na mashirika ya kiserikali na yasiyokuwa ya kiserikali imeanzisha miradi mbalimbali visiwani humo kwa lengo la kuhifadhi fukwe na mazingira ya baharini.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa serikali, lengo kuu la hatua hizo ni kuweka mazalia salama ya samaki, ili kuongeza idadi ya samaki. Hivi sasa tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwepo kasi ya kupungua kwa samaki.

Kati ya kilometa za mraba 875 za Mafia, kilometa za mraba 822 zipo chini ya hifadhi ya mradi huo wa hifadhi. Umuhimu wa MIMP unaelezwa kutoishia kwenye hifadhi na kutunza mazingira visiwani humo, bali unayo manufaa kwa wakazi takribani 10,000 wanaoishi ndani ya mipaka ya eneo hilo lililo chini ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema sasa ni muda mwafaka kwa watanzania kukinyima dhamana chama cha mapinduzi (CCM) kuongoza Serikali kwani imeshindwa kutekeleza mambo yaliyo wazi kabisa.

7. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa miaka takriban tisa ya Uongozi wa Serikali ya CCM WA awamu ya nne tumekuwa tukishauri sana kuhusiana na jinsi gani Kama nchi sekta ya Mifugo na Uvuvi inavyotakiwa kuendeshwa, lakini sikio la kufa ni la kufa tu halisikii dawa. Fedha zinazopitishwa katika Bajeti lakini hazitolewi na Serikali kwa ajili ya mipango inayopitishwa na Bunge. Hii inatokana na kuwa Serikali inakuwa na vipaumbele vyake ambavyo havipitishwi na Bunge, jambo hili linaonekana kama Bunge linafanya mchezo wa kuigiza.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani nawaomba watanzania wote wenye mapenzi mema na nchi yetu tujitokeze kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na mwezi Oktoba tuing'oe CCM katika kuongoza Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha,

Mkiwa Adam Kimwanga(Mb)
K.n.y. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-
Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.
20.05.2015

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 64(2) (a). Kanuni hiyo ya 62 inamfanya Mbunge asimame na kuelezea utaratibu uliojunjwa na Kanuni hiyo ndogo ya (a) inaonya kuhusu Mbunge ambaye

anazungumza pamoja na uhuru wa majadiliano, hatatakiwa ndani ya Bunge kutoa taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana dada yangu Mheshimiwa Mkiwa. Nilisimama hapa kusema kwamba, katika hii hotuba yake ukurasa ule wa saba anapotuhumu kwamba Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni na alikuwepo wakati Mheshimiwa Ole-Sendeka anatoa taarifa ya Maazimio ya Bunge. Lakini Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu haikueleza chochote kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka kuhusu Kiteto, Mvomero na Maeneo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hiyo inayokutaka wewe unayesimama kuonyesha kwamba Mbunge aliyekuwa anasema analidaganya Bunge hili, inatakiwa wewe uthibitisha kwamba kweli Mbunge yule alikuwa analidaganya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu naona sasa katika hotuba hizi za Upinzani, *trend* tunayoendelea nayo, zinakuja hotuba ambazo zinadaganya Bunge na Watanzania wote.

Sasa tusiposimama na kuwaambia Watanzania kwamba hawa wenzetu wamekuwa wakitumia uwanja huu wa Bunge kuwadaganya tu Watanzania kwa sababu tu Watanzania wanawasikia, kwa hiyo, wanaweza kuamini; sasa nataka kueleza hapa Watanzania kwamba, Msemaji huyu alikuwa anadaganya hapa. Haya aliyoyasema hayakuwa ya kweli. Amewadaganya Watanzania, amelidaganya Bunge kwa kutumia tu nafasi hii aliyopewa ya kusema hapa. Nita-*quote* hotuba ya Waziri Mkuu kuthibitisha kwamba alikuwa anasema uongo na niliposimama, nilikuwa sahihi kumwambia anadaganya Bunge na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema hivi; "Mheshimiwa Spika, Serikali imeendeleza juhudi za kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi hususan baina ya wakulima na wafugaji na maeneo ya hifadhi kwa kuwezesha zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika vijiji vya Halmashauri awamu kwa awamu. Halmashauri zilizohusishwa kwa awamu ya kwanza ni Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto Mipaka ya Vijiji vyote imepimwa ikijumuisha vijiji vilivyokuwa kitovu cha migogoro ya ardhi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu anaendelea, kazi iliyobaki kwa Serikali kujiridhisha na usahihi wa upimaji huo na kutoa maelekezo stahiki kabla ya zoezi hilo kuanza katika Halmashauri ya Mvomero." Haya ndiyo yalikuwa maagizo ya Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako, katika hali ya namna hii, hapa watu wanakuja kuwasilisha Kambi ya Upinzani ambayo eti ndiyo Serikali ambayo injiandaa kuchukua nchi, lakini wanaanza mikakati ya kuchukua nchi kwa kudaganya Watanzania, kueleza mambo ambayo siyo ya ukweli na ukweli uko. Tena hii Hotuba ya Waziri Mkuu wala haijapita hata wiki mbili toka imesomwa na watu wameshasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sitaki haya maneno wayatoe, acha tu zibaki kumbukumu za uongo na ukweli. Mwongozo wako tu, jaribu kuwaongoza wawe watilivu, wajue kwamba tuko makini na wala haya tunayoyapanga na kuyasema hatubahatishi na ukweli wa jambo hilo nimeusoma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe Mwongozo wako sasa utaona: Je haya niliyosema mimi na aliyoyasema Mheshimiwa Kimwanga yako sahihi? Kama hayako sahihi, utaona tu unatuongoza nini. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiwanga!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namheshimu sana dada yangu Jenista na...

MBUNGE FULANI: *(Aliiongea nje ya microphone)*

MHE. MKIWA A. KIMWANGA - K.N.Y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Tulia kama unanyolewa wewe!

MWENYEKITI: Unajua unaongea na Kiti! Mheshimiwa Kimwanga ongea na Mwenyekiti!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA - K.N.Y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Ndiyo naongea na kiti, lakini pia na huyo wa pembeni lazima nimpe vilevile dawa, ameze taratibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Azimio la Bunge lilielekeza nini cha kufanya na migogoro ya ardhi ya wakulima na wafugaji ilikuwa nchi nzima, lakini aliyoyaongea Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *speech* yake ni utendaji wa Serikali. Kwa muda wote waliopewa, haya Mheshimiwa anatuambia kwamba wamefanya Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi mpaka leo Kiteto haijatulia! Ni kipi kilichofanyika? Ukweli ni kwamba Azimio la Bunge halijatendewa haki na Waziri anapaswa kuishauri Serikali itendee haki Azimio la Bunge. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa Kiti ndiyo kilichoombwa mwongozo, kwa hiyo, mwongozo wangu nitautoa baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na wachangiaji, naanza na Mbunge wa Jimbo la Kiteto Benedict Nangoro!

MHE. BENEDICT N. OLE- NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam kwa jitihada nyingi wanazofanya kujaribu kuleta mapinduzi katika sekta hizi mbili muhimu zilizoko kwenye Wizara hii, maana mifugo na Uvuvi ni sekta kubwa na kwa kweli zote zina *potential* ya kuleta mabadiliko makubwa katika maisha ya Watanzania. Moja, zikisimamiwa vizuri kama sekta mbili muhimu lakini kama fedha za kutosha zitawekwa kwa ajili ya kutekeleza yale yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hizi mbili zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa rasilimali watu, rasilimali fedha, rasilimali vifaa. Maana ukitazama Bajeti inayopendekezwa ya Shilingi bilioni 68.8 bado ni kiasi kidogo mno ukilinganisha ukubwa wa sekta hizi mbili na ukilinganisha ukubwa wa nchi lakini pia gharama zinazotakiwa katika kuendeleza hizi sekta. Napendekeza tu kwamba sasa imekuwa ni jadi kwamba Wizara hii, kila mara inapata fedha kidogo kiasi cha kuwafunga mikono washindwe kutekeleza hata yale yaliyopangwa.

Kwa upande wa rasimali watu, Mheshimiwa Waziri ametupa takwimu kwamba ukichukua kwa mfano Sekta ya Uvuvi anatarajia kuwa na wataalam 664 lakini wanaohitajika ni

16,000. Unaweza ukaona kwamba uhaba ni mkubwa. Lakini ukija pia kwenye hiyo ya mifugo, kuwapata wataalam wa ugani 8,541 kati ya 17,325 wanaotakiwa, bado kuna uhaba mkubwa wa rasilimali watu kwa upande huu wa ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwa waganga mdaktari wa mifugo waliotajwa kwamba wamefikia 719, lakini ukichukua jumla tu ya mifugo yote, ukachanganya ng'ombe, mbuzi, Kondoo, kuku, unapata milioni 122.8.

Kwa hiyo, hii ina maana kwamba Daktari mmoja atakuwa ana kazi ya kutibu mifugo 170,515. Hata ufanye miujiza, hiki ni kitu kisichowezekana! Lakini kwa upande wa ng'ombe tu, madaktari hawa ina maana kwamba kila mmoja atatibu ng'ombe 35,000. Huu ni uhaba mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tu kwamba kwanza Serikali iwape Wizara hii *retention* ya asilimia 100 ili fedha hizi wanazotarajia kukusanya kwenye vyanzo vyao karibu shilingi bilioni 44, maana wametaja kwamba wanatazamia kukusanya shilingi bilioni 43.8 ibaki kufanya kazi ya kuendeleza hizi sekta mbili, bado hazitatoshwa, lakini angalau itasaidia kidogo kuwapa uwezo wa kufanya mambo mengi kidogo kuliko yale yatakayofanywa kwa shilingi bilioni 68.8. Wizara ndiyo ina sera ambayo imewekwa vizuri ya 2006, lakini pia mikakati ipo kwa sekta zote mbili. Kuna mkakati kwa Sekta ya Uvuvi na kuna makakati wa Sekta ya Mifugo na sekta zote mbili zina programu zake ambazo zimeandaliwa za miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua kama kwa mfano hii ya mifugo yenyewe, kwa mwaka wa kwanza zinahitajika shilingi trilioni 1.3. Kwa hiyo, ukilinganisha kinachopatikana na kinachohitajika ili kutekeleza kile kilichopangwa, maana yake ni mawili; bajeti ikibaki kwa sura hii, kitakachofanyika ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu pamoja na uhaba wa rasilimali fedha, watu na vifaa, mkazo uwekwe zaidi katika maeneo machache. Eneo la kwanza ni hili la kuhakikisha kwamba chanjo zinapatikana kwa mifugo ya aina yoyote ili tatizo la magonjwa lipungue kama siyo kwisha, kwa sababu hatutaweza kunufaika na hizi sekta kama mauzo kwenye masoko ya ndani na nje. Haya yanaweza yakakwazwa na ugonjwa wa mifugo, tusipoweza kumaliza magonjwa haya kwa mfano, *CBPP* na magonjwa mengine, mfano mdondo kwa upande wa kuku. Haya ni matatizo makubwa. Lakini kwa uwekezaji huu, hatutaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la pili ni la miundombinu ya kuendeleza mifugo kwa aina zote. Napendekeza kwamba Serikali ifikie mahali waunde *crew* maalumu kwa ajili ya miundombinu ya mifugo. Maana tukiendelea kutegemea sekta nyingine pamoja na sekta ya binafsi, hatutakwenda mbali. Kiasi cha majosho kinachotakiwa, minanda, *centers* hizi za *veterinary*; lakini siyo hilo tu, majosho, mabwawa, hatutaweza kutekeleza nadhani kwa sura tunayoenda nayo. Tukibaki katika sura hii, maana yake hatutaweza kufikia azma ya kuleta mapinduzi katika Sekta ya Kilimo na katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua mamlaka ya uvuvi bahari kuu, ndiyo, ni sekta kubwa, lakini idadi ya watu waliopo pale Zanzibar kwenye Makao Makuu ya Mamlaka ni ndogo mno, hawawezi kufanya kazi zinazotarajiwa zifanywe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, napendekeza tu pia kwamba Serikali iwezeshe Wizara kuanza mfuko wake, sana sana kwa ajili ya kujazia kile kinachopatikana kwa ajili ya miundombinu ya kuendeleza malisho na pia miundombinu ya uvuvi na kadhalika. Kwa sababu bila mfuko, hakuna kitakachowezekana na uvuvi unaweza ukawa na namna yake ya kujichangisha na kuwa na tozo, lakini ukawa na mfuko wa kutunisha Sekta ya Uvuvi. Mifugo pia ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba mifuko hii ianzishwe kwa mfumo kama ule wa Mfuko wa Barabara, kwa sababu mapinduzi na mafanikio yaliyotokea katika Sekta ya Barabara ni kwa sababu ya kuwa na TANROAD na kwa sababu ya kuwa na mfuko wa kutekeleza shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Vyuo vya Mifugo na Uvuvi, idadi ya watu wanaokwenda ni ndogo na kwa kweli hatutaweza kupiga hatua kubwa bila kuhakikisha kwamba tunawafundisha watalaamu wa ugani wa kutosha na Madaktari ili huduma hizi za mifugo na uvuvi ziweze kupatikana kwa idadi inayotakiwa. Maana kwenye kila kona watu wanahitaji huduma, lakini huduma hizi ni shida kupatikana kwa sababu ya uhaba wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa sana suala zima la migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Naiomba Wizara na Serikali, kipaumbele na rasilimali za kutosha zitolewe hasa kwa ajili ya kuendeleza nyanda za malisho; maana kuendeleza nyanda za malisho ni pamoja na kuwa na mkakati maalum wa kupambana na mbung'o, kupambana na kupe, kwa sababu magonjwa mengi ya mifugo yanaletwa hasa na kupe pamoja na mbung'o. Lakini bila kujenga mabwawa ya kutosha na kuwa na vyanzo vingine vya maji, hata maeneo ambayo yangefaa kwa kulishia, hayatatumika bila kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake unakuta kwamba maeneo yale yenye vyanzo vya maji vichache, vinaishia kuwakusanya watu waofanya shughuli zote. Kwa hiyo, unakuta mkusanyiko wa watu na mifugo unakuwepo kwenye maeneo machache ya *concentration*, kwa sababu ya maeneo mengine mengi kutoendelezwa na hapo ndipo panapokuwa kuna chimbuko la migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Naomba kwamba Serikali inue tu kufanya hili na Wizara ina wataalam; zaidi ya watu 300 ni *Ph.D holders* kwenye hiyo Wizara, lakini bila kupatiwa fedha na bila kupatiwa nyenzo, kisomo chao na idadi yao haitaleti mabadiliko na mapinduzi yanayotakiwa katika sekta hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nami naunga mkono pendekezo na ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu, iliyosema kwamba mapendekezo mawili yaliyotolewa na kamati ya teule, kama walivyotaja wengine, lakini pia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwamba maeneo mengine yabainishwe, yale ya hifadhi ambayo hayafai tena kuendelea kuitwa ni hifadhi, basi hayo yatolewe kwenye hifadhi na yawekwe kama sehemu ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii tunaweza tukapanua na kuendeleza maeneo ya malisho na mtawanyiko wa mifugo ukawa mkubwa zaidi ili kupunguza sokomoko katika maeneo ya uhaba wa malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipatia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa anayefuatia ni Mheshimiwa Lekule Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Koka, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum ajiandae na Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie bajeti ya Wizara hii. Napenda tu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyoandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisamehe niseme machache ya hali ambayo naiona hapa Bungeni. Ukiangalia hali ya nchi yetu haiendi vizuri, lakini kuna viashiria vingi vinavyokosesha nchi yetu amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hapa Bungeni, Wabunge tunaizungumzia nchi yetu kana kwamba siyo nchi yetu, kana kwamba ni nchi ya shida, kana kwamba ni watu walioko jehanamu, kana kwamba ni watu wanaonyanyaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wakisikia hali kama hii, kwa kweli watakata tamaa na wanaona kwamba Bunge hili ndiyo kichocheo kikubwa cha kusababisha amani ikosekane katika nchi hii. Kwa sababu kuonyesha chuki na dharau katika Bunge kama hili, itakuwa ni jambo ambalo ni kiashiria wananchi wasiamini Bunge hili na waone kwamba kuna vita kubwa iliyoko katika nchi hii. Sasa tunawaweka wananchi hofu.

Napenda kusema kwamba nchi hii ikikosa amani, hakuna chama chochote kitakachoweza kutawala nchi hii. Hata wewe uliyeko madarakani na anayetaka kuingia madarakani, wote mtapata shida na wananchi watapata shida kwa ajili ya vurugu zinazosababishwa katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kusema hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo na mchango wangu. Napenda kusema machache ambayo nayasemea kila wakati, lakini Serikali imekaa kimya, haijawahi kuyatendea kazi.

La kwanza, ni upimaji wa maeneo. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri katika jedwali la nane amebainisha maeneo ya malisho katika kila Wilaya. Sasa tunaomba maeneo hayo mliyobainisha, kwamba ni ya mifugo, basi muyaweke katika hati miliki ya kutambulika kwamba hilo eneo ni la wafugaji, ni eneo la malisho, wasiwekwe tena watu wengine, kama wakulima kuingia au kuwaweka tena wawekezaji katika maeneo yale. Nadhani hilo litapunguza matatizo ya migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine masoko. Masoko ya mifugo, kila hotuba ya Waziri inataja masoko ya mifuko, lakini masoko haya hayaonekani. Soko la Longido mlilolitaja leo ni miaka mitatu mnalitaja kwamba litajengwa, lakini hatuoni mwendelezo wa soko lile. Niwaambie, Halmashauri ya Kajado, pato lake kubwa ni la mifugo kutoka Tanzania. Wao ndio wanavuna na wanapata ushuru wa mifugo, lakini Tanzania hawapati na ng'ombe ni wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wanabeba mifugo kwa magari, wakifika karibu na Namanga, wanashusha ili mifugo watembeee kuvuka mpaka bila kupitishwa mpakani kwa magari. Kwa sababu hakuna utaratibu wowote Tanzania uliowekwa, mifugo kuvuka mipaka kama mazao mengine yanavyovushwa. Kwa hiyo, hakuna ushuru unaopatikana pale. Wakifika Kenya, ndiyo mifugo sasa inaanza kulipishwa ushuru. Naomba hili Serikali ilifanyie kazi, tupate utaratibu wa kuwa na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni viwanda vya nyama. Mwaka 2000, Serikali ilipitisha kwamba itajenga viwanda 10 vya nyama, kikiwemo kiwanda cha Shinyanga na Arusha. Lkini mpaka sasa tuko mwaka 2015, hakuna kiwanda chochote kilichojengwa. Naomba tu kuuliza, mnijibu baadaye kwamba nini kimeshindikana kujenga hivyo viwanda na ndiyo maana tumekuwa hatuna maeneo ya kuuza mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kuchimba mabwawa; ukiangalia, ingepaswa hizo fedha ziwe katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, lakini ziko katika Wizara nyingine ya Maji na Kilimo, lakini hizo fedha zinafanya shughuli nyingine, hakuna mabwawa yanayojengwa.

Sasa wewe Waziri unapotaja mabwawa katika Wizara yako ambayo hayana fedha, kwa nini unaweka kwanza kwenye Wizara yako? Kwamba mabwawa ya mifugo; na hauna fedha! Wizara nyingine ambayo ndiyo ina fedha haina hiyo mipango ya mabwawa. Sasa hapa ni tatizo kubwa. Naomba hili lirekebishwe. Fedha za mabwawa kwa ajili ya mifugo, zije katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mbegu bora. Hapa tunapata shida kwa sababu hakuna mbegu bora ya mifugo. Tunafuata mbegu bora ya mifugo Kenya, nami ni mnunuzi mkubwa sana wa mbegu bora za mifugo. Kwa sasa ukienda kununua dume mdogo, ni Shilingi milioni nne mpaka sita kwa ndama mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali yetu ingeturahisishia kutafuta mbegu bora ili tusiende tena kununua katika nchi jirani, nasi tuweze tukapata katika mashamba yetu. Tuna mashamba mengi na tuna watalaam kama alivyosema Mheshimiwa Ole-Nangoro kwamba tuna watalaam wa kutosha, hatuna shida ya wataalam, bali hawapewi fedha za kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mgogoro wa wafugaji na wakulima. Jamani Serikali sasa ione kwamba jambo hili italimaliza kwa sababu imeleta uhasama mkubwa, wananchi wetu wanauana, wanaharibu mali; hili tunaitegemea Serikali ione. Sijui sasa ni wananchi wangapi wanatakiwa wafe ili Serikali ione kwamba jambo hili ni zito! Mgogoro huu inawezekana kabisa kwisha, wakitenga maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna maeneo makubwa ambayo yanaitwa mapori tengefu, ukizunguka hata digidigi hayupo. Hakuna mnyama yoyote! Watu waliopo ni maaskari wanaozunguka kulinda eneo hilo ambalo halina wanyama. Naomba sasa maeneo hayo yabainishwe kama ni kuwapa wakulima, wapewe, kama ni kuwapa wafugaji wapewe, kuliko kuwaka maeneo ambayo hayana matumizi. Hakuna mnyama aliyeko pale, linalindwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru tena Wizara kwa hotuba yao nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ahmed, atafuatiwa na Mheshimiwa Koka.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia sasa hivi; Mheshimiwa Ole-Nangoro na Mheshimiwa Lekule Laizer kwa masuala mazima ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mifugo limechukua sura mpya Kitaifa. Ni tatizo kubwa sana baina ya wafugaji na wakulima. Naipongeza Kamati ya Mheshimiwa Sendeka pamoja na Waziri Mkuu mwenyewe. Wamesema vizuri, wameleta mapendekezo yao mazuri, lakini utekelezaji naona bado unasuasua. Lakini chanzo chake ni wafugaji wanaotoka kwenye maeneo ya mikoa ambayo wanafuga. Wafugaji wengi wanatoka Shinyanga, Mwanza, Manyara na maeneo mengine katika nchi hii. Ndiyo chanzo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakotoka kule, wanakwenda kutafuta maeneo mazuri ya malisho ya mifugo yao, wanakimbia kule kwenda huku, ndiyo chanzo. Sasa hivi tunakwenda kutatua tatizo, tunasema tuwatengee maeneo, hiyo ni *solution* moja; lakini *solution* ya pili ni

kutazama kwamba kwa nini wanakimbia? Tukawatengenezea maeneo yao, kule kule walikotoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga pale, hasa Jimbo la Solwa, wafugaji ni wengi tu! Matatizo ni makubwa. Mimi nina mfugaji mmoja anaitwa Mashiri, anatoka kwenye Kata ya Didia.

Katika *Operation Tokomeza*, alinyang'anywa ng'ombe zake 254 mpaka leo katika Mkoa wa Tabora, Kijiji cha Lumbe pale, Wilaya ya Kaliuwa. Tatizo ni kukimbia kutafuta maeneo mazuri ya malisho.

Kwanza kabisa naiomba Serikali, huyu mtu ameshitaki sana, amekwenda mpaka kwa Mheshimiwa Wasira, wakati ule alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, ameshitaki pale, ameleta malalamiko yake, Serikali kuu, Wizara ya Mambo ya Ndani, hajalipwa huyu mtu! Amenyang'anywa hivi hivi kwenye *Operation Tokomeza*, mpaka leo hajalipwa! Naiomba sana Serikali, kwanza katika hii taarifa ambayo Mheshimiwa Rais amepewa, uone ni namna gani uweze kumfikiria huyu mtu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni rasilimali kubwa sana. Katika Jimbo la Solwa, wafugaji na wakulima wanachukua asilimia kubwa tu, lakini mpaka sasa hivi ninavyokwambia sioni wafugaji wananufaika kwa namna ipi na rasilimali hizi. Shinyanga pale tuna kiwanda cha nyama, kuna mwekezaji alichukua, amejitahidi sana, lakini bado naona labda nataka kupewa msukumo kwa namna ambavyo aweze kuendelea katika suala zima la kuwa na kiwanda cha nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* ya wafugaji, tunaomba sana Serikali ilichukulie kwa umuhimu wake sana tu. Wafugaji hawa, pale katika Jimbo la Solwa Mkoa wa Shinyanga au nchi yote, wafugaji wakipata maeneo ya kufugia, wakitengewa maeneo yao mazuri, wakachimbiwa malambo yao, hawatakwenda kuhangaika.

Sasa hivi wanahangaika hangaika hivi na wafugaji asilimia kubwa ni Wasukuma. Sisi Wasukuma tunapata taabu sana! Wanadhaliika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mtwara kule wamefanya fujo kidogo tu, wamechukuliwa wamepelekwa *Thailand*, wamepelekwa wapi, Serikali yote imekwenda pale. Sisi tumekuwa na heshima tu, wala hatutaki kufanya fujo. Tukiamua kufanya mgomo wa wafugaji, tukasema hatuuzi nyama, mtalia! Kuna watu hapa hawalali bila kula nyama. Tukifanya mgomo tu wa kutokuuza nyama, nchi hii mtakuja kutubembeleza sana. (Kicheko)

MBUNGE FULANI: Hata hatuji! (Kicheko)

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine wanapenda kula nyama, tunapenda suala hili lishughulikiwe kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Serikali Kuu kuna ushuru ambao upo ndani ya sheria unaitwa *movement permit*. Kwa sisi pale kwa mwezi labda tunachangia shilingi milioni mbili. Kwa nini hizi fedha zisibaki? Serikali ibadilishe tu sheria kwamba hizi *movement permit*, ushuru kwa ajili ya kutolea mifugo, kutoa Shinyanga, Mwanza na mikoa mingine na kuleta Dar es Salaam au kutoa eneo fulani kwenda sehemu husika, zibaki kwenye Halmashauri ili ziweze kufanya kazi hii hii ya kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Tatizo hili angalau tuanzie kwa hatua hiyo. Tukishapata maeneo haya, hatua ya pili tutaendelea kuwahudumia vizuri wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu machinjio ya Tinde; Tinde pale mwaka wa juzi, 2014/2015 tuliomba shilingi milioni 200. Machinjio yale tumeshajenga. Tinde ni mji mkubwa sana unaoendelea na baada ya muda mrefu unaweza ukawa ni mji mkubwa tu na watu ni wengi. Sasa tumejenga machinjio haya; tuliomba fedha mwaka wa 2014 na tukaomba fedha mwaka huu 2015. Mheshimiwa Waziri hebu tusaidie hiyo shilingi milioni mia mbili tukamilishe ujenzi huu wa machinjio katika Kata hii ya Tinde. Nakuomba sana, hii imechukua muda mrefu, Tinde pale kuna mradi wa maji tunauendeleza; na sasa hivi tunataka tumalizie masuala haya ya machinjio na mengine ili tukamilishe mambo yote katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya nyama. Ukiwa na kiwanda kimoja hakisaidii. Huwezi kusema Wizara inasema tunatengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya viwanda wawekezaji waje. Kuna wawekezaji wanaweza wakaja wakaona hakuna ushirikiano mzuri. Ni jukumu la Wizara au Serikali au Wizara ya Nje au Balozi zilizoko nje ya nchi kutangaza wawekezaji wa Tanzania. Watanzania wenyewe kama hawatoshelizi waje kutoka nje, mwavutie waje. Kwa sababu ufugaji kama nilivyokwambia, katika ufugaji, kwenye Mkoa mzima wa Shinyanga kabla hatujagawanya mkoa kulikuwa na ng'ombe bilioni mbili na nusu. Lakini haichangii kabisa kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na viwanda zaidi ya viwili au vitatu, nadhani ufugaji utakuwa ni mzuri. Wafugaji watanufaika na rasilimali zao na vilevile Serikali itapata mapato na tatizo hili la wafugaji na wakulima na lenyewe litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina majosho 26 na Kata 26; ng'ombe ni zaidi ya 300,000 au 250,000. Bado tuna upungufu mkubwa sana. Vilevile tumeomba hizi fedha, mahitaji ni kama majosho 60 kwa kuanzia ili kuona namna gani ya kuweza kusaidia majosho yetu wafugaji waweze kufuga kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maafisa Ugani. Naomba Wizara ijue, katika Kata 26 vijiji 127 tuna Maafisa Ugani 38 tu. Sasa utaona kwamba hata kama Wizara mna mkakati wa namna yoyote ile, hata kama Serikali inataka kusaidia wafugaji, inafikaje kwa wafugaji kwa Maafisa ugani 38 tu? Haiwezi kufika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali ituongeze angalau Maafisa ugani wafike 100, pamoja na kuwapa nyenzo. Wanunulieni pikipiki hawa Maafisa ugani wa Kata waweze kuwafikia wafugaji kwa haraka. Miongozo, utaratibu, elimu kwa wafugaji itakuwa nzuri na matatizo yote yatakuwa yamekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, OCD katika kitengo hiki ni tatizo. Unaweza ukaongea na Afisa Mifugo ukaambiwa kuna tatizo fulani akakwambia hatuna hela ya mafuta, hatuna hela ya hivi. Wanashindwa! Hata Maafisa Mifugo wa Halmashauri na wenyewe wanapata tatizo la kwenda kwa wafugaji kwenye vijiji vyetu. Naomba sana kazi hii ishughulikiwe na hasa tatizo zima la migogoro ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga tuna ng'ombe wengi sana, lakini sioni wanunuzi wa ngozi na wala sioni masoko ya ngozi. Unasikia tu, masoko yako hapa, wanunuzi wanakuja, sijui wanafanya fanyaje. Ngozi na maziwa! Maziwa mengine mfano Kata ya Bukande kule ukienda Kata ya Mwakitolyo, ukienda kwenye Kata yenye wafugaji wengi, wengine maziwa wanakunywa, wanamwaga. Hawana masoko! Tuna ngozi nyingi, hatuna masoko. Hebu waambieni hao wanunuzi waje katika Jimbo la Solwa; tuna ngozi nyingi, tuna maziwa mengi, wayanunue ili sasa hata hawa wafugaji waweze kunufaika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, dakika zangu naona zimekwisha, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Koka, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Opolukwa ajiandae.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii. Naishukuru na kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya na kamwe niwaambie Watanzania Serikali hailali wala haichoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko macho na wala haijawahi kuchoka toka tulivyopata uhuru, iko macho na inafanya kazi yake vizuri, ndiyo maana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi tumejiwekea utaratibu wa muda wa uongozi na baada ya hapo wanakuja viongozi wengine wanaendelea kuchapa kazi kudhihirisha kwamba Watanzania wote Serikali ya Chama cha Mapinduzi iko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kibaha Mjini kwa kuniunga mkono, bila kumsahau mke wangu Selina na watoto kwa uvumilivu katika miaka yote ambayo nimekuwa nikiwatumikia wananchi wa Kibaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Nne, Mkutano wa Tano tarehe 15/6/2011 nilisimama hapa kuiomba Wizara hii nzuri kuwasaidia wananchi wangu wa Kata ya Pangani katika eneo linalojulikana kwa umaarufu wa eneo la mitamba; kwamba wananchi wengi walikuwa wanaishi ndani ya eneo hilo na nikaiomba Serikali itoe eneo hili kwa wananchi ili waweze kuishi kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, ilipokea ombi hili na mnamo tarehe 7/3/2012 kati ya zaidi ya ekari 27,000 Serikali ilikabidhi ekari nyingine na ilibaki na ekari 2,592 tu kwa ajili ya maendeleo ya shughuli zake za Chuo hicho cha Mitamba. Jambo hili lilipokelewa vizuri na wananchi na niko hapa kwa niaba yao kutoa shukrani za dhati katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia hii nzuri na utekelezaji huu mzuri wa Serikali bado kulijitokeza dosari moja kubwa ambayo leo nasimama hapa kwa niaba ya wananchi wangu kuiomba sasa Wizara imalize jambo hili ili kazi hii nzuri iliyofanyika iweze kuleta manufaa mazuri na wananchi wote waweze kufurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ekari 2,592 zilizobaki kuna eneo kwa maarufu linaitwa Vingunguti. Eneo hili lina ukubwa wa ekari 300 tu, ni eneo ambalo na lenyewe wananchi wameishi muda mrefu, na leo hii ninavyoongea na ninyi ni wanyonge, wamelalamika, wamekwenda karibu kila mahali kuanzia Wilayani, Mkoani kwenda kuiomba Serikali kwamba wao kwa nini katika jambo hili hawakufikiriwa na hatimaye bado wako katika eneo la Mtamba na wenyewe wameishi muda mrefu. Kama nilivyosema hapa, eneo hili kwa umaarufu linaitwa Vingunguti na unaweza ukaelewa maana ya Vingunguti ni kwamba kweli watu wako wengi, wanakaa na wanafanya shughuli zao kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa niaba ya wananchi hawa, namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali yetu, kwa ile nia nzuri waliyoifanya hata wakatoa zaidi ya ekari 23,000 kwa wananchi sasa, angalau wamege hizi ekari 300 ili wananchi hawa wajumuike na wenzao na wenyewe waweze kupata matunda ya Serikali yetu sikivu ambayo iliamua kutwaa maeneo haya yaliyobaki kwa ajili ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri tumeifanya, lakini ni sawa na baba aliyewapelekea watoto wake kumi zawadi akawapa watoto tisa na mmoja akamwacha. Kweli watoto wale tisa watafurahi, lakini watakapokaa pamoja na yule wa mwisho, watasikitika kuona pengine baba amefanya ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na wananchi hawa wamenituma kwamba wamsikie wazi Mheshimiwa Waziri akiwapa jawabu lililo na matumaini. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu, kwa kazi nzuri iliyoifanya, basi imalizie kwa kuhakikisha na wananchi hawa wanatolewa nje ya hilo eneo la Mitamba ili kusiwe na mgogoro wowote kati ya wananchi hawa na eneo hili la Mitamba kwa ajili ya maendeleo ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nizungumze kidogo kuhusu ubora wa nyama, lakini hata mifugo katika nchi yetu. Tunafahamu nchi yetu ni mojawapo ya nchi chache zilizoko Afrika zenye mifugo mingi na hususan ng'ombe. Ni jambo la kusikitisha kwamba nyama nyingi na hususan nyama ile ambayo ina thamani kubwa (*value added au processed meet*) nyingi bado inaingizwa nchini kutoka nche za nje. Hata mwingizaji mkubwa wa nyama hii ni jirani yetu Kenya. Hii ni kwa sababu hatujawa na mipango thabiti ya kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tunakubaliana kwamba njia pekee ya kusaidia na kupeleka uchumi chini kwa wakulima, wafugaji na kadhalika ni lazima tujenge utaratibu wa kuweza kuongeza thamani mazao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta hii ya Mifugo, bado hatujaweza kufanya hivyo. Kwanza kabisa aina ya ufugaji tunaoufanya inafanya hata wenye viwanda washindwe kupata nyama iliyo bora kwa ajili ya ku-process nyama yenye thamani kubwa (*prime meet*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukweli kwa sababu baadhi ya viwanda ambavyo wawekezaji wamewekeza wamefikia mahali wanalalamika kwamba hawapati mifugo iliyo bora kwa ajili ya kutengeneza nyama iliyo bora. Maana yake ni kwamba Wizara ina kazi ya kufanya, hasa kwa wafugaji, kuwasaidia ni namna gani watafuga mifugo yao kisasa ili kuhakikisha siku ya mwisho zao la nyama ya mifugo yao inakwenda kupata soko kubwa kwa kukubalika katika ku-process nyama na ili thamani ya nyama watayouza iendelee kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondokane na yale mawazo ya kupeleka nyama kule machinjioni Vingunguti na kwingineko kuchinja na kupeleka katika haya mabucha ya kawaida. Ndiyo maana siku zote bado thamani ya nyama kwa mfugaji inaendelea kuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ikubali angalau kusimamia vizuri na kuendelea kujenga viwanda hivi vya ku-process nyama. Hebu fikiria katika Jiji kubwa kama la Dar es Salaam, ukipita katika machinjio, natumaini ukifuata taratibu za afya wala huwezi kuthubutu kusema haya ni machinjio yanayohudumia wananchi. Ni wajibu sasa wa Serikali ifike mahali tukubaline twende kwenye *standard* na hususan kule ambako walaji wa nyama ni wengi kama Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda kilichojengwa pale Ruvu, huu ni mwaka wa tano wala hakijajulikana kitaisha lini. Sasa kile ni kiwanda ambacho kingeweza kusaidia kuchinja nyama kisasa na katika hali ya kiafya na ubora na usalama kwa ajili ya Miji ya Pwani pamoja na Kibaha, lakini toka kimewekewa jiwe la msingi na Mheshimiwa Rais ni zaidi ya miaka mitatu hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwamba kama kweli tunataka tuinue ufugaji, ni lazima tutengeneze utaratibu na miundombinu ya kuwasaidia wakulima wapate thamani ya

zao hili la mifugo ili wazidi kujikita katika ufugaji ulio bora wakitambua vyema siku ya mwisho wanaweza kupata faida na kuweza kuendelea kufuga vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuiomba Serikali, tumekaa hapa Bungeni kwa takriban sasa miaka mitano, lakini kila tunapokaa ni migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Nafahamu jitihada zinazoendelea, lakini naomba sasa tufike mahali tupate mwarobaini wa kudumu, tupate majawabu ya jambo hili na tuondokane nalo kwa maana linarudisha nyuma maendeleo ya mifugo na hata maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na ninawashukuru Watanzania wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Hamad Rashid akifuatiwa na Mheshimiwa Opolukwa na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla ajiandae.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwepo hapa tena leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yao ya wataalam kwa kazi ngumu wanayoifanya. Wanafanya kazi katika hali ngumu sana maana hawana rasilimali fedha na rasilimali watu pia ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba pamoja na matatizo waliyonayo, Wizara imejitahidi angalau kufanya utafiti wa hapa na pale. Ila ningeomba tu Wizara ingefanya jambo moja la busara zaidi. Wamefanya utafiti juu ya kujua idadi ya wavuvi, idadi ya vifaa vilivyoko na kadhalika, lakini hakuna utafiti uliofanywa kujua rasilimali zilizoko katika bahari na katika ziwa letu. Utafiti huo haujafanyika mpaka leo! Kwa maana hiyo, unaweza ukaongeza idadi ya wavuvi, idadi ya vyombo lakini kwa sababu hujui rasilimali, hatimaye utakuja kukuta watu wamewekeza lakini hawapati bidhaa inayotakiwa kwa sababu hakuna utafiti uliofanywa.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijitahidi kwanza kufanya utafiti juu ya rasilimali zilizoko katika bahari na zilizoko katika maziwa yetu, wakati huo huo ndiyo tunaweza tukapanga vifaa gani vinafaa kwenda kuvua. Hili halijafanyika mpaka leo.

Jambo la pili, nimeona hapa kuna viwanda vya maziwa, Mheshimiwa Waziri amesema uzalishaji wa maziwa ni mzuri na akasema viwanda vimefanya kazi vizuri. Lakini kwenye jedwali lake hapa kuna viwanda 82 na ukiangalia ni asilimia 26 tu ya uzalishaji. Sasa hili siyo jambo jema hata kidogo, ni lazima kuna tatizo la msingi kwamba viwanda vyote 82 uzalishaji asilimia 26, kuna tatizo kubwa la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri, Waziri hapa kwanza akatueleza tatizo ni nini, lakini nafikiri kuna tatizo la mahusiano baina ya wawekezaji na Serikali juu ya mambo mbalimbali ambayo yanatakiwa kutekelezwa. Kwa hiyo, jambo la kwanza namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze tatizo ni nini, kwamba lita laki sita zingezalishwa, lakini ni lita laki moja na kidogo tu ambazo zinazalishwa kutokana na matatizo ambayo yako viwandani ambayo Waziri katika hotuba yako hukuweza kuyaelezea. Hilo lilikuwa jambo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la uvuvi. Ukiangalia takwimu zako Mheshimiwa Waziri, utakuta zaidi mazao mengi yametokana na kwenye maziwa au maji baridi, lakini kwenye bahari kuu pengine ni asilimia 10 au 12 tu. Sasa hili siyo jambo jema hata kidogo. Ukiangalia ukanda mkubwa wa bahari tulionao ni kwamba bado hakujakaa *seriously* tukaangalia ni namna gani tutavuna rasilimali za bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kufurahisha, haya mazao madogo madogo yanaingiza fedha nyingi. Kwa mfano nimeona hapa kuna *crabs* wanaingiza fedha nyingi, *pronz* wanaingiza fedha nyingi ambao hawa kama *crabs* ni rahisi sana kufuga na ukavuna haraka sana. Sasa zile *quills* katika bahari zipo, haya mazao madogo madogo yanaingiza fedha haraka sana na inakuza ajira haraka sana. Nafikiri Serikali ingejielekeza huko, tungeweza tukapata ajira za haraka na mapato ya haraka sana. Ukiangalia *crabs* hapa, pesa wanazolingiza ni nyingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, nasikitika sana kwamba Serikali imejitahidi kupima haya maeneo ya wafugaji na imetoa orodha nzuri tu, kuna hekta 1,900,000, ni karibu 2,000,000, lakini ni kutoka mwaka 2014/2015. Sasa maeneo haya yameshapimwa, yamekaa, hayakuendelezwa. Ni dhahiri watatokea watu wengine watavamia, ama ni wafugaji au ni wakulima, au wawekezaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali inatengeneza *project* halafu haikamiliki, nalo ni tatizo la msingi. Kwa hiyo, migogoro haitatuki maisha! Kwa sababu hili ulilofikiria kama linaweza kutatua mgogoro, halitatui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Mheshimiwa Waziri angeeleza katika kupimwa huku ni wafugaji wangapi wangepaidika na *program* hii? Lakini haikuelezwa katika hii! Tungepima tungeaona ni hekta ngapi zipo hapa. Kwa kufanya hivi basi tumepunguza tatizo la aina fulani kwa kiasi fulani. *Data* hizo hazipo, nafikiri haitusaidii sana pamoja na kwamba Serikali imepima lakini watakaofaidika ni akina nani na kwa kiwango gani, tungepunguza tatizo. Hilo lingewezekana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano, ni suala la migogoro ya wakulima na wafugaji. Naona kuna tatizo moja la msingi. Kama binadamu tunaongezeka na mifugo ya kienyeji inaongezeka. Ukiangalia kasi ya kuongezeka kwa mifugo ya kienyeji na mifugo ya kisasa tofauti yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, huwezi kutatua hilo tatizo kama hujajielekeza kwenye ufugaji wa kisasa na kama *speed* yako ya kwenda kwenye ufugaji wa kisasa ni ndogo, tatizo hili litakuwa linakua kila siku kwa sababu *population* nayo inaongezeka kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza la kufanya, nakubaliana na wenzangu waliosema kwamba utalamu wa kupata mifugo ya kisasa na ku-*focus* katika maeneo ambayo yana matatizo makubwa kama Shinyanga, Mwanza na kadhalika, nafikiri tungepunguza usafirishaji au *movements* za wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na wenzangu kwamba ni vizuri tukaweka *retention scheme*, kwamba mapato yanayopatikana katika Sekta ya Uvuvi, kwa sababu hii Wizara huko nyuma ilikuwa ikiitwa Wizara ya Kitoweo, kwa hiyo, ilikuwa haipewi pesa za kutosha, maana yake ni Wizara ya Kitoweo tu. Lakini sasa ni Wizara na inasimamia sekta muhimu sana. Kama kuna sekta ambayo ingeweza kuondoa umasikini kwa haraka sana ni hii, kwa sababu sehemu kubwa ya sekta hii ni uvunaji zaidi kuliko uwekezaji.

Kwa hiyo, kama Serikali ikijipanga vizuri ikajielekeza katika katika uwekezaji mdogo tu unaotakiwa, nafikiri tungepigga hatua kubwa sana. Tungejenga viwanda vya kutosha vya nyama. Wenzetu Kenya, nina wasiwasi pengine viwanda vya maziwa vilivyopo mipakani kule vinauliwa ili viwanda vya jirani vifanye kazi vizuri zaidi na vinafanya kazi na mazao yanakuja ndani ya nchi. Sasa hili ni jambo ambalo linahitaji kuangaliwa sana. Serikali isipuuze kabisa kuwekeza katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi sana ni kukaa na *private sector*. Ni lazima tukae nao na matatizo yao tuyatatue. Mimi nilikutana na wazalishaji wa maziwa, wana matatizo

na wakienda kueleza matatizo yao hawapati *solution*. Kwa hiyo, inabidi kila siku ni kwenda na kurudi. Hebu tuweke mkakati wa kuona ni namna gani *Private Sector* itasaidia kupunguza matatizo na hasa katika kasi ya kuongeza ajira na kipato. Niliona niliseme hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongee kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu. Nimeona Mheshimiwa Waziri amerudia tena maneno ya kujenga bandari, nakubaliana nao. Lakini bado naendelea kusema na wenzangu wa uvuvi, bado hatupati hata senti tano kwenye uvuvi wa bahari kuu ukianza na leseni. Ukiacha leseni, hakuna mapato mengine. Hatuna ajira ndani yake, hatuwauzii hata maji, mafuta, hata chakula. Wanachukua rasilimali yote kwa kulipia leseni. Mimi naona hii siyo sahihi na nimewauliza wataalamu wa mamlaka, kwamba Kenya wanafanyaje? Mbona wanatumia bandari yao iliyopo hivi sasa kukusanya mapato? Kwa nini tusitumie Bandari tulizonazo katika kukusanya mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haiwezekani hivyo kuna njia nyingine. Unapompa leseni mwambie wewe una-*estimate* utavua kiasi gani? Nitavua tani kumi; basi mimi nipe *one-third* ya kodi yangu Kama ni 3% au 4% au 5%, huna haja ya kumfuata huko. Lakini leo wanavua samaki na mbaya zaidi wanavua samaki ambao wanataka ku-*export*, wanavua samaki ambao hawawahitaji wala hatujui wanawafanya nini. Sasa huo ni uchukuaji wa rasilimali na ufujaji wa mazingira yenyewe kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tukubaliane kwamba lipo tatizo la msingi, tukae tuli-*address*. Kama ni sheria, iletwe ibadilishwe. Lakini hatuwezi kuacha mtu unampa leseni achukue rasilimali. Ni sawa na kumpa mtu leseni ya mgodi, achukue dhahabu yote aondoke. Sasa itakuwa ni mambo ya ajabu sana! *This is what happening* katika *deep sea fishing*! Wataalamu wanasema ooh, nchi nyingine hazitozi! Lakini nchi nyingine zina mazingira mazuri! Hazitozi, lakini wana viwanda vya ku-*process*; hazitozi lakini bidhaa zinateremshwa pale. Kwa mfano, ukienda Namibia bidhaa zao zote zinateremshwa pale, ajira inatoka pale, huna haja ya kuwatoza *levy anymore*. Sisi hatuna hizo *facilities*, kwa hiyo, ni lazima utoze kwa njia yoyote ile huwezi kumwachia mtu akachukua rasilimali akaondoka tu kama kitu ambacho hakina thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba sana lisimamiwe vizuri, kwani kuna rasilimali kubwa sana zinachukuliwa ambazo hatujui zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wavuvi wadogo wadogo. Serikali imejitahidi sana kufanya Mikutano, Semina na kadhalika, lakini nafikiri kuna mambo ya msingi. Kwanza, nenda kwenye Soko la *Ferry* ambalo lilikuwa lihudumie pengine watu 5,000 au 6,000 lakini leo kuna watu zaidi ya 15,000 wanapata huduma pale. Mazingira yake, hivi kweli akienda mtu atatamani kununua na kula Samaki pale? Ile ndiyo hali ya mazingira ya masoko yote yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijitahidi kufanya jambo moja dogo sana tena ishirikiane na Serikali ya Zanzibar. Nendeni kwenye maeneo ambayo wavuvi wanakuja, wajengeeni *storage facilities* pale, halafu anzisheni *escalating centers*; hao samaki watasafirishwa wala hawana matatizo yoyote. Kama wanavyosafirisha *crabs*; wamejenga maeneo madogo sana, *crabs* wanapelekwa pale wanasafirishwa *live* wanakwenda Ulaya, hawafi. Hili linawezekana kufanyika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri sana, mkae na wavuvi wadogo wadogo mwangalie wana matatizo gani na tatizo la kwanza ni suala la kuhifadhi Samaki wao, wanapokuja wamechelewa hakuna soko Samaki wanaharibika, watengenezeeni utaratibu wa kuhifadhi bidhaa zao.

Viwanda vingi vilivyopo vinaagizia samaki kutoka nje, hakuna anayezalisha. Nenda Dar es Salaam, utakuta kwenye godown samaki wanatoka Japan, China na kadhalika ndiyo tunaokula hapa Tanzania sasa hivi, wakati tuna ukanda mkubwa wa bahari lakini samaki hawavuliwi vya kutosha na ajira inakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo la kuvuna, likiwekezwa vizuri kwa rasilimali kidogo na wataalamu wa kutosha wapo; tulikwenda Mbegani tuliona kuna utaalumu wa hali ya juu kabisa, lakini Chuo kile kimeachwa, hakuna chochote kinachoshughulikiwa na watu wamekata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna haja ya kuelekeza nguvu zetu, katika Kamati ya Bajeti, tutakaa tena kwa kweli, nitawashauri wenzangu kwamba ni lazima Wizara hii isaidiwe, kwa kuwa ni mahali pa kuvuna siyo pa kuwekeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo tu, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Opolukwa atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Peter Msolla na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya ajiandae.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati inayosimamia Wizara ya Mifugo pamoja na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo manne ya kuzungumza leo na ninayoyazungumza yatakuwa kwenye mfumo wa maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wafanyabiashara ambao wamekuwa wakipeleka mifugo kuiiza nchi za nje na sehemu mojawapo ambapo mifugo hii inakwenda ni nchi ya jirani ya Comoro. Napenda kuiuliza Serikali na hususan Wizara ya Kilimo; Wizara inajua kwamba biashara hii ipo ya wafugaji wetu kupeleka ng'ombe kwenda kuuza kwenye nchi ya Comoro? La kwanza!

La pili, naitaka Serikali iwaambie wananchi kwamba ni kwa nini Serikali iendelee kuruhusu biashara ya kuuza mifugo hai hususan nchi za nje badala ya kujikita katika kuhamasisha viwanda vya usindikaji nyama nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukilalamika kwamba tunapoteza fedha nyingi za kigeni kwa kuagiza chakula kutoka nje ya nchi pamoja na mambo mengine muhimu, lakini tunapouza bidhaa ambazo hazijachakatwa kwa mfano, bidhaa zinazotokana na Wizara ya Kilimo kama vile nyama, ni kwamba hatuwasaidii wananchi wetu na hivyo kuwafanya waweze kuwa na kipato duni na washindwe kuendeleza maisha yao kwa sababu hawapati kile ambacho Serikali ilipaswa kuwasaidia ili wakipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika *supermarkets* zetu kubwa hapa nchini, utakuta tunaagiza nyama ya ngombe kutoka *South Africa*, tunaagiza kuku kutoka *Brazil* pamoja na vyakula vingine. Ni kwa nini tuendelee kuagiza vyakula hivi wakati Tanzania kwa Afrika ni nchi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi, ikianza nchi ya Ethiopia, Sudan na Tanzania ni nchi ya tatu. Ni kwa nini tuendelee kuagiza nyama kutoka nchi za nje na hususan nchi ya Brazil na Afrika Kusini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia hatua hata katika migodi yetu hawatumii nyama inayotokana na mifugo wanaozalishwa nchini, wanaagiza nyama kutoka nje, mahali ambapo tungeweza kutumia mifugo yetu tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi hii ingeweza kupata kile inachokihitaji kwa maana ya kupata nyama ya kutosha na hizi fedha zinazotumika kuagiza chakula kutoka nje, hususan nyama ingeweza kutumika kwa ajili ya mambo mengine muhimu kama kuagiza madawa na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho awaambie Watanzania ni lini Wizara hii itasitisha utaratibu wa kuagiza nyama kutoka nchi za nje na hususan *South Africa* pamoja na Brazil wakati ambapo tuna nyama ya kutosha kabisa? Ukiangalia *NAFCO* kuna nyama ya kutosha! Mheshimiwa Waziri wa Mifugo naomba sana wakati utakapofanya hitimisho, angalau basi ulielezee hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na utaratibu katika Halmashauri zetu kutoza ushuru kwa wafugaji wanapokwenda Minadani, ushuru ambao haupo kisheria wala kikanuni. Hili nimeliongelea sana hata kwenye Kamati yetu ya Kilimo. Ni kwamba mfugaji anapopeleka ng'ombe kuza mnadani, sheria na hata kanuni inasema kama mfugaji hataweza kuza ng'ombe au mbuzi au kondoo wake, basi atarudi naye nyumbani na hatatozwa hata shilingi moja, ni mpaka mnada mwingine ufike ili apeleke ng'ombe wake tena kwa ajili ya kuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukichukulia Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, mfugaji anapeleka ng'ombe wake mnadani, auze au asiuze, ni lazima alipe ushuru wa shilingi 5,000/= kwa ng'ombe. Jambo hili nimeliongelea sana kwenye Kamati na Mheshimiwa Waziri alisema angetoa maekelezo nchi nzima. Suala hili linawasumbua sana wananchi wa Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na sijui kwa mikoa mingine kama linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja yake, basi awaeleze watumishi waliopo kwenye Halmashauri ambao wako chini ya mamlaka yake au Halmashauri ambazo zinakuwa na mifugo mingi, awaeleze kwamba kwa sheria jinsi ilivyo, pamoja na kununi ambazo zimetungwa kwa ajili ya biashara ya minadani, hawa ng'ombe wanaopelekwa kuuzwa minadani ni kwamba hawatakiwi kulipiwa ushuru wa aina yoyote kama anapokuwa hajapata mnunuzi.

Mheshimiwa Waziri nakuomba sana unapokuwa unahitimisha ulielezee suala hili kwa sababu limekuwa ni kero na usumbufu, mpaka sasa ninavyoongea kuna kesi Mahakamani zinazoendelea ambazo wananchi wamekaidi kulipa ushuru ambao haupo sawasawa, hauko kisheria wala kikanuni; lakini kuna kesi Mahakamani zinaendelea. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anapokuwa anatoa hitimisho alielezee vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, tumekuwa tukilalamika sana kwamba Wizara zetu hazina fedha. Kwa bahati mbaya sana, ukiangalia Wizara nyingi ambazo tumezitengea fedha kwenye bajeti iliyopita, nyingi zimepata chini ya asilimia 30, lakini tuna uwezo mkubwa kabisa wa ku-*generate* fedha kutoka ndani, lakini ni kwa sababu labda tumekuwa na Watendaji ambao hawafikirii, siyo wabunifu na inawezeka ni kwa sababu wamechoka na ndiyo maana wanahitaji kupumzika; nakuja na ushauri mmoja mzuri sana. Wafugaji katika nchi hii na hususan tukiangalia katika mikoa inayofuga mifugo mingi, wana uwezo mkubwa sana wa kuwa wamojawapo wa wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, au Wilaya ya Meatu, kuna zaidi ya ng'ombe 100,000. Katika Halmashauri ya Meatu tuna eneo ambalo kuna eneo ambalo linaitwa WMA ya Makao, hata Mheshimiwa Laizer ameongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, WMA hii ya makao kwa muda wa miaka mingi imepoteza sifa ya kuitwa hifadhi ya jamii. Ni eneo ambalo halina hata wanyama, utalii wa picha umeshindikana, lakini mpaka leo, hata katika ile Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka ilipendekeza kwamba maeneo ambayo yamepoteza sifa ya kuwa ni hifadhi za kijamii yafutwe ili wananchi wagawiwe maeneo haya kwa ajili ya kilimo pamoja na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia eneo hili kwa hesabu za haraka haraka, Halmashauri ya Meatu tulikuwa tunategemea zao la Pamba ili tupate SES kwa ajili ya kupata fedha ya kuendesha Halmashauri; na fedha ambayo tumekuwa tukipata kwa muda mrefu, ni kati ya Shilingi bilioni 1.8 mpaka 2.2 kwa mwaka kutokana na ushuru au SES ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukulia hili pori au hifadhi ya WMA ya makao ambayo ni pori la akiba, kama Meatu ina ng'ombe 100,000, tukafanya hesabu za haraka kwamba sasa tuwafanye wawekezaji ambao ni wafugaji waingize ng'ombe kwenye ile hifadhi, maana yake ni nini? Mara nyingi kwa Meatu ukame unanza kati ya mwezi wa Saba mpaka wa Kumi na Mbili, maana yake ni miezi sita.

Kwa hiyo, kama wafugaji wenye ng'ombe 100,000 wataamua kuingiza mifugo kwa mwezi mmoja kwenye eneo ambalo limeshapoteza sifa, ina maana kama watatozwa kwa mfano shilingi 20,000/= kwa mwezi kwa ng'ombe mmoja, aingie achunge wakati wa kiangazi, ina maana kwa mwezi mmoja tutapata Shilingi bilioni mbili.

Sasa kama itatozwa kwa muda wa mwezi wa kwanza wa ukame mpaka wa mwisho wa ukame ambao ni miezi sita kuanzia wa Saba mpaka wa Kumi na Mbili, maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Meatu itaweza kujitengenezea siyo chini ya shilingi bilioni 12 kwa mwaka. Leo hii hifadhi ile tunapata chini ya shilingi 250,000,000/= kwa mwaka kutoka kwa mwekezaji. Hao ndio tunaowaita wawekezaji wanaotaka kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Mifugo ikisaidiana na Wizara ya Maliasili, iangalie hili eneo ambalo naamini wawekezaji ambao ni wafugaji, wenye mifugo mingi tuwafanye wawe ndio wawekezaji wa ndani, waingize mifugo kwenye lile eneo. Kwanza limeshapoteza sifa. Ukienda pale huwezi kukuta hata kipepeo, wala mjesi! Utakuta ni eneo ambalo lina majani peke yake. Kwa hiyo, watakapoingiza mifugo na kwa sababu tutakuwa tumewafanya kuwa ndio wawekezaji wetu wa ndani, tutakuwa tumewasaidia sana na Halmashauri yetu itapata kipato cha kuwasaidia Watanzania. Shilingi bilioni 12 siyo fedha kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuwa anahitimisha, basi a-consider hoja hizi ambazo nimezieleza kwa ajili ya mustakabali wa kuwasaidia Watanzania ambao ni wafugaji wa ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Msolla atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya na Mheshimiwa Mhonga ajiandae.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ambayo ni muhimu na inaweza kuwa mkombozi kwa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nami vilevile nitangaze wazi kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na ni Mwenyekiti.

Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu kutoka Wizara hii ambao kwa kweli wamefanya kazi katika mazingira yasiyoridhisha hata kidogo. Hata haya matokeo kidogo tunayoyaona, ni kwamba wameweka nguvu za ziada mpaka wamefikia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inayo sera na mipango ya utekelezaji lakini haina nyenzo za kutekeleza. Naipongeze Serikali kwa ujumla kwamba baada ya miaka mingi ya Sekta ya Mifugo kuyumba ikiambatanishwa na Wizara nyingine; Kilimo, Maji na nyingine, hatimaye umuhimu ulionekana kwamba Sekta ya Mifugo na Uvuvi zinastahili kusimama peke yake. Hii peke yake ni nia nzuri, japokuwa vitendea kazi ndiyo havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuendeleo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu tumepewa rasilimali nyingi ikiwa ni pamoja na wingi wa mifugo, eneo kubwa la bahari na maziwa yenye Samaki, eneo la ukanda wa bahari wenye zaidi ya kilomita 1,450, zote hizi ni rasilimali. Vilevile naipongeze Serikali, tunasema sera yetu ni kuwa na mifugo ya kisasa na ya kibiashara. Kweli huko ndiyo tunakoelekea na inabidi kuwekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa hili tulilionalo kwamba tumeendelea kutunza hii mifugo na inaendelea kuongezeka kwa maana ya kwamba tunawakinga dhidi ya maradhi, magonjwa na malisho yanapatikana angalau kwa shida na maji bado yanapatikana, hii peke yake bado ni neema na kwamba, Serikali imefanya kazi kuhakikisha kwamba mifugo yetu bado ipo. Kwa sababu kama tusingekuwa na mifugo, mahitaji yetu ya mazao ya mifugo ikiwa ni pamoja na nyama, maziwa, ngozi, mayai, kuku na hata samaki, nchi yetu ingelazimika kuagiza kutoka nje kwa gharama ya shilingi trilioni 13.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote mnafahamu kwamba mwaka huu tunaoendelea nao tu ni kwamba bajeti yetu ilikuwa shilingi trilioni 19 na sehemu. Hata hiyo, hatujaweza kuifikia; je, tungekuwa na mzigo mwingine wa shilingi trilioni 13.2! Mahitaji yetu yangekuwa ni shilingi trilioni 32.4 huko mbele. Kwa hiyo, tuishukuru Serikali kwamba hata hiki kidogo tulichonacho tumeendelea kukitunza na kimeweza kusaidia wananchi wakapata hicho kidogo kinachopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu, katika maadui wakubwa tulioanza nao toka tumepata uhuru walikuwa watatu; ujinga, maradhi na umaskini. Sote tutakubaliana kwamba kwa upande wa ujinga na maradhi angalau tumepiga hatua. Lakini kwa upande wa umasikini bado tuko huko, hali yetu haijatutoka. Pamoja na kwamba tunasema uchumi wa nchi yetu umeongezeka, lakini hali ya mtu mmoja mmoja na hasa wananchi wanaoishi vijijini hali ya uchumi wao ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengine wametangulia kuzungumza hapa, nini kifanyike. Nami nasema ili tuweze kufikia malengo ya Taifa, kwamba ifikapo mwaka 2025 Tanzania iwe ni nchi yenye uchumi wa kati inayotegemea zaidi viwanda kuliko kilimo *per-se*, ni lazima tuwe na uzalishaji wenye tija, kisha tuongeze thamani ya mazao kama walivyozungumza watu wengine; na tatu tuwe na masoko ya kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma tumetilia mkazo mkubwa sana katika ujenzi wa miuondombinu na huduma za jamii. Nafikiri sasa ni wakati muafaka kwamba tuongeze juhudi kwenye uzalishaji, kisha tuongeze thamani na tatu tuwe na masoko ya hakika. Hii inagusa sekta zote ikiwa ni pamoja na Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bahari wenzangu waliotangulia kuzungumza wameshaeleza mengi sana kwamba tuna ukanda mkubwa wa bahari unaofaa kwa uvuvi wa kina kirefu.

Vilevile tuna maziwa, lakini hatujatumia hii fursa tuliyonayo kwa muda mrefu. Tulikuwa na TAFICO, ilifanya kazi nzuri sana. Ilianza kuvua kwenye Bahari ya kina kirefu, lakini ulipokuja utaratibu wa kubinafsisha mashirika, TAFICO ilikuwa ni mojawapo. Leo hata miundombinu yake bado iko pale pamoja na kwamba imechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa katika ripoti yetu ya Kamati kwamba Visiwa vya Shelisheli vyenye watu takribani 85,000 tu zaidi ya asilimia 75 ya nguvu kazi yao wameajiriwa katika uvuvi na kila mwaka wanaongeza kwenye pato la Serikali kiasi cha Shilingi bilioni 185. Hili siyo pato dogo. Je, sisi ambao tuna bahari kubwa na maziwa! Hatujawekeza! Kwa hiyo, tusitegemee kuvuna mahali ambapo sisi wenyewe hatujawekeza vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumezungumzia juu ya mifugo. Ni kweli Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo, hususan ng'ombe katika Bara la Afrika, lakini mchango wetu ni mdogo sana katika pato la Taifa, nafikiri ni asilimia 4.2 tu hivi. Lakini Botswana yenye ng'ombe wachache sana, hawafiki hata milioni mbili, mchango wao katika pato la Taifa ni mkubwa. Mifugo ni ya pili katika kuchangia Pato la Taifa baada ya Almasi.

Kwa hiyo, vilevile kama walivyozungumza wengine mambo ya miundombinu na thamani ya kuboresha mazao yetu, kama hayo yote yangefanywa na kuwa na masoko ya uhakika, tuna hakika kabisa mifugo ingeweza kuchangia sehemu kubwa ya pato letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mwaka 2008/2009 Serikali iliweka azma ya kwamba katika utafiti itawekeza kidogo kidogo mpaka hatimaye tuweze kufikia asilimia moja ya pato ghafi la Taifa. Hiyo ilitekelezwa kwa mwaka mmoja, baada ya hapo fedha kwa ajili ya utafiti imeshuka. Ukitembelea katika Vituo vya Utafiti vya Mifugo na hata Uvuvi, kwa kweli hali ni mbaya, hakuna vifaa na Watafiti walio wengi wamekata tamaa na wengi ni ambao wamekaa kwa muda mrefu karibu wana-*retire* na hata hawa wahitimu sasa hawataki kujiunga huko kwa sababu wanaona hakuna *incentive* ambayo ingeweza kuwasaidia kuendelea kuwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu Serikalini ni kwamba tuendeele kuboresha hii Sekta ya Utafiti na Maendeleo kwa sababu hata nchi zilizoendelea ni kwa sababu toka mwanzo ziliwekeza zaidi katika utafiti na maendeleo. Sisi vinginevyo tutakuwa ni watumiaji wa matokeo ya utafiti uliofanywa na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa sana juu ya Soko la *Ferry*. Tulitembelea pale, hali ni mbaya. Kama ilivyosomwa kwenye ripoti yetu kuna haja ya pale mahali kuangaliwa upya, ule msongomano upunguzwe ambapo sasa karibu watu 15,000 wanatumia lile soko kwa siku badala ya watu 2,000 ambao mara ya kwanza lile soko lilikuwa limepangiwa. Tumeshauri kwamba wanaweza kwenda Temeke, Kinondoni, lakini vilevile na maeneo mengine huko Mtwara na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia huu ujenzi wa bandari unaolenga pale Mbegani, tunafikiri haitakuwa vyema kubomoa kile chuo eti kwa ajili ya bandari tu. Tunashauri Serikali iangalie mahali pengine kama vile Kilindi, ambapo ni mahali panapoweza kufaa na wakaweka hata *special economic zone* ili kusudi kuwe na shughuli nyingi zaidi kuliko kuweka bandari tu. Kwa

hiyo, sehemu ya uvuvi kama alivyosema mjumbe mmojawapo, ni sehemu ya kwenda kuvuna tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna njia nyingi za kuboresha mifugo na siyo kwenda kununua madume kutoka nchi nyingine. Licha ya *Artificial Insemination (AI)*, sasa hivi unaweza kufanya *embryo transfer* ambayo inarahisisha sana na ni njia nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, atafuatiwa na Mheshimiwa Muhonga na Mheshimiwa Mulugo ajiandae.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ningependa nichukue nafasi hii pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ni mazingira magumu kwa sababu, kwa mfano kwenye bajeti ya mwaka 2014 tuliona fedha waliyoomba ilikuwa ni kidogo sana tukaomba waongezewe fedha. Kwa furaha kabisa Serikali ikasema inawaongezea fedha za maendeleo ili zifikie shilingi bilioni 23. Kwa masikitiko, mpaka sasa hivi zile fedha tulizoomba hawajapata hata shilingi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia majukumu ya Kamati ni kuishauri Serikali, tukizingatia kwamba kile tunachokiomba kitaongeza tija pamoja na uchumi wa nchi. Sasa kama hilo halikuchukuliwa, maana yake ni kwamba, walitaka kufunika kombe mwanaharamu apite. Mimi napenda niishauri Serikali kwamba lile ambalo haliwezekani, tuambiane ukweli kwamba haliwezekani ili wahusika waweze kutafuta njia mbadala ya kufanya yale ambayo yangefanyika kwa ajili ya mazuri tu na maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima. Migogoro ya wafugaji na wakulima bado ipo, Serikali imejitajidi sehemu mbalimbali lakini kuna kwingine ambako Serikali inajua kuna matatizo lakini bado hawajaona umuhimu wa kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachoonekana kabisa ni kwamba, kama kila Halmashauri itawezeshwa ikatengeneza matumizi bora ya ardhi kila Kijiji wakajua kwamba wakulima wanakaa wapi, makazi ni wapi, wafugaji wanakaa wapi na maeneo ya huduma na hifadhi ni wapi; nina hakika kabisa hiyo migogoro itakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo naliona kwenye kijiji kimoja tu katika Kata moja ya Tarafa ya Ngerengere. Kwenye Kata ya Matuli, Kijiji cha Diguzi; hawagombani hata siku moja. Kila mmoja anajua anakaa wapi na wanakwenda kukutana wapi. Uzuri ni kwamba wafugaji hawakutaka kusubiri Serikali iwawekee miundombinu, waliamua kuvuna ng'ombe wao wakajenga majosho na marambo ya maji na sasa wanaishi kwa amani, wamepunguza ng'ombe zao na vijana wao wengine wameanza mradi wa kukusanya maziwa, wanatengeneza *cottage cheese*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wizara ijue kuna watu kama hao, wasaidiwe, kwa sababu tangu wale vijana wameanza, hata wazee na wafugaji wengine wanachukua ushauri wao kwamba sasa tupunguze ng'ombe, tuongeze ng'ombe wa kisasa na tuendeleo kuongeza miundombinu ya kuhakikisha kwamba ng'ombe wetu wanakuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo ambalo bado watu wanapigana bakora ingawa hatusemi, tunaingia humo kwenda kuwasuluhisha. Kuna kijiji kinaitwa Magera, Halmashauri imejitahidi wametenga maeneo, lakini tatizo linakuja kwamba, hawa wenye ng'ombe ni lazima wapite kwenda kutafuta maji kwa ajili ya ng'ombe wao, wanahitaji kupata rambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba niishukuru Serikali kwamba imetoa marambo mawili katika Tarafa ya Ngerengere; na yale maeneo ambayo wamepata marambo, katika Kitongoji cha Ekenywa, Kijiji cha Sinyaulime, sasa hivi ugomvi wa kupigania maji kwamba ng'ombe wamekula mazao, umekwisha.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee na hii juhudi ya kuhakikisha kwamba wafugaji kule ambako wameshatengewa maeneo wanahamasishwa, wanachangia na Serikali inawasaidia wajenge miundombinu ya majosho, maji na shule. Kwa sababu wengine wanahama hama kidogo wanasema tunafuata shule na huduma za afya ambazo ni haki zao, lakini katika kufanya hivyo, kunatokea matatizo wanagombana na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuzungumza ni kwamba, Sekta ya Utafiti ni muhimu sana kwa hii Wizara. Wanakuwa na Sekta ya Utafiti ambayo itasaidia sana kupunguza magonjwa ya ng'ombe ambayo yanavuna ng'ombe wa wafugaji kama hayana akili nzuri. Lakini nawapongeza kwamba wamejitahidi kuzalisha chanjo zao hapa nchini ambazo zimepunguza sana yale magonjwa ambayo yalikuwa ni sumbufu. Sasa tunachoomba ni kwamba, waongezewe mtaji ili waimarisha waweze kuzalisha zaidi na tuweze kuuzia nchi jirani ili tuweze kuingiza fedha za kigeni. Uwezo wanao kwa sababu wana *infrastructure* na wataalam ambao ni *committed*, ila tatizo limekuwa ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu uvuvi. Wavuvi wetu wanapokwenda kuvuna, siku nyingine wanapata baraka wanapata wanunuzi. Siku wakikosa wanunuzi wale samaki wanakaa mpaka jioni wanaharibika. Ushauri ambao tulikuwa tumetoa kwa Wizara ni kwamba waangalie namna ambavyo watawasaidia kuwapa mkopo wa kuweza kuwa na majokofu katika mialo ili samaki watakapokuja waweze kuwaweka mle waweze kupata fursa ya kupanga bei wanayoitaka, hata kama wasiponunuliwa siku hiyo kesho yake wavuvi wanaweza kwenda kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba, tulipoonana na wale wavuvi wa *ferry* waliomba kutengenezewa chombo ambacho kitaratibu shughuli za uvuvi na mialo mbalimbali katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati, tumekubaliana nao kwamba sasa wanataka kufanya kazi wakiwa na mwelekeo, wakiwa wanashirikiana na Serikali na wakiwa wanasikiliza ushauri wa Serikali.

Kwa hiyo, ninaomba Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ambazo zimeguswa Dar es Salaam, waanze Dar es Salaam, waende Mwanza na sehemu zote ambazo kuna wavuvi wanaovua samaki kwa wingi lakini wanakuwa na vikundi mbalimbali ambavyo katika kupingana kwao shughuli haziendi na Serikali inakosa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie malisho. Nimesoma kwenye kitabu na tuliambiwa pia kwenye Kamati kwamba kwa sasa hivi kipaumbele kimojawapo ni kuangalia malisho. Hivi hii haiwezi ikawa ni biashara kwa vijana wetu wanaomaliza Vyuo Vikuu, Wizara ikawahamasisha kwa sababu wanafahamu vizuri sana kuhusu lishe ya wanyama? Wasaidiwe, wafungue mashamba, wapewe mbegu safi waweze kufunga na kuuzia wakulima.

Pia wale ambao wamesoma ujuzi mbalimbali waje pamoja waweze kusindika mazao kama wale vijana waliomaliza *SUA* wakaanzisha *Shambani Milk*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na wengine wanaweza wakaanzisha *extension* pamoja na ufugaji wa kuku wa kienyeji ambao wana fedha nyingi sana. Siku hizi kuna ndege wanaoitwa kware ambao kwa kweli ni biashara nzuri na kubwa, wanauza *tray* ya mayai kuanzia shilingi 15,000/=. Sasa kama wanaweza wakafuga, wakauza na wakafundisha wananchi kufuga, naamini kwamba tutakuwa tumetengeneza ajira kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niseme kwamba sekta hii ni muhimu sana katika kuboresha uchumi wa nchi hii.

Ni muhimu sana kutengeneza ajira kwa vijana wa aina zote; wenye ujuzi wa masoko, ujuzi wa kufuga, wasiokuwa na ujuzi wa kufuga, wote watapata kazi kwa sababu hakuna atakayeshindwa kufuga kuku wa kienyeji ambao duniani sasa hivi wanaitwa *yellow meat* na ndiyo wananchi na watu wengi ambao wanaangalia afya zao wanapenda kula. Ajira iko hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye uvuvi. Tuna vijito vingi sana huko milimani na katika vijiji, tunaomba Wizara iwapelekee Maafisa Ugani waende wakawafundishe kuchimba mabwawa kwa sababu nimeona kwa mwaka kuna vijana wenye mabwawa mawili kule Tegetero, wanavuna samaki mara mbili na kipato chao ni Shilingi milioni 12 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kijijini kijana ambaye amemaliza Darasa la Saba, Shilingi milioni 12, wakati wale samaki hawahitaji kuletewa Daktari tena, ni wewe kubadilisha maji na kuwawekea chakula; naomba Wizara iangalie namna ambavyo itaboresha ufugaji wa kuku katika vijiji vyetu na vijana waweze kupata kama sehemu ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kusema kwamba hawa wanaozunguka na mifugo yao, Serikali imekuwa na tabia ya kufukuza watu katika maeneo, hawawaelekezi waende wapi. Wanaondoka na mifugo yao wanakwenda kwingine. Tatizo lililopo sasa hivi katika Mkoa wa Morogoro ni katika Wilaya ya Morogoro Vijini na Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali imeelewa nilichotaka kusema. Naomba kuunga mkono hoja, nawatakia hii Wizara kila lakheri, ila Serikali iwawezeshe ili waweze kuwezesha uchumi na kutengeneza ajira. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mhonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mulugo.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango wangu mdogo sana katika Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya. Vilevile nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifugo na Uvuvi ni Sekta nyeti na ndiyo maana iliundiwa Wizara kwani ni eneo rahisi sana la kuongeza mapato, lakini nasikitika kwamba Serikali imekuwa haitoi bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Wizara hii kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Sekta ya Uvuvi. Naomba niseme nasikitika sana kuona sekta hii inavyofanya kazi kwa kudorora ukizingatia kwamba nchi yetu tunayo bahari

ambayo ina eneo kubwa tu, tunaweza tukapata mapato ya kutosha kupitia uvuvi wa bahari kuu. Vilevile tunayo maziwa makubwa kama Victoria na Nyasa ambayo yangetumika vizuri tungeweza kupata pato la kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo maziwa mengine ya kati, naona katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri, ameyainisha hapa, kuna Ziwa Rukwa, Mtera, Nyumba ya Mungu, Kitangiri, Singida, Kindani, Burunge na mengine madogo madogo kama Eyasi, Jipe na Mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa kama Serikali ikiweza vya kutosha tunaweza kupata pato kubwa sana la Taifa. Kwa kiwango ambacho kinachangiwa sasa na sekta ya uvuvi cha asilimia 2.4%, bado ni ndogo sana. Kwa hiyo, inabidi juhudi ziongezwe ili kuboresha sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa sekta hii kwanza utaongeza ajira kwa sababu sasa hivi tuna tatizo la ajira sana kwa vijana, lakini pamoja na hivyo tutaongeza pia pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingi sana umekuwa ukitolewa kuhusiana na uvuvi wa bahari kuu. Nikifumba macho namwona Mheshimiwa Hamad Rashid toka tumeingia Bungeni mwaka 2005, nakumbuka anaongelea suala hili, lakini nafikiri Serikali inatakiwa kufanya utafiti wa kutosha kuangalia ushauri ambao unakuwa ukitolewa. Hata Kambi ya Upinzani na Mbunge mmoja mmoja pia tumekuwa tukitoa ushauri juu ya upatikanaji wa mapato kutoka katika uvuvi wa bahari kuu na maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ili kuboresha sekta ya uvuvi na iwavutie watu wengi katika yale maeneo ambayo kuna maziwa au kuna shughuli za uvuvi, tumesikia hapa baadhi ya Wabunge wanashauri kwamba katika yale maeneo ambayo kuna wavuvi, wahakikishe kwamba, inawekwa miundombinu ambayo itawawezesha wale wavuvi kutunza samaki wao ikiwemo kununua majokovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado naona umuhimu wa kuongeza viwanda vidogo vidogo vya samaki ili iwavutie watu kufanya kazi ya uvuvi, lakini pia itatoa ajira, lakini pia kufuatia upatikanaji wa ajira bado pato la nchi litaongezeka kwa sababu watu watavua samaki kwa wingi kwa sababu kuna *mechanism* za kuwasindika lakini pia kutakuwa na *mechanism* za kuwatunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika sekta nyingine, lakini kabla sijafika katika sekta nyingine, naomba niongelee wavuvi wa Kigoma. Wavuvi wa Kigoma bado wanavua katika hali duni kwa kweli na ziwa lile unajua kuwa lina kina kirefu. Naamini Serikali ina uwezo kabisa wa kuwekeza katika yale maziwa makubwa, kwa mfano, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, kuna samaki wazuri sana wanaopatikana hapo. Serikali yenyewe inaweza ikawekeza na ikapata pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Ziwa Tanganyika, wavuvi wamekuwa wakivamiwa sana na wavamizi kutoka nchi jirani na wamekuwa wakinyang'anywa mashine zao. Kwa hiyo, badala ya kuendelea mbele wanarudi kuwa masikini na wamekuwa na tabia ya kuchangisha mafuta wao wenyewe, kuchangia maboti ya maaskari kwa sababu bajeti ya maaskari ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, unakuta ni lazima waingie hasara, kile kiwango kidogo cha pesa wanachokipata wachangie mafuta kwa ajili ya boti za askari kwa ajili ya ulinzi, lakini bado wanaendelea kuvamiwa. Kwa hiyo, Serikali iongeze bajeti ya ulinzi katika Ziwa

Tanganyika ili wavuvi wavue salama. Hata hivyo, bado wanavua katika hali duni sana na kazi hiyo haiwakwamui kabisa katika kuwaondoa katika lindi la umaskini. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ijaribu kuongeza uwekezaji katika sekta ya uvuvi ili kuwasaidia wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo; sekta hii ni nyeti, lakini bado nayo tunaona inachangia 2% tu katika pato la Taifa. Katika ukanda wa Afrika ya Mashariki Tanzania ni ya pili, lakini katika Afrika Tanzania ni ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi, lakini bado tunaona kabisa sekta hii ya mifugo haijakuwa na tija kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali naamini kuwa ikigawa ardhi kwa matumizi bora ya ardhi, wale wafugaji wakafundishwa ufugaji wa kisasa na watu wengine wakafundishwa kulima majani kwa ajili ya mifugo, kukawa kuna hospitali za mifugo, madawa ya kutosha ya mifugo, Maafisa Ugani, kukawa na *mobile Doctors* ambao watawafikia wake wafugaji ambao wako maeneo ya mbali, naamini kabisa mifugo ingekuwa bora, kuliko ilivyo sasa mifugo yetu kwa kweli imekonda, kwa sababu ukizingatia wafugaji wamekuwa wakihamahama kufuata malisho, majosho na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie ni kwa jinsi gani inaweza kuboresha kwa sababu mifugo ni mali, mifugo inatoa mazao mengi; kuna maziwa, ngozi, nyama na tukienda kwa upande mwingine labda kuku, kuna mayai na kuna nyama yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna viwanda vya kutosha vya kusindika mazao ya mifugo na hili limekuwa ni tatizo kubwa ndiyo maana hatuoni tija. Viwanda vya maziwa kwa mfano Tanga *fresh* na kile cha Ubungo ni vidogo, yaani ni viwanda vichache ambavyo haviwezi kuwa na uwezo wa kusindika maziwa yote yanayozalishwa nchini na ndiyo maana tumemsikia Mheshimiwa Mbunge pale kutoka Solwa akilalamika kuwa watu wanamwaga maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujifunze kwa wenzetu mfano, Rwanda. Rwanda wao wameamua kuondoa umaskini kwa kuwahamasisha wananchi maskini kufuga wanampa mtu ng'ombe, yule ng'ombe akipata motto, anampa jirani yake na wanazalisha maziwa mengi ya kutosha kwa mtu mmoja mmoja.

Kwa hiyo, ule ufugaji wanaoufanya unawasaidia kuwaondolea umaskini, kwa sababu wameanzisha *centers* za kuuza maziwa, katika vijiji vyao. Kwa hiyo, wananchi wanakuwa na maziwa, yale ya ziada yanayobaki baada ya matumizi ya nyumbani, wanayapeleka katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasindika haya maziwa, wanatengeneza mafuta ya samli, lakini vile vile wanapeleka katika kiwanda ambacho, yaani sasa hivi ukienda Rwanda maziwa ni kama maji tu, yako mengi sana. Naamini Tanzania tuna uwezo wa kuweza kuanzisha *centers* za kukusanyia maziwa na vijana wengi sana hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza ikaamua kuwachukua vijana na kuwapa elimu, wakapewa mikopo, wakafungua *centers*, wananchi ambao wana ng'ombe wakawa wanapeleka maziwa yao pale ya ziada yanayobaki, kunakuwa kuna vifaa vya kuchemshia maziwa na majokovu ya kuyahifadhi. Kwa hiyo, mkiwakopesha vijana wanaweza kununua magaloni wakawa wanaweka kwa ujazo tofauti tofauti, yaani inakuwa ni ajira na maziwa yakaweza kutumika badala ya kumwagwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inasikitisha sana kuwa inauza ngozi ghafi, tumeua viwanda vyetu, kwa nchi za wenzetu kama Ethiopia tunanunua mabegi, mikanda na viatu

ambavyo vimetengenezwa na wanyama ambao wako katika nchi yao. Hata hivyo, inasikitisha sana kuona Tanzania bado tunauza ngozi ghafi. Matokeo yake ni kwamba tunapeleka ngozi kule, wenzetu wanatengeneza ajira kwa vijana wao, halafu vile vitu ambavyo wanatengeneza kule vinarudi tena huku, kwa nini tunawapa ajira watu wengine na sisi tuna uwezo wa kuwa na viwanda vya kutengeneza vitu hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaanzia hata katika viwanda vidogo vidogo va *SIDO*, kuna baadhi ya watu ambao nawajua wanatengeneza viatu. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kama mkiwaelimisha watu zaidi wakaweza kufanya kazi hii, lakini bado kuna umuhimu wa kuboresha viwanda vyetu, mfano, iwe Morogoro, Mwanza na Moshi vikafanya kazi vizuri, badala ya kusafirisha ngozi ambayo ni ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda nao unakwenda lakini nitajitahidi nimalize, viwanda vya nyama vimekufa, *Tanganyika Packers* tunasikia kila siku kwamba wamepeva wawekezaji, lakini hakuna kinachofanyika. Katika eneo la kiwanda, nikipita pale Dar es salaam, naona watu wanacheza tu mpira na vifaa hakuna hata kimoja. Nimetembelea Kiwanda cha Nyama Shinyanga kwa kweli hali ni hivyo hivyo tuliahidiwa kuwa kitafufuliwa, lakini labda mtatupa majibu kimefikia hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kupoteza ajira mpaka hapo, lakini vile vile na masoko. Wafugaji wangeweza kupata masoko wakaboresha hali zao za maisha na wangeacha kuzunguka na mifugo barabarani kama mkiwatengenezea mazingira mazuri ambayo nimesema, wangeweza kutulia kwa sababu wangukuwa na uhakika wa masoko ya mifugo yao ambayo wanaifuga. Kwa maana hiyo wangepata masoko wakaboresha maisha yao, hali ingekuwa nzuri na Tanzania ingepata pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha nyama ambacho kinapelekwa nje ni kidogo sana na ukitaka nyama bora, upate kutoka South Africa, hiyo ni aibu kwa kweli. Naamini uwezo tunao wa kufanya vizuri na tukaongeza pato la nchi na umaskini ukaondoka kwa sababu ukikutana na mtu mwenye mifugo yeye mwenyewe kakonda na mifugo yake imekonda. Hiyo hali kwa kweli siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye migogoro. Nchi yetu ni moja tunasema ina amani, lakini maeneo mengine kwa kweli hawana amani. Ukienda maeneo ya Kilosa ambako tumekuwa tukisikia matatizo kila siku inasikitisha sana. Nimeangalia siku moja kwenye Televiseni nikaona wanyama wanavyokatwa miguu wanauawa na kufa. Ni vitu ambavyo vinasikitisha, lakini naona tatizo liko kwa Serikali kwa sababu halitaki kupanga maeneo, haitaki kuwapa wakulima elimu kwa ajili ya ukulima wao, haitakiwa kuwapa wafugaji elimu bora ili waweze kufuga mifugo yao vizuri ili kuwasaidia kupata pato lao, lakini pia na kuwaondolea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuwa mifugo ni mali na Serikali ikifanya kazi yake vizuri kwa kuhakikisha kuwa inatenga maeneo ya kutosha, inawapa elimu hawa wafugaji, migogoro hii itakwisha kwa sababu hakutakuwa na haja ya mfugaji kuhama hama wakati amejengewa joshu, amefundishwa jinsi ya kutengeneza malisho kwa kupanda majani na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Serikali baada ya hapa wakati ikijibu, watupe mikakati yao yaani ni vipi mtahakikisha kwamba migogoro hii inakwisha na amani nchini inarudi, maana yake tuna amani maeneo mengine, lakini maeneo mengine ya wafugaji na wakulima na wafugaji huko Kilosa, Morogoro, amani hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa inawezekana kama mtafanya *homework* yenu vizuri na ushauri mwingi umeshatolewa, Tume mbalimbali zimeshaundwa, hebu pitieni yale majibu muangalie ni jinsi gani mnaweza kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Philipo Mulugo!

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nitajikita sana kuchangia masuala ya uvuvi kwa sababu Jimboni kwangu Songwe, Wilaya ya Chunya, vijiji vyangu vya Maleza, Mbangala, Mkwajuni, Some, Udinde, Rukwa, Iyovy, Kambi Katoto kote kule kumezungukwa na Ziwa Rukwa. Kwa hiyo, Wizara hii kwangu leo ni muhimu sana angalau na mimi niweze kujikita namna gani Wizara itanisaidia kwa wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Songwe kwa muda ambao tumekaa nao kwa miaka mitano, tumeshirikiana katika kufanya mengi sana kule Jimboni na nataka kuwahakikishia kuwa nipo na naendelea kupiga kazi waliyonituma na nitaendelea kufanya hivyo awamu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti siyo kuchangia suala la uvuvi lakini kabla sijaingia huko angalau nichangie suala la mifugo kidogo, kwa sababu Wilaya Chunya kama ambavyo huwa nasema kila siku, ni Wilaya kubwa sana katika nchi hii. Ni Wilaya yenye ukubwa wa Kilomita 29 ukilinganisha na Wilaya zingine kama za Longido kule au Simanjiro na ndiyo hivyo hata Serikali ilivyotenga eneo la wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma takwimu hapa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, wametenga vijiji 16 vyenye eneo la hekta laki nne na hamsini na moja. Hakuna Wilaya ambayo imetengwa hilo eneo kama siyo Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka mwone tu kuwa ni wadau muhimu sana kuchangia Wizara hii siku ya leo, mimi na Mheshimiwa Mwambalasa pale kaka yangu. Nilikuwa naongea naye muda siyo mrefu, akasema kwamba mdogo wangu wewe changia tu uniwakilishe kwa kuwa tuko Wilaya moja, mimi natoka Jimbo la Songwe na yeye anatoka Jimbo la Lupa. Maeneo kama ya kwake kule, maeneo kama ya Matwiga na kule Mapogoro, Halmashauri yetu inachimba visima kwa ajili ya malisho na malambo kwa ajili ya ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakwama mambo hayo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kwa sababu kama nilivyosema, ndiyo Wilaya pekee iliyopewa hekta laki nne na hamsini na moja kwa ajili ya maendeleo ya mifugo, lakini kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji hasa kwenye Jimbo langu, nataka kumshukuru sana Mheshimiwa Ole-Sendeka na Kamati yake walikuja na Mheshimiwa Selasini wa Rombo na Mheshimiwa Jenista Mhagama walifika mpaka Kijiji cha Mwambani kwa ajili ya kuona migogoro ya wafugaji na wakulima na kuwasuluhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo nataka kukuhakikishia kwamba, Mkuu wetu wa Wilaya anafanya kazi vizuri sana. Baada ya pale hatuna migogoro tena ya wakulima katika Jimbo la Songwe, ipo lakini ni migogoro midogo ambayo ma-VEO na ma-WEO na Mheshimiwa Diwani na mimi mwenyewe kama Mbunge na Mkuu wa Wilaya tunashirikiana kuimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Deodatus Kinawilo anafanya kazi nzuri sana. Kamati ilipofika na wakawa wameunda Kamati ya Wilaya ambayo Mwenyekiti ni ndugu yangu Julius Ngasa, anafanya kazi nzuri sana kuzungukia kila Kata kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sasa eneo la uvuvi. Kama nilivyosema vijiji vingi vya Jimbo la Songwe tumepakana na Lake Rukwa linakwenda mpaka Sumbawanga kule. Sasa nilikuwa najaribu kupitia kitabu hiki cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona popote ambapo pameongelea maendeleo ya uvuvi katika Ziwa Rukwa, kama ilivyo kwenye mikakati mingine katika Maziwa ya Tanganyika, Nyasa, Victoria, lakini kule Rukwa sijaona chochote, hakuna maendeleo yoyote, sijawahi hata kuona kama kuna vikundi vyovyote vya uvuvi zaidi ya Mheshimiwa Diwani au Mbunge anatoa nyavu vijana wanavua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata wale *fisheries*, wale Mabwana Samaki, ukiangalia Wilaya ya Chunya nzima tuna Mabwana Samaki labda watatu tu Wilaya nzima, lakini nimeorodhesha vijiji hapa ambavyo vinaishi kwa ajili ya uchumi wa kutafuta kwa njia za uvuvi wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aliingize Ziwa Rukwa katika mipango yake ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Ziwa Rukwa ni kama halina mwenyewe, kama ni mamba, wako ziwa Rukwa, nasikia mamba ndiyo mnafula kule Ziwa Rukwa na watu wanakufa, kila wiki kule napata misiba ya watu waliokamatwa na mamba na hakuna fidia yoyote na inaonekana kila mwaka mnafula fedha kwa ajili ya kwenda kuvuna mamba 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuvuna mamba 60 haitoshi, mngeweka hata mamba 200 kwa kila mwaka labda, kwani ukienda Ziwa Rukwa, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, utakwenda kujionea mwenyewe, hali siyo nzuri sana kwa wananchi wale kila mwaka ni misiba kwa sababu ya mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuongelea habari za upungufu wa samaki Ziwa Rukwa. Ziwa Rukwa kwa kweli kwa sasa kama nilivyosema limebaki kama ni yatima, hakuna anayeliangalia, sijawahi kuona hata Naibu Waziri au Waziri au mtu yoyote kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenda kutembelea au kuzungukia kuona maendeleo ya uvuvi katika Ziwa Rukwa, hakuna.

Kama nilivyosema hawana maboti, tofauti na programu zingine kama za Lake Nyasa, Lake Victoria kama nilivyosema, sasa sijui kama Serikali inatambua kweli kama hili ziwa lipo au halipo, hata hizi takwimu za kusema kuwa kuna wavuvi kadhaa, kuna samaki kadhaa, sijui mnazitoa wapi hamjatembelea Ziwa Rukwa kuja kuona kwamba ni namna gani jinsi ambavyo wananchi wanaishi kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana, mwaka jana Ziwa Rukwa lilifungwa kwa miezi sita, tukasema kuwa labda tufanye utafiti, sijawahi kuona hata Serikali inakuja pale inafanya utafiti wa kuona ni kwa nini samaki wamefungua. Baada ya hapo tukafungua, wakavua samaki tena wakapungua, mwaka huu mwezi wa Kwanza Ziwa likafungwa tena, wakaja kulifungua tarehe 1 Mei, mwezi huu tulionao ndiyo Ziwa limefunguliwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimepiga simu kule kwa wavuvi, kule Udinde, Maleza, Some, Manda, Iyovyoo wanasema samaki tena hakuna, Mheshimiwa Waziri tuma wataalam wakafanye utafiti wa Ziwa Rukwa, ni kwa nini samaki wanapungua? Nakumbuka mwaka 1978

nilikuwa na miaka saba tulipandikiza samaki walikuwa wanaitwa Singida zamani, wale samaki wametukomboza sana mpaka tumesoma na shule, lakini leo hii samaki Ziwa Rukwa hakuna. Halafu uvuvi holela unaoendelea kule Lake Rukwa wanatumia kokoro, watu wanavua tu samaki, hakuna udhibiti wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya hata akisema kuwa atume watu sasa atatuma watu kwenye vijiji vingapi? Hakuna! Hata Mabwana Samaki wenyewe hakuna, nenda Uinde hakuna Bwana Samaki, nenda Maleza hakuna Bwana Samaki, nenda Some hakuna Bwana Samaki, nenda Iyovyoy hakuna Bwana Samaki, nenda, Manda, nenda Mkwajuni ndiyo utakuta Bwana Samaki yupo mmoja, naye anakaa Mkwajuni, lakini hakai kule kwa sababu hana vifaa, hana boti na hana chochote cha kuweza kuwazungukia wale wavuvi na kuona kama wanavua uvuvi halali au uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanavua kwa makokoro na ndiyo maana labda samaki wanakwisha, lakini vile vile mkishafunga Ziwa udhibiti unakuwaje? Nilikuwa napigiwa simu na wananchi wangu mwezi wa Pili, wa Tatu, wa Nne wanasema mbona wenzetu wa ng'ambo ya kule wanavua samaki na sisi ukanda wa Chunya hatuvui samaki? Nikasema ni kwa sababu Mkuu wetu wa Wilaya ni mtu mzuri sana, anadhibiti, ana vitendea kazi ambavyo mpaka vimefanya watu wamedhibitiwa kwa ajili ya kuvua samaki holela, lakini upande wa ng'ambo ya kule Ziwa ni lile lile na Wizara ni ile ile na nchi ni ile ile, wenzetu wanavua samaki.

Kwa hiyo, tunaomba mnapokuwa mnafunga ziwa, basi mfunge Ziwa lote, lakini siyo ng'ambo ya Sumbawanga kule wanavua samaki, ng'ambo ya huku Momba wanavua samaki, mimi Jimboni kwangu ndiyo wananchi wanalalamika, tunaonekana sisi viongozi tunafanya mchezo wa kuigiza kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa hapo, naomba Wizara ifanye utafiti wa samaki wa Ziwa Rukwa, visamaki ni vidogo mno, hata samaki hawakui ni kama wamedumaa tu. Kwa hiyo, naomba Wizara ilianguilie hili *otherwise* tutaendelea kuhangaika na hivi wanasema kwamba watafunga tena, sasa wananchi watakwenda wapi na miaka yote wanategemea uchumi wao kutoka Ziwa Rukwa?

Naomba sana hili suala ni suala ambalo nimeona nichangie kwa ajili ya Ziwa Rukwa upande wa mifugo kama nilivyosema angalau kuna amani sasa hivi. Namshukuru sana Mkuu wa Wilaya kwa kuunda zile Kamati za Vijiji na Kamati za Jimbo na Wilaya, tunashirikiana vizuri sana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Chunya mambo yanakwenda vizuri, lakini suala la Lake Rukwa ndiyo kilio changu kama Mbunge wa maeneo ya kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hata Mbunge wa Momba angesema hayo hayo na Mbunge wa maeneo ya Sumbawanga upande wa kule Muze angesema hayo hayo, samaki hakuna sasa hivi, hakuna vikundi vya uvuvi, sijwahi hata siku moja kusikia kuwa, Maafisa wa Serikali kutoka Wizarani wanakuja kuweka mikakati pale Halmashauri kuwa angalau kuwe na mikopo midogo midogo kama ambavyo tunakopesha wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona tunawakopesha wachimbaji wadogo wadogo, ni kwa nini tusiwakopeshe hata wavuvi wadogo wadogo tuwe na mikakati basi ya kuwanunulia maboti, wavue warudishe mikopo yao kama kawaida, ni jambo ambalo nilitaka kuliongelea hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi jioni wafuatao wajiandae, ndiyo watakuwa ni wachangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, atafuatiwa na

Mheshimiwa Sara Msafiri, mchangiaji atakayefuata atakuwa ni Mheshimiwa Saleh Pamba na mchangiaji mwingine atakuwa ni David Kafulila.

Kuna tangazo; Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, Dkt. Fenella Mukangara, anaomba niwatangazie Wabunge wote kwamba mazishi ya Mwandishi wa Habari Samwel Chamlomo yatafanyika saa kumi, Ibada ya mazishi itaanza saa nane huko Kikuyu na mazishi yatafanyika saa nane kwenye makaburi ya *Saint John*, Kikuyu na Ibada itafanyika nyumbani kwake eneo la Mlezi. Kwa hiyo, wale wote wakaokuwa na nafasi wajumuike kwenye Ibada ambayo itaanza saa nane.

Baada ya hayo, naomba kusitisha Bunge hadi saa kumi jioni.

(Saa 8.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dunstan Kitandula!

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niwe mchangiaji wa kwanza jioni hii ya leo. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametujali uzima na anaendelea kutufanikisha katika mambo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu kibajeti wote tumeshuhudia kwamba ni mwaka mgumu sana kimapato. Ni changamoto kubwa katika Taifa letu, changamoto ambayo imesababisha mambo mengi, tumeshindwa kuyakamilisha kwa jinsi tulivyokuwa tumekusudia. Imani yangu ni kwamba changamoto hii ya kibajeti ya mwaka huu itatupa funzo la kujipanga vizuri ili tuweze kujitegemea wenyewe katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie makusanyo tuliyokuwa tumeyatarajia kwa Wizara hii na kile tulichokipata. Katika mwaka wa fedha tunaomaliza tulikuwa tumekusudia kupata makusanyo kutoka sekta ya uvuvi ya takribani bilioni 11.6. Makusanyo tuliyoyapata kwenye sekta hiyo ni takribani bilioni 1.3 sawasawa na asilimia 98. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye sekta ya kilimo tulitarajia makusanyo ya bilioni 12.7, tumekusanya bilioni 6.4, takribani asilimia 51. Kwa nini nayasema haya? Nayasema haya kuonesha umuhimu wa sekta ya uvuvi katika Wizara tunayoijadili. Pamoja na kwamba wakati mwingine sekta hii imeonekana kama mtoto yatima, lakini ushahidi wa kimakusanyo unatuambia kwamba tukiweka nguvu zaidi katika sekta ya uvuvi, tuna uwezo mkubwa sana wa kupata mapato. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa kwa ushahidi huu iweke nguvu katika sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri katika hotuba yake anakiri kwamba sekta ya uvuvi ni sekta inayotuhakikishia usalama wa chakula, ni sekta inayotuhakikishia ajira, lakini sekta inayotuhakikishia utulivu wa mawazo kwa raia wetu. Kama haya ndivyo, basi wakati umefika, ni wakati muafaka sasa tuwekeze nguvu katika maeneo haya. *(Makofi)*

Cha kusikitisha ni kwamba, mchango wa sekta hii unashuka siku hadi siku. Hili linasikitisha! Umeshuka kwa asilimia mbili ukuaji wa sekta hii, lakini hata mauzo yetu nje ya nchi yamepungua na Waziri na timu yake wanatuambia kwamba kupungua huku ni kwa sababu ya ukosefu wa soko, jambo ambalo sikubaliani nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani nalo siyo kwa sababu nimeamua kuwa mkaidi tu, hapana, tafiti za Kimataifa zinaonesha kwamba, kama kuna sekta ambayo ukuaji wake umekuwa mkubwa katika sekta ya kilimo ni katika eneo hili la ufugaji wa samaki na uvuvi. Hata hivyo, pamoja na ukuaji huo, bado kuna nakisi kubwa, bado kuna pengo kubwa la kufikia mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sio kweli kwamba soko halipo, ninachokiona mimi ni kule kutochangamkia soko hili. Kwenye *marketing* sisi kuna kitu kinaitwa *first mover advantage*. Ukishashika soko anayekuja mara ya pili anapata shida ya kuingia kwenye soko hilo, tatizo letu lipo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakenya wanafanya vizuri hawana tatizo la soko, Waganda wanafanya vizuri hawana tatizo la soko! Wanigeria sasa hivi wanapunguza, yaani kwa jinsi ambavyo wamekamata soko lao hata ule uingizaji wa samaki kutoka Mataifa ya Asia umepungua. Kwa hiyo, soko katika Afrika ni kubwa na sisi tuna uwezo wa ku-*penetrate* kwenye soko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni sekta inayovutia mpaka Mataifa makubwa. Kwa miaka kumi na tano iliyopita China ndiyo ilikuwa inaongoza kwenye sekta hii, sasa anapigwa vikumbo na Wamarekani, Wajapan na Vietnam. Kama mataifa makubwa haya yameona umuhimu wa kujiingiza kwenye sekta hii, sembuse sisi Taifa dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishasema sana juu ya jambo hili na takwimu hizi ukizipitia zinasikitisha kidogo. Ukiangalia takwimu zilizotolewa na Wizara juu ya *potential* tuliyonayo, ukubwa wa eneo la Bahari, Maziwa na Mito na kile ambacho tunavuna havilingani hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua hata ukuaji wa idadi ya wavuvi, ukiangalia takwimu zile zilizotolewa zinaonesha wavuvi wetu wengi wanapatikana, takribani laki moja na tatu wanapatikana kwenye Ukanda ya Ziwa, lakini Ukanda wa Ziwa ni mdogo ukilinganisha na maeneo ya uvuvi kwenye Ukanda wa Bahari, nini kimetokea? Maana yake ni kwamba, uwekezaji umefanyika mkubwa kwenye eneo la Maziwa yale kuliko kwenye eneo lingine lolote lile. Tutumie rasilimali zetu ili tuwaondoe wananchi kwenye lindi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo lilikuwa linazungumzwa na wenzangu nami niliseme kidogo. Serikali imetuhidi kujenga Bandari ya Uvuvi, jambo jema la kutuhakikishia tunaziba mianya ya mapato, lakini eneo linalopendekezwa lina changamoto kubwa. Haingii akilini kufikiria eneo kama Dar-es-Salaam ukaenda ukaongeza Bandari ya Uvuvi pale kwa msongamano tulionao. Sasa hivi tunapata shida ya kutafuta fedha, ili tugharamie wananchi wale wasogee kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kufikiria kupeleka Bandari hii mahali kama Dar es Salaam haingii akilini, lakini hata Bagamoyo haingii akilini! Tuna ujenzi mkubwa sasa hivi tunaukusudia wa Bandari pale Bagamoyo. Sasa ujenzi huu halafu twende tukapeleke tena ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, nadhani siyo sahihi. Ili kuleta utulivu katika nchi yetu, lazima rasilimali hizi na mambo haya ya kimaendeleo tuyagawanye kwenye maeneo mbalimbali. Njooi Tanga, leteni Bandari hii Tanga, Mkinga, Moa, tuna kina kirefu, tuna eneo kubwa, tupo tayari njooi tuje tuwekeze eneo lile tuweze kuleta maendeleo kwenye maeneo mengine katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuzungumzia, ni sekta ya usindikaji wa maziwa. Tuna changamoto kubwa sana katika eneo hili. Hotuba ya Waziri inatuambia tuna viwanda 82. Viwanda hivyo 82 uwezo wake wa kusindika ni lita 640,800, kwa siku, lakini tunazosindika ni lita 167,070 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake tunatumia uwezo wa viwanda hivyo 82 tulivyonavyo, tunatumia asilimia 26 tu ya uwezo wa viwanda hivi. Lazima kama Taifa tujiulize kuna nini na kwa nini hatutumii *potential* ya viwanda tulivyonavyo kwenye kusindika maziwa yetu? Kwa nini maziwa yetu mengi yanamwagwa badala ya kusindikwa, kwa nini Wakenya wanasindika zaidi kuliko sisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Sara Msafiri!

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati, akianza Mwenyekiti wetu wa Kamati Profesa Msolla na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, tunajua ina changamoto nyingi sana na tumekuwa na ufinyu wa bajeti kwa kipindi hiki cha mwaka huu, lakini wamejitahidi kidogo kwa hatua moja wamesogea. Kwa hiyo, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda pia kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ni kwa muda mrefu sana kwa Mkoa wa Morogoro tumekuwa na migogoro hii ya wakulima na wafugaji, lakini Bunge la Bajeti lililopita kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba Serikali itaanza kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji na kuhakikisha inaweka matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutoa shukurani kwa Serikali yangu, kwa sababu kwenye mpango wa awali Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro wamewekwa kwenye mpango na hivi tunavyoongea Halmashauri ya Kiteto wameshamaliza upimaji bado kuhakiki na wapo mbioni kuja kwenye Wilaya ya Mvomero. Watanzania wote ni mashahidi, wamekuwa wakishuhudia migogoro mikubwa sana kwenye Wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro na Wilaya zingine za Mkoa wa Morogoro zimekuwa na migogoro mirefu sana na ya kudumu ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua, hata tuweke sheria hivi, kama kutakuwa hakuna mipango ya matumizi bora ya ardhi, migogoro hii itakuwa inaendelea tu.

Kwa hiyo, njia pekee ni kuhakikisha ardhi inapimwa, wakulima wajulikane wandima wapi, wafugaji wajulikane wanafuga wapi! Kama ni eneo la wafugaji basi, kama mkulima yupo hapo ajue anabadilisha shughuli za uchumi, ahakikishe anafuga na kama mfugaji yupo kwenye eneo la wakulima basi anawajibika kuondoka au kuhakikisha anabadilisha shughuli zake, aanze kushikiri kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni hatua kubwa sana kwa Serikali na niombe tu kwamba, kupitia mipango mingine inayokuja, tunajua sasa hivi tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu hasa Chama changu cha Mapinduzi kihakikishe kinaweka kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuhakikisha kwamba ardhi ya Tanzania yote inapimwa ili kuepuka hii migogoro inayoendelea mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata yale maeneo ambayo tunasema yameanza kupimwa, endapo kama mwananchi yupo kwenye eneo la wafugaji, lakini anataka kulima na eneo lile lote ni la wafugaji, basi achague eneo lingine la kwenda kuishi. Hata kama ni nje ya Mkoa wa Morogoro lakini aende kwenye maeneo ambayo anafikiria kazi zake anazozifanya zipo sambamba na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nimesikitishwa sana na hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo imesomwa hapa na dada yangu Mkiwa kwenye ukurasa wake wa kumi na nane. Ukisoma kwenye ukurasa ule wa nane utaona kwamba kauli hii iliyotumika ni kauli ambayo ni ya uchochezi, kwa sababu ukisoma kwenye ukurasa wa nane wanasema kwamba Watanzania wamekuwa wakisikia kwamba Serikali hii iliyokuwa madarakani inawaambia wafugaji wapunguze mifugo yao, waache ufugaji wa kuhamahama, wafuge kisasa. Kwa hiyo, wanasema hii kauli kwamba ni kashfa kwa wafugaji, kwa sababu wafugaji wao mifugo ni utajiri, basi wanatakiwa wao waendeleo kufuga tu wasiwe na ukomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kauli kama hizi kwa vingozi wenzetu wanazozitoa, wajue kwanza wanawachonganisha wananchi, wanawachonganisha wakulima na wafugaji, wananchi na Serikali yao. Kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza akakaa, akawa anafanya kazi nje ya mipaka ya eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukitaka kujenga nyumba, huwezi ukajenga mpaka eneo la mwenzako, hata kama tunasema kuna hifadhi za maliasili zina mipaka. Hata kama tunasema kuna hifadhi kwenye maeneo ya jeshi kuna mipaka na hata wakulima wana mipaka. Hata kama Serikali inataka kuchukua eneo lolote lile kuna utaratibu. Kwa hiyo, kuwaambia wafugaji kwamba waendeleo kufuga, wawe na mifugo kama wanavyotaka wao, siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumeendelea kusisitiza kwamba kuwe na usawa kwenye mgawanyo wa rasilimali. Usawa huu ni pamoja na kwenye huduma za kijamii. Hawa wafugaji wote ni mashahidi, wanafanya ufugaji wa kuhamahama. Leo yupo Kiteto, kesho yupo Mvomero, Ulanga, Kilombero, Morogoro Vijijini, mara sijui yuko wapi! Hivi mtu anayefuga na kuhamahama hivi lini atafanyiwa mikakati ya kuwekeza kwenye eneo moja? Akinamama watapataje huduma za afya, watoto watapataje huduma za afya, watoto watakwendaje shuleni? Maana yake mfumo wa ufugaji wa sasa uliopo baba, mama na watoto ni kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mfugaji ana mifugo 4,000 lakini ana nyumba ya tembe tu kwa sababu kesho na kesho kutwa malisho yakiisha itabidi ahame. Hizi huduma tunazozipeleka kwa wananchi, kama leo hii hotuba ya Kambi ya Upinzani inasema kwamba Serikali inavyowahamasisha wafugaji wakae eneo moja ili wajengewe miundombinu ya ufugaji na ili waweze kufuga kwa faida na wapunguze mifugo yao, wanasema kwamba ni kashfa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hii si sawasawa na hii siyo haki na haya masuala ya kuhamahama yalishapitwa na wakati. Enzi za Hayati Mwalimu Nyerere yalishakwisha. Tulishafanya *villagization policy*, ujamaa na kujitegemea. Watu wakaacha kuhamahama, wakaanzisha Vijiji, vikarasimishwa tukapata maendeleo. Leo hii kiongozi anasimama anasisitiza wafugaji waendeleo kufuga kadri wanavyotaka na wahame kwa kadri wanavyotaka! Serikali inapotaka kuleta nguvu kuwaongezea uwezo waweze kufuga kisasa na kupewa elimu ya ufugaji bora, wanasema ni kashfa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haiwezi kukubalika kwa sababu hata hiyo fursa sawa kwa wananchi wetu haiwezi kupatikana, kwamba jamii moja inasoma, jamii nyingine inaamka

asubuhi mpaka usiku inatembea na mifugo haipati huduma zote za kijamii, hii sio sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusisitiza, tunajua Watanzania asilimia 80 wanaishi Vijijini na hawa ni wakulima na wafugaji. Hilo halipigiki! Kwa hiyo, tunaomba Serikali yetu sasa kwa kipindi hiki kinachokuja hasa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iwe na mkakati maalum wa kusaidia haya makundi mawili. Haiwezekani mkulima analima, anavuna hana soko na mfugaji anafuga, ana mifugo mingi hana soko! Tutaondoaje umaskini kwa aina hii mtu ana rasilimali lakini hana sehemu ya kuzipeleka.

Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ihakikishe inawezeza kwenye makundi haya makubwa ya wakulima na wafugaji, kwa sababu hawa ndio wanaoishi vijijini na ndiyo asilimia themanini ya Watanzania. Hatuwezi tukaondoa umaskini kwa kuliacha hili kundi kubwa la wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni masuala ya utafiti lazima yaongezwe. Sasa hivi ni soko huria, usipotaka Msukuma aje Morogoro atakuja Mchina kuwekeza, atafuga kisasa na atalima kisasa. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe tunafanya utafiti wa kutosha tunawajengea uwezo wakulima na wafugaji na wananchi wote ili waweze kwenda kwenye ushindani wa soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nimeona niliseme haiwezekani mfugaji ana ng'ombe 4,000 anakuja anaomba joshu la Serikali. Wakulima wanalima, wanaikopesha Serikali mazao, wanalipwa kidogo kidogo, basi ifikie hatua na kwa wafugaji kuwe na mpango maalum, wapunguze ng'ombe zao, wawekeze kwenye majosho, Serikali iongezee, hela ikipatikana nao walipwe kidogo kidogo, wasikae wanaisubiri Serikali kwa asilimia yote. Isipofanya wataendelea kubaki hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wameanza, wanalima, wanavuna, wanaikopesha Serikali na wao waanze kupitia vikundi vya vya wafugaji, wajenge majosho, waishirikishe Serikali, washirikishe *private sector*, waone namna ya ku-*compansate* gharama wanazozitumia, lakini wasisubiri kuingojea Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Marombwa, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa Lwanji wajiandae.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku hii ya leo. Pia nikupongeze kwa kazi kubwa unayoifanya, Kiti kimekutosha kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wachangiaji waliopita kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, lakini pia Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya, kwa kipindi kifupi lakini naona wanajitahidi sana. Nawapongeza kwa sababu kwanza wamekuwa wakitembelea maeneo na kuweza kujua hali halisi ya wananchi na shughuli wanazozifanya katika maeneo yao. Vile vile mimi binafsi kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana kwa jitihada waliyoifanya katika kuendeleza soko la samaki la Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na tatizo kubwa la umeme, lakini sasa hivi jenereta zimeshanunuliwa, pamoja na kwamba pia na umeme wa *line* ya 33Kv unakwenda huko, ina

maana tutakuwa na uwezo wa kuhifadhi samaki kwa uhakika, kwa sababu tutakuwa na *standby generators*, kama tutakuwa na ule umeme wa *grid*, lakini vile vile hata jenereta peke yake zinaweza zikafanya kazi. Pia nawapongeza kwa kutengeneza mwalo wa Kirando na kufuatilia mifugo hususan ng'ombe katika mashamba yaliyopo maeneo ya Nkansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia kwa jitihada nyingine ya kuanzisha kituo kwa ajili ya kuendeleza ufugaji bora wa kisasa, lakini pia kudhibiti magonjwa huru ikizingatiwa kwamba Kanda ya Nyanda za Juu Kusini hususan Mkoa wa Rukwa tumo katika Kanda ya magonjwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mambo yote hayo hatuwezi kusema kwamba hakuna changamoto. Naomba nitoe changamoto kwa upande wa pili, kwa upande wa Wavuvi kwa ujumla. Ukiangalia hiki kitabu taarifa nyingi zilizoenezwa ni taarifa za mifugo zaidi, za uvuvi zipo lakini ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo hatujayatendea haki ipasavyo. Ukiangalia maeneo yote yanayozunguka Maziwa, wananchi wake hawajafaidika vizuri na rasilimali zilizoko katika Maziwa na hata ukifuatilia katika takwimu za maeneo ya watu waliodumaa, utakuta kwamba Mikoa ambayo wananchi wake wako kandokando ya Ziwa ni wale ambao wanaonekana kuwa na lishe duni na kudumaa, wakati tunaambiwa kwamba samaki ndiyo chanzo kikubwa cha *protein*, ndiyo chanzo kikubwa cha madini mbalimbali.

Sasa ni kwa nini hapo ni lazima tujiulize ni kwa nini. Kwa nini hawa wananchi wapo jirani na samaki lakini bado wamedumaa, bado wanakosa hayo madini? Ni kwa sababu hawajawezeshwa kiasi cha kuweza kuvuna rasilimali zao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najisikia vibaya sana, mara nyingi unakuta wakati mwingine ikifika usiku naanza kupigiwa simu, mama tunadaiwa bili, tunadaiwa kulipa ushuru. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Nyasa, Wilaya ya Nyasa inategemea hasa zao la kahawa kwa upande wa Umatengo, lakini zao la samaki na dagaa kwa upande wa ziwani. Hata hivyo, hawa wavuvi bado mpaka leo wanavulia vile vimitumbwi vidogo vidogo ndiyo wakashinde huko, ukimkuta upepo, maarufu tuncita (Mbelu) anachukuliwa huko huko, aliyepona bahati yake.

Kwa hiyo, unakuta kwanza kipato anachopata ni kidogo sana, lakini wakati huo huo pamoja na hicho kipato kidogo bado anahitajika achangie Halmashauri yake ili iweze kujiendesha. Sasa najjuliza, hivi hawa wananchi wavuvi peke yao wao ndiyo hawastahili kuwekewa mtaji wa kuwatoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano katika mazungumzo tunayosema hapa mara kwa mara. Tunasema ujenzi wa reli ni uti wa mgongo, Taifa ili liweze kuendelea tuwekeze kwenye reli. Tunaposema kuwekeza kwenye reli ina maana Serikali yenyewe inatafuta fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye miundombinu ya reli, hali kadhalika kwenye barabara kuwezesha uchukuzi na sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hawa wavuvi ambao wamekosa hata *seed money*, miaka nenda rudi wanavua kwa yale magogo na maisha yao ndiyo hayo, Serikali ina mpango gani wa kuona kwamba sasa tunachukua hatua za makusudi, kuchukua boti kuwapa wale wananchi waweze kuanzia kama mtaji wao na wenyewe wapate ruzuku inayoonekana kwa macho. Kwa mfano, ruzuku ya mahindi isipotolewa, watu wote hapa tunapiga kelele, hawa wa boti ruzuku zao mbona hazionekani moja kwa moja, hizo vocha wao kwa nini wasipewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia hata kwa upande wa Maendeleo ya Vijana, ajira pamoja na michezo, nimeangalia katika ugawaji wa fedha zilizotolewa kila Mkoa, nimekuta mikoa hii ambayo imetoka katika maeneo haya ya Maziwa, kwa mfano, Mkoa wangu wa Rukwa hakuna kijana aliyewezeshwa, Ziwa Nyasa hakuna kijana aliyewezeshwa. Sasa hizo fedha na zenyewe zilitolewa vipi kiasi kwamba vijana hawa wengine hawakuweza kupata?

Kwa hiyo nadhani tuone kwamba kuna haja ya kusaidia watu, haiwezekani miaka nenda rudi tunazungumza hilo hilo na kwa bahati nzuri Wizara imeanzishwa rasmi kwa ajili ya kazi hiyo, nadhani imeanzishwa siyo tu nadhani ndiyo ukweli kwa nia njema ya kuona kwamba hii sekta inakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hawa Waheshimiwa Mawaziri kama watakuwa hawawezi kupata bajeti ya kutosha ili wafanye hayo yanayowezekana, nadhani itakuwa bado hatujaitendea haki Wizara yao. Kwa hiyo, nafikiria kwamba na ili kuwezesha hilo, kwanza Wabunge wenyewe tuwe na ile dhamira njema, tuwe na hayo maamuzi, kwa sababu wanaotoa bajeti hapa wanaopitisha ni Wabunge, tuiseme ni Serikali, ni Bunge. Kazi ya Bunge ni kupitisha Bajeti, sasa iweje kila siku tunaisingizia Serikali wakati sisi ndiyo tunaopitisha bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema kwamba tuweke hata Kamati yetu ya Bajeti, huku kwenye Uvuvi kwa nini tuendeleo kupiga kelele kila siku? Kwa nini hatujaona kwamba haya Maziwa Makubwa yatusaidie? Kwa nini hatujaona kwamba sasa wale Wavuvi ambao wapo mwambao mwa Bahari ya Hindi, Wavuvi walioko Kanda ya Ziwa Tanganyika, Wavuvi waliopo kando ya Ziwa Nyasa wanafaidika na rasilimali ambazo zipo katika Ziwa Nyasa. Samaki wanakaa mle mpaka wanazeeka kwa sababu wapo katikati ya maji hawawezi kuvuliwa. Kwa hiyo, naomba sana tuone namna bora ya kuiongeza bajeti katika eneo hili. Vile vile naomba utafiti ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa tumesema kwamba wananchi wavulie nyavu za aina fulani, lakini kwa kuangalia kila siku naona kuna tatizo fulani ambalo sijapata majibu. Dagaa wale nikiwa wakati huo msichana sana, walikuwa wanakuwa wakubwa kiasi kwamba unaweza hata ukapata mafuta ya dagaa, lakini siku hizi huwezi kupata dagaa wakubwa kwa nini? Ziwa Nyasa siku hizi huwezi kupata dagaa wakubwa kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwamba labda yawezekana ile kusema kwamba wavulie nyavu za size fulani, huenda wale dagaa wanazaliana wengi sana kiasi kwamba sasa wananyang'anyana chakula, hayo ni maono yangu ya kawaida. Kwa hiyo, naomba pengine ufanyike utafiti, je, ile hali tu ya kuzuia tusivue katika maeneo hayo inatosha au pengine kuna sababu ya ziada inayowezesha pengine watu wakavua na kuweza kuwafanya hao dagaa waweze hata kukua.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nakushukuru ila saa yako inakimbia sana.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Marombwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa Lwanji!

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza naunga mkono bajeti hii, lakini kwa leo lengo langu sana ni kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msemaji aliyemaliza hapa alikuwa anazungumzia ni namna gani sekta ya uvuvi katika nchi yetu haipewi kipaumbele. Ukiangalia hiki kitabu kama alivyosema Mheshimiwa, naangalia kuanzia ukurasa wa 43 mpaka ukurasa wa 71 unazungumzia uendelezaji wa sekta ya mifugo. Kurasa karibu 30 zinazungumzia maendeleo ya mifugo, lakini kuanzia ukurasa wa 72 uendelezaji wa sekta ya uvuvi una kurasa tisa tu! Kuanzia pale ukurasa wa 72 unaishia mpaka ukurasa wa 80. Sasa tunajuliza ni kitu gani kinachosababisha mpaka sekta hii ya uvuvi katika Wizara hii haipewi kipaumbele chochote na badala yake kipaumbele kinapewa sekta ya mifugo peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama kutakuwa na uwezekano ushauri wangu baadaye, kwamba, ni vizuri katika Wizara hii kuwepo na Naibu Mawaziri wawili, mmoja ashughulikie mifugo na mwingine ashughulikie uvuvi kama ilivyokuwa kwenye Nishati, kuna anayeshughulikia madini na anayeshughulikia nishati. Tukifanya hivi tutaipatia kipaumbele Wizara ya Mifugo kwa sababu kutakuwa na mtu *specific* ambaye anashughulikia suala hili, lakini kwa sasa sisi Wavuvi hatupewi kipaumbele kabisa, hakuna kipaumbele!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mwenzako anapewa kurasa 30, wewe unapewa kurasa kumi, wewe ni *minor* katika hiyo Wizara, ushauri wangu wa kwanza ndiyo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka tu nijue kwenye ukurasa wa 76, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki ya Dunia, imeandaa mradi wa *Southwest Indian Ocean Featuring Governance and Shared Growth Program*, unaitwa (*SWIOFISH*) unaotarajia kuanza Julai 2015. Mradi huu unalenga kuboresha fursa kiuchumi, kijamii na mazingira miongoni mwa jamii za Wavuvi kutokana na rasilimali za uvuvi katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi, ndiyo kitu gani hiki na huu mradi unataka kuzungumzia jambo gani kwa wavuvi waliokuwa kwenye bahari ya hindi. Naomba sana suala hili tupatiwe ufafanuzi ili tuweze kujua kuna nini ndani ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti hii ambayo imeletwa mbele yetu, naiomba Serikali, kwa muda mrefu sana naishauri Serikali, mafunzo mengi yanatolewa kwa wavuvi ambao hatuwajui sisi. Mimi natoka kwenye sehemu ya uvuvi, Wilaya ya Rufiji ndiyo inayozalisha zaidi ya asilimia ya Kamba (*prawns*) katika Tanzania yetu, lakini hakuna hata mtu mmoja aliyepata mafunzo hayo. Hebu mtuambie hayo mafunzo ambayo yanatolewa kwa watu 30, watu 40 Wilaya ya Rufiji inayapata wapi hayo mafunzo? Wamepewa watu gani hayo mafunzo na hasa ukizingatia ndiyo Wilaya inayozalisha Kamba kwa wingi katika Tanzania. Hilo nataka kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kujua na nataka kushauri, kwa muda mrefu tuna matatizo makubwa sana sisi watu wa maeneo ya Delta Mto Rufiji tunaozalisha samaki aina ya kamba. Matatizo yetu ni kwamba sisi sasa tunakuwa tu watoaji wa mbegu za Kamba kwa viwanda vingine, Wilaya ya Rufiji ndiyo inazalisha hizo mbegu kuzipeleka kwenye kiwanda cha *TANPESCA* pale Mafia na wao wanapata *billions of shillings* kutokana na sisi kuwapeleka hizo mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kulikuwa na mgogoro wa kimazingira, hivi wenzetu hawa wa *TAFIRI* wamefanya utafiti gani? Sisi tuliomba kwa muda mrefu, hebu fanyeni tathmini za kimazingira ili na sisi wakazi wa maeneo ya *Delta* ya Mto Rufiji tuweze kufuga samaki aina ya kamba kama wanavyoweza kuzalisha wale wenzetu wa Mafia ambao sisi tunawapelekea mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kungekuwa na uwezekano wa sisi kuzalisha kwa sababu sisi ndiyo tunawapelekea mbegu, tungeweza kuchimba mabwawa yetu, tukazalisha na Serikali ikafanya utafiti wa kina, naamini sekta hii ya uvuvi kwenye Wilaya ya Rufiji ingekuwa imetoa mchango mkubwa kuliko sekta nyingine zozote katika nchi yetu hii. Kwa sababu wale wenzetu wa Mafia wanapata fedha nyingi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kutokana na samaki aina ya kambak mbegu zenyewe zinatoka Rufijik lakini Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ndiyo inayopata pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na sisi tunaomba wenzetu wa *TAFIRI* wanafanya kazi gani? Kwa nini hawaji Rufiji kuchunguza, waangalie, waone, ili kama kuna uwezekano wa kufuga, wakati huo ilikuwa imeshindikana, sasa hivi kama wenzetu wa Mafia wanafuga, kwa nini sisi wa Rufiji tusifuge hawa samaki aina ya kamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana fanyeni *research*, fedha mnazo, mje na sisi Rufiji kule eneo la *Delta* ili mtuongoze, kama tunaweza kufuga vizuri, kama hatuwezi kufuga vile vile mtuambie. Haiwezekani *research* iliyofanyika mwaka 2000 ikawa *valid* mpaka leo mwaka 2015, haiwezekani! Kwa sababu dunia yetu inaendelea kisayansi, kiteknolojia, tunaomba sana Kitengo cha *TAFIRI* kifanye *research* hiyo ili waweze kuja kule kwetu na kuweza kuangalia uwezekano. Kama tunaweza kufuga samaki aina ya kamba itakuwa ni bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, tuna migogoro Rufiji, hasa migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Serikali imeweka mipango yake, tunashukuru sana mipango hiyo inakwenda vizuri, lakini migogoro hii Rufiji ni mikubwa mno. Wenyewe mmeona juzi tu, hata wiki bado, watu wamepigana kule katika Kijiji cha Kilimani. Wenyeviti wawili wa Vijiji, Wilaya ya Rufiji, pamoja na Askari mgambo wa Kijiji wamepigwa na wamepigwa na wafugaji, juzi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mkuu wa Wilaya ndiyo amekwenda kutatua lile tatizo, lakini Mkuu wa Wilaya tunamwumiza mno! Rufiji matatizo yetu makubwa ni hayo tu ya migongano baina ya wakulima na wafugaji. Ukiangalia kwa kiasi kikubwa sana tatizo tulilokuwa nalo sisi linatokana na baadhi ya wafugaji ambao wanaingia Wilaya ya Rufiji bila vibali. Je, Serikali ina mkakati gani sasa, sisi Rufiji tumeweka mkakati, lakini wao wanaingia kibubu bubu, je, Serikali ina mkakati gni wa kuhakikisha kwamba wale ng'ombe wote walioingia kwa njia za panya wanaondolewa kwenye Wilaya yetu ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna uwezo wa ku-*accommodate* ng'ombe zaidi ya laki tatu, lakini hili limejitokeza na jana Mkuu wa Wilaya amekwenda, amesuluhisha ule mgogoro, lakini naomba wale Viongozi wawili wa Vijiji pamoja na yule Askari wamekamatwa, wakawekwa ndani, kwa sababu walikuwa wanakwenda kuangalia nini kinachoendelea kwenye mgogoro huu. Kwanza wamepigwa na wafugaji, wakakamatwa na Askari, wakawekwa ndani, Wenyeviti wawili wa Vijiji, hii ni dhambi kubwa! Dhambi hii itatupeleka mbali sana na inaweza kusababisha vifo, kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kusema ndani ya Bunge hili kwamba wenzetu wafugaji wana nguvu sana ya pesa, wakulima sisi hatuna nguvu ya pesa. Wenzetu wana nguvu sana, anauza ng'ombe wawili wanapata pesa nyingi, wanaweza wakatumia njia zozote, sisemi

kama walihonga au walifanya nini, lakini hakuna hata kesi moja ambayo mkulima na mfugaji ameliwa mazao yake au mkulima amepigwam yule mkulima akapata haki, haipo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Viongozi wetu wa Wilaya wachunguze ni sababu gani zilisababisha wale watu wawekwe ndani ili tuone na sisi kwamba haki inatendeka. Hata hivyo, niombe kwamba hebu mje Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishazungumza siku moja kwamba Wilaya ya Rufiji tulikuwa na haya mabwawa *ox-bow lakes* nyingi sana, zimekauka zote, hivi watalaam wa mazingira wapo wapi? Waende wakaangalie hizi athari za ng'ombe hazionekani, hizi faida ninyi ni ng'ombe tu, mimi sikula ng'ombe mpaka nafikisha miaka 18, ndiyo nimekula ng'ombe, nilikuwa nakula samaki tu kwa muda wote huo, na wala sikuwa na matatizo yeyote na nipo *giant* kutokana na samaki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba waje watu wa mazingira Wilaya ya Rifiji, waje waone athari kubwa zinazosababishwa na ng'ombe waliokuwa katika Wilaya ya Rufiji, *oxbow lakes* zaidi ya nane zimekufa, lakini watupe na mwongozo tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati fulani ambayo ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri walikwenda kule, walipokwenda walikuwa wanapita pembeni tu hawakufika katika migogoro. Sasa mfike kwenye migogoro, msikae kwa siku moja au mbili, mkae kwa muda mrefu, muone ni namna gani mnaweza kutusaidia sisi watu wa Rufiji ambao tunahangaika sana na ng'ombe na mpaka sasa hivi uchumi wetu wa Rufiji unapungua. Sisi ni wakulima na wavuvi, lakini ule uvuvi wetu na ukulima wetu unashuka chini sana kutokana na suala hili la ng'ombe. Naomba mje, huo ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Yussuf Hussein ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa naunga hoja kwa asilimia mia moja. Pili, nakubaliana na maoni ya Kamati ambayo yametolewa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya mifugo pamoja na uvuvi ni muhimu sana hasa kwa wananchi kwa sababu ya kupunguza umaskini pamoja na kuongeza lishe. Wananchi wengi hapa Tanzania wamehamasika sana, utakuta kuwa kila familia, kwa wastani ina mifugo ya aina mbalimbali; ina ng'ombe, ina nguruwe au kuku au mbuzi, tatizo ni moja tu, tatizo kubwa tullionalo ni Afisa Ugani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wafanyakazi wenzake wanafanya vizuri kwenye Wizara hii na wamesema kuwa, Wagani wameongezeka, kwa mfano, 2013/2014 tulikuwa na Afisa Wagani 6,041 ambao walikuwa ni wa mifugo. Mwaka 2014/2015 tumekuwa na Afisa Wagani 8,541, lakini hitaji ni 17, 325. Hapo unaweza ukaona kuwa, kuna upungufu mkubwa sana. Tatizo sio kusema kuwa hawasomi, tatizo wahitimu wapo na wanahitajika, lakini hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ombi kwa Serikali yangu inayohusika, naomba sana iweze kuajiri. Naamini vibali vinaombwa, kwa hiyo, naomba vibali vitolewe ili hawa watu waweze kuajiriwa. Tulishapitisha kuwa, kila kijiji kiwe na Afisa Kilimo na kiwe na Afisa Mifugo, lakini unakuta hakuna mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, elimu ni muhimu; hasa unakuta mkulima au mfugaji anafuga, lakini hana taaluma ya mifugo, hajui jinsi ya kutibu magonjwa, hajui jinsi ya kutoa lishe hasa kwa upande wa kuku au vyakula vingine. Kwa hiyo, unakuta ni tatizo kubwa. Kwa hiyo naomba sana hili jambo litiliwe maanani la kuweza kuajiri Maafisa Ugani kwenye vijiji vyetu kusudi wananchi wafugaji waweze kupata elimu ya kutosha kuweza kuhudumia mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa ambalo nimeliona ni kwa upande wa Wataalam wa Uvuvi. Wataalam wa Uvuvi bado ni wachache na sisi tunahamasisha sana kuhusu ufugaji wa samaki katika mabwawa, lakini unakuta tatizo ni kuwa, bado hawajawa wengi kwa hiyo na yenyewe inaendeleza hapo. Naomba nayo waweze kupata hao Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Vyuo Vikuu pia. Tuna vyuo ambavyo vinatoa Cheti, tuna vyuo ambavyo vinatoa Diploma. Kwa hiyo, wahitimu wako wengi, lakini wako mitaani, kwa hiyo, naomba sana waweze kuajiriwa. Vyuo Vikuu kama *SUA* na chenyewe wako wahitimu wa fani mbalimbali ambao wanaweza na wenyewe kufanya kazi hiyo ya kutoa elimu kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine ni kuhusu bajeti. Tumeona kuwa bajeti ni ndogo. Bajeti ikiongezwa hii Wizara inaweza ikafanya kazi vizuri sana. Tumeona kuwa nchi yetu ya Tanzania ni nchi ya tatu kwa upande wa mifugo, lakini bado haijafanya vizuri kwa upande wa mapato! Kwa hiyo, huwezi kufanya vizuri kama Bajeti ni ndogo, lakini kama bajeti inatosha naamini kuwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake watafanya kazi vizuri sana na kuweza kutekeleza mambo yote waliyoyapanga yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti. Utafiti kwenye sayansi na teknolojia sasa hivi ni muhimu sana na utafiti hauwezi kufanyika kama hela haitoshi. Kwa hiyo, nashauri kuwa ile asilimia moja ya *GDP* ambayo tulishauri hapa Bungeni kuwa, iwe inatengwa kila mara, naomba iweze kutengwa kusudi watafiti waweze kufanya utafiti.

Hatuwezi kuendelea bila ya utafiti. Sasa hivi ni sayansi na teknolojia, kwa hiyo, tukitaka kuendelea lazima tufanye utafiti. Wako watafiti wengi wa vyuo hivi vidogo vidogo, wako watafiti wengi kutoka Chuo Kikuu cha *SUA*, lakini hawapati fedha za kutosha kusudi waweze kufanya utafiti wao tuweze kupata jinsi mpya kwenye mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda, viwanda bado ni vichache. Juzi juzi niliongelea kuhusu Kiwanda cha Ngozi, Morogoro, kuwa Kiwanda chetu cha Ngozi, Morogoro hakifanyi kazi tena na huo ni mfano mmojawapo kwenye viwanda vingine ambavyo havifanyi kazi, hasa vya upande wa mifugo. Kwa hiyo, naomba na nashauri kuwa, Serikali yangu iweze kufufua viwanda kama hivyo, kwa sababu, vilikuwa vinasaidia sana kwenye ajira; hasa ajira za vijana na akinamama, walikuwa wanafanya vizuri kwenye viwanda hivyo. Kwa hiyo, naomba viweze kufufuliwa, hasa pia viwanda yva usindikaji ili kuthaminisha mazao ya mifugo kwa upande wa maziwa, kupata mazao mbalimbali na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea Ethiopia. Ethiopia ni nchi ambayo ina mifugo mingi, lakini huwezi kukuta hata mnyama mmoja wa Ethiopia amechanjwachanjwa au amekatwakatwa ngozi yake. Wanathamini sana ngozi za mifugo yao na wanatengeneza viatu, wanatengeneza nini kutokana na ngozi, ndiyo zao lao kubwa. Kwa hiyo, naamini kuwa, tukitunza mifugo yetu vizuri na sisi tukapata soko kufuatana na mambo ya ngozi tunaweza kupata mazao na kupandisha kipato chetu cha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kumaliza bila ya kuongelea migogoro ya ardhi. Ni kweli, Serikali tunafanya vizuri, tumepanga mipango yetu mizuri kwenye bajeti hii, kuwa itatekelezwa.

Mpaka sasa tumeona Kiteto imeanza kutekelezwa, Mvomero tayari imeanza kutekelezwa. Ninachoomba sana tena sana, kwa sababu, hii migogoro ni mibaya sana, wakulima tunawahitaji, wafugaji tunawahitaji. Kwa hiyo, naomba sana tuheshimiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa ushuhuda kwa mfano, kule kwetu, hata Morogoro pale, unakuta kuna mahali ambapo wanakaa vizuri, wanaendelea vizuri, lakini unakuta sehemu nyingine hawakai vizuri! Kwa hiyo, naomba elimu na yenyewe iweze kutolewa kusudi tuweze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Ranch*. *Ranch* Mheshimiwa Waziri amesema zinaendelea vizuri, lakini ningeomba ziwepo na *ranch* za unenepeshaji kusudi tuweze kunenepesha mifugo na tuweze kuuza hii mifugo kwa muda mfupi, kusudi tuweze kutunisha pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu stahiki za wafanyakazi. Kuna wafanyakazi ambao wako kwenye sekta hii ya mifugo na hasa hasa, namaanisha Wahadhiri na Walimu. Wengine kwa kweli, unakuta stahiki zao sio nzuri, wanafunzi na wenyewe! Juzi juzi nimeshuhudia Chuo cha *LITI* pale Morogoro wamegoma!

Mheshimiwa Mwenyekiti, waligoma, lakini nashukuru walikwenda wakawaona wakaongea, lakini walikuwa na matatizo yao kuhusu mambo ya stahiki zao za malipo ya wanafunzi pamoja na vyeti vyao vya *LITI* wanavyopewa; wanasema kuwa havithaminiwi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anamalizia aweze kuwaelezea kuhusu hivi vyeti vya *LITI*, hasa kwa watu wa Stashahada na hawa wanaopata *Certificate* pamoja na *Diploma*, waweze kuelewa wanakwendaje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba pia, wanafunzi wetu tuweze kuwaeleza kuwa, kwenda darasani siyo kusema umesoma. Hapana! Kusoma hakuishi. Kwa hiyo, kitu kikubwa *Curriculum* yetu tuweze kuendelea vizuri na kufundisha kwa bidii sana jinsi ya ujasiriamali kusudi mwanafunzi ajue akimaliza kusoma aweze kujijiri yeye mwenyewe. Hasa kwa upande wa mifugo ni rahisi kujijiri wewe mwenyewe kwa sababu, wafugaji wanaopenda kufuga sasa hivi ni wengi, ila tatizo ni elimu, kwa hiyo, ujasiriamali ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo machache ambayo nilikuwa nayo, naomba kuunga mkono tena hoja. Nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lwanji!

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nichukue nafasi hii awali ya yote nikupongeze kwa jinsi unavyomudu hicho kiti na pia, nimpongeze Mnadhimu, Waziri wa Nchi, katika muda mfupi alioteuliwa kwa kweli, anajaribu kuongoza vizuri na si kujaribu tu, naona ni kama vile hii kazi alikwenda kuisomea mapema. Tunashukuru sana kwa hilo na ndiyo maana nyumba hii kidogo inapata utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna umuhimu wa Kamati ya Kanuni, ingejaribu kuangalia tufanye nini kuhusu ule uhuru mpana anaopewa mtu wa kuzungumza lolote hapa, ikiwemo uchochezi. Maana wananchi wetu wanaelewa nini maana ya uchochezi na nini maana ya upinzani wa kujenga. Sasa tunachokiona hapa muda mwingi ni uchochezi! *Reckless, impunity!* Yaani wanazungumza! Kwa kweli, sijawahi kuona kitu cha namna hii katika miaka yangu 10 ya hapa Bungeni na jinsi tunavyokwenda joto ndiyo linazidi kupanda. Hawajali amani tuliyonayo hawa watu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Lekule Laizer aliyooonea hapa asubuhi. Kweli, hatuwezi kuchezea amani tuliyonayo. Ni kisiwa pekee kilichobaki hapa sisi, nadhani ni bustani ya Eden, watu hawajui. Watu hawawezi kuwasikiliza kwa sababu ya matatizo, mkayakuza, mkaya-*amplify*, mkadhani kwamba, wananchi wanaweza waka-*riot*, haiwezekani!

MBUNGE FULANI: Cheap popularity.

MHE. JOHN P. LWANJI: *This is cheap popularity, you are very right!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa, kila mmoja hapa amepewa nafasi ya kutoka nje kutembea kwenda kujifunza kule masuala ya Kibunge, masuala ya maendeleo. Mbona tumekwenda nchi jirani hapa, unaambiwa bwana, uwe na tahadhari unapotembea na tunakushauri ikifika saa kumi na mbili afadhali ulale kabisa! Hakuna amani hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri tupime, tuone jinsi tunavyoweza ku-*regulate*, huu uhuru kwa kweli, umezidi na nadhani Kamati ya Kanuni ingeangalia ifanye nini ili kuweza kuwadhibiti hawa watu ambao ndimi zao hazina staha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye hoja, nawapongeza Waziri wa Mifugo na Naibu wake kwa kuja na Mpango mzuri wa maendeleo ya mifugo na uvuvi kwa mwaka 2015/2016. Pia, nipongeze kwa utekelezaji wa Wizara hiyo, japo wamekuwa na matatizo ya ufinyu wa bajeti na kila mmoja anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nina mambo machache, upungufu ni mwingi kutokana na tatizo hilo, lakini ningepomba tu kitu cha kwanza nisije nikasahau, kwa muda mrefu nimekuwa nikizungumzia ile *Ranch* ya *Tanganyika Packers* ambayo iko Kata ya Kitaraka, Tarafa ya Itigi, Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *Ranch* imeshindikana kuibinafsisha, huo ndio ukweli! *Book value* ya hiyo *Ranch* ni sifuri. Majengo yale hayawezekani mtu yeyote kuyahusha tena, haiwezekani. Kwa hiyo, nashauri, toka awamu ya pili nafikiri ya tatu ile wameshindwa! Ile *PSRC* sijui nini, majina yamebadilika *Holding Corporation* sijui, wameshindwa kubinafsisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja watu wengi wa Mataifa ya aina mbalimbali, wameshindwa kuweza kuchukua hiyo *Ranch*, lakini imeleta mfarakano kwa wananchi, wananchi hawana raha kukaa katika ardhi yao na maeneo yao. Mifugo ina shida ya mahali pa kuchungia na malisho yake yanakuwa haba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali ione uwezekano wa kuwapa eneo hilo wananchi wa Kitaraka, Msisii na maeneo hayo ya Doroto, ili yaweze kuwanufaisha. Badala ya kukaa, ni miaka nenda rudi sasa hivi, *almost 30 years now!* Kwa hiyo, ningepomba wakati wa majumuisho mje na jibu ambalo sisi tunaweza tukawaeleza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida, hakuna asiyejua, Mkoa wa Singida na jirani Mkoa wa Shinyanga ndiyo tunaofuga kuku kwa wingi sana hapa nchini, kuku wake watamu, tunakula sana kuku wa maeneo hayo hapo, lakini wananchi wake hawanufaiki, hawapigi maendeleo na mfugo huu kwa sababu ya tatizo la ugonjwa huu wa kideri, sasa Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ni wanafuga kwa muda mfupi, ugonjwa unakuja unawafagia wote, wanabaki mikono mitupu, wale wanaofuga kuku wa kisasa katika miji na nini wao wananeemeka, lakini hawa kuku wa kienyeji ambao ndiyo wazuri hata ukienda katika hoteli yoyote, bei yake ni ghali kwa sababu ya ubora wake, wana hawa...

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Wizara hii ije na utaratibu mzuri; dawa zinachelewa na zinapokuja tayari kuku wamepukutika na bei iko juu! Sasa wanashindwa na baadaye hata hao kuku wachache wanaopatikana bei ya mlaji inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna huu ugonjwa huu ambao nao unaitwa ndigana baridi. Hili nalo ni tatizo katika Mikoa hii. Dawa hizi kupatikana mara nyingi zinakuwa haba na hasa wakati wa masika. Kitaalam nafikiri inaeleweka, wakati wa masika ndiyo magonjwa hayo ya *foot and mouth*, sijui midomo na miguu ndiyo yanakuwa kero. Kwa hiyo, ningeomba hatua za makusudi zichukuliwe kuhakikisha kwamba, dawa au pembejeo za mifugo zinapatikana kwa wakati, ili wananchi waweze kunusuru mifugo yao, ili chanjo hizi ziweze kupatikana waweze kuchanjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala ya majosho, mengi yamekufa. Sasa tunafanya nini na athari ya kutoogeshwa ng'ombe mapema ndio hayo mlipuko wa magonjwa. Kwa hiyo, ningeomba nalo hili litazamwe sambamba na elimu iweze kutolewa ya jinsi ya ku-*manage* haya majosho, ili yaweze ku-*sustain*, tuweze kuboresha mifugo yetu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu hupata minada mara moja au mara mbili kwa mwezi. Ni siku zao za mapumziko na wao huwa wanatoka siku hizo, hawafanyi kazi, ni siku hiyo ya kwenda kusherehekea kule minadani, kupata vitu na kuweza kupumzika, lakini minada hii, minada yetu bado haijawa mizuri. Kuna ushuru holela, mtu akifika pale na mifugo yake auze, asiuze inabidi alipie ushuru. Hili suala limezungumzwa na wachangiaji wengi. Hebu mngeliangalia vizuri muweze kuona nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, vyoo hamna katika minada hii. Halmashauri nafikiri zinazohusika na mambo haya, mngeweza kuwaomba waweze kuboresha maeneo hayo, badala ya watu kwenda kule na kuanza kupata maradhi. Vyoo hakuna na pale ambapo vipo vinakuwa pungufu, inakuwa kero badala ya kuwa nanihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hilo la minada, tumekuwa na tatizo kwamba, minada hii inakuwa mbalimbali. Kwa hiyo, nafikiri kungekuwa na utaratibu tu kila kijiji kingekuwa na mnada wake. Wale wachuuzi wangukuwa wanakwenda Kijiji kwa Kijiji kwa terehe tofauti wanayopanga, lakini unakuta asubuhi mtu anatoka na ng'ombe wake anatembea kilometa kadhaa. Sasa mpaka kufika kule ng'ombe ana kiu, akifika mnadani kule, uzito umepungua na bei imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1974/1975 tulifanya *operation* vijiji ambapo tulitenga maeneo mawili, ya malisho pamoja na maeneo ya wakulima, lakini utaratibu huo umekufa. Hakuna Kijiji ambacho tulikuwa tumetenga, mimi nilishiriki katika *operation* vijiji, tulitenga kabisa, upande huu utakuwa kwa ajili ya malisho na upande huu utakuwa kwa ajili ya kilimo, lakini watu wame-*violate*, sasa sijui kama kuna uwezekano au kama Wizara hii inaweza ikasaidia ili tuweze kurudi jinsi tulivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi, ningeomba elimu ya uvuvi itolewe zaidi na iwepo Sera ya kuwa na mabwawa. Tuna bwawa moja pale ltagata, sisi tumechimbwa pale

Kata ya Mgandu, Wilaya ya Manyoni, bwawa zuri sana na kuna mipango ya kufanya *irrigation*, lakini halijapandwa samaki! Ningeomba Wizara iangalie uwezekano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi jioni hii kuchangia katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mifugo, suala hili, sasa hivi ni janga la Kitaifa, suala la mifugo ni janga la Kitaifa, miongoni mwa majanga ya Kitaifa, naliita hivyo kwa sababu kila siku kuna migogoro ya wakulima na wafugaji. Kinachoniuma si ile migogoro tu ya wakulima na wafugaji, lakini ni ile mifugo yenyewe kupigwa mapanga kama nao kwamba ni wanadamu wana akili. *(Makofi)*

Sasa kama mifugo inakatwa kwa mapanga, wale ni wanyama hawana akili wanaathiriwa namna ile, hili ni janga la Kitaifa. Serikali kwa miaka hamsini iko madarakani, masuala haya yapo, matatizo haya yapo kila siku vinakuja vitabu na hotuba nzuri tu na maelezo, lakini mkakati hasa wa kutatua matatizo haya, kuwaendeleza wafugaji, kuwaendeleza wakulima ni vitu ambavyo havionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lekule Laizer amezungumza hapa kwa masikitiko makubwa na wenzake wote waliokuwa wanazungumza, wamezungumzia namna ambavyo wafugaji hawatendewi haki, wamezungumza namna ambavyo mifugo tuliyonayo ndani ya Tanzania hii haijatuletea tija stahiki. Sasa kama kwa miaka hamsini hatujaweza kutumia rasilimali hii ya mifugo kwa faida ya Taifa letu, tunategemea miaka mingine mingapi tutaweza hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya Tanzania ni kubwa, kuna ardhi ndani ya Tanzania nadhani haijawahi kukanyangwa na mwanadamu tokea Mungu aiombe, iwaje leo kuwe na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji? Ni kwamba hakuna mpango ambao umepangwa kwa ajili ya kuendeleza wafugaji, kwa ajili ya kuendeleza wakulima na kwa ajili ya kuendeleza mifugo yetu. Yanakuja maneno mazuri watu waingiziwe fedha watumie, basi, lakini mipango hasa madhubuti ya kwamba tunataka tuondokane na tatizo hili, tunataka mifugo itusaidie katika kuendeleza Taifa na kuendeleza wafugaji wenyewe hakuna ni maneno tu ya kisanii yameandikwa humu watu wapate fedha, basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa sipendi kuwasema nyie wana CCM, lakini inanishangaza mtu, tunakwambia Serikali ya CCM imechoka hebu pumzike kidogo, mnasema aah tunakuoneeni. Halafu unakuja unasimama unasema mifugo yetu inatolewa ndani ya nchi, inapelekwa hailipiwi kodi, haitusaidi *yakuuluna malaa yafaaluna*, mwasema nini mwakataa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayaingii katika akili ya mwanadamu mwenye akili unasema kitu hiki kizuri, kitu hiki kizuri halafu unakuja kulaumu kitu kile kile, mnasema nini mnakataa nini mnakubali nini. Kubalini kwamba mmechoka mpumzike kwa heshima kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme nitoe mfano tu, miezi miwili iliyopita nilitembelea mikoa ya Kusini, kuna ongezeko kubwa....

MHE. ALI K. MOHAMMED: Zungumza habari ya karafu.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Hii ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi nitazungumzia karafuu tutakapokuja kwenye Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda Mikoa ya Kusini, nikakuta ongezeko kubwa la mifugo katika Mto Rufiji, lakini pia nikakuta ongezeko kubwa la mifugo katika misitu ile ya Muhoro pale. Sasa kama masuala haya hayajapangiwa utaratibu, mifugo sasa inaingia katika Mikoa ya Kusini, bila utaratibu, bila kuwekewa mpango, matokeo yake nini sasa? Unahamisha mapigano kutoka huku unayapeleka na mikoa ya Kusini tunategemea nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la *soil erosion* ile mito itajaa maji, hata hiyo wanayosema kama wanazalisha *prawns* kwa wingi, watakuwa hawapatikani kwa sababu ile mito itajaa, lakini vyanzo vya maji navyo vitaharibika na misitu nayo yote itaathirika. Kwa hiyo, lazima tuwe na mipango madhubuti na itekelezwe, isiwe mipango ya kubaki kwenye vitabu na bajeti zipite, halafu mipango haitekelezwi, tunarudi pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye hawa mayatima katika Wizara hii, maana yake wanatajwa tu maendeleo ya mifugo na uvuvi, lakini uvuvi ni mayatima. Kuna wenzetu wamezungumza hapa kwamba ndani ya kitabu hiki ni kurasa kumi na tatu tu ndiyo zimezungumzia uvuvi, lakini maeneo ya uvuvi yote yanaonekana kama yametengwa, maeneo yote ya uvuvi hayajapewa kipaumbele na suala la uvuvi kabisa halijaguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika ukurasa wa 18 na 19, Mheshimiwa Waziri anazungumzia kwamba mapitio ya sheria na kanuni yameshapitishwa na ameshakwenda katika Baraza la Mawaziri ili kuona kwamba tunabadilisha sheria zetu na kanuni zetu kulinda uvuvi katika bahari zetu na kuwaendeleza wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyohisi ni lugha tu hizi, hata bajeti ya mwaka jana alizungumza haya, lakini bado uvuvi haramu unazidi kuendelea. Mabomu yanaendelea kutumika katika bahari, wavuvi kutoka nje ya nchi yetu wanaendelea kuja Wachina na Wajapani wanavua katika nchi zetu na kuondoka na samaki. Sasa hizi sheria na kanuni kila mwaka, lugha tunabadilisha, tunabadilisha, zinafanya kazi gani? Au hizi boti ulizozitaja hapa za *patrol* katika bahari hiyo kweli zitaweza kujikidhi kuzuia uharamia unaoendeshwa katika bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali katika hili haijajipanga na inapaswa kujipanga. Katika maeneo ambayo Taifa letu linaweza likajikomboa kwa haraka sana ni suala hili la mifugo na uvuvi, lakini bado tunalizungumza kinadharia tu, lakini hatujaliendeleza vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni namna gani ya kuboresha wavuvi wetu. Sasa hivi samaki wamepungua sana katika nchi yetu na zaidi katika bahari, lakini wamepungua kwa sababu gani, hakuna mipango endelevu yoyote inayofanywa ya kuhifadhi matumbawe, kuzuia uvuvi haramu unaofanywa, ya kuwafanya wavuvi waende wakavue katika *deep sea* kuwatengenezea zana za kisasa na vyombo ambavyo vitawafikisha kule kwenda kuvua hakuna, ni maneno tu yanazungumza na sasa hivi samaki wamekuwa ghali sana na pia wamekuwa adimu sana kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi katika bahari zetu bado kabisa kabisa, sisi tupo katika zone pale, katika pembe ya Kisiwa cha Pemba, kila siku meli za uvuvi, *diving*, *fishing* kutoka Kenya na sehemu nyingine zinaingia na hakuna hatua yoyote ambayo inachukuliwa, hata vikosi vinavyohusika ukivipigia simu wanakwambia hawana mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkumbusha Mheshimiwa Lekule sasa, kwamba ukiwapigia simu kuna mashua inasafirisha karafuu, baada ya dakika tano utazikuta boti zinakuja, lakini ukiwaambia kuna boti hapa inafanya *fishing*, au inafanya *diving* wanakwambia hawana

mafuta. Kwa hiyo, hali ya ulinzi bado katika bahari yetu na tunaendelea kuibiwa wakati sisi wenyewe tupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa suala la mwisho la *sea erosion*, sasa hivi, bahari inakula ardhi kwa kiasi kikubwa sana. Suala la upandaji wa mikoko kando kando ya bahari yetu ni suala ambalo halijatiliwa mkazo wowote na Wizara hii, halijatajwa hasa katika kitabu hiki cha hotuba. Sasa kama pale Msimbati mmeona mnataka mjifunze wapi au hamjaona? Sasa tujifunze wapi, Msimbati tumeona, katika kipindi cha dakika 40 tu, kimechukua zaidi ya mita ya 120 za ardhi, sasa tunataka tujifunze wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* ni kupanda hii mikoko, hizi mbegu hatununui, hatufanyi kitu chochote, ni msimu tu ukifika tunaokota, tunapanda basi, lakini bajeti yote hii haijazungumzia wakati ardhi kila siku inaliwa na bahari. Sasa kama hili hatujalifanya, matokeo yake tutafika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tutakuja kukuta kwamba nchi hii asilimia kubwa imeshaliwa na bahari na bahari inakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, naiomba Wizara, pamoja na mambo yote inayoyafanya, lakini suala la upandaji wa mikokoto kando kando ya bahari kuzuia *erosion* litiliwe mkazo mkubwa kulikoni masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie Mheshimiwa Waziri katika bajeti yako ya mwaka jana ulisema kwamba umezalisha vifaranga milioni 20 vya samaki kwa ajili ya wafugaji wa samaki, lakini...

Si bado dakika tatu?

MWENYEKITI: Muda umekwisha.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Ya kwanza hiyo!

MWENYEKITI: Muda umekwisha.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilufi.

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata fursa hii niweze kuchangia Wizara hii ya Ustawi na Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hekima zinatambulisha kwamba ni raha ukiwa kiongozi makini upate rafiki wa kukukosoa uweze kujisahihisha kuliko kupata rafiki wa kukusengenywa. Kwa hiyo basi, naomba kuwaambia rafiki zangu wa Chama cha Mapinduzi kwamba, Wizara hii ndiyo ni mhadumu kwa Watanzania wafugaji wasiopungua milioni 20 pamoja na mifugo isiyopungua milioni 20. Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu, mtambue kwamba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, ni Wizara hatari sana kama kuna mtu ataweza kuitekenya na ikakasirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema ya kwamba utumishi wa Wizara hii ndiyo tanuru la kukaushiwa kura za CCM, ama ni jiko la kupikia imani ya Watanzania kukipigia kura Chama cha Mapinduzi.

Hivyo, naomba kwamba, kwa kuwa uwiano wa ardhi, kwa mahitaji ya mifugo na wananchi, wakulima, wafugaji pamoja na mahitaji ya hifadhi hayana uwiano na kwa sababu kuna sheria zilizopitwa na wakati na kuna kanuni gandamizi, nashauri kwamba Wizara hii ipate

mashirikiano na Wizara nyingine waweze kutatua kero za wafugaji ambazo Wizara hii kwa hotuba yake inapendekeza kuzitua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa pekee, napenda kusema kwamba, Wizara hii ndiyo bima kwa maslahi ya wafugaji na ndiyo rufaa kwa wafugaji na vile vile ndiyo kimbilio la wafugaji na vile vile Wizara hii ndiyo bima kwa maslahi ya kuvunwa kura za CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa nawaomba na wafugaji wanaomba Wizara hii na wanaomba Serikali iwepo sikukuu maalum ya kusherehekea ufugaji bora na unywaji maziwa. Wafugaji wanaomba pawepo sikukuu maalum kama ilivyo Sikukuu ya Wakulima, Sikukuu ya Wafanyakazi, kwa hiyo, wafugaji wanaomba wawe na siku yao ya kusherehekea ufugaji bora pamoja na unywaji wa maziwa ili waweze kuamsha ari ya kuthaminika ufugaji, ufugaji bora pamoja na kukuza mahitaji ya kunyweka maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wafugaji wanatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, Kandali Mstaafu na vile vile wanatoa shukrani za dhati kwa Profesa Msolwa na wanatoa shukrani za dhati kwa aliyekuwa Naibu Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Benedicto Ole-Nangoro, kwa jinsi walivyoshirikiana na wafugaji pamoja na mlezi wao na Mheshimiwa Rais akasitisha Operesheni Tokomezwa. Nampongeza sana Mheshimiwa Kinana, alikuwa sikio sikivu na aliwasiliza wafugaji waliotoka maeneo mbalimbali na akasiliza madhila yaliyotokea. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Kinana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi nazitoa kwa sababu mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, Mheshimiwa Kinana hata kama humpendi lakini kwa mema aliyotenda na dhamira zake njema, ni lazima zipewe heshima ya utu na ubinadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawana ugomvi na huruma zilizotendeka dhidi ya watumishi dhulumati waliosababisha vifo vya mifugo na kuhakikisha kwamba panapotea uhai wa baadhi ya wafugaji. Kwa hiyo, wafugaji wanaomba kumkumbusha Mheshimiwa Rais kwamba, pamoja na huruma aliyowatendea katika kuzisitisha operesheni mbalimbali, wafugaji wanasema kwamba, palikuwa na operesheni mbalimbali zilizotendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, operesheni hizo ni Operesheni ya Ihefu ya Mbeya, Operesheni Hamisha Wafugaji, walioitwa wafugaji haramu, wavamizi na vilevile palikuwa na Operesheni Kimbunga, hadi sasa pana Operesheni za Idara ya Maliasili na Idara ya Wanyamapori, ambazo zinaitwa kwamba kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake. Pia kuna operesheni zinaitwa mla ni mla leo, mla jana kala makombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi dhuluma zinazotendeka zinazalisha rushwa na tozo katili kwa wafugaji na mara nyingine Wizara hizi zinakuwa zinaruhusu wafugaji kwenda kupeleka mifugo yao kunywa maji katika bustani za hifadhi. Sasa wanapokuwa wameona kwamba, hawana pesa wanakamata mifugo hiyo. Kwa hiyo, naomba vile vile hizo operesheni ihakikishwe kwamba hazitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa neema ya uongozi wa siasa bora na utawala bora na uwajibikaji makini ni masikio sikivu, ningepomba machungu ya jamii ya wafugaji na vile vile naomba Serikali, kama alivyo Mheshimiwa Kinana amezunguka kwenye maeneo ya wafugaji akatoa kauli mbalimbali, basi naomba utumishi wa Serikali uwe na masikio sikivu ya kujua madhila yanayowapata wafugaji na wanachukua hatua za kubadilisha sheria gandamizi zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, je, maagizo yote yaliyotolewa na Mheshimiwa Kinana, Wizara hii leo mtatuambia mmejenga maridhiano gani na Wizara mtambuka. Hivyo, maeneo ambayo yanahitajika yapitiwe upya, yaliyopitwa na wakati, hayana wanyamapori, kwamba yabadilishwe, yalianzishwa mwaka 1952 kabla hata ya kupata uhuru wa Tanganyika. Naomba leo mtuambie Wizara hii kama mko sambamba na siasa na sera na maagizo ya Katibu Mkuu, mmechukua hatua gani ili wananchi waweze kuelewa kwamba mawazo ya Mheshimiwa Katibu Mkuu yanapotolewa yana thamani ya kusadikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba bajeti hii mtuambie kwamba ninyi mtakuwa na mashirikiano gani na Wizara mtambuka. Wizara ya Maliasili inawapa mashirikiano gani? TAMISEMI, ma-DC, Wizara ya Ardhi imetengua vipi sheria? Wizara ya Sheria, je, imepokea vilio vya wananchi ikaandaa sheria au mkakati wa kupelekwa *Cabinet paper* kwa ajili ya kutenguliwa dhuluma? Je, Wizara ya Maji, mnashirikiana vipi mtupe maji kwenye mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliamishwa mifugo kutoka lhefu, imepelekwa Rufiji na maeneo mbalimbali, Serikali iliahidi kupeleka huduma kwa wafugaji, ziko wapi hizo huduma na kwa nini huduma hizo sasa zisije zikawa ni agenda majukwaa ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna maridhiano, je, vipi maeneo bila masahihisho ya kisheria yakaweza kutolewa. Mheshimiwa Waziri mmesema unataka kurudisha maeneo, kuna kutenguliwa kwa sheria gani ambazo umependekeza kuzileta, je, kuna *Cabinet paper* gani mlizoandaa. Naomba tusiwe na maelezo ambayo kwa kweli yanafunika funika, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa tahadhari kwamba, mrina asali hagombani na nyuki, naomba Watumishi wa Serikali wa Wizara Mtambuka waache kugombana na kura za wafugaji, majuto ni mjukuu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Serikali na hususan TAMISEMI, hebu nendeni mkarekebishe makovu mliyoyatenda, Meatu mlichoma nyumba za watu, kasoro hizi Wizara ya Maliasili ambayo haina sikio sikivu, kuna mambo ya hatari kabisa, tumekwenda na Naibu Waziri, nakupongeza Naibu Waziri wa Maliasili Mheshimiwa Mgimwa, una tabia njema, una masikio sikivu, lakini unakwamishwa. Mheshimiwa Rais Kikwete mtani wangu, ichunguze Wizara ya Maliasili chukua hatua ngumu hata kama yule mtu unampenda kwa uswahiba, wa kwamba huyu ni kijana anapaswa kuleleka, lakini je, ana masikio sikivu ya kuleleka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe wafugaji walikuja kuunga mkono hapa ujenzi wa Katiba na walipokuja hapa ikagundulika Katiba haina haki za malisho. Sasa Katiba mpya imetoa haki kwa makundi mbalimbali, wafugaji, wakulima, wavuvi na wengineo.

(Hapa kengele ililia)

MHE. JOHN S. MAGALLE: Ya kwanza?

MWENYEKITI: Ndiyo, endelea!

MHE. JOHN S. MAGALLE: Kwa hiyo, sasa nashauri, Baniani mbaya kiatu chake kizuri, wafugaji walikuja wakiunga mkono Serikali. Nashauri na kuhimiza Serikali, ikiwa mmegundua kuna haki za malisho, nashauri Wizara ya Maendeleo ya Mifugo iwe chachu ya kuhamasisha sasa sheria ya haki ya malisho, iundwe haraka sana ili wafugaji waweze kupata haki ya malisho na haki za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo na kasoro za Wizara ya Sheria kutokuwepo na haki kwa wafugaji. Siasa ni taa ya ukombozi iliyoondoa wakoloni, siasa ni taa na nuru iliyoleta mapinduzi matukufu Zanzibar, ikaleta ukombozi kwa Bara la Afrika.

Sasa napenda kuwashauri ndugu zangu wa CCM, mdharau mwiba huota tende, ogopeni sana mfumo wa Vyama Vingi. kwa hiyo, napenda kuwashauri CCM mdharau mwiba huota tende na siasa na mtu aliyekata tama, kama wafugaji ambavyo wamekata tama, watakakoegemea majuto ni mjukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali naomba iache visingizo vya kuzibaziba matatizo yanayozungumzwa na wakulima na wafugaji. Utumishi hasi wa Wizara mtambuka TAMISEMI, Maliasili, Ardhi naomba kwa kweli sasa mkutane mtutolee suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Waziri wa Uratibu wa mambo ya Bunge, dada yangu Mheshimiwa Jenista Muhagama, nakushauri hakikisha unaitisha Wizara mtambuka mtatue matatizo haya, kabla watu hawajaanza kukimbilia na kunyemelea na kuwashawishi. Mtu aliye na dhiki ni mwepesi kutetereka. Wakoloni walilaani sana siasa za TANU na wakadharau siasa za TANU, lakini matokeo yake CCM au TANU na Afro-Shiraz walipoungana walikomboa Bara la Afrika.

Msidharau siasa za Wapinzania hususani pale ambapo wanazungumza na kukosoa kwa maslahi ya ustawi na maendeleo ya nchi. Pana kejeli ya kwamba Mfugaji ukimwona kakondeana na mifugo imekondeana. Hivi ukimkuta mtoto ana kwashakoo wa kulaumiwa ni nani? Ni mama mzazi. Ukikuta mbwa kakondeana, wa kulaumiwa ni mfugaji wa mbwa.

Sasa kama hakuna malisho kwa mifugo, hakuna maji kwa mifugo, nani wa kulaumiwa? Ni Serikali ambayo inapaswa kutoa huduma hizo. Kwa hiyo, nawaombeni jengeni morali, msipojenga morali kwa kweli ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kinana nampongeza kwa juhudi zake, lakini nashauri kwamba, Waziri wa Nchi na Uratibu wa Sheria asimamie masuala ya kujenga umoja ni nguvu ya kutatuliwa matatizo ya wafugaji. Ahsanteni. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Ukimkuta mtoto amekondeana ana utapiamlo wa kulaumiwa ni wazazi wote wawili, baba na mama, siyo mama peke yake. *(Makofi)*

MHE. JOHN S. MAGELLE: Kwa hiyo ni CCM na Serikali walaumiwe.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Kilufi atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Dkt. Kafumu!

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wafugaji wote wa Tanzania wakiwemo wa Mbarali, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kabla sijachangia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati ya Bunge ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kunusuru Vijiji 21 ambavyo baadhi ya Watendaji wa Serikali wasio waadilifu walitaka kuviingiza kwenye hifadhi wakati wakijua kwamba hifadhi ile ni mpya, eneo tulilolitoa lilikuwa linatosha, wasingepaswa kutuibia eneo lingine la wananchi.

Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana hawa walioona umuhimu wa kuacha eneo hili likiwemo la wafugaji, naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa uandilifu waliouonesha, naomba na Watendaji wengine wafuate msimamo wake wa kuwapenda Watanzania kwa kupenda jamii ya wafugaji na kuwapenda wakulima na kutetea wanyonge ambao kimsingi baadhi ya watendaji wasio waaminifu wanaungana na mafisadi kuwahujumu wakulima na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii nimesema mara nyingi kwamba, kama kuna laana tunaitafuta ni pamoja na kutowajali wafugaji. Nawaambia ndugu zangu, niliwahi kusema hapa Bungeni kwamba wafugaji hawa ni watu watakatifu. Kwa wale Wakristo wanafahamu kuzaliwa kwa Yesu Kristo walikuwa ni watu wa kwanza kumwona, walikuwa ni wafugaji, watu hawa si watu wa kawaida, ni watu wa kuheshimu sana katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tunavyozungumza namtaka Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri Mkuu kwa ujumla na Serikali watamke, je, wametenga maeneo ya malisho? Katika bajeti hii ukiangalia ukurasa 134-135 inaonekana bajeti ni shilingi bilioni sitini na nane mia nane na kumi milioni mia nne na nne elfu, lakini ukiangalia matumizi peke yake ya Wizara wamechukua bilioni 46 na ukiangalia fedha za maendeleo ambazo tunadhani zinaweza zikagusa maeneo ya wafugaji ni bilioni 22, hizi ni miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa ningeshauri hizo bilioni 46 ziende kwenye miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuboresha maeneo ya wafugaji ambao hawana mabwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao, lakini hawana majosho ya kutosha kwa ajili ya afya ya mifugo yao. Kwa hiyo, ningependa fedha hizi nyingi ziende kwenye Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Mifugo kuliko kupeleka kwenye matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanikiwa sana kutenga maeneo ya wanyamapori, kila siku nasema hili jambo lakini naonekana sieleweki sijui. Tunashindwaje kutenga eneo la malisho? Tumetenga maeneo mpaka tunahamisha watu kwa ajili ya kutenga maeneo ya hifadhi za Taifa kwa ajili ya wanyamapori, tunashindwa nini kutenga eneo la wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itamke, sijaona mkakati wowote ule wa kutenga maeneo ya malisho. Tumekuwa tukizungumza zungumza kama vile wafugaji hawa hawana faida katika Taifa hili. Naomba katika kujibu hili, kama sitajibiwa ni mikakati gani imepangwa kutenga maeneo ya malisho, sitapitisha kabisa Bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Naomba nizungumze, mara nyingi tumekuwa tukisema kuhusu kutenga maeneo ya malisho ya wafugaji. Tumeshindwa matokeo yake tunasababisha mapigano kati ya wakulima na wafugaji. Haya yanafanyika Serikali inaona na Wizara inaona, nani wa kuwatetea wafugaji kama Wizara haisemi chochote, ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia wafugaji wakinyanyaswa kwenye mipaka ya hifadhi, Wizara ambayo tunategemea ingewatetea, imekaa kimya. Nani wa kuwatetea wafugaji sasa? Awatete nani wafugaji katika nchi hii ambao wameshika uchumi, leo wanaoneka ni kama watu wasiofaa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa anachangia anasema yeye kule hajawi kula nyama ya ng'ombe mpaka amekuwa mtu mzima, yeye alikuwa anakula samaki. Kwa hiyo, wafugaji wamepelekwa kule imeonekana ni mzigo. Hivi kweli jamani wafugaji ni mzigo katika Taifa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokosekana ni mipango mizuri ya namna gani wafugaji watengewe maeneo, namna gani wawezeshwe kuwa na majosho na malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao, tunashindwa nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama sitapata majibu, katika kujibu kwamba maeneo ya wafugaji yametengwa malisho hayajatengwa, sitakubali kupitisha hii bajeti ya Wizara.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mifugo ni uchumi, wafugaji wakiandaliwa mazingira mazuri, kukawa na viwanda ambavyo nilikuwa naviangalia hapa ambavyo vimeandaliwa vya kusindika nyama sijui vya kufanya nini. Nikawa nawauliza wenzangu hivi umewahi kula nyama iliyosindikwa ya Tanzania ya mifugo yetu. Kila ninayemuuliza anasema sijaona, sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa kumeonekana Viwanda vingi vya Kusindika Nyama. Sasa hizi nyama zinasafirishwa nje au inakuwaje? Sijaelewa. Kwa hiyo, naomba tulikuwa na viwanda vingi, vingine tumewapa wawekezaji, naomba Serikali iangalie namna nyingine, viwanda hivi vilitoa ajira kubwa kwa vijana wetu, vilitoa ajira kwa Watanzania, leo wamepewa watu wamekaa navyo hakuna kitu. Maeneo ya malisho ranch zilikuwepo za Taifa baada ya kushindwa wamepewa watu wanachezea tu na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mbarali NARCO wafugaji wako kule wanakodishiwa yale maeneo. Kwa mwaka anatakiwa alipe kila ng'ombe mmoja shilingi 10000 kumlisha kule kwenye ranch, imegeuka ni baishara. Hivi Serikali hamuoni? Nendeni Mbarali mkaone wale wafugaji jinsi wanavyokodishiwa maeneo ya malisho ambayo yalikuwa ni halali yao wangepewa wao wangeweza kulipa gharama ambazo Serikali inataka kulipa, lakini wamepewa watu wanachezea na wanakodisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akilima heka moja, kila heka moja ni gunia tatu anatakiwa alipe kwa mwaka. Jamani nchi hii Tanzania? Mimi sikubaliani kabisa. Naomba Mheshimiwa Waziri kama nasema uongo, unda Tume ikaangalie NARCO kule Mbarali, watu wanavyochezewa, wafugaji wanakodishiwa maeneo. Naomba hili lipate majibu na uende ukaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANAPA wamewatesa sana wafugaji. Huko mipakani wanatozwa fine bila sababu ya msingi na wakati mwingine kwa kuonewa tu. Wakimbilie wapi? Mbona sioni Wizara inawasaidia hawa watu? Wanamalizwa tu, wanateswa tu, wanatozwa fine na wakati mwingine kuliwa mifugo yao. Hivi hawa wangaliwe na nani kama Wizara haiwaangalii?

Kwa hiyo, naomba na wakati mwingine ile operation ilipokuwa inafanyika hata zile bunduki ambazo walipata kisheria kwa ajili ya kulinda mifugo yao na zenyewe zilichukuliwa na mpaka leo hawajarudishiwa zile bunduki zao. Sasa kuna nini na kuna tatizo gani? Nani awatete kama siyo Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara isiwe mbali na wafugaji. Sasa kama inakuwa mbali na wafugaji, kuna sababu gani ya kuwa na Wizara ya Mifugo? Sioni sababu, lazima tuone wafugaji kimbilio lao iwe ni Wizara. Kama Wizara haiwezi kuwatetea wafugaji, basi afadhali kuivunja isiwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule lhefu wakati wa zoezi la kuhamisha wafugaji, zoezi lile lilifanyika kwa kuua mifugo ya wafugaji kwa maelfu na maelfu. Ile taarifa ambayo ilichunguzwa

ikiongozwa na Jaji Othmani haijatokea, mkaone madhara yaliyofanyika kule lhefu. Mifugo ya watu ili uawa kwa kufungiwa mahali pamoja eti mpaka alipe *fine* ya elfu kumi, mfugaji kwa ng'ombe zake ndipo awaondoe awahamishe, matokeo yake aliua ng'ombe wale walikuwa hawapewi maji wala chakula. Walikufa ng'ombe wengi na wengine wafugaji wakaamua kujiua, lakini Serikali imekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifanye uchunguzi, wale ambao mifugo yao ilikufa walipwe fidia. Haiwezekani wafugaji wakapoteza mifugo kiasi kile, rasilimali ambayo ni uchumi wa Taifa, halafu waliohusika wakaachwa tu hivi hivi na wafugaji wale wakapata hasara. Naomba Serikali ifanye uchunguzi, ile mifugo iliyokufa kule kwa kupitia ile taarifa, wafugaji wale ambao mifugo yao ilikufa walipwe fidia. Haiwezekani mifugo ile ikafa hivi hivi tukanyamaza, ni dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MODESTUS D. KILUFI: *Ooh sorry!*

MWENYEKITI: Muda umekwisha Mheshimiwa!

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono baada ya kupata majibu ya kuridhisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Kandege!

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE--: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo nami niweze kuchangia na nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja lakini *on condition basis*. Ni ukweli usiopingika kwamba, kwa mara nyingine tena naikumbusha Wizara ahadi yake waliyoahidi kumaliza tatizo juu ya Ranch ya Kalambo tangu Waziri aliyetangulia aliahidi kwamba atamaliza mgogoro huu na Waziri aliyepo leo amepata fursa ya kwenda Kalambo, akaenda kutazama mgogoro ule lakini mpaka ninavyoongea leo hii majibu yake hayajapitikana na ndiyo maana nimesema naunga mkono *on condition basis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naomba nitoe taarifa kabisa kwamba, nakusudia leo kwa mara ya kwanza kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, ajiandae atoe majibu ambayo yatakidhi haja kwa ajili ya wananchi wa Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Ranch* ya Kalambo, wananchi walitoa kwa Serikali wakiwa wanaamini mazao ya kwao waliyokuwa wameyapanda walikuwa wanaruhusiwa kutumia ardhi ile na walikuwa wanaendelea kupata ujuzi wakijifunza namna ambavyo *Ranch* ilikuwa inafanya kazi vizuri, lakini ajabu na bahati nzuri na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameorodhoshwa kwamba, katika *Ranch* ambazo zinamilikiwa na Serikali ni pamoja na *Ranch* ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *Ranch* hii ya Kalambo Serikali imegeuka kuwa mpangishaji, inapangisha mtu ambaye hastahili kumiliki. Wamiliki wananchi ambao walitoa ardhi yao bila fidia, wananchi wa Kijiji cha Katapulto wanadai ardhi yao irudi kwa sababu wanahitaji na ardhi ile inatumika si kwa ajili ya kufuga bali inatumika kwa ajili kilimo na

anayelima mle anawakodisha wenye ardhi yao stahili, ardhi ya kwako unalazimika kuanza kuikodi. Jambo hili halikubaliki hata kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri akiwa *back bencher* huku jinsi ambavyo alikuwa anaeleza ni namna gani Wizara hiyo haifanyi vizuri unakwenda kufanya vizuri. Naomba ule moto uliokuwa nao usije ukawa unabadilika. Tusije tukaanza kujiuliza huko mkienda mnakutana na nini? Kile mlichokuwa mnakisema kabla kinaonekana kinabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupata majibu, wananchi wa Katapulo lini mgogoro wa ardhi na Ranchi ya Kalambo unatatuliwa. Mheshimiwa Waziri najua unajua kwamba, sina ungomvi na wewe, lakini katika hili sina urafiki na wewe, ninachotaka ni kupata suluhu wananchi warudishiwe ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchangia kuhusiana na suala zima la uvuvi na hasa Ziwa Tanganyika. Ukisoma katika kitabu hiki kurasa nyingi sana zimeandikwa kuhusiana na masuala ya kilimo na ufugaji kwa maana ya ng'ombe na mifugo mingine, lakini suala la uvuvi limeelezwa kwa kiasi kidogo sana. Amelisema vizuri RC wa Mkoa wa Rukwa ambaye amepata bahati ya kuwa Ziwa Tanganyika, lakini pia na Ziwa Nyasa. Ukitafuta nini ambacho Serikali inafanya kuwasaidia wananchi hawa ukilinganisha na nguvu ambayo inaelekezwa kwa wakulima kuna utofauti mkubwa sana.

Sasa leo natarajia Wizara hii ituletee majibu, ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inamsaidia mvuvi naye atokane na hali duni ili ajivune katika nchi yake kwamba, hakika rasilimali ambayo mwenyezi Mungu ametujalia Tanzania naye anafaidika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulianzishwa utaratibu kwamba, kwamba zipo *fiber boats* ambazo ilikuwa ruzuku itoke kule ili wananchi wetu waweze kupata boti zile za kisasa kwa bei iliyo nafuu. Haya ambayo tumeyasikia mbona hatuoni utekelezaji wake. Serikali ina mpango gani kupitia Wizara hii? Inawezekana, sidhani kama ni bahati mbaya, lakini ni nini ambacho kimetokea? Inawezekana *concentration* kubwa iko kwa suala la mifugo, mkawa mmejisahau kutotilia maanani suala la uvuvi. Uvuvi ni sekta muhimu sana.

Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yako ambayo na wewe unajua kuna *report* ambayo umekabidhiwa wewe mwenyewe juu ya watu ambao wako tayari kusaidia sekta ya uvuvi kuhakikisha kwamba, kwanza tunapambana na uvuvi haramu, hizi meli kubwa kubwa ambazo zinaingia ambazo hatuna uwezo nazo wa kuweza kuzikabili, kuna makampuni yako tayari. Kuna mwekezaji kutoka Israel ameleta *paper* Wizarani kwako mpaka leo hii majibu bado hayajapatikana na hilo unalijua. Ni vizuri utuambie umekwama wapi, unahitaji msaada upi ili tuweze kusaidiana. Lakini lengo zima ni kuhakikisha kwamba tunawasaidia Watanzania kwa ujumla wake, tumsaidie mkulima, lakini pia tumsaidie mfugaji na tumsaidie mvuvi. Hiyo ndiyo Tanzania tunayoitaka sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunawapa maneno ya kusema Wapinzani hata kama hawana hoja. Naona sasa hivi hoja ambayo wamebaki nayo katika Kamusi wamekutana na neneo kuchoka, lakini unachoka pale ambapo unafanya kazi na naamini hicho ndicho kinachofanyika. Sasa tusije tukawapa *slogan* ya kuondoka nayo *unnecessarily* mambo tunayafanya mazuri ninachoomba Wizara husika hebu tutilie maanani haya ambayo yako kwenye mpango wa Wizara zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusiana na ufugaji na hasa kuendeleza mifugo, ng'ombe aina ya Ufipa. Ng'ombe hawa ni ng'ombe wa asili, ng'ombe ambao size yake ni kubwa wana nguvu kubwa sana huhitaji kuwafunga ng'ombe

wanne ukaenda kulima, unahitaji kuwafunga ng'ombe wawili wanatosha. Hata hivyo, jitihada ambazo zinafanyika na Serikali kuhakikisha kwamba, ng'ombe hawa ambao wana uwezo mkubwa sana wa kupambana na magonjwa, hatuoni jitihada za Serikali kuendeleza badala yake wanatuambia tufuge ng'ombe wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wa kisasa sidhani kama wanafaa kwa kila maeneo. Sisi hawa ng'ombe tunawatumia kwa kilimo, sitarajii kwamba ng'ombe wa kisasa ambaye mnatuhamasisha tufuge, tutakwenda kumtumia kulima kama maksai. Hawezi! Yule ng'ombe unahangaika, unapima mpaka joto leo kalalaje? Hatujazoea ng'ombe wa hivyo, tunataka ng'ombe hawa wa Kifipa ambao wana nguvu, wana uwezo mkubwa, mtusaidie kuhakikisha kwamba kizazi hiki hakipotei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ng'ombe wanaokuja wa watani zangu na tumewakaribisha ili mradi wafuate masharti, wale wa kufunga ng'ombe wanne wanne hatuwahitaji, wale tunahitaji kwa ajili ya kuchinja, lakini si kama wanyama kazi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Wizara yako na kile Kituo ambacho umekitaja kiko Sumbawanga, hebu tazima uwezo wake, uwezo wake ni mdogo hauwezi kutusaidia kuendeleza ng'ombe hawa aina ya Ufipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusiana na suala zima la usindikaji wa maziwa. Katika hotuba yake, yeye mwenyewe amekiri kwamba tunavyo viwanda 82 lakini *absorption capacity* ni asilimia 26 tu. Maana yake ni nini? Ni kwamba *either* viwanda hivyo havina mtaji wa kutosha ndiyo maana vinashindwa kununua maziwa ya kuyasindika, sisi tunabadilika kuwa soko la maziwa kutoka nchi jirani, wakati tuna maziwa mengi sana ambayo hatujaweza kuya-process na kuweza kuyatumia hapa nchini na pia kuweza ku-export.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii unayo wewe mwenyewe, tunaomba tupate majibu, kwa nini ni asilimia 26 tu ya viwanda hivyo 82 vinaweza kutumika na hiyo asilimia 74 ni kwa ajili ya matatizo gani, kama tatizo ni mtaji upo uwezekano kabisa wa ku-side na benki kwa sababu wanajua *for sure* maziwa haya yakiwa *processed* Watanzania wakahamasishwa kutumia maziwa, tunahitaji kutumia maziwa, kwa hiyo, soko lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu ukiwaunganisha na mabenzi, hakika wana uwezo mkubwa wa kuweza kulipa na hivyo hatutakuwa na tatizo kuhusiana, kwanza utumiaji wa maziwa na faida zake, lakini pia itaongeza faida kwa mfugaji atafaidika, hatakuwa hata na sababu ya kuhama hama kwa sababu mahali alipo ana uhakika maziwa yake yatakusanywa, atapata bei nzuri, hatakuwa na sababu ya kwenda huko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala lingine la kuhusiana na ngozi. Ukisoma katika ripoti, kiasi gani kama Taifa tunapata kutokana na usindikaji wa ngozi, *almost* ni zero. Ukiuliza ni kwa nini, unaambiwa kwamba ngozi ambayo tunazalisha Tanzania sehemu kubwa inapelekwa nchi za Kenya na bora ingekuwa inapelekwa Kenya tukapata hata kodi, hata hiyo kodi hatupati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachofanya watu wanadanganya kwamba amepeleka mazao labda amepeleka mahindi, kumbe kaweka chini ngozi. Hebu Serikali mtafute jibu, kwa nini mtu ahangaike, akatafute soko la ngozi nchini Kenya wakati angeweza kuuza ngozi yake kwa bei nzuri hapa, hatahangaika na habari ya kuanza kutafuta *panya routes* akihakikishiwa hapa hapa ata-process ngozi ya wanyama na akapata faida kwa Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono baada ya kuridhishwa na majibu ya Serikali. Nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Dkt. Kafumu!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU-: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kama mchangiaji wa mwisho ili nami niseme kama Wabunge wengine walivyosema, habari ya wafugaji ambao kwa sasa imekuwa ni gumzo kubwa sana katika nchi yetu, kwa sababu wanaonekana kama yatima fulani hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii na kwa kuniponya na ugonjwa ambao niliupata nikiwa Jimboni. Nawaambia wananchi nimepona sasa, tuendeleo kuchapa kazi tujitayarisha kwa ajili ya uchaguzi. Wale waliodhani kwamba nimetupiwa, niko vizuri. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Tutakupa.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU-: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, nampongeza Waziri, kaka yangu Dkt. Kamani, kwa kazi nzuri anayofanya, kuna mageuzi tumeyaona, lakini Naibu Waziri rafiki yangu Shigela, sisi Wasukuma tunawaita Wamasai Shigela, nakupongeza na wewe, uliweza hata kufika Igunga kuangalia wafugaji wenzako wanavyopata tabu kidogo. Nawapongeza pia watendaji, ndugu yangu Yohana Budeba, Katibu Mkuu, rafiki yangu tulisoma wote Chuo Kikuu cha Brussels, hongera kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba niseme kwanza tatizo la wafugaji katika nchi yetu, kama nilivyo tatizo la wakulima, ni ongezeko la watu linalotokea duniani na linalotokea kwetu. Nakumbuka mji wa mzee Kafumu miaka ya 57 mpaka miaka ya 65, ulikuwa mdogo tu, lakini baada ya kufika miaka ya 80, kaka zangu walikuwa na kila mtu akawa na ng'ombe zaidi ya 200 na ule mji haukutusha. Kwa hiyo, wakaondoka na vivyo hivyo miji mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeongezeka lakini rasilimali ya ardhi imebaki ile ile na hii ni changamoto sana kwa Taifa na tunatakiwa tujipange kweli kweli, tutaendelea kulaumiana, wengine wanakataa tukienda Rufiji, lakini maeneo hayatoshi tena, ni lazima twende tutafute malisho. Kwa hiyo, ni changamoto kwa Taifa kujaribu kutafuta utaratibu ambao utawafanya watu wakae mahali kwa tija, lakini pia Serikali lazima ifikirie kuyageuza maeneo mengine ambayo yalikuwa ni hifadhi, lakini yamekosa sifa, wananchi wakae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali iwafundishe wakulima na wafugaji, stadi mpya za maisha na kuwajengea miundombinu. Changamoto ya nchi yetu ni kwamba, bajeti yetu, uchumi wetu hauhimili maendeleo ya watu wetu, hii itakuwa ni changamoto kubwa na tutalaumiana sana, lakini tukitengeneza mkakati hata kama ni mdogo, tutasaidia. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilianganalie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Opolukwa amesema, eneo la makao linaweza likageuzwa kuwa eneo la malisho, ni kweli. Liko eneo la Wembele kule nyumbani kwetu na lenyewe bado linahesabika kama hifadhi ya aina Fulani. Naiomba Serikali ifikiri kuligeuza pia jambo hili, wabakize eneo dogo tu la hifadhi kwa ajili ya ndege, lakini eneo lingine lote liwe la wafugaji, lakini pia wakulima. Tutapunguza matatizo, lakini kama tutaacha mambo yabaki kama miaka 65 iliyopita, kwa kweli tutakuwa na tabu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi niseme, kwa namna ya pekee kule Isakamaliwa, ambako ni kwenye eneo la Mbuga ya Wembele, wakulima na wafugaji wanapigana. Naiomba Serikali tena wapeleke mkakati wa kwenda kulipima lile eneo, lakini pia waliondoe kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mkuu wa Wilaya mama Pangani ameshamwandikia barua Waziri wa Maliasili na Utalii aliangalie hili jambo, lakini pia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi mshirikiane kuhakikisha kwamba eneo hili linapimwa vizuri ili watu hawa wasiendelee kupigana. Vinginevyo tutaendelea kuona mauaji kwa sababu tumeshindwa kujipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme, ujenzi wa mabwawa ni jambo zuri sana kwa maeneo ambayo yana ukame mkubwa. Kwa mfano, Wilaya ya Igunga, ni kati ya Wilaya kame Tanzania, ni mbuga ambayo haina maji na hata mvua ikinyesha maji yanatembea na yanapotea haraka. Kwa hiyo, ni vizuri tuyahifadhi maji haya kwa ajili ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru tuna mabwawa kadhaa pale, lakini hayatutoshi. Nilipoingia Bungeni hapa mara ya kwanza, niliomba Serikali itafute mradi mkubwa wa kujenga bwawa lingine. Serikali ilijaribu kufanya upembuzi yakinifu lakini sijui iliishia wapi. Najua mabwawa haya yatajengwa kwa pamoja Wizara ya Maji na Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, mnatakiwa mshirikiane sana kujenga mabwawa makubwa na hasa katika Wilaya hiyo ya Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nikishauri chama changu, kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 kwenda 2020, najua tutakiwa madarakani tena, basi tuingize kwenye Ilani kujengwa kwa bwawa moja kubwa Igunga, ili wananchi wale kwa kweli waweze kupata maji, kama ambavyo mradi wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria unaanza kutekelezwa, bado hautatoshia maeneo yote, ningependa sana Serikali itusaidie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kushauri Serikali ni juu ya Jeshi la Magereza. Katika nchi yetu hili ni jeshi ambalo linafanya kazi sana katika kuzalisha mazao, lakini kuzalisha mifugo. Wana miradi mizuri sana na mashamba makubwa sana ya mifugo, lakini wakati mwingine yanaendelea kubaki kama mashamba yasiyoendelezwa. Naiomba Wizara, washirikiane na Magereza kuendeleza mashamba haya, maana yake Magereza hawawezi kukopa wakaendeleza mashamba yao kwa sababu wao siyo *core business* yao, lakini wakiungana na Wizara, wanaweza kuendeleza mashamba haya ya mifugo.

Kwa mfano kule Ubena kuna shamba, Kitengule kule, King'ang'a na sehemu zingine nyingi, yanakuwa yamebaki tu kama *acreage* zilizo wazi, lakini Wizara ikishirikiana nao, wanaweza wakapata wawekezaji wakaweza kuyaendeleza mashamba haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kusema, ni juu ya ufugaji wa samaki au uvuvi. Niishukuru Serikali kwa kuanzisha mradi wa kuanzisha au wa kutengeneza vifaranga katika eneo la Igunga. Kuna mradi mzuri sana wa kuzalisha vifaranga kwa ajili ya ufugaji wa samaki, wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali basi mradi huu upelekwe na sehemu zingine, uwe *rolled up* kwenda kwenye mabwawa mengine, utasaidia sana wananchi wetu, kwa sababu tukiwa na bwawa na wananchi wanaweza kufuga kwa tija, ni mradi mzuri sana. Kwa hiyo, waongeze pia kasi ya kufundisha wananchi ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Igunga pale tuna vijana wanahitaji kufundishwa, lakini pia wanahitaji kupewa mkopo kwa ajili ya kuanzisha miradi hiyo ya samaki ili iweze kuwa endelevu, lakini kwa maana ya ufugaji wa samaki na uvuvi, nawapongeza sana Serikali kwa kuleta jambo hili kwenye nchi kame na mliendeleze sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sitaki kungoja kengele, nasema bajeti ya kaka yangu ni nzuri sana, lakini atekeleze basi. Wakati mwingine tunatengeneza vitabu vizuri sana kama hiki, lakini utekelezaji unakuwa chini ya asilimia 50. Naomba safari hii basi tekelezeni haya mliyosema ili tuweze kuwaendeleza wafugaji wetu na wananchi wengine waweze kuona Serikali yao inawatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Dkt. Kafumu.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Tanzania ni ya tatu baada ya Botswana na Ethiopia kwa kuwa na ng'ombe wengi zaidi ya milioni 19. Wafugaji wengi nchini toka Mwanza, Shinyanga na Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa Viktoria pamoja na makabila ya Masai, Wairak, wanazunguka nchi nzima na mifugo. Mifugo hii badala ya kuwa baraka imekuwa kero inapoingia katika mashamba ya wakulima. Vifo vinatokea kwa sababu ya mapigano ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri yafuatayo:-

- (i) Serikali itenge maeneo ya wafugaji na ya wakulima *(good land plan)*.
- (ii) Wafugaji wapewe elimu ya kina kujua jinsi ya kufuga kibiashara, wengi wanafuga kwa mazoea.
- (iii) Endapo mfugaji atapangiwa eneo na mifugo yake wakaongezeka na eneo alilopangiwa halitoshi basi auze mifugo yake afanye biashara nyingine. Wafugaji watakaokiuka sheria ichukue mkondo. Bunge litunge sheria ya kusimamia hili.
- (iv) Wafugaji wahamasishwe na kufundishwa kupanua wigo wa biashara *(diversify)*, ili pia kuokoa mali yao ya mifugo hasa pale gonjwa la ndigana kali litakapotokea.
- (v) Serikali ianzishe viwanda vya nyama ili kuwawezesha wafugaji kuuza mifugo na hivyo kufanya ufugaji kibiashara. Sheria ya *PPP, CTI, TPSF*, watafutiwe ili sekta binafsi iwekeze katika kuanzisha viwanda vya nyama. Soko la nyama Comoro, Saudi Arabia na kadhalika liko kubwa, sekta binafsi ishirikishwe kikamilifu.
- (vi) Viwanda vya nyama vianzishwe maeneo yenye mifugo mingi, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dodoma, Singida na kadhalika.
- (vii) Uhamilishaji wa mifugo uende sambamba na elimu ya ufugaji mifugo ya nyama na maziwa. Mfano kunenepesha ng'ombe kwa ajili ya nyama na kadhalika.

- (viii) Serikali ilinde na kuendeleza viwanda vya maziwa. Maziwa mengi yatokane na viwanda/mifugo yetu, mayai yatokane na ufugaji wa kuku nchini. Serikali iache kuagiza kuku, mayai na samaki kutoka nje ya nchi.
- (ix) Badala ya kuagiza samaki China, Serikali ikope/inunue vifaa vya uvuvi katika bahari kuu kwa kuishirikisha sekta binafsi au kutafuta uwekezaji toka nchi za nje, mfano Thailand ni hatua nzuri.
- (x) Serikali ipunguze kodi katika vifaa vya ku-process ngozi. Ngozi italeti pato zuri, viwanda vya ngozi vinasuasua kwa sababu Serikali haioni thamani yake na hasa kwa vile hakuna kiwanda cha viatu nchini. Kiwanda cha ngozi Moshi, process kubwa zinafanyika Nairobi. Kiwanda hiki kiwezeshe, ili process ifanyike nchini ili iuzwe ngozi iliyoongezwa thamani (*value added*).
- (xi) Chuo Kikuu cha Sokoine, wataalam wafanye kazi zaidi, watoe taarifa za tafiti za jinsi ya kufanya mifugo iwe ya tija nchini. Maabara zao zipatiwe vifaa vya kisasa ili tafiti ziwe za uhakika.
- (xii) Serikali baada ya kufanya haya ipige marufuku mifugo kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo lolote lingine nchini. Kila wafugaji waishi katika maeneo yao.
- (xiii) Idadi ya wafugaji na idadi ya mifugo yao ihesabiwe na kila mfugaji alipe kodi kiasi ili kupata pato la Taifa.
- (xiv) Wafugaji wa Tanzania katika maeneo mbalimbali wasipeleke mifugo nchi jirani kutafuta soko. Nchi jirani wanaotaka mifugo/nyama waruhusiwe waingie katika minada ya nchini wanunue mifugo. Kuwapelekea mifugo kunalazimisha wanunuzi kulipa bei ndogo kwa wafugaji wa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali na wafugaji watafanya haya, naamini kutakuwa hakuna ugomvi na hifadhi zetu za Taifa zitalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri na utendaji wao mzuri. Wizara ya Mifugo ni Wizara mama katika Kanda ya Ziwa. Tumezungukwa na Ziwa Viktoria, Wizara hii ikiboreshwa italeti tija kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa. Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, niunge mkono maoni ya Kamati na ushauri kwamba mikakati thabiti ya kuimarisha sekta za mifugo na uvuvi inahitajika ikiwezekana Wizara hii iwekwe kwenye mpango wa *BRN*. Serikali iboreshe miundombinu ya machinjio ya kisasa na viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya mifugo na bidhaa zake. Kwa kuboresha miundombinu, Serikali na wananchi watakuwa na uhakika wa masoko ya mifugo na bidhaa zake ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Kanda ya Ziwa tuna migodi mbalimbali ambayo inahitaji huduma za vyakula. Katika Kanda ya Ziwa, hasa Mkoa wa Geita, hakuna miundombinu ya machinjio ya kisasa. Niiombe Serikali ione umuhimu wa kujenga machinjio ya kisasa Geita, viwanda vya samaki Geita, viwanda vya nyama Geita. Serikali ikiweka miundombinu hii muhimu wananchi watashiriki katika uchumi wa nchi yetu. Wananchi wataavutiwa kuuza mifugo yao kwa faida kulingana na uwepo wa masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuwepo kwa uhaba wa watumishi (wataalamu wa mifugo na uvuvi) katika vijiji vyetu. Nashauri Serikali ibaini maeneo yenye upungufu wa wataalamu kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hizi katika maeneo hayo. Serikali ione umuhimu wa kuweka kipaumbele katika kuajiri wataalamu hawa kwa kuzingatia uwepo wa shughuli za sekta hizo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kanda ya Ziwa Serikali ione umuhimu wa kuleta wataalamu wa kutosha hasa katika sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi watakaosaidia wananchi katika kuboresha uchumi wao kupitia rasilimali zilizo kwenye maeneo husika. Ikiwezekana wataalamu waajiriwe moja kwa moja mara wanapohitimu vyuo vya mifugo na uvuvi kama ilivyo katika sekta ya elimu. Naomba Serikali izingatie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi, inasikitisha kuona sekta hii ilivyodorora hali ya kuwa nchi yetu ina maziwa makubwa, Tanganyika, Victoria, Nyasa na mengine madogomadogo pamoja na bahari ya Hindi lakini bado uvuvi siyo wa tija na uchangiaji wake katika pato la Taifa ni mdogo sana. Kiwango cha 2.4% ya uchangiaji kwenye pato la Taifa ni kidogo sana ukilinganisha na maziwa tuliyonayo na ukubwa wa bahari tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za ziada zinatakiwa katika uboreshaji wa sekta hii. Uboreshaji utasaidia sana upatikanaji wa pato la Taifa kwani kwa kuanza na wavuvi wakubwa wa bahari kuu na maziwa makubwa wataweza kutoa kodi. Ushauri mwingi umekuwa ukitolewa na Kambi ya Upinzani na Mbunge mmoja mmoja jinsi ya ukusanyaji kodi kwenye uvuvi kwenye bahari kuu na maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inatakiwa isaidie upatikanaji wa viwanda vya samaki kwa kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika sekta hiyo ili usindikaji samaki ufanyike hapahapa nchini. Hii itasaidia wavuvi kupata soko la samaki wao lakini pia ajira itaongezeka kwani wavuvi wataongezeka kwani itakuwa sekta inayovutia, lakini pia vijana watapata ajira kwenye viwanda hivyo na nchi itapata kodi hivyo pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo. Sekta hii ni nyeti sana inachangia pato la Taifa kwa 2%, haitoshi. Nchi yetu katika ukanda wa Afrika Mashariki ni nchi ya pili na Afrika ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo lakini bado Serikali haijafanikiwa kufanya sekta yetu hii ya mifugo iwe yenye tija. Serikali igawe ardhi kwa matumizi bora ili wafugaji wapewe maeneo yao, wafundishwe ufugaji wa kisasa, ili mifugo iwe na tija, majosho mengi yajengwe na hospitali za mifugo, madawa na madaktari wa mifugo waongezeka na uwekwe utaratibu wa *mobile doctors* wa mifugo kuwafikia wafugaji walipo ili wasaidie katika kutoa chanjo na kutibu mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba hatuna viwanda vya kutosha vya usindikaji mazao ya mifugo, mfano maziwa, ngozi na nyama. Viwanda vya maziwa *Tanga Fresh*, Azam na kile cha Ubungo bado havitoshi kusindika maziwa yote yanayozalishwa nchini. Wenzetu

Rwanda wamefanikiwa kutumia sekta hii vizuri, mfano wao wanahamasisha ufugaji wa kisasa na wamewatengeneza soko la uhakika la maziwa, wanazalisha maziwa mengi na kuyauza kwenye viwanda vya usindikaji maziwa na wanatengeneza samli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu wanauza ngozi ghafi, kwa nini? Nchi kama Ethiopia wanatengeneza bidhaa za ngozi zinazotokana na wanyama waliopo nchini kwao, mikanda, mabegi, viatu vinatengenezwa nchini mwao na kuongeza pato la nchi hiyo na ajira. Viwanda vyetu vya Morogoro, Mwanza na Moshi havifanyi kazi, vimedorora. Wananchi wanakosa ajira na tunapeleka nje ngozi zetu matokeo yake tunauziwa bidhaa zilizotengenezwa nje na ngozi iliyotoka nchini kwetu kwa hiyo, tunatengeneza ajira kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya nyama vimekufa, *Tanganyika Parkers Dar-es-Salaam*, kiwanda cha nyama Shinyanga, ajira zimepotea lakini pia wafugaji wamekosa masoko ya nyama ambazo zingeweza kusindikwa hapa nchini kwa matumizi ya hapa nchini lakini pia kuuza kwa wingi nje. Kiwango kinachouzwa nje kwa sasa ni kidogo, tukisindika wenyewe tutauza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii sehemu nyingine kuna amani kwingine ni vita. Migogoro ya wakulima na wafugaji unatia umasikini sana. Badala ya wananchi kuendelea na kunufaika na mifugo yao na kilimo chao wanauana na kutiana umasikini. Serikali imeshindwa kutatua migogoro hiyo. Inasikitisha kuona mifugo inauawa bila hatia na mashamba pia huchomwa moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi kwenye mifugo, mifugo ni mali tupime ardhi, wapeni elimu ya ufugaji, wahakikishieni masoko wataacha kugombana na wakulima kwani watakuwa na maeneo yao na huduma zote zitapatikana hapo. Serikali itueleze ni jinsi gani itaondoa migogoro hiyo kabisa.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mengi muhimu kama ifuatavyo:-

- (i) Migogoro wa ardhi kati ya Chuo cha Mifugo Mpwapwa (*LITI/TARILI*) pamoja na kijiji jirani cha Kibodya wa kugombea mpaka, sasa umefikai hatua gani kwa kuzingatia kwamba kijiji hiki kimeandikishwa kisheria tangu kipindi kirefu nyuma? Wananchi wa Mpwapwa wangependa kusikia kauli ya Wizara kuhusu migogoro huu wa mipaka.
- (ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Mheshimiwa Rais alikwisharidhia kuwa kipandishwe hadhi na kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sokoine (*Affiliated University*) of Sokoine. Mpango huu umefikia hatua gani au Mheshimiwa Waziri unasemaje kuhusu utaratibu huu hapo baadaye?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Kwanza nianze kwa kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu tumekuta tunazungumzia mifugo na uvuvi kama sehemu muhimu kwa maendeleo ya nchi, lakini mifugo kwa pekee imeendelea kuwa sehemu ya kuzusha ugomvi na kuzuia maendeleo ya jamii hasa katika maeneo ya wakulima. Wizara ina mpango gani sasa katika kuhakikisha inapunguza au kumaliza kabisa matembezi ya wafugaji au kuzura kunakofanywa na mifugo nchi nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu kumekuwa na malalamiko ya migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na mbuga kwa upande mmoja; na kwa ranchi kwa upande wa pili; na wakulima kwa upande mwingine. Katika Jimbo la Chalinze na Mkoa wa Pwani migogoro hii imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Rufiji, mifugo imekuwa ikichukuliwa kiholela na Askari wa *Selous* na hata pale panapotokea mifugo imeingia, pia hukamatwa. Tatizo hapa ni utaratibu unaofanywa baada ya kukamata mifugo hiyo. Matendo ya kuua mifugo kwa kutumia bundunki/risasi na hata mifugo inapogawanywa, hakuna haki kabisa. Sasa, Wizara ituambie inafanyaje juu ya hatari hii ya kiusalama hasa katika Wilaya ya Rufiji na lile lililotokea katika ranchi ya Ruvu ambapo uonevu na unyanyasi unaonekana wazi.

Mheshimiwa Waziri, kulikuwa na mpango wa kuanzisha machinjio pale Vigwaza/Miswe. Mradi ule ulianza na kwamba umekwama. Wizara itoe majibu wakati wa kuhitimisha, maana kukamilika kwa mradi huu ni moja kati ya jawabu la migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. GAUDENTIA M. KABAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kutoa pongezi kwa kazi, hotuba na mikakati mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari eneo la Kirumi Wilaya ya Butiama kuna maandalizi ya mwaka. Mnada huu utasaidia sana kuondoa wizi wa mifugo kutoka Tanzania kwenda Kenya. Hivyo, mnada utaweka mazingira ya wafugaji kuuza mifugo yao kwa nchi jirani ya Kenya.

Swali, ni lini mnada huu utaanza ili usaidie wafugaji hawa na kuleta pato Serikalini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezaji wa thamani kwa maziwa yanayozalishwa nchini ni jambo muhimu sana linalopaswa kupewa msukumo wa kipekee. Viwanda vya kusindika maziwa vilivyopo hapa nchini bado havijatumika ipasavyo. Lazima tujiulize, kwanini ni asilimia 26 tu ya uwezo wa viwanda hivi ndiyo vinatumika? Serikali ina wajibu wa kufanya utafiti ili kubaini changamoto zinazokabili viwanda hivi ili kupata majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikibidi tushauri wenye viwanda hivi kushirikiana na wafanyabiashara waliopo tayari kujiingiza kwenye Sekta ya Usindikaji wa kutumia viwanda vilivyopo kwa makubaliano na wenye viwanda kuwasindikia maziwa/*products* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo tutafanya hivi, tutakuwa tumetatua tatizo la viwanda kuzalisha chini ya uwezo wa viwanda hivyo, tutaongeza ajira, tutawezesha viwanda kushusha *overheads* zao, ku-*augment revenue* na hali kadhalika tutaokoa kiasi kikubwa cha maziwa yanayoharibika kutokana na kushindwa kusindikwa. Aidha, Serikali itajihakikishia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inisaidie kuanzisha mifuko itakayotoa mikopo katika maeneo ambayo wakazi wake wanategemea maliasili za majini. Jimbo la Nkasi Kusini karibu na Ziwa Tanganyika hakuna kabisa ruzuku zilizokwishatolewa kwa ajili ya kuwakwamua wavuvi. Uvuvi unaofanyika sasa hivi ni wa kijima na hauwezi kuleta mapinduzi ya kuwakomboa wavuvi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Wampembe Jimbo la Nkasi Kusini wananchi wake wanategemea uvuvi tu, lakini hakuna juhudi za Serikali kuwasaidia hata kidogo. Naomba Wizara ione umuhimu wa kuwapa mikopo ili wanunue vifaa vya kisasa vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ikiwezekana kutafuta mwekezaji ambaye anaweza kuuza kwa bei nafuu bidhaa zinazohitajika kuboresha uvuvi na akopeshwe ili na yeye auze kwa bei nafuu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Ziwa Tanganyika ni masikini bila sababu. Wapo Maafisa Uvuvi, wote hawajengi mazingira ya kuwaelimisha wavuvi, badala yake sio rafiki tena kwani wamejenga mahusiano ya kuwatoza faini kila siku na sasa wanaonekana kama sio watu wa kusaidia Sekta hii na Wavuvi kwa ujumla wake.

Nashauri kwamba waelimishwe, wafanye kazi waliyotumwa kusaidia wananchi badala ya kuwahesabia makosa kila wanapokutana. Pia bei ya vifaa vinavyoingizwa nchini ipunguzwe ili kuwasaidia wavuvi.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pamoja na mchango wangu wa maandishi niliokwishaotoa, nalazimika kuchangia tena kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Migogoro hii imekuwa na matokeo siyo mazuri sana kwa pande zote mbili: Watu wameuawa, wamekatana mapanga na matukio yanaendelea bado, kwa nini? Naiomba Serikali ilianganalie jambo hili namna ya kulisuluhisha kwa namna ya kudumu. Nani atakuja kututatulia migogoro hii? Ni sisi wenyewe! Wataalam wetu wakune vichwa, tuachane na matatizo ya kijima kama haya ya kukatana na mapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo imetawanyika nchi nzima na wafugaji ni kama watumwa wa mifugo yao kwani hawaonekani kunufaika na utajiri wa mifugo walionayo. Elimu inahitajika, namna ya kuja na utaratibu utakaokuwa na manufaa kwa wafugaji na wananchi wengine na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujenge miundombinu ya kusindika mazao ya mifugo; kama nyama isindikwe, ngozi isindikwe na kutumika humu ndani ya nchi. Maziwa ni muhimu sana kwa lishe lakini bado hatujaanza kuyasindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku bado haitoshi kwa wafugaji. Hii ni changamoto kubwa. Why? Kidogo kwenye kilimo unaweza kuliona japo kidogo, lakini kwenye sekta hii ni vigumu kuona juhudi iliyowekezwa. Hakuna majosho na hakuna *extension officers* wa kutosha.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo tuna mashamba darasa ya kilimo; kwenye Sekta ya Ufugaji tuna vyuo tu ambavyo siyo rahisi wafugaji wote kwenda kupata mtaalamu kuhusu ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mashamba darasa ya ufugaji yaanzishwe maeneo ya wafugaji; na pili, kwa kuwa wataalam (wagani) katika sekta hii ni wachache ni lazima waongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti ili kuwasaidia wafugaji, ni lazima viwanda vya mazao ya mifugo viendelezwe au kufufuliwa. Kwa mfano:-

- (i) Viwanda vya Nyama;
- (ii) Viwanda vya Ngozi;
- (iii) Viwanda vya Maziwa; na
- (iv) Viwanda Kwako na mifupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaweza kuwahamisha wafugaji kupunguza mifugo wakati hawana mahali pa kuipunguzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matatizo ya wakulima na wafugaji ni vema maeneo ya wafugaji yakafungwa na kuhifadhiwa ili kuanzisha ufugaji wa kisasa kwa kuanzisha ranchi za wananchi ili kuwawezesha wakulima na wafugaji kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa jitihada zake kwani kwa muda mfupi sana viongozi wa Wizara hii wameonyesha umahiri katika kuiongoza Wizara hii.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja bajeti ya Waziri.

Mheshimiwa Waziri, naomba unipe ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo na wapo Watanzania wenye uwezo wa kufuga kisasa, lakini tumekosa eneo lenye miundombinu na linalofaa kwa ufugaji wa kisasa. Je, kwa sababu hapo awali kulikuwa na kugawa ranchi ya Ruvu. Je, utaratibu huo umeishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Maligisu Wilayani Kwimba walianzisha mnada wa mifugo. Leo ni zaidi ya miaka minne baada ya mnada kwa upande wa Maswa kufungiwa na wafanyabiashara na kuhamia Maligisu; je, ni lini Mnada huo utatambuliwa na Wizara yako? Suala la mnada huo nilishakuwasilishia, naomba suala hili lifikie kikomo tupate kibalali na kutambuliwa na Wizara ili kuondoa dhana potofu ya kisiasa, twende na uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba kupitia kwa Mkurugenzi, tuliomba gari hata lililotumika, lakini likiwa katika hali nzuri ili Ofisi ya DALDO iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ina changamoto nyingi. Kwimba ni moja ya Wilaya kubwa; pamoja na kugawanywa mara kadhaa, ombi la gari hilo liko Ofisini kwako na suala hili tulishaongea Ofisini kwako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na Watendaji wote waliopo katika Wizara hii na taasisi zote chini ya Wizara hii kwa hotuba yao yenye uchambuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku hizi kumejitokeza migogoro mikubwa kati ya Wafugaji na Wakulima, napenda kujua Serikali ina mpango mkakati upi ambao utaondoa migogoro hii ambayo inapelekea mauaji katika sehemu mbalimbali hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge lako Tukufu, ni viwanda vingapi vimeanzishwa kwa ajili ya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi? Kuwepo kwa viwanda hivi kutasaidia kuwapatia wafugaji na wakulima masoko ya kuuza mazao ya mifugo na samaki na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa mgogoro wa makundi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aniambie idadi ya viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi kwa maeneo ya Kanda ya Ziwa, Wiko ya Pwani (Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara). Viwanda hivyo vimechangia uchumi wa maeneo hayo kwa kiwango gani hasa katika ajira na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, Serikali imepima Vijiji vingapi katika maeneo yenye migogoro mikubwa kati ya wafugaji na wakulima hasa Manyara, Morogoro na Pwani (Rufiji) na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, Serikali imechimba malambo/mabwawa mangapi kwenye maeneo yenye mifugo ili kuwawezesha wafugaji kuacha kuhamahama na hivyo kulinda mazingira yasiharibiwe, lakini pia kuzuia migogoro ya mara kwa mara baina ya wafugaji na wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu; Je, Serikali imewekeza kwa kiwango gani kwenye sekta hii? Pia napenda kujua iwapo Serikali ina mpango mkakati wa kuelimisha, kuhamasisha na kusaidia wananchi kuanzisha mashamba ya kufuga samaki ili kuondoa umasikini unaowakabili Watanzania na hivyo kuinua hali ya uchumi kama inavyopendekezwa kwenye MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa Mpango mzuri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2015/16. Aidha, niwapongeze kwa utekelezaji mzuri wa Mpango wa Mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku ya pembejeo za mifugo inachelewa kutolewa hali iliyopelekea mifugo kutoogeshwa kwa wakati na kusababisha magonjwa ya mara kwa mara ya mifugo

Kuchelewa kwa chanjo ya ndigana baridi kumesababisha magonjwa ya midomo na miguu kwa ngo'ombe wengi.

Dawa zipatikane mapema kabla ya masika kukabiliana na ugonjwa huu mbaya.

Kuchelewa kwa dawa chanjo za mdondo kumesababisha kuku wengi kufa. Mikoa ya Singida na Shinyanga ndiyo yenye kuku wengi wa kienyeji wanaowaletea kipato wananchi wake.

Serikali ichukue hatua za makusudi kuisaidia mikoa hii ipate dawa/chanjo kwa wakati. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa kila alipo afisa ugani kuwepo pembejeo za kutosha wa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majosho mengi yamekufa, nashauri Serikali ihakikishe inafufua majosho na pia kuhakikisha kila kijiji kina josho. Serikali ihakikishe inatoa mafunzo ya mara kwa mara juu ya menejimenti ya majosho. Fidia za kutosha zitengwe kwenye eneo hili la majosho kuepusha milipuko ya magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minada ni tegemeo la maisha ya wafugaji, wakulima na walala hoi. Hata hivyo, bado hakuna mfumo mzuri wa kutoza ushuru wa mifugo, hutozwa kiholela na bila kujali kama mteja kauza mifugo yake au la, ilimradi kaingiza mifugo sokoni. Vyoo havitoshi au hakuna kabisa, hivyo huhatarisha afya za wananchi.

Minada ifanywe kila kijiji mara moja kwa mwezi ili kuwahakikishia wananchi kupeleka mifugo kwenye minada iliyo karibu badala ya kupeleka mifugo mbali. Kila Halmashauri iwe na mkakati huo wananchi wauze mifugo yao kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zichukuliwe kuhakikisha kila mnada unakuwa na mizani ili kuwapatia bei halali na nzuri wafugaji. Serikali imefikia wapi juu ya suala hili la mizani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya uvuvi itolewe zaidi na iwepo sera ya kuwa na mabwawa kila kata na kila kijiji ili shughuli za uvuvi ziweze kufanyika hata pale ambapo hakuna mito na maziwa. Nashauri Bwawa la Itagata, Kata ya Mpanda samaki wapandwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Serikali itenge maeneo ya malisho kila kijiji ili kuepusha migogoro ya wakulima na wafugaji. Wakati wa Operesheni Vijiji Mwaka 1974/75 yalitengwa maeneo maalum ya malisho na maeneo maalum ya kilimo kila kijiji. Mpango huu umekufa, Serikali ihuishe mpango huu.

Napenda kujua ni nini hatima ya *Holding Ground ya Tanzania Packers* Kitaraka?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali imeshindwa kabisa kuwapatia Wananchi wa Vijiji vya Katanda, Kighanga, Kibwera, Mlamba na Mushabaiguru maeneo ya malisho kama ilivyowapatia wawekezaji wachache?

Sasa ni muda mrefu sana tangu Serikali imeahidi kumega sehemu ya Ranchi ya Kitengule na kuvipatia maeneo ya malisho ya kudumu Vijiji vya Kihenge, Katandu, Kibwera, Mushabaiguru na Mlamba katika Kata ya Kihanga, Wilaya ya Karagwe, Mkoa wa Kagera. Tunaomba leo tuelezwe ni ekari ngapi zimetengwa kwa ajili ya vijiji vyetu hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. DK. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za ruzuku kwa mifugo kutoka Kampuni ya Bajuja International Ltd Uyui wafugaji hawaipati. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kwa Serikali kwa kutatua mgogoro wa Wakulima na Wafugaji Kiteto. Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, amefanya kazi nzuri. Pia ninawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kuanzishwe Agency za Mifugo na Uvuvi na Miundombinu ili kutatua kero mbalimbali na kuvutia wawekezaji.

Hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Ilolansimba, Isikizya, Uyui, Tabora, Oktoba 2010, bado Igalula hatuna malisho japokuwa aliahidi kuwe na malisho ya nyasi za kupanda kama Mabuki na Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kuku wa kienyeji unaleta pato kubwa vijijini; hivyo, Serikali iongeze Maafisa Ugani ili ufugaji bora uongeze ajira na Pato la Taifa hasa vijijini. Pia iongeze dawa ya kideri na mdondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *Deluxe Train* na zile za mizigo zisimame Goweko ili Wafugaji wauze kuku.

Uyui na Igalula Wafugaji wapate elimu ya ufugaji bora na wa kisasa, wapelekwe *NAIC* Arusha kuboresha na kunenepesha mifugo.

Mabwawa ya Nsololo na Bwawa tarajiwa la Goweko Mlimani yaletewe vifaranga bora vya samaki (*fingerings*).

Serikali iongeze *fee* za leseni kwa uvuvi wa bahari.

Mwisho, maeneo ya Muyenze, Ntalasha na Lutende tunaomba tupatiwe kilomita tano za pori kwa ajili ya kufugia ng'ombe na mbuzi.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia hoja moja tu na ninapenda Wizara inipe majibu ya kina.

Katika Wilaya yangu ya Tarime kwenye Halmashauri ya Mji tuna Mnada wa Magena ambao ni wa Kimataifa na ambao ulielekezwa kukarabatiwa na kufufuliwa ili uwe Mnada wa Afrika ya Mashariki lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea umetelekezwa. Hali hii ilipelekea upotevu wa mapato na siyo kwa Taifa tu bali kwa Halmashauri, Kata na Kijiji au Mtaa husika na ukosefu wa ajira huku baadhi ya watu wachache wanafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha ni kwamba, ng'ombe wanaotoka Mikoa jirani na nchi jirani ya Uganda, hupewa kibali wapelekwe Mnada wa Magena uliopo Tarime, lakini cha ajabu hawaelekei huko bali wanaelekezwa kwenye barabara ya Ngerengere, ile *security road* njia panda kumwamo ambapo hutozwa ushuru kidogo na rushwa ndiyo zimetawala kwa watoza ushuru, polisi.

Ninaomba majibu ya kina ni nini Mpango Mkakati wa Wizara kuendeleza Mnada ule wa Kimataifa kama ilivyopangwa, kwani Mnada wa Magena ni muhimu kwa Soko la Afrika ya Mashariki na utakuza uchumi wa maeneo yanayozunguka kupitia dhana ya *multiplier effect*. Nisipopata maelezo ya kina nitashika kifungu kwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa kujua ni nini mkakati wa Wizara katika kutoa ardhi mbadala kwa wafugaji hasa wale ambao wanapakana na Hifadhi ya Serengeti, kwani wananyanyaswa na baadhi yao kuuaawa au kulemazwa na Askari wa Game. Kwa nini Wizara hii isishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ardhi ili kutoa utatuzi wa hili janga.

Kama kweli tunataka kuendeleza ufugaji ni bora tutengeneze miundombinu ya ufugaji ikiwa ni malisho na unyweshaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kujua utaratibu wa ujenzi wa machinjio ya kisasa kwa sababu hayana *value for money*; mfano, ni ule wa Magabiri Kata ya Kitare Wilayani Tarime, uliogharimu shilingi milioni 16, lakini kiuhalisia ni kama bure tu. Je, Wizara huwa mnafanya ukaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya. Pia niwapongeze na kuwashukuru Watendaji wa Wizara hii wakiwemo Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali katika Wizara hii.

(a) Mapinduzi ya Ufugaji; Serikali iandae Sera Maalumu ya Ufugaji ili kuwatoa wafugaji wetu kutoka kuchunga kama enzi ya ujima na kuwafanya wawe wafugaji.

(b) Elimu itolewe kwa wafugaji wote.

(c) Mifugo yetu itafutiwe soko ndani na nje ya nchi, viwanda vya nyama, viwanda vya maziwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la malisho nchini na Wilayani Tarime; elimu itolewe kwa wafugaji ili wapunguze mifugo yao kwani maeneo ya malisho hapa nchini hayatoshi. Maeneo ya malisho yatengwe kwa kila Halmashauri. Wafugaji wetu waelimishwe ili wafuge mifugo ya kisasa. Wilaya ya Tarime ina tatizo kubwa la malisho, ninapendekeza Bonde la Nyarungu linalopakana na Hifadhi ya Serengeti lirudishwe kwa wananchi ili kupunguza adha ya wafugaji katika Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza Serikali ilipe fidia kwa wananchi waliopata tatizo la mifugo kuuawa katika Operesheni Tokomezwa, wakiwemo Wananchi wa Tarime katika Vijiji vya Kagonga, Mangucha na Masanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja ya kutumia mazao ya uvuvi ili kuongeza Pato la Taifa:-

(a) Serikali idhibiti uvuvi haramu.

(b) Wavuvi waelimishwe ili waache uvuvi haramu.

(c) Ulinzi katika Bahari Kuu uimarishwe.

(d) Ulinzi katika Maziwa yetu Makuu uimarishwe.

(e) Utafiti wa kutosha ufanyike ili kubaini ni namna gani Sekta ya Uvuvi inaweza kuongeza Pato la Taifa.

(f) Mazao ya uvuvi yatafutiwe soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara ni moja ya mikoa yenye mifugo mingi sana Tanzania; hivyo, uhitaji wa malambo na majosho ni muhimu sana.

Wilaya ya Hanang ni moja ya Wilaya za Mkoa huo ambayo nayo ina uhitaji mkubwa wa malambo na majosho. Je, ni mpango gani Wizara inao juu ya Wilaya hiyo? Aidha, ni muhimu Wilaya ya Hanang ikaongezewa Maafisa Mifugo walau kila Kata ili kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa muda mrefu baina ya ranchi ya Taifa ya Kalambo na wananchi wa Kijiji cha Katuka. Napata matumaini kwa Serikali kuweka kwenye orodha miongoni mwa ranchi ambazo bado ziko chini ya uangalizi wa Serikali, hivyo kuwepo na uwezekano mkubwa wa kupatikana ufumbuzi wa mgogoro huu kukiwa na nia ya dhati ya Serikali kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii alipata fursa ya kutembelea ranchi ya Kalambo na kupata taarifa juu ya mgogoro huu na wananchi wa Kijiji cha Katepuko ambao walitoa ardhi yao kwa Serikali (NARCO) bila ya kupatiwa fidia yoyote ya ardhi na mazao ya miti waliyootesha tofauti na Vijiji vingine vya Mao na Mbuluma ambao walipatiwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali itoe majibu ya uhakika na hasa baada ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kutembelea eneo husika na hivyo kuwa na taarifa ya kutosha juu ya mgogoro huu. Kwa mara ya mwisho nilivyochangia Wizara hii nilitoa shilingi na kuahidiwa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana wa wakati huo kwamba ufumbuzi wa tatizo hili ungefikiwa. Kwa bahati mbaya hadi ninapochangia leo ufumbuzi bado, hivyo nakusudia kuondoa shilingi kama Serikali kwa kupitia Waziri mwenye dhamana haitanijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni lile linalohusu ufugaji wa ng'ombe mbegu ya asili ya Ufipa. Aina hii ya ng'ombe wana kimo kikubwa na wanafaa sana kwa kukokota jembe kwa kuwafunga wawili tu (Maksai) ambao wana nguvu ya kuweza kumudu kazi hii na pia wana uwezo mkubwa wa kupambana na magonjwa kwa kulinganisha na aina nyingine za ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao wajibu wa kuulinda aina hii ya mbegu zisipotee, naitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi na zinazotoa majawabu ya kuendeleza aina hii nzuri ya mbegu ya ng'ombe aina ya Ufipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo mdogo wa Kituo cha Kupambana na Magonjwa ya Mifugo kilichopo Sumbawanga kushindwa kubaini magonjwa yanayolipuka kama yalivyojitokeza katika Vijiji vya Kalaela, Ilambila, Mwimbi na vingine vingi kumepelekea kutopata ufumbuzi kwa wananchi kutibu mifugo kwa mujibu wa maelekezo ya watalaam wachache waliopo bila mafanikio na kushuhudia mifugo ikiendelea kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusiana na ruzuku ya dawa za mifugo kwa kutokuwafikia wananchi wa Kalambo kwa kutokuwa wazi kwa kubainisha maduka yanayotakiwa kutoa huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani kwa hotuba nzuri sana ya Bajeti. Aidha, napenda pia niwapongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Telele pamoja na Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara itupatie fedha kiasi cha sh. 50,000,000,000/= pekee ili kukarabati Malambo ya

- (i) Lwami;
- (ii) Kauzeni; na
- (iii) Doya.

Malambo haya yapo Wilaya ya Mwanga, yamejaa udongo na hayaweki maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa mategemeo.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Program Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo na Ufugaji. Huu mkakati ulionekana hasa katika maeneo ya wafugaji wa Misenyi, Jimbo la Nkenge. Nkenge tuna shida ya Malambo, mwaka huu limejengwa moja maeneo ya Kakuyu, lakini Kijiji cha Bubale hakuna mabwawa ya kunywesha mifugo na majosho hakuna, je, ni lini hii program itafika Misenyi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa Wilaya ya Misenyi tuna matatizo makubwa ya maeneo ya kulisha ng'ombe na mifugo mingine, watu wameuawa, watu wamepoteza mifugo yao katika Operation Tokomeza na mpaka leo haijulikani nini kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Kata ya Kakuyu na Kata ya Mabale wananyanyasika sana ukizingatia kule Kakuyu Kijiji cha Kakuyu mwekezaji alipewa upande wa mto ambako mifugo ilikuwa inapata maji, hivi tunavyojadili hapa Bungeni Wanakakuyu hawana pa kulisha au kunywesha mifugo yao.

Je, ni lini tatizo la Kakuyu litakwisha kati ya wakulima, wafugaji na wawekezaji? Leo nitaondoa shilingi kama sipati majibu.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Napenda nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya uvuvi. Wavuvi wanafanya kazi ngumu ya kuvua bila kujali mvua, jua au upepo mkali. Hawapati msaada sana toka Serikalini. Hivyo, sasa ni wakati muafaka wa kufikiriwa katika:-

(a) Kupatiwa ahueni ya kodi katika vifaa vifuatavyo:-

- (i) Mashine za boti;
- (ii) Nyavu za kuvulia; na
- (iii) vifaa vya kuokolea (*life jackets*)

(b) Wavuvi wasaidiwe kupata ufadhili au wabia wenye nyenzo na vifaa vya kisasa vya uvuvi ili waboreshe pato lao linalotokana na uvuvi.

(c) Kutokana na uduni wa kipato kwa wavuvi wa Kitanzania, siyo rahisi kwao kuweza kuvua bahari kuu. Hivyo, iwekwe sera au kanuni za kuwataka wavuvi toka nje ambao ndiyo

hasa wanaovuna bahari kuu nchini Tanzania. Basi waingie ubia na wavuvi wadogo wa Tanzania kwa lengo la kuwawezesha wavuvi hao kuongeza kipato chao na kupata ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuendeleza Uvuvi na Mabwawa. Uvuvi huu umewasaidia sana wananchi wa Egypt. Bado Tanzania hatujaupa uzito. Wakati umefika kutoa *priority* kwa kuwasaidia vijana/wananchi waweze kutengeneza mabwawa ya samaki na kuendeleza uvuvi kwa njia hiyo. Tutapunguza umaskini na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafugaji wapatiwe maeneo yao ya ufugaji ili kupunguza ugomvi kati yao na wakulima. Aidha, ni vyema wakaelimishwa umuhimu wa kuwa na ufugaji ulio na tija, *zero grazing* na kupunguza idadi ya mifugo na kufanya maendeleo yao binafsi na mengine.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa na Waziri Mheshimiwa Kamani, Naibu Waziri, Mheshimiwa Telele, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba hii ya bajeti vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa Mifugo wachache; napenda kuishauri Serikali kusomesha Maafisa Mifugo wengi ili Serikali iweze kupeleka Maafisa Mifugo hadi kwenye vijiji. Hii itasaidia sana wafugaji wengi kupatiwa elimu, kupata taaluma ya namna bora ya ufugaji ili mifugo iwe na afya itakayoongeza soko la mifugo, kuwafanya ng'ombe watoe maziwa mengi, kufanya ng'ombe kuwa na nyama yenye ladha nzuri na mifugo ipate huduma ya matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutenga maeneo ya malisho; naishauri Serikali iwe inatenga maeneo ya malisho ya mifugo ili kuondoa migogoro ya wafugaji na wakulima. Waziri atoe maelezo wakati wa kujibu hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda Kidogo cha Ngozi; napenda kuiomba Serikali kukikumbuka Kiwanda cha Ngozi Sepuka, Wilaya ya Ikungi kutengewa fedha za kukiendeleza pamoja na kupeleka wataalam wa kutengeneza vitu vinavyotokana na ngozi mfano, mikanda, viatu na mikoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda Kidogo cha Kusindika Maziwa, Sepuka Wilaya ya Ikungi. Naomba Serikali kupeleka fedha kwenye kiwanda hiki ili kiweze kufanya kazi ya kusindika maziwa kitaalam ili maziwa hayo yawe na kiwango cha soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu na naunga mkono.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED-: Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi, kulingana na Shirika la *Smart Fish*, ambalo linashirikiana na Serikali kukabiliana na tatizo la uvuvi haramu, Tanzania ndiyo nchi pekee barani Afrika ambapo uvuvi huo haramu unafanyika kwa kiwango kikubwa. Uvuvi huo hufanyika katika maeneo makubwa ya Pwani kuanzia Dar es Salaam, Mtwara hadi Tanga, Visiwani, na kumekuwepo ripoti za mabomu kutumiwa katika bahari ya Kaskazini mwa Zanzibar. Hata wataalam wanaonya kwamba iwapo uvuvi wa watumiaji mabomu hautasitishwa, hatimaye Tanzania huenda ikasalia na bahari isiyo na viumbe hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwa na ongezeko la uvuvi haramu hasa katika mwambao wa Bahari ya Hindi kuanzia Tanga mpaka Mtwara. Wavuvi hawa haramu wanaotumia baruti huleta athari kubwa si tu kwa mazingira bali hata kwa watumiaji wa samaki ambao wameuawa kwa baruti zenye sumu. Ila kitu cha kushangaza ni kuwa, wakati wa

uchaguzi mkuu wa Rais na Wabunge wa mwaka 1995, 2000, 2005 na hata uchaguzi wa mwaka 2010 doria za kuzuia uvuvi haramu husitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika chaguzi zote hizo maafisa uvuvi wa sehemu husika huwa wanafanya kazi kwa kupewa maelekezo kutoka ngazi za juu kwamba doria zisimamishwe wakati wa kipindi cha kampeni ili Chama Tawala (CCM) kisinyimwe kura kwenye vijiji vya wavuvi. Serikali ina kauli gani kuhusu haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifugo; Tanzania ni nchi ya pili kwa wingi wa mifugo barani Afrika baada ya Ethiopia kwa kuwa na ng'ombe milioni 22.8, mbuzi 15.6 na kondoo 7.0, lakini kipato kinachopatikana kutokana na bidhaa ya ngozi ya mifugo hiyo hailingani na idadi ya mifugo iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti wa mwaka 2013 uzalishaji wa vipande vya ngozi ya ng'ombe umeshuka kutoka milioni 3.4 hadi 2.9, mbuzi 4.4 hadi 3.6 na kondoo milioni 2.0 hadi 700,000. Sababu kubwa zinazochangia kushuka kwa uzalishaji wa ngozi ni kutokana na kutokuwa na viwanda vya kutosha vya usindikaji wa ngozi pamoja na utoroshaji wa ngozi kwenda katika jirani kupitia njia za panya. Je, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha shughuli za uzalishaji na usindikaji wa bidhaa hiyo zinafanyika hapa hapa nchini kuanzia hatua ya awali mpaka ya mwisho, ili kuhakikisha Taifa linanufaika kiuchumi tofauti na ilivyo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Bodi ya Nyama Tanzania imeundwa chini ya Sheria ya Nyama, namba 10 ya mwaka 2006 na kuzinduliwa tarehe 14 Novemba, 2008. Imepewa mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa sheria ya nyama na kusimamia uzalishaji, usindikaji na biashara ya nyama na bidhaa zake unazingatia viwango vya ubora ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Je, ni kwa kiwango gani Bodi imewezeshwa ili kutimiza majukumu yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya machinjio nchini yamekithiri kwa uchafu uliopitiliza na kuhatarisha maisha ya walaji wa nyama, mazingira yanayozunguka pamoja na wanaofanya kazi katika machinjio hayo. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa machinjio yanayohatarisha afya za walaji, mazingira na wanaozunguka maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Mayai na Maziwa, hivi karibuni kumezuka mjadala juu ya nchi za jirani zinavyofanya soko la mayai na maziwa nchini kuwa la ushindani mkubwa. Watanzania wanaonekana kuzidiwa na uingizaji holela wa maziwa na mayai toka nchi za jirani, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa wafanyabishara wa ndani wanapata uhakika wa soko katika nchi yao?'

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atupe taarifa juu ya tetesi za uwepo wa Kiwanda cha Kuchakata Nyama ya Punda ambacho kinamaliza wanyama hawa ambao ni wanyama kazi.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza na kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote tunafahamu kuwepo kwa migogoro ya Ardhi kati ya wakulima na wafugaji kwa miaka mingi sasa.

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi atueleze kama hakutakuwa na athari ya uamuzi wa kujenga kituo kipya cha upimaji wa uzito wa magari kilichojengwa mwaka 2014/2015 katika eneo kati ya Ruvu na Chalinze. Hakuna asiyefahamu kwamba eneo hilo wafugaji ni wengi na wametumia eneo hilo kwa miaka mingi. Kuwepo kwa kituo hicho

kunakaribisha magari mengi sana kusimama kwa muda mrefu na kwa hali hiyo kukaribisha wafanyabiashara ambao pia wameanza kujiwekea makazi mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wafanyakazi hao wakulima pia wameanza na wataendelea kujisogeza katika eneo hilo lenye mvuto na kwa hali hiyo kukaribisha migogoro mipya kati ya wakulima na wafugaji na sasa na wafanyabiashara. Nashauri Mheshimiwa Waziri atoe kauli kuhusu hali hiyo iwapo haitaathiri wafugaji katika eneo hilo na hivyo kuongeza migogoro kati ya wafugaji na wakulima badala ya kudhamiria kupunguza migogoro hiyo.

MWENYEKITI: Sasa naomba nimwite Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mgimwa. Dakika tano!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kidogo kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Vile vile naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mifugo ni tatizo mtambuka, ambalo lina-*involve* Wizara zaidi ya tano, kwa maana ya Wizara ya TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi yenyewe, Viwanda na Biashara, Maji na kadhalika. Kusudi tuweze kutatua tatizo hili, lazima hizi Wizara zote ambazo nimezitaja zinatakiwa zifanye kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa ku-*respond* kidogo, kwenye maeneo ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Opolukwa, Mheshimiwa Mzee Ole-Nangoro, Mzee wangu Mheshimiwa Laizer na Mheshimiwa Shibuda, kuhusu suala la Wizara ya Maliasili na Utalii kuyaachia baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kuna wafugaji kutoka Kanda ya Ziwa, hasa kwenye kanda ya BBK, (Biharamuro, Biligi na Kimisi) walikuja pale Wizarani wakieleza hili tatizo. Sisi kama Wizara tuli-*take action* tukaenda kuangalia tatizo kwa ujumla na bada ya kuliona tatizo tulimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukapata nafasi ya kuzungumza na mwenzetu Dkt. Kamani, tukafanya mkutano mkubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo, kwamba jambo hili lishughulikiwe na Wizara mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kweli nataka nikuhakikishie, tumeanza kulishughulikia na sisi kama Maliasili na Utalii, tumeainisha mapori tengefu 16, ambayo tayari tumeshayapeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kuyaachia kusudi shughuli nyingine ziweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha na idadi ya mapori tunayo hapa, kwa hiyo, tunamngoja Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe *respond* kwa sababu haya mapori yalitokana sheria mbalimbali ya uanzishwaji wake, kwa hiyo, lazima zile sheria zifuatwe kusudi tuweze kuya-*release*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe angalizo tu, kwamba ni kweli tutayatoa mapori 16, lakini sisi kama wafugaji, kama Wizara husika pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ijpange vizuri na itengeneze utaratibu mzuri kwa ajili ya kuyatumia hayo mapori 16 tutakayoyatoa. Itatokea tena siku, kama hatutajipanga vizuri, tutahitaji kutoa mapori mengine na mengine, hatimaye yatakwishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na sisi Maliasili na Utalii, tutajipanga vizuri kwa kuhakikisha yale maeneo 16 tutakayoyatoa ya Mapori Tengefu yatatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna malalamiko mengi ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge, tunaomba Waheshimiwa Wabunge na wenyewe watusaidie, kwa sababu kuna wakati mwingine inajitokeza, kunakuwa kuna *deal* kati ya wafugaji na askari wetu wa wanyamapori, wanakubaliana kwenye baadhi ya maeneo, inapotokea tatizo wamesigana, matatizo ndiyo yanapoanza na kwa sababu wafugaji wanakuwa wana watetezi wanakuwa wa kwanza ku-shout.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuwaambie wafugaji wetu wasitoe rushwa kusudi mifugo yao waingize kwenye mapori yetu. Kwa sababu wakitoa rushwa wanawashawishi maaskari wetu kuchukua, watakaposhindana tu pale ndani, ndiyo matatizo yanapotokea.

Kwa hiyo, kuna tatizo la pande zote mbili na sisi kama Wizara tumeshaanza kuchukua hatua kwa wale askari wetu ambao wana matatizo, kuna baadhi ya askari zaidi ya 10 tumeshawasimamisha. Kwa hiyo, nataka nitoe hilo angalizo, lakini kubwa kuliko yote, nataka niseme tu, pamoja na nafasi tuliyoitoa ya kuachia hayo Mapori Tengefu 16, bado ni kosa la jinai kuingiza mifugo ndani ya hifadhi zetu za wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba nimwite mtoa hoja, naanza na Naibu Waziri. Dakika 15!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kulitumikia Taifa hili kama Mbunge na kama Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Napenda pia kuishukuru familia yangu, mke wangu, vijana wangu na wapiga kura wa Jimbo la Ngorongoro, kwa ushirikiano wao katika kunifanikisha kuweza kulihudumia Taifa hili na nianze mchango wangu kwa kusema, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu maelezo na hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano; Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuongoza nchi yetu kwa busara na hekima ambayo imeendelea kuleta amani, utulivu na mshikamano katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kumshukuru Rais kwa kuendelea kuwa na imani nami katika wadhifa huu alionipa wa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano kuwa Wabunge.

Napenda pia kumshukuru Waziri wangu, Dkt. Titus Mlengeya Kamani, kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, katika kipindi hiki.

Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa wote kwa ushirikiano waliotupa katika utendaji wetu wa kazi ndani na nje ya Bunge, nawaahidi ushirikiano wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara, Taasisi zake zote, Bodi mbalimbali zilizoko chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaotupa katika kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro, ambao walinipa kura na kunichagua kuwa mwakilishi wao wa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naahidi kuwa karibu nao ili niweze kulisukuma gurudumu la maendeleo pamoja na wao na naahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote na kama itawapendeza wakati ujao wanikumbuke katika ufalme wao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kuchangia hoja kwa kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia kwa kusema hapa Bungeni au kwa maandishi. Nitangulize kusema kwamba mtoa hoja, Waziri, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani atakapokuja kuhitimisha atawatambua rasmi wote waliochangia kwa maandishi na kwa kusema lakini kwa ujumla wao wote tunawashukuru sana kwa michango yao. Tunathamini michango yao hiyo na tutaendelea kuifanyia kazi. Michango yote tumeitolea majibu na pia tutaandaa bangokitita kwa ajili ya majibu mengine ambayo hatutaweza kuyasema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kulikuwa na hoja mbalimbali, ni nyingi sana, lakini kwa muda mfupi tuliopewa hatutaweza kukamilisha tutayasema haya ambayo yatawezekana kwa muda ambao tumepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya ujenzi wa machinjio ya Tinde, Wizara itenge shilingi milioni mia mbili kukamilisha ujenzi huo. Jambo hili lilizungumzwa na Ndugu yangu Ahmed Ali Salum, Mbunge wa Solwa. Wizara inahamasisha Halmashauri kuingia ubia na sekta binafsi katika kukamilisha ujenzi wa machinjio ya Tinde. Tunasema hivi kwa sababu kwa kweli kilio cha Wabunge wengi hapa kuhusiana na Wizara yangu ni kwamba inapata bajeti ndogo sana. Sasa tukianza kutafuta tena pesa kama hizi milioni mia mbili kwa ajili ya kukamilisha machinjio haya ya Tinde hali yetu inaweza kuendelea kuwa mbaya zaidi. Kwa sababu Halmashauri ni Serikali tosha, tunawashauri waingie ubia na sekta binafsi, watafute mwekezaji ili waweze kukamilisha machinjio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine, lini Serikali itasitisha uingizwaji wa nyama ya ng'ombe na kuku katika nchi hii. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Opolukwa, Mbunge wa Meatu. Majibu yake ni kwamba Serikali hairuhusu kuingiza nyama ya kuku kulingana na tatizo la udhibiti wa mafua makali ya ndege. Pia nyama ya ng'ombe huingizwa kwa kiwango kidogo kwa matumizi ya soko maalum. Soko maalum ni kama vile mahoteli makubwa na migodi. Kwa kweli tuna nyama ya kutosha hapa nchini kwa sababu tuna mifugo yetu ya kutosha. Kwa soko la ndani tu tunasema tunakwenda mnadani, tunakula nyama choma na vitu vya namna hiyo. Hata hivyo, hoteli zile ambazo wanataka nyama ambayo ni viwango vikubwa, ndiyo hiyo ambayo tunaagiza kwa kiwango kidogo kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ya upungufu wa majosho, jambo hili limezungumziwa na Mheshimiwa Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mbunge wa Morogoro Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya hoja hii ni kwamba Wizara na mamlaka nyingine za Serikali na Serikali za Mitaa zitaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi na ukarabati na uendeshaji wa majosho hapa nchini. Yatasha kusema tu kwamba katika kipindi cha miaka kumi, jumla ya majosho 348 yamejengwa kwa jumla ya shilingi bilioni saba na majosho 640 kukarabatiwa kwa jumla ya shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa kuhusu mafunzo kwa wafugaji kuhusiana na masuala mbalimbali ya wafugaji. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine na Mheshimiwa Betty Machangu. Hawa walikuwa wamechangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mafunzo kwa ajili ya wafugaji kuhusu masuala mbalimbali, hawa ni wadau wetu wa maendeleo, kwa hiyo, kama Wizara tuna jukumu kuendelea kutoa elimu ya ufugaji bora wa mifugo yaani ng'ombe, kuku na samaki kuhusu mfumo wa unenepeshaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na malalamiko kwamba katika Hotuba ya Waziri tumeeleza zaidi juu ya mifugo kuliko uvuvi. Tunachukua jambo hilo lakini sidhani kama lilikuwa limedhamiriwa, limetokea tu. Ushauri ulitolewa kwamba labda mbele ya safari wawepo Naibu Mawaziri wawili, mmoja wa kushughulikia samaki na mwingine wa kushughulikia mifugo katika Wizara hii, nadhani ni jambo la msingi. Katika Serikali ijayo ni kiasi cha kujenga hoja ili jambo hilo likubaliwe kama ambavyo wametoa mfano wa Wizara ya Nishati na Madini. Nadhani ni jambo ambalo kwa kuwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu italiangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa kuhusu masoko ya mifugo na mazao yake. Hoja hii ilitwa tena na Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyangwine lakini hili ni kama nilivyokuwa nimesema masoko tutaendelea kuyatafuta na tutahamasisha pia sekta binafsi kushiriki na Serikali katika jambo hili la ujenzi wa machinjio na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na mazao ya samaki. Ni lazima tuhangaikwe kuwatafuta watu ambao watatusaidia kuwekeza katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Msolla ni kuhusu hali ya masoko ya samaki katika soko la feri lililoko Ilala Dar es Salaam, Kirumba Mwanza na Kasanga kule Rukwa. Ni kweli Kamati yetu ilitembelea maeneo haya na hasa hili soko lililoko Dar es Salaam na kuona kwa kweli hali yake siyo nzuri hata kidogo. Kuna msongamano mkubwa, hakuna uongozi, hakuna bodi, basi ili mradi kila kitu kimekaa ndivyo sivyo. Taasisi na wadau mbalimbali kupitia Wizara yetu tumewasilisha maoni kwa Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili wavuvi wapatiwe eneo mbadala badala ya pale feri kwa sababu kuna msongamano mkubwa sana pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile suala la msongamano na wafanyabiashara kuwa wengi na miundombinu inazidi kuwa duni, hili tumelizingatia. Hata hivyo, Halmashauri na Manispaa ya Ilala inaandaa upya sheria ndogo za uendeshaji wa soko zitakazowezesha kuundwa kwa bodi ya uendeshaji wa soko la feri. Hili jambo tumelizingatia na hasa kwa sababu Kamati ya kisekta imetembelea na kushauri kwamba lazima tufanye jambo hilo ili kuweza kuwasaidia hawa wavuvi na kuwatafutia maeneo mbadala. Tuna sehemu kubwa sana ambayo tukiweka miundombinu kule wanaweza kuendelea kufanya shughuli zao za uvuvi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya miundombinu ya mifugo ambayo imetolewa pia na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na Mheshimiwa Suleiman Nchambi. Maelezo ni kwamba Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeendelea kutoa elimu ya ufugaji bora wa mifugo, mfumo wa unenepeshaji na matumizi endelevu ya rasilimali za mifugo. Elimu hii hutolewa kupitia redio, runinga, vipeperushi, vijitabu na kadhalika. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa elimu juu ya miundombinu ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya migogoro ya wafugaji na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Hoja hii kwa kweli karibu kila Mbunge aliyesimama ameizungumzia. Waliozungumzia hoja hii ni Mwenyekiti wa Kamati ya sekta, Mheshimiwa Profesa Msolla, Mheshimiwa Ole-Nangoro, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Hamad Rashid na wengine wengi. Majibu ni kwamba Serikali itayazingatia mapendezo ya taarifa ya Kamati Teule katika utatuzi wa migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Kamati hii mtakumbuka iliongozwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka na wamependekeza mambo mengi na kwa kweli tunadhani isingekuwa kwamba muda umekuwa ni mdogo sana, wamependekeza mambo ambayo tukiweza kutekeleza mapendekezo ya Kamati Teule tunaweza kwa kiasi kikubwa kupunguza hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sisi kama Wizara tumeshaelekezwa na Waziri Mkuu kwamba maeneo yetu yale ya mashamba ya NARCO na sisi tuyaangalie. Tuna mashamba makubwa sana ambayo kwa kweli mifugo iliyomo mle ni kidogo sana, ni vizuri tukafika mahali kwa kweli maeneo yale tukayabaini na tumeshayabaini ili kuweza kuwapa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama alivyosema Naibu Waziri wa Maliasili, jambo hili ni mtambuka linahusisha Wizara mbalimbali. Kwa moyo wa dhiti kabisa, kama wote tutazingatia jambo hili, tunaweza tukafika mwisho kwa sababu Tanzania ni yetu sote, wakulima na wafugaji na hatuna sababu ya kuendelea kugombana kwa sababu sote tunategemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya tathmini ya mashamba yetu ya NARCO imewasilishwa ofisi ya Waziri Mkuu hata Wizara ya Maliasili na Utalii na yenyewe imeshapeleka mapendekezo yake Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa hiyo tunasubiri tu Waziri Mkuu atuambie endeleeni kama mlivyopendekeza ili tuweze kukamilisha na kumaliza migogoro hii ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo, Mheshimiwa Dkt. Kamani atakuja kutoa maelezo kwa masuala mengine yaliyosalia, ahsante sana.

MWENYEKITI: Unga mkono hoja.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitangulia kuunga mkono hoja hii lakini narudia kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara nyingine ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia bajeti yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge lakini nikupongeze sana kwa jinsi ulivyotuongoza katika kikao hiki cha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kufafanua hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, napenda nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru wageni wangu waliokuja kunitia nguvu katika siku hii muhimu. Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Simiyu, wawakilishi wa wafugaji na wavuvi, Wenyeviti wa taasisi zilizo chini ya Wizara yangu lakini zaidi kwa namna ya kipekee mke wangu mpendwa, nawashukuru sana. Wanasema kila alipo anayejibidisha yuko mwanamke nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nirudie kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Busega kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia. Napenda kuahidi kuwa nitatumia muda wangu, nguvu na maarifa yangu yote kuhakikisha tunatafuta rasilimali kwa ajili ya ustawi wa wananchi wote wa Busega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa jitihada zao za kuisimamia Wizara yangu na kutoa ushauri kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta hizi mbili za mifugo na uvuvi zinaleta tija na kubadili hali ya uchumi wa wananchi pamoja na Taifa kwa ujumla. Kwa kweli wamesimama bega kwa bega na sisi kuona kwamba mipango tunayoifanya inafanikiwa. Hoja ambazo wamekuwa wakizitoa zimekuwa kichocheo na chachu katika kubadili fikra na mtazamo katika utendaji kazi wa Wizara na hivyo kuweza kufikiria nje ya utamaduni uliozoeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kumshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, dada yangu, kwa michango na ushauri alioutoa katika taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia ama kwa kuongea au kwa maandishi, kwa michango yao mizuri yenye lengo la kujenga na kubadili taswira ya sekta hizi ninazosisimamia. Vilevile kwa Waheshimiwa Wabunge ambao hawakupata fursa ya kuchangia kutokana na ufinyu wa muda pia tunakaribisha michango yao ya mawazo kwa muda wowote watakaona nafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 23 wamechangia bajeti hii kwa kuzungumza na 25 wamechangia kwa maandishi. Aidha, jumla ya Waheshimiwa Wabunge wanane walichangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika masuala yanayohusiana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, nitajitahidi kufanya ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo sitatoa ufafanuzi wasidhani kwamba tumezipuuza au si za muhimu lakini ni kwa sababu tu ya muda. Aidha, kwa zile ambazo tutakuwa hatujazitolea majibu, naahidi kuwa Wizara yangu itaandaa majibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa nianze kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zitakuwa hazijatolewa maelezo na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wingi wa michango uliotolewa katika muda huu mfupi, wa asubuhi mpaka sasa hivi kwa Waheshimiwa Wabunge 48 kuchangia, inaonesha jinsi sekta hizi mbili zilivyo muhimu katika maisha ya wananchi wa Taifa letu. Waheshimiwa Wabunge, nakubaliana nanyi kabisa kwa sababu mimi binafsi naamini kwamba sekta hizi ni za muhimu

sana. Asilimia arobaini ya kaya zote za kilimo zinajishughulisha na ufugaji lakini wananchi zaidi ya milioni nne wanajishughulisha na uvuvi, hii si idadi ndogo. Pia ongeza kuna watu wanaojishughulisha na biashara, wasindikaji lakini walaji wenyewe, karibu asilimia mia moja ya Watanzania wanahitaji protini za aidha mifugo au samaki. Kwa hiyo, sekta hizi ni muhimu sana, nakubaliana na uchungu wenu mliokuwa nao lakini kama mlivyokuwa mnaeleza wenyewe na kuonesha kuguswa kwamba kikwazo kikubwa cha utendaji wa Wizara ni ufinyu wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa jinsi walivyotutetea lakini kwa sasa kuna hiki tulichoomba, naomba mtupitishie tu tukatende kazi kwa sababu mimi nina hakika nina jeshi la kutosha. Nina timu ya wataalam, kama baadhi yenu mlivyoshuhudia, tuna wataalam, tuna wasomi katika Wizara hii wanahitaji rasilimali fedha wakafanye kazi. Nina hakika kama hizi tulizoomba zikipatikana licha ya mahitaji yale makubwa, naamini kutatokea mabadiliko ya kweli katika sekta hizi kwa wananchi na kwa kipato cha Taifa. Kwa hiyo, naomba tu muendeele kutuunga mkono ili tuhakikishe haya tunayoyaomba yanapita na ili wataalam wakaweze kufanya kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi makubwa sana yamezungumzwa katika michango ya Waheshimiwa Wabunge. Limezungumzwa sana hili la migogoro ya wakulima na wafugaji. Hili ni suala kubwa na kwa kweli bila kulipatia ufumbuzi wa haraka, kwanza linatishia amani, watu wanapopoteza maisha yao siyo hali nzuri, kwa hiyo, ni lazima litafutiwe majibu ya hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inachukua hatua na baadhi mmeshazona. Kuna timu zimeshaundwa, kwanza tu Bunge lenyewe kuunda Kamati Maalum kushughulikia suala hili inaonyesha jinsi sisi wawakilishi wa wananchi tunavyoguswa na suala hili na tunavyotaka mabadiliko. Pia upande wa Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda timu ambazo siyo tu zimekwenda kutengeneza taarifa lakini zimekwenda kutenda na kufanya utatuzi wa migogoro hii. Hii inaonyesha kwamba kuna kazi ya makusudi inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuelewe kwamba hii migogoro imelelewa au imekuwa kwa muda mrefu. Ugonjwa ukiingia kwa muda mrefu huwezi kuuondoa kwa siku moja. Kwa hiyo, muipe muda Serikali ikafanye kazi, nina hakika hatua kwa hatua migogoro hii itapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule Mvomero, kazi ya upimaji ardhi imeshafanyika. Wizara ya Ardhi ilihamishia timu kule ili kupima na kuainisha maeneo kwa kutenga maeneo ya vijiji na kuelekeza mpango wa matumizi bora ya ardhi, ni hatua mahsusi zinachukuliwa. Kama nilivyosema nchi hii ni kubwa hatuwezi tukaona mabadiliko ya mara moja lakini muamini kwamba hatua zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kuteuliwa kuwa Waziri tumeitisha vikao kadhaa na wadau hasa wa sekta ya mifugo na tulikuwa na mkutano mkubwa wa wadau wa mifugo uliofanyika mwezi wa tisa Jiji Mwanza ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa mgeni rasmi. Kuna maamuzi na maelekezo mengi yalitolewa na tayari maamuzi hayo yanafanyiwa kazi. Wiki mbili au tatu zilizopita tulikuwa na mkutano mkubwa wa wafugaji ambao ulifanyika Jimboni kwangu, wafugaji waliamua wakutane na Mawaziri watatu tulihudhuria, mimi mwenyewe, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Maliasili na Utalii, tulikutana na wawakilishi wa wafugaji wa nchi nzima kujadili tena na kuangalia maeneo ambayo bado yanaleta ukakasi. Maamuzi yalitolewa na mengine tuliekeleza na yameshaanza kuchukuliwa hatua. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba

Serikali hii haifanyi chochote, kuna hatua madhubuti zinafanyika na naomba Waheshimiwa Wabunge mkubaliane tu kwamba kuna kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile labda nitumie nafasi hii kuwaasa wananchi na wadau wote wa ardhi, wawe wafugaji au wakulima. Ardhi ya Tanzania ni ileile tangu tumepata uhuru lakini kwa sababu ya huduma nzuri za afya, kuongezeka kwa elimu na watu wanaanza kujitambua jinsi ya kujitunza na ubora wa lishe, idadi ya Watanzania itaendelea kuongezeka, maana yake na mahitaji ya ardhi yataendelea kuongezeka kwa makazi, kilimo, ufugaji na shughuli nyingine mbalimbali, jibu ni matumizi bora ya ardhi. Tunavyosema tu kwamba tupewe ardhi, ardhi haitashuka kutoka kwingine, kwa hiyo, ni lazima wote tuwe tayari kushirikiana, hatuwezi kuishi bila wafugaji, wakulima wala makazi na tunahitaji maeneo ya hifadhi kwa ajili ya vyanzo vya maji, kuboresha hali ya hewa, utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala ni letu wadau wote na Waheshimiwa Wabunge maamuzi mengine yanafanyika kwenye Halmashauri zetu. TAMISEMI ni mdau muhimu sana katika masuala haya ya migogoro na sisi kule ni Madiwani, naomba na kule tukashiriki kutoa michango yetu kuhakikisha kwamba hili tatizo tunalipunguza. Nafahamu tatizo halitaisha mara moja lakini hatua lazima tuchukue. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kuhusiana na suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja nyingine muhimu sana iliyozungumzwa ni kuhusiana na kupuuzwa, kulionekana kama ni kupuuzwa au kupewa kipaumbele cha chini sekta ya uvuvi. Waheshimiwa Wabunge, siyo kweli kwamba sekta hii inapewa uzito wa pili au wa chini. Kwanza, kimapato katika mchango wa Taifa ina mchango mkubwa sana kama ile ambayo Mwenyekiti wa Kamati alizungumzia habari ya *import substitution* kwamba kama ingebidi kuagiza mazao ya uvuvi kutoka nje basi nchi hii ingetumia fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo ni la kihistoria kidogo katika muundo wa Wizara ilivyoanza mwanzo kulikuwa na idara zilizofahamika mapema katika Idara ya Mifugo. Unafahamu hizi Idara zimeunganishwa, Uvuvi ilitokea Maliasili ikaingia pale ikiwa na Idara moja. Sasa hivi niwahakikishie na kuwatoa hofu kwamba Wizara inaangaliwa kutengenezewa muundo mpya na imeshafikia hatua nzuri kwa maana ya sekta ya uvuvi itaongezewa idara na hivyo ni *automatic* kwamba hata tutakapokuwa tunatoa taarifa katika kitabu itakuwa na maeneo mengi ya kutolea taarifa. Hata hivyo, japo kuna kurasa chache bado kuna mambo mazito na ya muhimu sana yameelezwa katika kitabu chetu na hata katika mipango ya maendeleo imepewa uzito mkubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwatoe shaka ni kwamba sekta ya uvuvi ni ya muhimu na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Kandege na wengine wote mliofikiri kwamba sekta hii imepuuzwa siyo sahihi, ni mambo ya kihistoria lakini kuna kazi kubwa inayoendelea na tunatambua sana. Mimi mwenyewe nimeshiriki mara nyingi sana kuhakikisha kwamba tunaongeza idara hii ili ionekane zaidi ndiyo maana tunaitisha uwekezaji, tunaitisha makongamano ya wavuvi na vilevile kushirikisha TAMISEMI ili iweze kuitambua vizuri Idara hii ya Uvuvi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni la usindikaji na uendelezaji wa mazao ya mifugo na uvuvi. Ni kweli sekta hizi zimekuwa zikifanyika kiutamaduni zaidi kwa muda mrefu lakini sasa hivi kuna kazi kubwa inafanyika, mpango wa *modernization* ya mifugo na uvuvi kwa maana kwamba kubadilisha kabisa mtazamo na sura na jinsi ya kuzifikiria sekta hizi ili zionekane dhahiri jinsi zinavyoweza kubadilisha hali ya maisha ya watu. Katika *modernization* hii inakuwa shirikishi sana, wataalam mbalimbali watahiriki katika kuandaa *modernization* hii lakini vilevile wadau wengine namna ya

kupata rasilimali za kutekeleza mabadiliko haya zinafanyiwa kazi. Mabadiliko haya ni pamoja na kuboresha uzalishaji wote kwa maana ya kwamba kuwe na mbegu bora katika ufugaji wa samaki, ufugaji wa mifugo, aina ya mifugo ambayo itakuwa na tija zaidi na kuwa na matokeo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itahusisha usindikaji wa mazao haya. Hizi takwimu ndogo mlizoonza za mabadiliko ni za muda mfupi, za kuongezeka viwanda vya usindikaji, ni kwa sababu kuna juhudi za makusudi sasa hivi zinaendelea za kutangaza. Wapo hata Watanzania wenye mitaji ya kushiriki katika usindikaji lakini kwa sababu walikuwa labda hawana ufahamu wa kutosha au Serikali ilikuwa haijawapa uelewa wa kutosha, sasa hivi tunatangaza vya kutosha. Tuna vijitabu vya kutangaza fursa za uwekezaji kwa sababu tunaamini kupitia usindikaji, uongezaji thamani ndiyo kutakapokuwa na soko la uhakika la mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiki mlíchokizungumza, habari ya kuhamisha ajira kwenda nchi nyingine kwa sababu tunauza aidha mifugo hai au tunapeleka ngozi zikiwa hazijasindikwa ni kwa sababu hatujafanya ya kutosha katika usindikaji. Sasa haya mabadiliko mnayoyaona ni ya kipindi kifupi na mwelekeo sasa ni mabadiliko makubwa. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge hata ninyi kama mna watu ambao mnawafahamu ambao wanaweza kuingia katika usindikaji tunawakaribisha sana, milango ya Wizara iko wazi na tunaweka mazingira mazuri ili kuvutia usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la masoko, tunayo Idara maalum lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta masoko kwa ajili ya mazao ya mifugo na uvuvi ili kuhakikisha kwamba wafugaji na wavuvi wetu wanapata masoko ya uhakika ya mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia habari ya kuimarisha ufugaji wa mifugo michache. Hili lipo katika mpango na tayari hatua zimeshachukuliwa, tunafanya kazi kwa kushirikiana na wadau na taasisi zisizo za kiserikali kuhamasisha ili kuvutia uwekezaji katika mifugo michache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mfano tunafahamu kabisa kuku hasa wa asili ni muhimu sana katika uondoaji wa umaskini hasa kwa akina mama maeneo ya vijijini. Ndiyo maana Serikali imewekeza nguvu za ziada kuhakikisha kwamba tunazalisha chanjo za mdondo za kutosha ili kukidhi mahitaji ya nchi yetu. Bahati nzuri hatua ni nzuri, uzalishaji umeshaanza kupiga kasi, tunaingiza mitambo ambayo ni *automated* ili kuongeza uzalishaji hatimaye kukidhi mahitaji ya ndani na baadaye kuuza kwa masoko ya nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahamasisha tu wananchi kwa sababu mara nyingi nafahamu hasa maeneo ya vijijini watu wamezoea kuona kuku kama ni kitu rahisi tu. Msimu wa mdondo ukifika wanawaachia wanakufa bila kujali kwamba wanapoteza pesa nyingi sana lakini gharama ya chanjo hizi ni ndogo sana, dozi moja ni shilingi 25/= ambayo kila mwananchi anamudu. Kwa hiyo, nawahamasisha kuingiza maarifa kidogo na Maafisa Ugani wetu wako kule ili kuhakikisha kwamba watu wananufaika na rasilimali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa kwa uzito mkubwa ni habari ya uhaba wa Maafisa Ugani. Ni kweli Maafisa Ugani hawatoshi na sisi Wizara tumekuwa tukiwasilisha maombi yetu ya kuongezewa Maafisa Ugani. Naamini kadri bajeti ya Serikali inavyozidi kuwa bora, tutazidi kupewa nafasi ili kuhakikisha kwamba upungufu wa Maafisa Ugani kwa uvuvi na kwa mifugo unapata majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wazo kuu tunakotaka kuelekea ni kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani hawa wanapohitimu kutoka kwenye vyyo waajiriwe moja kwa moja kama ilivyo

kwa watumishi wa Idara ya Afya, Walimu na kadhalika. Kwa hiyo, tunaamini kwamba Maafisa Ugani na wenyewe wakianza kuajiriwa moja kwa moja itasaidia sana kuziba upungufu huu, vilevile sisi Serikali tunaendelea kuzalisha wataalam. Kwa hiyo, tumeshajiwekea mpango wetu wa kuhakikisha kwamba uwezo wa vyuo vyetu vya FETA na LITA unakuwa mkubwa waweze kudahili wanafunzi wengi zaidi ili kupunguza hii gap kubwa iliyopo kati ya walipo na mahitaji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumziwa sana habari ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara lakini hili ni kama nilivyolieleza katika *modernization* ya mifugo labda cha kuongezea hapa ni kwamba ni vema wafugaji wetu wakatambua kwamba mifugo siyo tu kitu cha ziada katika familia bali mifugo ni zao kama unavyolima kahawa, chai, mpunga na kadhalika. Kama ni zao ina maana kuna muda wa kuvuna, kuna muda wa kuweka pembejeo na kuhakikisha kwamba inakupa manufaa kwa kuwa na hiyo mifugo siyo tu kuwaangalia kwa sura. Ndiyo maana sisi tunaweze sana katika kuhakikisha mbegu bora za mifugo zinapatikana kwa urahisi ili wafugaji wetu wawe na ng'ombe na mbuzi wa thamani zaidi ambao wanakuwa kwa muda mfupi zaidi na akampeleka sokoni na kupata bei nzuri na kama ni ng'ombe wa maziwa basi awe na maziwa ya kutosha na kuwa na ziada ya kusindika lakini na huduma ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili la kufuga kibiashara ni jambo la msingi sana na tunahamasisha watu ambao wanaweza kufanya biashara ya mifugo wafanye. Nimesikia baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia habari ya usumbufu katika biashara ya mifugo wanaposafirisha nje ya nchi. Nirejee kusema kwamba nchi yetu haijazuia kusafirisha au kuuza mifugo nje ya nchi kwa sababu bado usindikaji wetu wa ndani haujafikia kiwango ambacho tunaweza tukatumika rasilimali zote za mifugo hapa nchini. Kwa hiyo, lazima mifugo isafirishwe nje ikiwa hai na masoko yapo makubwa kwenye nchi za kiarabu, Comoro, Kenya na Zambia. Masoko yapo tunachofanya ni kuimarisha minada yetu ya mipakani ili kuhakikisha kwamba mifugo inayosafirishwa inakuwa na vibali rasmi. Vilevile niwahamasisha wafanyabiashara watumie nafasi hiyo kupata leseni halali na vibali vinavyostahili ili wasafirishe na kufanya biashara vizuri. Maana kama unaona nchi inahitaji mifugo ina maana kuna soko na kama kuna soko zuri tulitumie kwa sasa kabla hatujaanza kusindika mifugo yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa habari ya maziwa kusindikwa kwamba viwanda vinafanya kazi chini ya uwezo wake. Ni kweli, vinafanya chini ya uwezo wake kwa sababu bado kuna changamoto kwanza katika ukusanyaji wa maziwa kwa sababu maeneo mengi ya vijijini hayana umeme. Naishukuru na kuipongeza Serikali yetu kwa sababu kupitia mpango huu wa umeme vijijini sasa nishati hii inaweza kupatikana kwa gharama nafuu. Maziwa ni mazao ambayo yanaharika kwa muda mfupi sana, ni chakula ambacho kinapendwa na kila kiumbe hata wadudu waharibifu na wenyewe wanapenda maziwa hayohayo, huwa yanaharibika kwa mufa mfupi sana, sasa katika viwanda ili yasindikwe ni lazima yawe na ubora ule. Kama ni maeneo ya mbali ya vijijini yanahitaji vifaa maalum kwanza vya kuyapooza yakiwa hukohuo halafu baadaye kuyasafirisha mpaka kwenye viwanda. Kwa hiyo, katika mazingira hayo maeneo ambayo yapo mbali na mfumo wa uchukuzi na mfumo wa nishati ya umeme inakuwa siyo rahisi kuyakusanya yote lakini mabadiliko haya ya kuongezeka kwa viwanda ina maana vinasambaa na kufika maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kilichokuwa ni kikwazo, upatikanaji wa malisho unaomfanya ng'ombe atoe maziwa mengi kwa hali ya sasa bado ni ule wa msimu. Wakati wa mvua malisho ni mengi na maziwa yanakuwa mengi lakini wakati wa kiangazi malisho yanakuwa haba kwa hiyo maziwa yanapungua. Sasa kwa mwekezaji kama upatikanaji wa maziwa haupo muda wote inakuwa ni gharama na kwa sababu ni biashara kunakuwa na *cost benefit analysis* lazima aangalie. Kwa sasa tunavyohamasisha katika *modernization* yote hii ya mifugo ni pamoja na upatikanaji wa chakula bora cha mifugo katika maeneo yote. Kwa hiyo,

kama ni maziwa yatapatikana msimu wote wa mwaka itakuwa na tija kwa wenye viwanda kuwekeza na kuona kwamba wanapata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ni changamoto lakini kama Wizara vilevile tunaongeza uzalishaji wa mitamba bora wa maziwa na katika mashamba yetu tunazidi kuyaimairisha kwani tuna *livestock multiplication units* zipo tano katika nchi yote lakini zimegawanyika katika Kanda mbalimbali za nchi yetu lakini tunahamasisha watu binafsi vilevile kuwekeza katika uzalishaji wa mitamba. Mwitikio ni mzuri mmeona katika taarifa yangu watu binafsi sasa hivi wanaweza kuuza mitamba zaidi ya 10,000 kwa mwaka. Hii ni hatua nzuri, mahitaji ya mitamba katika nchi yetu ni takribani 50,000 kwa mwaka, sasa bado kuna pengo lakini sisi Serikali tunaboresha mashamba yetu na kutumia teknolojia ya kisasa kama ya uhaulishaji (*embryo transfer*) inasaidia kuongeza mitamba ya kisasa kwa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa ni vifaa duni vya uvuvi hasa mwambao wa Ziwa Tanganyika na maeneo mengine. Hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, namshukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, niwaarifu kwamba kama mngefuatilia taarifa yangu vizuri mmeona juhudi za makusudi zinazofanywa za kuweka mazingira bora kwa wavuvi wa kawaida ili waweze kubadilika kutoka katika hali ya uduni na kuwa na uwezo mkubwa zaidi. Moja ya hatua ambazo tunachukua kwanza ni kuwawekeza miundombinu, ujenzi wa mialo ambapo wanaweza kuleta mazao yao wanapotoka kuyavua lakini vilevile tunatoa elimu ya namna ya kuyaandaa yale mazao ili yasiharibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya mialo tayari tunaweka vyombo vya kuhifadhiya yaani majokofu ya kuhifadhi samaki pale wanapokuwa wamefikishwa ili hata asipopata soko kwa muda ule aweze kupata soko muda mwingine kwa bei nzuri. Hiyo kazi inaendelea lakini vilevile tuhamasishe na Serikali za Mitaa katika maeneo hayo kuchukulia shughuli hii kama ni shughuli muhimu ya uchumi katika mipango yao waipite kipaumbele kwa sababu siyo Wizara tu itakayowekeza katika hili wadau wake ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tunazidi kuboresha upatikanaji wa vifaa vya uvuvi kwa maana ya boti na nyavu. Kupitia sekta binafsi tunahamasisha upatikanaji wa vifaa hivi na kweli kuna mwitikio mzuri, sasa vifaa hivi vinaendelea kupatikana kwa urahisi zaidi kuliko hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii tumeona ni wadau muhimu sana kwa sababu inaanza kuwashirikisha wavuvi. Sisi tunawaunganisha wavuvi hawa katika vikundi vya ushirika na kupitia ushirika huo wanaweza kupata dhamana ya mikopo. Pia kila mvuvi na familia yake wanaingia kwenye mfumo wa kupata stahili za mafao. Kwa mara ya kwanza, jamii hizi za kawaida tulikuwa tunaongea pensheni ya uzeeni, sasa kupitia Mifuko hii ya Jamii walau tumeshapata mfumo wa kuwa- *engage* wavuvi ili hata wanapozeeka waweze kupata pensheni zao. Vilevile kupitia mfumo huohuo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama nilivyosema, sasa wanaweza kukopesheka kwa namna rahisi zaidi na kupata vifaa vya uvuvi vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali kupitia Benki ya TIB imewawezesha wavuvi. Kumekuwa na mpango maalum wa kuwawezesha mafundi au wataalam wa kutengeneza hii mitumbwi mikubwa au boti za kisasa ambazo zinaweza zikaenda kwenye maji ya kina kirefu ili wavuvi waweze kupata mavuno mengi zaidi tofauti na kutumia vifaa vya kienyeji ambapo hawaendi mbali sana na matokeo yake unakuta maeneo yamezidiwa uwezo kwa sababu ya wingi wa vifaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hili la viwanda vya nyama ambalo kwa namna fulani nimeshaligusa. Kwa upande wa Serikali kumekuwa na juhudi, kwanza, kulikuwa na viwanda hivi vya siku nyingi vya *Tanganyika Parkers*, Waheshimiwa Wabunge wamevizungumzia ambavyo vilibinafsishwa. Kimoja kile cha Shinyanga ambacho kilipata mwekezaji mzawa lakini kutokana na uchakavu ulivyokuwa mkubwa mtaji wake haukuweza kutosheleza, kwa hiyo ikabidi atafute mbia mwingine ambaye sasa ndiyo wanaendelea naye. Tunategemea kwa juhudi ambazo wanaendelea nazo hiki kiwanda kitafufuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kipo kiwanda kile cha Ruvu ambacho kwa kweli hakivutii sana, Waheshimiwa Wabunge wanapopita pale barabarani wanakiona lakini hakiendelei. Hata hivyo, sasa hivi kiko katika hatua nzuri za mchakato huu wa manunuzi kwa sababu ni lazima taratibu zifanyike. Mjenzi wa mwanzo alikuwa na udhaifu wa kiufundi, kwa hiyo, ikabidi mkataba wake usitishwe na sasa mchakato unaendelea, tayari mtaalam mwelekezi amepatikana na nafikiri kazi ya ujenzi inaweza ikaanza wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme tu kwamba, kwa sababu aliyeweka jiwe la msingi katika kiwanda hiki ni Mheshimiwa Rais mwenyewe, kinamgusa sana na angependa akizindue tena kabla hajastaafu. Kwa hiyo, nategemea Waheshimiwa Wabunge tutaona kazi inaendelea pale muda si mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna wawekezaji wengine binafsi ambao wanaendelea kuingia katika nchi yetu. Pale Morogoro kuna *Tendaji Foods*, kuna *Allanasons* ambao wameonesha nia ya kujenga kiwanda kingine pale Ruvu. Pia wako wengine kule Mkuranga, wako *Chobo Investments Mwanza*, pale Iringa Halmashauri na wenyewe wana ubia wake wanajenga kiwanda cha nyama. Kwa hiyo, kuna shughuli zinaendelea sehemu mbalimbali, ninaamini mambo yatabadilika kwa sababu sasa ni juhudi ya makusudi kwenye Wizara kuona kwamba kuna uwekezaji unaingia katika usindikaji wa nyama. Kwa hiyo, tujipe muda, mabadiliko haya mtayaona baada ya muda si mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lilizungumzwa suala la maeneo huru ya magonjwa. Hili lilizungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge. Hii ni fani ambayo kidogo hatujaiona hapa nchini lakini kama itatekelezwa tunaweza kuwa na hakika ya kufanya biashara ya mazao ya mifugo hata kwa nchi ambazo zina sheria ngumu sana ya uingizaji wa mazao ya mifugo. Kwa hiyo, kuna taratibu zake, kuna jinsi ya kukinga kuingia mifugo katika eneo lile ili isiweze kuingiliana na mifugo kutoka nje, kuna taratibu za udhibiti wa magonjwa katika maeneo husika. Eneo hilo likiishatambulika na kuthibitishwa basi manufaa yake ni kwamba mnaweza kuuza kwa soko zuri zaidi tofauti na hii biashara ya sasa hivi ambayo tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi hii inaendelea na tayari Wizara imshatenga fedha kwa ajili ya kuimarisha Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa pale Sumbawanga. Tumeshapata majengo yaliyokuwa ya Wizara hapo zamani lakini baadaye yakachukuliwa na Halmashauri, sasa yamesharejeshwa na kazi ya ukarabati itaanza. Mkipitisha hii bajeti itatusaidia hata kwenda kasi zaidi ili kuhakikisha kwamba mpango huu unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafugaji wazuri sana, niupongeze Mkoa wa Rukwa kwa kazi nzuri ya usimamizi. Nikiri kabisa kwamba nimeona ng'ombe wazuri Rukwa na ningeoomba kuhamasisha Halmashauri za Wilaya katika maeneo mbalimbali ya wafugaji waende Nkasi na Kalambo wakaone ufugaji mzuri wa ng'ombe ambao wana tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezunguzwa hapa kwamba utafiti hauna fedha. Ni kweli, dhamira ile ya Serikali ya kutenga angalau asilimia moja iende katika maeneo ya utafiti, bado haijatekelezwa. Hata hivyo, Wizara haijaka tu, Watafiti wetu wanaandika maandiko mbalimbali kutafuta ufadhili katika taasisi mbalimbali zinazohusiana na mambo ya utafiti na kazi

haijasimama, inaendelea. Kwa upande wa uvuvi, utafiti unafanywa na wenzetu wa TAFIRI na kwa upande wa mifugo kuna miradi ambayo imeshakubalika na mamlaka mbalimbali. Tunafanya kazi na *Bill & Melinda Gates Foundation* ambao wanasaidia katika utafiti hasa uwanda ule wa maziwa Nyanda za Juu Kusini, lakini pia kuna *COSTECH* na maeneo mengine, kwa hiyo, tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa juu ya uzalishaji wa chanjo za mifugo. Hili nimelizungumzia na kwamba tunaendelea kuimarisha *Tanzania Vaccine Institute (TVI)* ili iweze kukidhi mahitaji ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya migogoro ya mifugo na wananchi. Mheshimiwa Kandege ameligusia kidogo kule kwake akasema ni hekta 10 ambazo zina mgogoro. Niliwahi kutembelea kule, bahati mbaya mvua ilikuwa inanyesha sana nikashindwa kuingia ndani kwenye vijiji. Hakuna sababu ya kuwa na ugomvi na Mheshimiwa Kandege kwani tulikuwa pamoja, hata akinisulubu hapa atafurahi lakini ukweli anaufahamu kwamba, nilifika huko, nikaangalia yale mazingira bahati mbaya sikuweza kukutana na wananchi kwa sababu hali ya njia haikuwa nzuri kutokana na mvua ambazo zilikuwa zinanyesha sana na hatuwezi tukamlaumu Mungu kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba maeneo haya ya mashamba ya mifugo au maeneo ya mifugo yaliyokuwa yametengwa na Serikali yalikuwa yamepimwa na ni halali kwani yana hati lakini kwa sababu ya kutosimamia vizuri labda makazi na kupanuka kwa shughuli za wananchi wakati mwingine wanaingia katika maeneo haya ya Serikali, aidha, kwa kufahamu au kutofahamu. Kwa hiyo, ni wajibu wetu wote viongozi kuwaonesha wananchi, kwa sababu kama tutaendelea kukatakata kila eneo, hatimaye hatutakuwa na eneo. Tuna vyo na tunahitaji maeneo ya kufundishia. Chuo cha kilimo au mifugo kinahitaji ardhi ya kufundishia na eneo la kufanyia utafiti, vinginevyo mhitimu wako atakuwa wa nadharia tu, hana mahali pa kufanyia mafunzo kwa vitendo. Hata haya mashamba ya *NARCO* yana wajibu mkubwa kwamba, ni lazima yazalishe kwa ajili ya kuhudumia Wananchi. Kwa hiyo, naomba tu maadam Mheshimiwa amesema nitatuma wataalam wakaone kama kweli hilo eneo linalogombaniwa linahalalisha kuleta chuki kubwa kati ya Serikali na wananchi. Kama ni eneo ambalo haliwezi likabadilisha sana, nafikiri Serikali ni ya wananchi itaangalia namna bora ya kumaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie kuhusu mgogoro wa wanafunzi wa *LITA*. Kilichogombewa hapa na wanafunzi wa *LITA* Morogoro ni kwa sababu hawakufahamu tu, kuna mfumo ambao umebadilishwa sasa hivi wa kutoa vile vyeti kwa *level* ya *certificate* na *diploma*. Sasa hivi tunatumia *NTA Level Four, Level Five, Level Six* na kadhalika na huu ni mfumo wa kimataifa. Vilevile, *NACTE* wameshaidhinisha na unatambulika. Hata Watanzania wanapoenda nchi za nje, anaondoka na *Advanced Diploma* ambayo sisi huku tunasema ni *equivalent* na *degree*, lakini akienda kule anapigwa kwanza shule kwa miezi tisa au mwaka mmoja kisha ndiyo anaingia kuchukua *masters*. Sasa huu ni mfumo mpya na naomba vijana wa Tanzania ambao wako vyo na wana wasiwasi na mfumo huu waondoe mashaka. Serikali ni miongoni mwa waajiri, hivyo haiwezi ikakuwekea mfumo ambao itakunyima ajira. Kwa hiyo, waondoe mashaka wala hakuna sababu ya kuandamana na badala yake wasome ili wapate vyeti vyao ili wasonge mbele na maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda haujaisha kuna suala moja tu ambalo napenda nilizungumzie kuhusu minada hii ya Upili ukiwemo mnada wa Kirumi. Nafahamu kuna biashara kubwa ya usafirishaji wa mifugo kwenda Kenya kupitia mpaka wa Sirari.

Napenda kuwatoa hofu kwamba tayari Wizara imeshapeleka fedha kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sasa na ya haraka ili mnada ule angalau uanze kufanya kazi. Tunataka wafanyabiashara wetu wa mifugo wasipate usumbufu usio wa lazima kwa sababu tutaweka huduma pale. Jana tulikaa na timu ya wataalam wangu tukasema ni lazima tutafute jibu la kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara. Naomba mamlaka za Mkoa wa Mara na Wilaya ya Butiama kwa sababu wao ni Serikali, tushirikiane kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo lililopo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Longido nimtoe hofu Mheshimiwa Kaka yangu kwamba, mnada wa Longido ni ajenda kubwa sana katika Wizara yetu. Ni kutokana na matatizo ya uhaba wa fedha tu, kama tungekuwa tumepata fedha wala Mheshimiwa Mbunge asingelalamika hapa badala yake angekuwa anatupongeza tu. Ni hivyo hivyo kwa minada ya Kasesya ambayo ni ya mpakani, tunapenda yote ifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitandula alizungumzia habari ya bandari ya uvuvi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri malizia.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Basi nimjibu kwamba, pale Mbegani siyo ile bandari ya uvuvi inatakiwa kujengwa pale. Kimsingi pale ni chuo lakini bandari inayojengwa eneo lile ni ile kubwa ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hofu kwamba ingeweza kuingia na kuchukua eneo la chuo lakini Wajumbe wa Kamati wamezungumza vizuri tu kwamba, kile chuo ni maarufu siyo Tanzania tu, kinajulikana dunia nzima. Tunapata wanachuo kutoka sehemu nyingi za Bara la Afrika na nje ya Afrika. Hivyo ni vizuri tukakilinda ili kiendeleo kuleta hadhi na fedha ya kigeni kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo nawashukuru sana. Ndugu yangu Mheshimiwa Marombwa, *shore fishing* ni mpango mzuri na mkubwa ambao utaboresha maisha ya wananchi kwa sababu una *component* ya kuhakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika shughuli hizi za uchumi ukiwemo na ufugaji wa kamba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awaweke wananchi wake katika mkao wa kupokea mradi ule ambao tutauzindua mwezi Julai mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tu kwa heshima na upendo wapitishie hii bajeti kwa sababu ndiyo itakayoweza kuondoa hizi kero nyingi ambazo wamezisema. Ahsante sana na baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 99 – WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

Kif. Administration and HR Mgt.....Tsh.4,859,154,400/=

MWENYEKITI: Watakachangia mshahara wa Waziri ni Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Mfutakamba, kama hauko kwenye orodha hii ya vyama usisimame, ninaowataja ni wale walioko kwenye orodha. Wengine ni Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Ahmed Ali na Mheshimiwa Assumpter. Wale ambao sikuwasoma hawakupitishwa na vyama vyao. Naomba nianze na Mheshimiwa Selasini.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba kabisa, kama hawakuandika ni makosa yao.

MWENYEKITI: Sawa Mheshimiwa, *list* hii hapa ninayo, nitakuongeza kama muda utaruhusu.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Niongeze kabisa.

MWENYEKITI: Sawa.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Huu utaratibu ufutwe. (*Kicheko*)

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nilipeleka jina langu lakini sijalisikia.

MWENYEKITI: Sasa Mwenyekiti siyo niliyeweka huu utaratibu, ni sisi wenyewe ndiyo tulijiweka utaratibu huu. Sasa naomba tukae, nimeshamruhusu Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mimi sina shida na mshahara wa Waziri, lakini naomba tu maelezo kwa sababu mimi ni mmoja kati ya waliokuwa Wajumbe wa Kamati Teule ya Bunge, tuliokuwa tunachunguza migogoro ya wakulima na wafugaji. Katika uchunguzi wetu tuligundua kwamba nchi hii ina sera na sheria nzuri sana lakini tatizo ni utekelezaji. Pia tuligundua kwamba watendaji mbalimbali wa Serikali katika Wilaya zetu ndiyo hasa chanzo cha migogoro ambayo inaendelea kati ya wakulima na wafugaji kwa kutofuata sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Wilaya yangu ya Rombo pamoja na kwamba hakukuwa na aina hii ya migogoro lakini hivi sasa wafugaji kutoka nchi jirani ya Kenya wanaingia katika vijiji vya Ngareni, Ngoyoni na ukanda wa chini wa Wilaya ya Rombo wakilisha mifugo yao katika mashamba ya wananchi. Sina uhakika kama Serikali inajua lakini binafsi nilishakwenda kutembelea eneo hilo na baadhi ya wakulima waliolalamika walikamata mifugo wakaifikisha mpaka Polisi, kufika Polisi wakageuziwa kibao kwamba wao waliiba mifugo ya hao wafugaji. Sasa jambo kama hili ni jambo ambalo linaudhi na naomba Serikali ieleze ni hatua zipi ambazo inawachukulia watendaji kama hawa ambao badala ya kuondoa migogoro wao wanazidi kuikaribisha na kuilea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya Tanzania ni kwa ajili ya Watanzania. Kwa hiyo, hakuna *provision* ya watu kutoka nje kama siyo wawekezaji kuja kulisha mifugo katika ardhi ya Tanzania na kusema wana haki hiyo. Kwa hiyo, watendaji wowote ambao wanaruhusu jambo hili kwa njia zozote zile ni kinyume cha sheria na kinyume utaratibu. Kwa hiyo, nitafuatilia kuona kwamba uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Rombo kama wameliona suala hili ili tujue hatua stahiki za kuchukua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nisiporidhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri nitaomba kutoa shilingi ingawa ameomba tusichukue shilingi yake. Katika mchango wangu kwa maandishi niliainisha kabisa ambacho nakwenda kukiongea. Ni dhahiri kabisa ili tuweze kuwa na ufugaji wenye tija ni lazima tuboreshe miundombinu kwa maana ya malisho, manywesheo na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu au hitaji langu ni kwamba tunatambua kabisa na kwenye Hotuba ya Waziri ameanisha baadhi ya minada katika nchi yetu na hata wakati anajibu ameanisha minada mkakati katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Katika mchango wangu wa maandishi niliainisha mnada wa Magena ambao iko katika Halmashauri ya Mji wa Tarime na pale Magena ni karibu kabisa na mpaka wa Kenya na Waziri wakati anajibu hapa ameanisha Kenya kama soko kubwa sana la mifugo na kwa sasa hivi ule mnada umetelekezwa licha ya kwamba tunaangalia soko la Afrika la Mashariki. Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hapa ameanisha mnada wa Kirumi katika Mkoa wa Mara ambao upo mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ule mnada wa Magena ambao ulikuwa ni mnada wenye kuleta tija na uchumi kwa nchi siyo tu kwa Watanzania lakini hata kwa Halmashauri ya Mji na wakazi wa Tarime ukichukua *concept* nzima ya *multiplier effect* kwamba tungeweza kujenga na maduka pale watu wetu wangeweza kunufaika kwa kuuza vyakula na kadhalika. Ni kwa nini Serikali imeamua kuutelekeza na mbaya zaidi mifugo ambayo inatoka nchi ya jirani na Mikoa mingine inaonyeshwa kabisa inapewa kibali inakwenda kwenye mnada wa Magena wakati haupo kwani umeshatelekezwa, haufanyi kazi badala yake unakuta ng'ombe zinalazwa kwenye barabara ya Kumwamu ili kesho yake iondoke kwenda Kenya na kinyume cha hapo Serikali inakosa mapato, wananufaika baadhi ya watendaji ambao siyo waaminifu na Mapolisi. Nilitaka kujua ni nini mkakati wa Serikali kuuhisha ule mnada na kuufanya uwe mnada wa kisasa kwa sababu ni mnada ambao ungeweza kutoa huduma kwenye soko la Afrika Mashariki. Mnada wa Magena upo Tarime nimeuandika lakini hukunipa jibu ndiyo maana nikasema nisiporidhika nitakamata shilingi, naomba majibu ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuguswa kukubwa kwa Mheshimiwa Mbunge kuhusu mnada wa Magena. Kulikuwa na matatizo kidogo ya kiuendeshaji wakati mnada ule unafanya kazi. Kimsingi ulikuwa ni mnada wa mwanzo (*primary market*) na kwa sheria zetu mnada wa awali haupaswi kuwa ni mnada kwa ajili ya usafirishaji wa mifugo nje ya nchi. Matokeo yake kwa sababu ulikuwa hauna mamlaka hayo, ng'ombe wengi walikuwa wanatoroshwa kwa magendo kwenda nchi jirani bila kufanya hicho kitu kizuri anachopendekeza Mheshimiwa Mbunge cha kulipa mapato Serikalini. Kwa hiyo, Serikali kupitia mamlaka ya Mkoa wa Mara yenyewe iliomba mnada ule ufungwe ili kuwe na udhibiti mzuri wa mifugo inayosafirishwa kwenda Kenya ndiyo kukaja na hilo pendekezo la kuweka mnada wa upili ambao una uhalali wa kusafirisha mifugo nje, ule Mnada wa Kirumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kirumi pako *strategic* kwa maana kwamba njia ya kupitisha mifugo ni moja tu ni lazima apite pale darajani. Kwa hiyo, wakaweka ule mnada pale

kwa sababu inawezesha sasa Serikali kufanya uratibu wa mifugo yote inayosafirishwa. Kwa sababu Wilaya ya Tarime peke yake haina ng'ombe wa kutosha wa kusafirisha kwenda Kenya, ni lazima watoke huku kwenye *catchment* kubwa ya Mikoa ya Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita na maeneo mengine ya jirani kama Tabora. Kwa hiyo, ndiyo maana mamlaka yenyewe wakachagua mnada huo mwingine na kawaida Wizara mara baada ya kuletewa mapendekezo inaenda inakagua eneo hatimaye inajiridhisha na kupanga usiamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mbunge anadhani sasa mnada ule umepata sifa itabidi tu mchakato uanze kwa taratibu zilezile, mamlaka ya Wilaya itengeneze mapendekezo ambapo Mheshimiwa Mbunge ni Diwani, yaletwe Mkoani na hatimaye Wizarani na sisi tutaleta wataalam wetu halafu tuone namna ya kufanya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mnada wa Kirumi Mheshimiwa Waziri anaeleza kwamba kuna njia moja tu labda kwa jiografia ya Mkoa wa Mara, Kirumi ni mojawapo lakini pia hata kama ng'ombe wanatoka sehemu nyingine yoyote nje ya Mkoa wa Mara unaweza kupita njia nyingine nyingi tu. Cha zaidi, kuna mapato tutakuwa tunayapoteza kwa maana baada ya Kirumi tuna Wilaya ya Rorya na wao wanafuga ng'ombe, tuna Wilaya ya Tarime, tuna Wilaya ya Serengeti kama kuna ng'ombe zinazuzwa zikitokea Serengeti haziwezi kupita Kirumi ina maana hapo pia tunapoteza mapato. Kwa hiyo, napendekeza na kama alivyosema, naomba tuwe na nia ya dhati ya kuhuisha ule mnada sasa hivi, pale Magena pafupi sana kufika Kenya na wao ndiyo soko kubwa sana la mifugo. Tufanye Magena ndiyo liwe soko la Kimataifa kwa Afrika ya Mashariki na hilo eneo lipo na limetengwa kubwa tu. Huu udhibiti mwingine unawezekana kwa sababu huwezi kusema kwamba unadhibiti ng'ombe wakiwa Kirumi wakati umeacha eneo kubwa sana na wafugaji wapo, Serengeti wanafuga, Tarime tunafuga na Rorya tunafuga, kwa hiyo, hapo pia mapato yanaweza kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Serikali mlichukue hilo na mlifanyie kazi na nawahakikishia tutapata mapato mengi, kwani sasa hivi mapato mengi sana yanapotea kwa hiyo *system* mliyonayo ya mnada wa Kirumi, mnada wa Kirumi unaweza kuwepo lakini na huu mwingine ukuzwe hadhi na kuwa mnada wa Afrika ya Mashariki pale ni *center*. Naomba nirudishe shilingi yake lakini uniahidi uliyoyasema kwamba unakwenda kuyafanyia kazi.

MWENYEKITI: Shilingi ulikuwa hujachukua, kwa hiyo umetoa ushauri tu. Ulisema unakusudia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Nilisema nitachukua shilingi yangu, nilisema mwanzoni kabisa natoa shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther nasikiliza sana, ulisema unakusudia kutoa shilingi kama hutajibiwa vizuri na bahati nzuri umesema vizuri ili mpate hayo masoko na Mkoa wote wa Mara ufaidike. Muache tu aendelee kutenda kazi, kwa hiyo, shilingi ulikuwa hujatoa, sasa huo ushauri Serikali inauchukua. Tuendeleo, namuita sasa Mheshimiwa Mkiwa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani tuliongelea kuhusiana na jinsi ambavyo tunaishauri kila siku Serikali kupata fedha katika bahari kuu lakini haitaki kuchukua mipango hiyo. Mwaka jana wakati kama huu na kwa Wizara hii tuliyo nayo leo, mimi binafsi nilishauri kwamba kuwepo na bandari ya uvuvi ambapo meli kubwa zinazochukua mali zetu waje bandari ili kuona ni kiasi gani cha samaki ambazo wamevua waweze kulipa mrahaba uweze kuisadia nchi yetu. Mheshimiwa Waziri sikuona

anaongelea suala hilo matokeo yake ameongelea bandari ndogondogo za Rufiji, Mafia na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana walisema wanafanya upembuzi yakinifu na hapa nimesikia bado wanabishana hiyo bandari ijengwe wapi. Sasa najiuliza huo upembuzi yakinifu umekwishafanywa au bado na ni lini sasa Serikali yetu itaweza kupata fedha kupitia Bahari Kuu? Naomba hili Mheshimiwa Waziri anijibu vizuri ili tuweze kujua nchi yetu itaongezaje mapato kinyume cha hivyo nitatoa shilingi, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa kuguswa kwa Dada yangu Mkiwa Kiwanga. Ni kweli na wala hakuna kubishana kuhusiana na umuhimu wa bandari ya uvuvi, ni kitu kiko dhahiri kwani manufaa yake kwa Taifa letu ni makubwa sana. Labda hakuzingatia wakati natoa hotuba yangu, kwanza, mwaka jana mlitupitishia shilingi milioni 300 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu lakini vilevile tunayo Sheria ya Manunuzi inayotuongoza hakuna njia ya mkato. Kilichofanyika kwanza ni kupata Mtaalam Mwelekezi ambaye atafanya tathmini na kuona ni eneo lipi sahihi na muafaka la kujenga hiyo bandari. Mimi kwa matashi yangu ya kisiasa naweza kupendekeza popote lakini hii ni taaluma, ujenzi wa bandari ni sayansi, huwezi ukaenda kwa hisia, kuna mambo mengi yanaangaliwa katika ubora wa bandari, sasa tuache wataalam wafanye kazi yao Mheshimiwa tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Wizarani kati ya jambo linalotukera ni pamoja na kutokuwa na hiyo bandari. Tilituma timu kwenda nchi za nje kujifunza na kuona ni jinsi gani bandari za uvuvi zinavyofanya kazi, watu wameenda Korea, Ufaransa na huko Ufaransa na mimi nilienda nikashuhudia bandari ya uvuvi ya wenzetu inavyofanya kazi, ina manufaa makubwa sana lakini sasa hatuna njia ya mkato tuache wataalam watushauri hatimaye tutafanya. Wala hakuna kubabaika kwamba litajengwa eneo gani wataalam watatuongoza tu, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkiwa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema kwamba tunawasubiri wataalam sasa yapata ni mwaka mzima na tunaendelea kupoteza mapato, mnaumwa sawa lakini bado tunaendelea kupoteza mapato ya nchi hii au labda kuna kitu ambacho kiko nyuma ya pazia ambacho sisi Wabunge hatukifahamu? Hizi meli ni za akina nani kwa sababu ni mwaka mzima, kama tungekuwa na nia ya dhati tungekuwa tumeshalishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kamani anasema kwamba anakwenda kulishughulikia, ili nisitoe hiyo shilingi litachukua muda gani, kwa sababu sasa ni mwaka, ili libaki kwenye historia watakaokuja pia watakuja kuliulizia, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zote zitafuatwa na kwa muda stahiki na asiwe na hofu. Hili la meli nyingine labda ni taarifa anataka kunipatia kwamba labda kuna wawekezaji wengine wanaotuhusu huko, mimi sikuwa na taarifa hiyo, lakini hawawezi kutuzuia hata kama kuna wawekezaji wa Tanzania ambao wanamiliki hizo meli bado wangekuwa na manufaa zaidi kama kungekuwa na hii bandari ya uvuvi. Kwa hiyo, sidhani kama vingekinzana

kwa namna yoyote ile. Zile bandari ndogo ndogo alizosema siyo bandari ni mialo tu ya kupokelea samaki. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani na Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kilufi.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza swali la Mheshimiwa Waziri. Katika maelezo yangu nilionyesha na kutia mashaka juu ya wafugaji wanavyopata taabu kwenye maeneo ya mipaka kwa kutozwa faini bila mpangilio na hasa maeneo ambayo mpaka haujawekwa ikiwemo Wilaya ya Mbarari. Kwa sababu wanaotendewa vibaya ni wafugaji nilitaka kuona yeye anashirikiana vipi na Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo imeonyesha nia ya kuja kurekebisha mgogoro ule wa mpaka pamoja na Mheshimiwa Rais nimshukuru sana pamoja na Waziri Mkuu. Sasa nilitaka kujua mgogoro huu wa wafugaji ambao ni wa muda mrefu anashirikiana vipi na Wizara kuona jambo hili linaisha mapema ili wafugaji ambao yeye anawaongoza waweze kuepukana na taabu hii ya kutozwa faini bila ya mpangilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nilizungumzia suala la maeneo ya NARCO ambayo Serikali imewapa watu binafsi ambayo wanawatoza faini wafugaji...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kilufi, unatoa hoja moja tu na siyo mbili, umeshasema ya kwanza na ya pili, unatakiwa kuzungumzia hoja moja.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, kwa sababu hoja zangu zote hazikujibiwa ndiyo maana nimezungumza na hiyo nyingine lakini nashukuru kwa maelekezo yako.

MWENYEKITI: Kanuni inakataa.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Nashukuru kwa maelekezo yako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kuhusiana na suala la Mheshimiwa Kilufi kumwambia tu kwamba Wizara yetu ina nia thabiti ya kuhakikisha kwamba migogoro ya wafugaji inakwisha ndiyo maana tumekuwa tukichukua hatua. Kama nilivyoieleza wakati nafanya majumuisho hapa kwenye Hotuba yangu, tulikuwa na Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwenye mkutano uliowakilisha wafugaji wa nchi nzima kuyajadili na kuyapatia majawabu mambo mbalimbali ambayo yanawakera. Kwa hiyo, pamoja na hilo, mimi mwenyewe pamoja na Wizara yangu kwa ujumla tuko tayari kuwianisha ratiba zetu na wenzetu wa Maliasili na Utalii ili kuhakikisha mgogoro au mpaka ule unamalizwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi tuko pamoja kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaishi kwa amani kwa sababu unawatetea sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kilufi.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wananchi wa Mbarali na hususani wafugaji wanamsikia, je, yuko tayari kuja kuona matatizo haya ambayo nayazungumzia kwa kukutana na wafugaji wale walau akaona kilio chao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri uko tayari kwenda, kubali yaishe.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa ningependa kufika Mbarali, nafurahi sana na niko tayari. (Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kandege.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ametoa kuhusiana na suala zima la migogoro baina ya ranchi za Taifa na vijiji vinavyozunguka ranchi hizo na katika maelezo ambayo ametoa alipata fursa ya kutembelea ranchi ya Kalambo na amekiri kwa bahati mbaya hali ya mvua ilizuia yeye kwenda kufanya kazi aliyokuwa amekusudia na amesema ana mpango wa kutuma watumishi wakafanye kazi hiyo ambayo yeye mwenyewe alishindwa kuifanya. Naomba kusikia kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, mimi niko tayari kumpunguzia kazi hiyo ya kuwaita wananchi wa kutoka vijiji vya Katapulo ili aje apate usahihi juu ya jambo hili kulikoni yeye kuwatuma hawa ambao nina uhakika saa nyingine wanaweza kupotosha. Naomba *commitment* yake.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Wizara yetu pamoja na kwamba tunazo za ofisini na kwenye maabara lakini sehemu kubwa ni kazi za *field*. Ningependa watu wangu wafike kule, waone na kujiridhisha kwa sababu kuona ni kusadiki. Kwa hiyo, nafikiri tusiwasumbue wakulima, namhakikishia Mheshimiwa Kandege kwamba tutafika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lwanji.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa kusema na maandishi nilizungumzia suala la iliyokuwa ranchi ya *Tanganyika Parkers*, Tarafa ya Itigi, Wilaya ya Manyoni. Nilipenda kujua kutoka kwa mtoa hoja kwamba Serikali itaachia lini ranchi hiyo kwa sababu ni karibu miaka ishirini na tano, thelathini wameshindwa kuiiza. Sasa eneo lile halitumiki kwa wananchi kwa kisingizio kwamba eneo hilo ni mali ya Serikali. Miundombinu yake yote imekufa, wawekezaji wamekuja mara nyingi pale wameshindwa ku-*bid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani itakuwa si halali kuendelea kulihodhi eneo lile wakati watu wana shida ya maeneo ya kufugia na kulima. Tunasumbuliwa sana na wananchi hata imetokea vijiji kwa vijiji vinaanza kugombania maeneo hayo ambayo hayaruhusiwi na Serikali kufanya shughuli za maendeleo. Napenda kujua kama wana mpango wowote wa kuweza kuliachia hilo eneo ili liweze kugawiwa wananchi waweze kufanya shughuli za maendeleo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Kitaraka lilikuwa linatumwa na NARCO ni *holding ground*, maana yake ni eneo ambalo mifugo waaosafirishwa wanapumzishwa ili wasipoteze sifa na ubora kwa sababu wanakusudiwa kwenda kuchinjwa au kwenye minada. Kwa hiyo, baada ya *Tanganyika Parkers* kutofanikiwa na kubadilishwa, Serikali iliyachukua yale maeneo na sasa yamerudishwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napozungumzia *modernization* ya mifugo, ni pamoja na kuboresha na kuhuisha biashara yote ya mifugo. Kwa hiyo, kwanza tumeshaanza kuyatambua maeneo yote ya namna hiyo pamoja na Kitaraka ili tuone sasa ambavyo tutayaendelea na kuboresha biashara ya mifugo katika nchi hii. Nina hakika hata wananchi wa Mkoa wake watanufaika pale Serikali itakapoanza kuyatumia haya maeneo kwa uhalisia wake kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge awatulize wananchi tuyalinde haya maeneo ya Serikali. Mikoa mbalimbali wamejitolea maeneo kwa ajili ya ufanisi wa shughuli za Kitaifa kama nchi, sio kama eneo, tufanye kazi kama Taifa. Kwa hiyo, naomba waendeleo na heshima hiyo na imani ya kulilinda hilo eneo ili lije kuwa la manufaa kwa wananchi wa eneo hilo na Taifa kwa ujumla.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lwanji.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshukuru sana kama majibu hayo angewaeleza wananchi wa Kitaraka yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwa sababu hawaelewi. Katika hali ya ufinyu wa bajeti tuliyonayo na hali halisi ilivyo kuendeleza eneo lile itakuwa ni ndoto. Kweli ilikuwa ni *holding ground* lakini ilitumika zaidi kama *ranch* pia kwa sababu mifugo yote ya Kanda ya Ziwa na Magharibi ilikuwa wanachunga pale, wanatunzwa pale, wanalishwa wakishanenea ndiyo wanasafirishwa kupelekwa Kawe Dar es Salaam kwa ajili ya machinjio.

Sasa wananchi wamekaa miaka mingi na wao wana mifugo yao wangependa kufanya shughuli kama hizo lakini hakuna kinachofanyika. Kila siku ni *vandalism* vitu vimeibiwa, hakuna miundombinu yoyote kusema kwamba wanaweza kuja kuhuisha eneo lile, sisi inatuwia vigumu sana kuwaeleza wananchi. Kwa hiyo, kama alivyoomba Mheshimiwa Kilufi Waziri aje awaeleze yeye mwenyewe ili atupe ahueni sisi na hasa kwa kipindi hiki, tutashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri upo tayari kwenda kueleza wewe mwenyewe ukishirikiana na Mbunge?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, itabidi tutekeleze tu hilo jukumu kwa manufaa ya Taifa letu, kwa hiyo, tutakuja. Vilevile nitashirikisha mamlaka nyingine ambayo ni Msajili wa Hazina kwa sababu wakati wa ubinafsishaji Msajili wa Hazina ndiye alipewa jukumu lile wakati ikiwa *CHC* halafu baadaye Msajili wa Hazina lakini sasa Wizara tupo pamoja na tutakuja kutoa maelezo hayo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mhandisi Mfutakamba.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimesisitiza suala zima la utatuzi wa kero hizi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuanzisha *agency* ya mifugo, uvuvi pamoja na miundombinu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linalokuja ni kwamba dawa za ruzuku hazipatikani. Mheshimiwa Waziri atueleze hii *Bajuta International*, wafugaji wote wa Wilaya ya Uyui hizi dawa za ruzuku hata tone moja halipatikani na fedha nyingi zimetolewa karibu shilingi bilioni sita hela za Kitanzania. Sasa hizi dawa za ruzuku zinakwenda wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kawaida hizi dawa za ruzuku zina utaratibu wake wa jinsi zinavyogawiwa. Halmashauri za Wilaya zinahusika sana kubaini ni maeneo yapi yapate hizo dawa za ruzuku. Sioni kama ni sahihi hapa kuzungumzia *Bajuta International* kwa sababu nafahamu ni kampuni nyingi ambazo huwa zinapewa hizo fursa za kusambaza hayo madawa. Kwa sababu sina takwimu hapa kama

Bajuta International ndiyo walisambaza dawa katika eneo hilo analolizungumzia Mheshimiwa Mfutakamba lakini tutaangalia kama kweli dawa hazijafika basi tuone hatua stahili zinazostahili kuchukuliwa kwa sababu ni haki ya wananchi wa Jimbo lake. Kwa hiyo, tutafuatilia Mheshimiwa kuona dawa hizo kama hazikufika, kwa nini hazikufika, nani awajibike lakini tuangalie kwa siku zijazo kuhakikisha kwamba dawa zinafika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Betty Machangu.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeongelea kuhusu viwanda vya ngozi vya Moshi, *Himo Tanneries* na kiwanda kilichopo Moshi Mjini. Nikasema kwa mfano kiwanda cha ngozi cha Himo kinafanya *semi processing* lakini *process* zingine zote zinafanyika Nairobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuendeleza Taifa hili kutategemea sana Serikali itakavyokuwa imeshirikisha sekta binafsi. Hawa ni sekta binafsi ambao wanajaribu kujiendeleza lakini inafika mahali wanakosa dawa za kuweza ku-*process* ngozi kiasi ambacho ni lazima ngozi iende Nairobi kwa ajili ya hatua za mwisho. Ni lini Serikali itasaidia viwanda hivi viweze kujikwamua na kuleta ajira nyumbani na kuweza kufanya hizo *process* zote hapa Tanzania?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Machangu ni ya msingi sana na mimi naungana naye kwa sababu ni muhimu sana tukajitosheleza katika usindikaji wa haya mazao ya mifugo, kilimo hapa nchini na madawa yanayohitajika ni moja ya nyanzo muhimu. Bahati mbaya sana wakati tunapopitisha hapa, wakati ule wa Muswada ule wa wa Kodi hatuangalii kwa makini baadhi ya maeneo ambayo yanakuja kutugusa na kutuathiri katika uendelezaji wa sekta hizi muhimu za wananchi wa kawaida kwa sababu wazo kuu ni kuleta nafuu kuwezesha viwanda hivi viweze kufanya usindikaji mkubwa na vikue. Mimi kiwanda cha Himo nimekitembelea, nimeona wanavyojibidisha na wakaeleza baadhi ya vikwazo vyao ni pamoja na hicho alichokisema kwa sababu madawa yanawekewa kodi kumbe yangeweza kuondolewa baadhi ya ushuru ili yawe nafuu na kuvutia usindikaji wa ngozi hapa nchini. Kwa hiyo, nafikiri tusebiri ule muda muafaka wa kuangalia mahitaji muhimu kama madawa ya viwanda vya ngozi tuweze kuyapunguzia kodi ili waweze kuyaingiza kwa gharama nafuu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhwani Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata nafasi ya kusema neno hapa. Sikusudii kukamata shilingi ya Mheshimiwa Mawaziri ila nitafurahi sana kama atanisaidia ufafanuzi katika zile hoja alizokuwa anajibu ili watu wa Chalinze nao wapate kujisikia raha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na jambo niliomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri kutokana na huu mvutano ulioibuka baina ya wafugaji wangu pale Chalinze na maeneo mengine ya Kibaha Vijijini na watu wa ranchi ya Ruvu. Kwa kipindi kirefu sana pale kumekuwa na utaratibu ambao mimi binafsi kama Mwanasheria siridhiki nao hasa pale wanapokamata mifugo, wanaamua wenyewe juu ya *percentage* wanayoitaka lakini pia hata wale ambao mifugo yao imekamatwa hawapewi nafasi ya kusikilizwa. Wakati mwingine lazima tufahamu kwamba ng'ombe hawana akili nzuri, unaweza ukawazuia wakaingia katika ranchi za watu ikawa tabu, ni vyema tukapeana nafasi hata ya kusikilizana ndiyo utaratibu wa kisheria ili haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo hilo nilikuomba maelezo pia juu ya ule mgogoro uliopo katika eneo la Selous kule Rufiji.

MWENYEKITI: Ni hoja moja tu Mheshimiwa.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hoja ambazo zipo sawa kwa sababu zote ni migogoro inayotokea baina ya wafugaji na maeneo ya hifadhi kwa maana ya maeneo ambayo yametendwa kwa sababu maalum. Kwa sababu kule Rufiji imetokea kitendo kibaya kwamba hata ng'ombe tumeambiwa kwamba wamepigwa risasi, watu wanatumia nafasi hiyo kutumia ng'ombe kama sehemu ya kulengea shabaha si jambo jema lakini pia yapo malalamiko kwamba baadhi ya wachungaji wamepotea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa hoja ni moja.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni utaratibu gani mzuri wanauweka kama Wizara ili kuhakikisha kwamba haki ya wachungaji na mifugo inapatikana kabla watu hawajachukua hatua nyingine ambazo hazifurahishi wananchi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpe pole kwa wafugaji wake kuuliwa ng'ombe kule Selous lakini niseme tu kwamba hilo eneo halipo kwenye mamlaka ya Wizara yangu. Hata hivyo, kwa manufaa ya wananchi wa Jimbo lake ni kwamba kwanza sio sahihi lakini Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alishalitolea maelezo suala hili wakati tulipokutana na wawakilishi wa wafugaji kama wiki mbili, tatu zilizopita na kwamba wameshachukua hatua kwa wale watu waliofanya kitendo hicho kwa sababu kwanza ni kinyume cha Sheria ya Haki ya Wanyama lakini vilevile ni aina fulani ya unyama kwa sababu huwezi ukauwa mnyama wa kufugwa ambaye hawindwi. Kama unataka kuua mnyama wa kufugwa kuna namna yake, wanasema *humane killing* ambayo ndiyo inatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa huu mgogoro wa wafugaji na eneo la ranchi ya Ruvu, kwanza ieleweke kuingiza mifugo katika eneo la ranchi siyo sahihi lakini kama walivyosema kwamba mifugo haina akili nzuri inaweza ikatokea ikaingia, kwa sababu nililetewa malalamiko haya na wawakilishi wa wafugaji kule nimefuatilia kuona ni nini hasa kilichofanyika. Nimebaina kuna kukosana kwa mawasiliano ambapo hakukuwa kuzuri sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hali hii haitajitokeza tena kwa siku zijazo lakini pande zote tuheshimiane, NARCO inahitaji wafugaji wa jirani kwa maana ya kwamba tunapojenga viwanda pale tunahitaji *out-growers*, wafugaji wazuri ambao wataleta mifugo ili iweze kusindikwa. Vilevile maeneo haya ni vizuri tukayalinda, tukayatunza ili kuhakikisha kwamba kampuni yetu ya Taifa inafanya kazi vizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani!

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa mujibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nilikuwa nataka tu nitoe angalizo moja. Mheshimiwa Waziri mimi ndiyo mwakilishi wa watu wa Chalinze, unapokutana na wafugaji wangu ni muhimu na mimi ukanishirikisha kwa sababu mambo haya ni lazima niyatolee majibu. Ni aibu sana leo hii mimi Mheshimiwa Mbunge nakuja hapa nauliza jambo ambalo ofisi yako imeshalifanyia kazi, si jambo zuri. Mimi binafsi sijaridhika na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ni juu suala la haki. Haki hizi za wanyama kama nilivyosema kwamba wanyama hawa hatuwataji kama watu ambao wana akili ya kufikiria kama sisi. Hata kama wameingia kwa makusudi, hata kama wameingia kwa bahati mbaya lakini utaratibu mzuri lazima uwekwe ambao unafanana na utaratibu wa kisheria ili kutoa haki kwa sababu siyo wakati wote wataingia wenyewe. Wakati mwingine kweli watu watawachunga kwa makusudi wawaingize kwenye ranchi lakini wakati mwingine wanaweza wakaingia kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wizara yako ikiwa kama ndiyo wasimamizi wakuu wa haki za wanyama na wachungaji wao, wakaliangalia suala hili vizuri ili kuhakikisha haki inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Anayefuata ni Mheshimiwa Ahmed.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Sina tatizo na Mheshimiwa Ndugu yangu Kamani lakini kwa majibu yake kuhusu huu mgogoro wa wafugaji na wakulima amejibu vizuri lakini kwa uwepesi kidogo siyo kwa uzito wake kama tatizo lenyewe lilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tatizo hili linaanzia kuhama kwa wafugaji kwenye maeneo yao ya asili walikotoka. Mikoa ambayo wafugaji wanatoka yanajulikana, Shinyanga, Mwanza, Manyara hata kwa Ndugu yangu pale Mbarali na sehemu nyingine, wanahama wanakuja kwenye maeneo ambayo tayari kuna malisho na maji mengi kwa ajili ya mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba Waziri Mkuu na Serikali tayari pale Mvomero wameshaanza mikakati ya kutatua migogoro hiyo, naipongeza sana, ni juhudi nzuri. Wasiwasi wangu ni kwamba mtakapokuwa mnatatua tatizo hili kwenye maeneo yenye migogoro, ni sahihi kabisa, Kiteto, Mvomero na maeneo mengine, wafugaji wanaweza wakatoka tena kule wakahamia kwingine wakiona kule kuna maeneo mazuri kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri, wakati mnaendelea na utatuzi huu, kwa sababu sasa hivi hali imetulia lakini muda wowote mgogoro unaweza ukabuka tena, mkafanya yote kwa pamoja kwamba maeneo ambayo yana migogoro mkatatua na maeneo ambayo wafugaji hao wanatoka kwa mfano Mkoa wa Shinyanga, Jimbo langu la Solwa, Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine ili sasa mkapunguza hili wimbi la wafugaji kutoka kwenye maeneo yao kuja Mvomero na maeneo mengine ambayo kuna maji na malisho kwa ajili yao. Nataka ufafanuzi na nimuombe Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba mikakati hii iende sambamba kwenye maeneo ambayo yana migogoro na kwenye maeneo ambayo wafugaji watoka ili sasa kupunguza wimbi kubwa la wafugaji kuhamia maeneo mengine. Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ushauri aliutoa Mheshimiwa Ahmed. Ni kweli kwamba bila ya kupeleka maarifa na huduma hii kwenye maeneo ambako ndiyo chanzo cha mifugo tutakuwa hatujatoa jibu la uhakika la matatizo haya. Kwa hiyo, hiyo itazingatiwa lakini nimuombe wakati wa kupitisha bajeti, tuiptishe tu kwa sababu ndiyo itakayotuwzesha kufanya haya yote ambayo anayatamani Mheshimiwa Mbunge. Mimi nilipoenda ziara kule Rukwa, nilikuta wananchi kutoka Jimboni kwangu wamehama kwa sababu hii ambayo naizungumza lakini wangependa sana wawe na amani hukohuko waliko. Kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge tupitisha bajeti hii ili watendaji wakafanye kazi na kusaidia kupunguza migogoro hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahmed.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kamani, bajeti tunaipitisha wala haina wasiwasi, naomba tu mikakati hii kama akiweza kuniambia ni lini anaweza kuianza ili na sisi tukienda kwenye Majimbo yetu kule tuwaambie kabisa wafugaji msiwe na wasiwasi, muarobaini unakuja, Mheshimiwa Kamani Waziri wa Mifugo anakuja na matatizo haya yamefika mwisho wake. Ahsante.

MWENYEKITI: Amesema matatizo haya kwa sababu yalianza muda mrefu, kwa hiyo utatuzi wake utakuwa wa muda mfupi na muda mrefu. Mheshimiwa Lekule Laizer.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niombe ufafanuzi wa jambo ambalo nimezungumzia kwenye hotuba yangu. Kwanza Waziri alisema kwamba wametenga bajeti kwa ajili ya mnada wa Longido jambo ambalo nilisema isije kuwa ni danganya toto kama bajeti zilizopita kwamba kila siku inawekwa lakini haitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ambao nauhitaji sana ni huu kwamba ni utaratibu gani ambao wafanyabiashara wa mifugo wamewekewa ili nao washiriki katika soko hili la Afrika Mashariki ambalo halionekani wazi kwamba mfugaji anaweza kupeleka ng'ombe Kenya na kwenda kuuza, wanapita tu njia za panya bila kuwa na utaratibu. Hata leseni Mheshimiwa Waziri unayoisema hakuna utaratibu waliowekewa wafugaji kupata leseni za biashara ya mifugo. Nashangaa sana biashara zingine zina leseni, biashara zingine zinapitishwa mpakani kwa utaratibu kabisa unaoelewewa lakini mifugo hakuna utaratibu unaoelewewa. Ukipeleka ng'ombe pale Namanga hakuna utaratibu unaozewesha kupitisha ng'ombe mpakani kama bidhaa zingine. Nataka Mheshimiwa Waziri atueleze utaratibu kama upo na kama haupo atatuambie wafanyabiashara wa Tanzania ambao wanafanya biashara ya mifugo, awaeleze ni njia gani watumie kwenda kuuza mifugo katika nchi jirani ambayo wanaitegemea kwa ajili ya masoko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo ambayo kwa kweli mimi yalinigusa nilivyoingia Wizara hii ni pamoja na matatizo ya usafirishaji wa mifugo kwenda nje ya nchi kwa njia hii ya panya. Kwa sababu madhara yake licha ya Serikali kupoteza mapato, wafugaji wanadhulumiwa sana kwa sababu anampa mtu mwingine halafu akifika kule yule mtu anapotea na wale ng'ombe kwa hiyo anakuwa amepoteza ambapo ni hasara kubwa. Wale ng'ombe wanaopelekwa kwenye mnada wanakuwa ni wale ng'ombe wazuri kwa hiyo inaumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa manufaa ya Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wengine wote wanaotaka kufanya biashara ya mifugo hai kwenda nchi yoyote. Kwanza, huwa kuna leseni ya biashara ambayo ni kwa biashara ya Kimataifa. Biashara ya ndani ya nchi leseni hii inaweza ikapatikana tu kwenye Halmashauri, Wilaya, Mkoa haina shida lakini kama ni kusafirisha nje ya nchi basi leseni hizi hutolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara ambapo vilevile mfanyabiashara atafanyiwa yale makadirio ya kawaida tu ya mapato na TRA ambapo ni jambo la kawaida kwa mfanyabiashara yeyote. Pia huwa kuna *movement permit*, baada ya kuwa sasa ameshapata hiyo leseni yake anachukua *movement permit* kwa idadi ya mifugo ile ambayo anasafirisha, utaratibu upo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo, hata mimi sihamasishi biashara ya pembeni kwa sababu haina tija, ni *risk* kwa mfanyabiashara, ni vizuri kufanya biashara halali. Nizitake ofisi zetu zinazotoa *movement permit* ambapo ni Idara ya Tiba ya Mifugo wanapaswa kuhakikisha kwamba mifugo inayosafirishwa iko salama haina magonjwa, ndiyo umuhimu wa hiyo *movement permit*. Vilevile niitake Wizara ya Viwanda na Biashara ambao ndiyo inatoa hizi leseni basi wawe wanafanya urahisi ili wafanyabiashara wasiwe wanahangaika na kudhani ni kitu kigumu sana kisichowezekana, ni kitu kinachoweza kufanywa na Mtanzania yeyote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nisaidie kuwaelewesha wafanyabiashara. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lekule.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema jambo ambalo halipo, wala unaponiambia nisaidie, nisaidie kwa jambo ambalo halieleweki? Ukienda Halmashauri yoyote hawana kibali cha kukupa kupeleka ng'ombe Kenya, hata ukienda Wizarani hakuna. Tumejaribu sana jambo hili na ni kwamba Serikali haikuweka utaratibu wowote wa mifugo kwenda nje. Kwa hiyo, naomba kama haupo basi mtuwekee utaratibu huo au muwaruhusu tu wafanyabiashara wapeleke kama wanavyopeleka lakini tutaona kwamba sisi wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo hatujawekewa njia sahihi ya kuingia katika soko hili la Afrika Mashariki. Ukisema kwamba eti mfanyabiashara aende Dar es Salaam na aende Wizara nyingine ni jambo ambalo kwa kweli hukutoa majibu sahihi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu labda ya muda na kwa sababu suala hili ni mtambuka, nimuombe Mheshimiwa Mbunge atupe muda ili Wizara yangu ikutane na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kutoa maelekezo ambayo yatakuwa waziwazi katika vyombo vya habari au kwa namna yoyote ile ili kuwarahisishia wananchi kupata hivi vibali. Kama imeonekana kama alivyoeleza kwamba kweli wafanyabiashara wanahangaika na mimi nisingependa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi isingependa wananchi wake wahangaika katika kufanya shughuli halali katika nchi hii. Kwa hiyo, tuwatafutie majibu ambayo ni rahisi, mepesi ili waweze kupata mahitaji hayo ya leseni na vibali vingine vinavyostahili kwa ajili ya kufanya biashara hiyo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyopewa kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), naongeza muda wa nusu saa ili Kamati ya Matumizi imalize kazi yake. Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja. Naanza kabisa kumwambia naondoa shilingi kama sitapata majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tano nipo katika Bunge hili na nimeuliza swali hili zaidi ya mara saba kama ukienda kwenye *Hansard* utaona kuhusu matatizo vitalu ambayo yanasumbua katika Taifa zima hasa katika Wilaya ya Misenyi. Kuna Kamati Teule tano tangu nimekuwa Mbunge na mmojawapo nilikuwemo mimi, tulienda na tukafikia muafaka tukaleta katika Bunge lakini hakuna utekelezaji uliotokea. Kuna taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro baina ya wakulima na wafugaji na wawekezaji, hivi tunavyoongea bado naona hakuna majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huko kwetu katika ranchi ya Misenyi, ranchi yetu ina hekta 23,998 lakini katika hiyo ranchi tuna ng'ombe 2000 tu. Hapo hapo wananchi ambao wamenyang'anywa sehemu zao, tunazo *block* mbili, Kitalu Na. 3 na Kitalu Na.7. Hiki kitalu

nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri na kwenye maandishi nimesema hajanijibu. Sasa nilikuwa nataka kusema hivi, katika hicho Kitalu Na.7 ambacho kimechukuliwa na JKT na wanaondoa wananchi huku wakitaka kuwalipa fidia, kwa nini katika hizi hekta 23,000 zisikatwe, JKT ikachukua kule halafu wananchi wakabaki kwenye maeneo yao wakawa na amani. Hata Kitalu Na. 3 wamechukua eneo lote la maji wananchi hawana pa kuchota maji, wanyama hawana mahali pa kwenda kunywa maji. Ningependa kusikia jibu moja tu hasa la Kitalu Na.7, JKT waache kuwapiga viboko watu wetu, waache kuwakosha amani wana wa Misenyi. Nataka nielewe, je, wataacha kufanya hivyo mpaka muwatafutie eneo lingine? Naomba jibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpe pole Mheshimiwa Mshama kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuweka mazingira sahihi ya wananchi wake kufanya shughuli jirani na maeneo haya ya vitalu vya ranchi ya Taifa ya Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikutana na Mheshimiwa Mshama kama alivyosema lakini yeye ni mzoefu katika utumishi wa umma, mambo ya kisheria huwezi ukayatolea matamko tu bila kufuata kanuni. Hivi vitalu vimetolewa kisheria kwa wamiliki mbalimbali ambao wapo pale, nikitoa tu tamko hivi kesho nitakuwa Mahakamani kwa sababu sikuzingatia sheria. Mgawanyo huu ulitolewa na Waraka wa Baraza la Mawaziri, Na. 2 wa mwaka 2002. Sasa ili kubadilisha maamuzi hayo ni lazima mchakato uleule upite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshaipokea hoja ya Mheshimiwa Mshama, tulishakaa, barua nimeipata na mimi mwenyewe kwanza nilikuwa mmoja wa Wajumbe kwenye Kamati ya Bunge ambayo ilienda kule, naifahamu hii shida. Kama maagizo ya Waziri Mkuu kwamba tuangalie maeneo ambayo uwekezaji kwanza hauko sawa ili yabadilishwe matumizi yake, tumeshafanya tathmini lakini ni lazima utaratibu uleule ufuatwe, Mheshimiwa Mbunge naomba uvumilie tu. Utaratibu ni uleule, tayari sisi Wizara tumeshaandika Waraka wetu kwenda Baraza la Mawaziri tunasubiri Mheshimiwa Rais chini ya Uenyekiti wake aone namna sahihi ya kupata usuluhishi wa suala hili nay eye anaguswa. Niwatoe hofu wananchi kwamba Serikali imeshachukua kilio ambacho kimewasilishwa na Mheshimiwa Mshama nyakati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tu labda suala la kupiga viboko hili ni la kiutu na ni haki za binadamu, nashauri haki za binadamu zizingatiwe tu kama kweli hilo lipo. Vinginevyo kwa upande wa Wizara yangu sisi tumeshatekeleza wajibu wetu, tunasubiri tu zile taratibu za kawaida ambazo ni za kiuendeshaji na za utawala bora kwamba huwezi ukajiamulia, vinginevyo kama mtu mmoja mmoja tu atakuwa anaamua baada ya muda sasa nchi itakuwa kila mmoja anatoa maagizo tu. Kwa hiyo, tunafuata tu utawala bora Mheshimiwa Mbunge, awe na imani Serikali ya Chama chako hiki hiki itatimiza wajibu wake na wananchi wa Misenyi wasiwe na hofu kwa sababu Mbunge anafanya kazi yake, kilio chao kimeshafika na Waziri nimekisikia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mshama, mrudishie tu hiyo shilingi usiichukue.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijairudisha atanijibu nalomuuliza sasa hivi bado sijamrudishia shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri ameongea kitu hapa. Nimeingia humu ni miaka mitano, kabla sijaja hapa suala hilo lilikuwepo na matokeo yake ni kwamba kama kutatua tatizo la watu inachukua miaka mitano na kwa suala la Kakunyu ni zaidi ya miaka kumi, sasa leo tumepata suluhisho ambalo lililetwa na ile Kamati Teule ya mwisho, hii ni ya tano.

Mimi nilichokuwa naomba tu Mheshimiwa, nilichomtajia cha msingi na kikubwa kuliko vyote ni kile Kitalu Na.7. Tunaelekea kwenye uchaguzi, watu nimeenda nimewasomea hii, niliamini kabisa hili ni tamko la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe Waziri kwa kuwa hapa hakuna suluhisho na yule aliyeingia JKT hajapata kibali cha kuwa chini ya mamlaka yake, wote tusebiri, JKT isubiri na wananchi wakae kwenye nafasi zao, kama mkiwalipa waondoke, kama hamtawalipa waachie nafasi na muwapeleke JKT kwenye nafasi zingine, sisi tuna eneo la kutosha Misenyi. Kama nilivyoieleza hekta 23,999 ni nyingi kwa ng'ombe 2000. Kwa nini tusiamue angalau kwenye maeneo ya makazi ya watu ili wananchi wakae kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka hilo tu kwa sababu hapa kuna tamko la Bunge na tayari kuna ambalo anasema wamepeleka kisheria, sasa wale ni sisi wahusika, wamewagawiwa na wananchi wakiwa ndani yake! Mimi ningetaka hilo jawabu la Kitalu Na. 7, JKT isubiri na wananchi wabaki kwenye nafasi zao mpaka watakapokuwa wamewalipa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa sana hisia za Mheshimiwa Mshama lakini kama nilivyojibu kwenye ufafanuzi wangu, *collective responsibility* ndiyo Serikali inavyofanya kazi. Uamuzi wa kuvigawa hivi vitalu ulitolewa na Baraza la Mawaziri kwa ujumla wake, mimi peke yangu kutoa uamuzi vinginevyo, kwa kweli atakuwa ananibebesha msalaba ambao siyo sahihi maana yake kwanza nitakuwa nimekiuka, nimemdharau hata Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba kwa sababu sisi Waraka kama Wizara tumeshapeleka. Kwa hiyo, ni suala la muda tu mfupi lakini hiki anachosema cha kupiga hicho mimi nimesema siyo sahihi na ndiyo tamko zuri la kumtia *comfort* kwamba wananchi wakae na amani, hawachapwi viboko kama walikuwa wanachapwa viboko, kwa maana kwamba kuwe na amani lakini kwamba kitalu hiki apewe nani, hapa siyo mahali pa kutolea uamuzi.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ataondoka bila shilingi hapa. Mimi nawawakilisha watu ambao nataka niwasemee na unasema Baraza halijaamua lakini JKT iko Kitalu Na. 7, kama wanaendelea kukaa pale ina maana wanawaondoa bila kuwalipa haki zao. Hiyo *Cabinet* ilifanyaje utaratibu wa kuweka watu pale kabla ya waliopo hawajalipwa? Mimi ningependa kujua hilo na ningependa ijadiliwe hivi ni halali miaka mitano niko hapa, miaka mitano iliyopita Rais mwenyewe alikuja Kagera akasema hili tatizo Mama Mshama atalimaliza na mahali alipo nadhani ananisikia, leo nataka kurudi kule wataniuliza tatizo limeisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba lijadiliwe hili suala, wananchi wanapigwa, wengine wamekatiwa migomba yao, kwa nini tusememe JKT isubiri au Waziri mwenyewe analiamuaje, maana akisema arudi kwenye *Cabinet* sijui wanakaa lini, hili tatizo ni kubwa kwa watu wa Kakunyuu Kitalu Na. 7. Kumbuka JKT haikaagi na watu! Wale wana nguvu hawa hawana kitu chochote, niridhishe tu kwamba sasa hivi JKT isubiri tumalize huu mgogoro. Mimi ndiyo nachotaka, bila hivyo shilingi inaondoka.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ni mwakilishi wa wananchi, maneno anayoyasema anawakilisha kilio cha wananchi wake kwa kiasi cha kutosha na chenye uzito wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida anayoipata Waziri mwenye dhamana ya mifugo, masuala ya maamuzi ni ya pamoja ndani ya Serikali, Wizara zinazohusika ni lazima zikutane kwa pamoja. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameonesha umuhimu wa jambo hilo, naomba kumthibitishia, mimi kama kiongozi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninayeshughulikia Uratibu na masuala ya *Coordination* ya shughuli za Serikali tutafanya kwa haraka kikao cha pamoja, kati ya Wizara zote hizo zinazohusika, ikiwemo Wizara ya Mifugo, Wizara ya Ulinzi na wote ambao ni mtambuka katika sekta hiyo na kuona tunafanya nini kwa hatua za haraka na kama tutatoa tamko basi tulitoe tamko kama Serikali tukiwa na uelewa wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Assumpter aelewe kwamba kilio hicho tumekisikia, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeelewa uwakilishi wake kwa wananchi, lakini nimuombe aridhie shilingi hii irudi na Mheshimiwa Waziri hawezi kumaliza kesi hii yeye peke yake bila sekta hizo zote kuridhiana kwa pamoja na kupata maamuzi ya pamoja. Tunamhakikishia kwamba tutalifanyia kazi na Serikali kwa pamoja tutatafuta njia nzuri ya kufanya ili kulimaliza. Kwa hiyo, atuachie tuendelee nalo, amuamini Waziri atalisimamia, aiadini Serikali tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Mbunge aiachie hiyo shilingi ili shughuli zetu ziweze kuendelea. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Waziri, naamini kabisa kwamba hawataniangusha katika hili. Kwa kuwa mimi narudi kule nitakachokwenda kuwaambia ni kwamba hatoki mtu hapa na mtu asipigwe mpaka tutakapokuwa tumemaliza muafaka. Kwa hiyo, nakurudishia shilingi yako na naamini mmenielewa. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*Tshs.1,391,815,203/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Policy and Planning*.....Tshs.1,142,171,056/=

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate maelezo ya kifungu kidogo 220300, *Fuel, Oils, Lubricants*, ambacho mwaka huu kimetengewa shilingi milioni 37 ukilinganisha na shilingi milioni 57 ya mwaka jana. Suala langu ni kwamba bajeti imeshuka sana na kwa bahati mbaya sana Kitengo hiki ni cha Sera na Mipango ambapo sasa hivi tuna changamoto kubwa sana ya migogoro mbalimbali na Kitengo hiki kilitakiwa kifanye kazi hasa hata kule Jimboni kwangu Kisarawe kuna tatizo kubwa sana la wakulima na wafugaji. Watu hawa wanatakiwa wapate mafuta ili watembeke kwa ajili ya kuona ni jinsi gani watatatua matatizo ya wananchi lakini bajeti imeshuka sana. Nataka kupata ufafanuzi kwa nini bajeti imeshuka sana katika eneo hilo? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa alichosema lakini kupanga ni kuchagua, ufinyu wa bajeti na kuongezeka kwa shughuli ndani ya Wizara inabidi turekebishe baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, hatukuwa na jinsi kwa sababu ya ufinyu wa bajeti.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – *Livestock Research and Training Inst.....Tshs. 14,783,301,054/=*

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naongelea kasma 220800, *Training Domestic*; haijatengewa shilingi hata moja na kasma hii inahusu taasisi za mafunzo, ikiwa na maana kwamba Wakufunzi au Wahadhiri walioko katika vyuo hivyo hawatapata nafasi ya kwenda kusoma. Sasa kama husomi wewe unayefundisha maana yake ni kwamba upeo wako unapungua na kwa hiyo uwezo wako wa kufundisha unapungua. Nataka kuelewa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri watashughulikia vipi mafunzo au maendeleo ya utumishi katika taasisi za mafunzo zilizo chini ya Wizara yake?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya eneo hili kwanza iko kwenye miradi ambapo sasa kuna mradi ambao unagharamiwa na wafadhili ambapo *component* hii ya mafunzo imebebwala lakini kuna shughuli nyingine iko upande wa Idara ya Kurugenzi ya Utafiti chini ya Wizara ambayo sasa inaratibu mafunzo na utafiti wote kwa ujumla katika Idara mbalimbali za Wizara.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 – *Government Comm. Unit.....Tshs. 246,685,412/=*
Kif. 1006 – *National Livestock Inst. – Mpwapwa.....Tshs.0/=*
Kif. 1007 – *Internal Audit Unit.....Tshs.342,559,166/=*
Kif. 1008 – *Procurement Mgt. Unit.....Tshs. 489,863,942/=*
Kif. 1009 – *Legal Service UnitTshs.188,004,995/=*
Kif. 1010 – *Information Comm.&Tech.....Tshs.398,574,236/=*
Kif. 7001 – *Veterinary Services.....Tshs.7,934,620,863/=*
Kif. 7005 – *Veterinary Council of Tanzania...Tshs.393,185,164/=*

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 8001 – *Animal ProductionTshs.4,826,712,569/=*

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo *Sub-Vote 8001, Animal Production*; kasma 410900, *Rehabilitation of Plant and Equipment*. Kwa muda mrefu tumekuwa tukizungumza habari za kufufua kiwanda cha nyama kilichoko kule Mbalizi, Mbeya. Mheshimiwa Waziri Mkuu mara kadhaa ameeleza mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kwamba kiwanda hicho kinafufuliwa ikiwa ni pamoja na kutafuta wabia lakini kama hawapatikani Serikali yenyewe kuchukua jukumu hilo. Napenda kufahamu kwa pesa hii iliyopo hapa, je, inajumuisha ufufuaji wa kiwanda kile cha nyama kilichopo kule Mbalizi Mbeya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tu niseme tu kwamba fedha hii makusudi yake ni ukarabati wa mitambo ambayo iko ndani ya Wizara. Kwa sababu hiki Kitengo ni cha uzalishaji ni kwa maeneo yale ya *artificial insemination*, maeneo ambapo kuna vituo vya mifugo, kama kuna mitambo ya namna hiyo ya kuhudumia vitu hivyo, ndiyo inacholenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na kiwanda cha nyama, nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza. Kimsingi Serikali imeshafanya *due diligence* ya kuwabaini na sisi kama Wizara tayari tumeshaandika Waraka kwa Baraza la Mawaziri ili liweze kutoa uamuzi ili kiwanda hicho kiweze kutumika. Naelewa jinsi anavyoguswa na watu wa Mbeya wanavyoguswa pia kwa ujumla kwa sababu lilishazungumzwa hata kwenye kikao chao cha uwekezaji wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu umuhimu wa kiwanda kile. Kwa hiyo, tayari Serikali iko hatua za mwisho, mwekezaji anaweza akaanza kazi wakati wowote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nazungumzia kasma 271200, *Current Grants to Households & Unincorporate Business*; naomba ufafanuzi juu ya walionufaika na fedha zilizotolewa katika miaka miwili iliyopita na wanufaika kwa mwaka unaoakuja katika kasma hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma hii inalenga kuendeleza zao la ngozi nchini, usindikaji, ubora na biashara yake. Kwa hiyo, katika Wizara kuna mpango wa kuendeleza zao la ngozi katika Halmashauri 75 nchini. Iko orodha ndefu, Mheshimiwa Mbunge akiihitaji tutampatia ili aelewe na mpango ule unaendelea na unategemea vilevile kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko katika kasma ya 220200, *Utility Supplies and Services*. Mwaka wa Fedha uliopita kulikuwa imetengwa shilingi milioni 12 lakini mwaka huu wa fedha imetengwa shilingi milioni 70 lakini hapohapo ukiangalia kifungu kidogo cha chini bajeti ya mafuta imeshuka.

Nilikuwa na hoja hapa kwamba tumetoka shilingi milioni 12 mpaka shilingi milioni 70 lakini uwezeshaji katika suala zima la mafuta ili wataalam waweze kutembea bajeti imeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuko katika Fungu moja, kama utaridhia, nia yangu hii shilingi milioni 70 kama hatudaiwi madeni mbalimbali ya umeme na maji basi angalau pesa hiyo tui punguze tuipeleke sehemu nyingine. Kama maeneo haya tumeondoka na madeni basi tuko pamoja lakini nina wasiwasi kwamba hapa tumetenga pesa nyingi zaidi lakini kuna vifungu vingine hali yake ni tete. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Jafo kuhusiana na nyongeza kubwa inayoonekana hapa. Kimsingi ni mabadiliko tu ya kasma. Hii *Utility Supplies and Services* inalenga kugharamia umeme, *internet*, maji na simu. Zamani gharama hizi za maeneo mengine ambayo ni vituo vya uzalishaji wa mifugo mfano Mabuki, Kitulo, mashamba yetu mbalimbali kikiwemo na kituo cha Nangaramo, yalikuwa yanalipwa kupitia Kifungu cha Utawala ambacho ni 1001 na 1002 na 1003, sasa Idara hizi zimebeba gharama zake halisi ndiyo maana anaona hali hiyo ilivyo hapo. Umeme ni muhimu sana kwenye haya mashamba, kama hamna umeme unawezaje kukamuaje ng'ombe 200 kwa mkono, unahitaji umeme kukamua na kupooza maziwa na vitu kama hivyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 9001 – Fisheries Development Div.....Tshs. 7,928,164,045/=

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba ufafanuzi kasma ya 270400, *Current Grants to Non Financial Public Units*, ni zipi hizo? Nina-declare interest mimi ni mvuvi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinalenga kuhudumia taasisi zilizoko ndani ya Wizara ambazo zilikuwa bado hazijajitegemea. Hapa kwa Idara hii tunacho Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU). Kwa hiyo, fedha hiyo ndiyo inalenga kuhudumia Kitengo hicho.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi niko katika sub-vote 230400, *Routine Maintenance and Repair of Vehicle and Transport Equipment*. Mwaka juzi kilitengewa shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kufanya repair ya magari na vyombo mbalimbali. Nashangaa mwaka huu umetenga shilingi milioni 85. Naomba ufafanuzi, je, hakuna matengenezo mengine ambayo yanahitajika ambayo kwa kweli yanawiana na hii amount ambayo ulitumia ya shilingi bilioni 1.4 hadi kufikia shilingi milioni 85, naomba ufafanuzi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hapa nishukuru Watendaji wa Wizara yangu huwa ni wakweli sana kwa sababu wanaweka gharama halisi. Tunamshukuru Mungu, kama mlikuwa mnafuatilia Hotuba yangu, tumepata boti mpya na magari mapya na ndiyo fedha hizi zinakusudia kufanyia service vifaa hivyo. Sasa magari mapya gharama zake zinakuwa chache, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 9002 – Aquaculture Dev. Div.Tshs.1,234,109,895/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kasma 4107700, *Feasibility Studies, Project Preparation and Design*. Vijana wengi nchini hawana ajira na kwa muda mrefu tumekuwa tukishauri Serikali kwamba ni vizuri sasa vijana wasaidiwe kuondokana na tabia ya kukaa bila kazi. Njia mojawapo ni kuwashawishi na kuwawezesha kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ikiwa kazi itakayofanyika katika kasma hii inajumuisha, kwa sababu nimeona katika karibu kila Idara ina fedha hizi, kazi hiyo ya walau kuwasaidia vijana kuandaa miradi yao pamoja na kuanzisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi alichosema Mheshimiwa Mbunge kuna ukweli lakini kasma hii inalenga zaidi kuandika taarifa za shughuli mbalimbali.

Kwa hicho anachokisema Mheshimiwa Mbunge, kimebebwa zaidi kwenye mipango yetu ya maendeleo ambapo Idara hii ya ufugaji wa samaki imeongezewa fungu ili iweze kukidhi hayo matamania ambayo anayazungumza Mheshimiwa Mbunge.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni 104(2) kwa kuwa, zimebaki dakika 10 ili muda nilioongeza umalizike, sasa nafunga mazungumzo yanayoendelea na sasa tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu!

KITABU CHA IV

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 99 - WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

Kif. 1003 – *Policy and Planning*Tshs.1,285,563,000/=

Kif. 1004 – *Livestock Research and Training Unit*Tshs.3,309,781,000/=

Kif. 1006 – *National Livestock Inst. – Mpwapwa*TShs. 0/=

Kif. 7001 – *Veterinary Services*TShs.3,626,953,000/=

Kif. 8001 – *Animal Production*TShs.7,028,161,000/=

Kif. 9001 – *Fisheries Dev. Division*.....TShs.5,574,467,000/=

Kif. 9002 – *Aquaculture Dev. Division*.....TShs.1,826,557,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri.

TAARIFA

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limepitia Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2015/2016, kifungu kwa kifungu na kupitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

*(Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016
yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Nawatakia kila la kheri na utekelezaji mwema na yale yote yaliyojitokeza basi yaweze kushughulikiwa. Hongereni sana. *(Makofi)*

Kuna Matangazo, Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge anawatangazia Wabunge wote kuwa wamegawa kwenye masanduku (*pigeon holes*) Taarifa mbalimbali za Mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa Mezani jana, tarehe 19 Mei, 2015. Hivyo, wanawaomba mkazichukue ili kutoa nafasi kwa nyaraka nyingine zitakazoendelea kupokelewa.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge, wakati Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa anaweka Mezani Taarifa hiyo ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ilikuwa inakwenda sambamba na Majibu ya Serikali kuhusu hoja hizo. Kwa hiyo, utaratibu wetu ni kwamba vile vyote vitu viwili vinakwenda sambamba.

MWENYEKITI: Ahsante kwa taarifa. Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 02.20 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 21 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)